UCHANGANUZI KIMTINDO WA MASUALA YA DINI NA MAMLAKA KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI

NA

KYOMUHENDO VICTOR

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA KIJAMII, IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA ILI KUTIMIZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA MOI

2025

IKIRARI

MTAHINIWA

Hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu chochote ili kutimiza mahitaji ya shahada yoyote. Hairuhusiwi kutolesha sehemu yoyote ya tasnifu hii bila ya ridhaa yangu na/au ya Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi:_________________________________ Tarehe:__________________

KYOMUHENDO VICTOR

SASS/DPHIL/KIS/02/2019

WASIMAMIZI

Tasnifu hii imetolewa kwa ajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi:_________________________________ Tarehe:__________________

PROF. SAMUEL MOSETI OBUCHI

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

Sahihi:_________________________________ Tarehe:__________________

PROF. MOSOL MARK KANDAGOR

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabarukia wapenzi wote wa Isimu na Fasihi ya Kiswahili.

SHUKRANI

Ninakishukuru Chuo Kikuu cha Makerere kwa kunipa fursa ya kwenda ng'ambo kusoma kozi hii na pia kufadhili masomo yangu.

Ninawashukuru sana wasimamizi wangu, Prof. Samuel M. Obuchi na Prof. Mosol M. Kandagor, siyo kwa kunisimamia tu, lakini pia kwa moyo wao wa kunielekeza, kunishauri na kunitia motisha ambayo imekuwa nguzo katika kukamilisha utafiti huu. Mchango wenu umekuwa nguzo katika kukua kwangu kitaaluma.

Tena, namshukuru Dkt. Magdaline Wafula kwa mchango wake mkubwa wa kitaaluma katika kuiumba kazi hii.

Ninamshukuru mama yangu ambaye amekuwa mhimili katika masomo yangu tangu shule ya msingi mpaka sasa.

IKISIRI

Utafiti huu unachunguza nduni mahsusi za kimtindo zinazotumiwa na waandishi wa riwaya teule za Kiswahili kusawiri maudhui ya dini na mamlaka. Riwaya zilizoteuliwa ni: *Paradiso* (2005) ya John Hamu Habwe, *Nguvu ya Sala* (1999) ya Kyallo Wadi Wamitila , *Asali Chungu* (1978) ya Said Ahmed Mohamed, pamoja na *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1978) ya Shafi Adam Shafi. Ingawa kijuujuu riwaya hizi zinachunguza maudhui ya dini na mamlaka, kiundani zinachunguza masuala kama vile jinsia, ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana, uhalifu mijini, umaskini, ufisadi, tamaa ya pesa na mali, na ukandamizaji. Haya ni masuala ibuka ambayo waandishi wa riwaya teule wanayaangazia kwa mtazamo wa dini na mamlaka. Mkabala wa kimtindo haujatumika sana kuchunguza masuala ibuka kama haya katika riwaya ya Kiswahili. Uchunguzi huu uliongozwa na malengo yafuatayo: kufafanua jinsi uteuzi wa kileksika unavyojitokeza kama nduni ya kimtindo katika kuchimuza masuala ya dini na mamlaka katika riwaya teule. Kuchanganua matumizi ya nduni za kisintaksia katika kuchimuza maudhui ya dini na mamlaka katika riwaya teule. Kuhakiki matumizi ya tamathali za usemi kama mbinu za kimtindo katika uchimuzi wa masuala ya dini na mamlaka katika riwaya teule. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uchimuzi. Uchanganuzi wa data uliongozwa na mihimili ya Nadharia ya Uchimuzi: ukiushi na usambamba. Utafiti huu ni wa kitaamuli na tulitumia muundo wa usanifu kifani. Mkabala wa kitaamuli ulitumiwa kwa sababu utafiti huu unazingatia fasiri ya ruwaza za nduni mahsusi za kiisimu, mintarafu ya masuala ya dini na mamlaka. Tena, tulizingatia mfumo wa kifalsafa wa kiufasiri. Data ilikusanywa kutoka riwaya nne za Kiswahili ambazo ziliteuliwa kimaksudi. Mahitimisho ya utafiti yaliwasilishwa kidhamira. Kuhusu lengo la kwanza, utafiti huu uligundua kwamba visawe na urudiaji ndiyo mikakati ya kileksika iliyotumiwa zaidi na waandishi kuibua masuala ya dini na mamlaka katika riwaya teule. Kuhusu lengo la pili, iligundulika kwamba anafora na usambamba wa kiusawe ndizo mbinu za kiusambamba zilizotumika zaidi katika riwaya teule. Aina nyingine za usambamba zilizotumiwa ni pamoja na epifora, tanakuzi, na mgeuko wa polepole. Kuhusu lengo la tatu, tamathali ya usemi iliyotumiwa zaidi kuchimuza maudhui ya dini na mamlaka ni sitiari. Hata hivyo, mbinu za tashbihi, kinaya na kejeli pia zilitumika sana katika riwaya zote zilizochanganuliwa. Kwa jumla, inadhihirika kwamba mamlaka yana dhima muhimu sana katika maisha ya wanajamii kwa vile yamefumwa katika mfumo wao wa kijamii, kisiasa, na kiuchumi. Utafiti huu unaonyesha kwamba waandishi wanadhamiria kujenga maudhui kuhusu masuala ya dini na mamlaka na wanatumia mbinu zinazoonyesha jinsi ambavyo matini zinajadili masuala ya muhimu katika jamii zinazosawiriwa. Utafiti huu unasisitiza haja ya kuziangalia matini kama mazao ya jamii husika zinazosawiriwa. Unabainisha utaratibu wa kuzichanganua riwaya za Kiswahili kwa kuzingatia ngazi za kileksika, kisarufi na kisemantiki. Utafiti huu unapendekeza tafiti nyingine za kimtindo zifanywe kwa kuzingatia nadharia nyingine kuchunguza masuala ya dini na mamlaka. Pia akili unde ihusishwe katika utafiti wa kimtindo.

ABSTRACT

The study examines specific stylistic features employed by the authors of selected Kiswahili novels to depict themes of religion and power. The selected novels are: *Paradiso* (2005) by John Hamu Habwe, *Nguvu ya Sala* (1999) by Kyallo Wadi Wamitila, *Asali Chungu* (1978) by Said Ahmed Mohamed, and *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1978) by Shafi Adam Shafi. Although the novels overtly depict the themes of religion and power, they covertly explore issues of gender, youth unemployment, urban crime, poverty, corruption, greed for wealth and power, and oppression. These are emerging issues which the authors address from religious and power perspectives. The stylistic approach has rarely been used to study these emerging issues in the Kiswahili novel. The study was guided by the following objectives: to explain lexical choice as a stylistic feature in foregrounding the themes of religion and power in the selected novels; to analyse the use of syntactic features in foregrounding the themes of religion and power in the selected novels; to discuss the use of figures of speech as stylistic strategies in foregrounding the themes of religion and power in the selected novels. Data collection and analysis was guided by the Foregrounding Theory. The study is qualitative in nature, using a case study design. We used a qualitative approach because the study is based on the interpretation of specific stylistic features in regard to the themes of religion and power. An interpretivism philosophical approach was used to guide the study. Purposive sampling was used to select four Kiswahili novels from which data was collected. The findings of the study were presented thematically. On objective one, the findings revealed that synonyms were the lexical strategies mostly used by the authors to depict themes of religion and power. On objective two, anaphora and synonymic parallelism were the dominant forms of parallelism used in the selected texts. Other forms of parallelism included: epiphora, antithesis and gradation. Regarding objective three, the figure of speech mostly used to foreground the themes of religion and power was metaphor. Other figures of speech including simile, irony and sarcasm also featured a lot in all the novels. Generally, it is clear that power plays a vital role in people's lives, especially as it is woven in their social, political and economic fabric. The study shows that the authors are deliberate in the portrayal of the themes and they employ techniques that show how texts discuss issues close to the lives of the communities they depict. Therefore, the study emphasises the need to look at texts as products of the communities. The study lays down a systematic way of analyzing Kiswahili novels using a stylistic approach which is based on the lexical, syntactic and semantic levels of language. We propose further stylistic studies using other theories to examine the issues of religion and power. Also Artificial Intelligence could be incorporated in stylistic research.

YALIYOMO

IKIRARI ii
TABARUKU iii
SHUKRANI..iv
IKISIRI v
ABSTRACT..vi
YALIYOMO...vii
VIJELEZI VYA ISTILAHI xi
SURA YA KWANZA 1
MISINGI YA UTAFITI 1
1.0 Utangulizi..1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti 1
1.1.1 Maelezo mafupi tangulizi kuhusu elimumitindo 1
1.1.2 Uchunguzi Kimtindo wa Fasihi ya Kiswahili 2
1.2 Suala la Utafiti 5
1.3 Malengo ya Utafiti 6
1.4 Maswali ya Utafiti...7
1.5 Sababu za Kuchagua Mada 7
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti...7
1.7 Umuhimu wa Utafiti huu 9
1.8 Muhtasari wa Sura 10
SURA YA PILI...11
MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA............................11
2.0 Utangulizi...11
2.1 Tafiti Tangulizi za Kimtindo katika Kiswahili 11
2.2 Kiunzi cha Nadharia 19
2.2.1 Nadharia ya Uchimuzi 19
2.2.1.1 Asili ya Nadharia ya Uchimuzi...22
2.2.1.2 Mihimili ya Nadharia ya Uchimuzi 23
2.2.1.2.1 Ukiushi..23
2.2.1.2.2 Usambamba...25
2.2.1.3 Mshikamano wa Uchimuzi 27
2.3 Pengo la Utafiti 27

2.4 Muhtasari wa Sura 28
SURA YA TATU 29
MBINU ZA UTAFITI 29
3.0 Utangulizi 29
3.1 Eneo la Utafiti 29
3.2 Muundo wa Utafiti 29
3.3 Wango wa Utafiti 30
3.4 Sampuli na Usampulishaji 30
3.5 Ukusanyaji wa Data 31
3.5.1 Mbinu za Kukusanya Data 32
3.6 Vifaa vya Utafiti 32
3.7 Uchanganuzi wa Data 32
3.8 Maadili ya Kiutafiti 33
3.9 Muhtasari wa Sura 34
SURA YA NNE 35
UTEUZI WA KILEKSIKA KAMA NDUNI YA KIMTINDO KATIKA KUCHIMUZA MAUDHUI YA DINI NA MAMLAKA KATIKA RIWAYA TEULE 35
4.0 Utangulizi 35
4.1 Maelezo ya Riwaya Teule 35
4.1.1 Riwaya ya *Paradiso* ya John Hamu Habwe (2005) 35
4.1.2 Riwaya ya *Nguvu ya Sala* ya Kyallo Wadi Wamitila (2003) 37
4.1.3 Riwaya ya *Asali Chungu* ya Said Ahmed Mohamed (1978) 38
4.1.4 Riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* ya Shafi Adam Shafi (1978) 40
4.2 Uteuzi wa Kileksika kama Nduni ya Kimtindo katika Usawiri wa Maudhui ya Dini na Mamlaka katika Riwaya Teule 41
4.2.1 Matumizi ya Visawe 41
4.2.2 Matumizi ya Vinyume 50
4.2.3 Mbinu ya Kuhamisha Nomino kutoka Ngeli Moja Hadi Ngeli Nyingine 52
4.2.4 Udunishaji 55
4.2.5 Utohozi 58
4.2.6 Urudiaji Kileksika 60
4.2.7 Matumizi ya Msamiati wa Kitathmini 77
4.2.8 Matumizi ya Uolezi 92

4.2.8.1 Uolezi wa Fasi....92
4.2.8.2 Uolezi wakati....95
4.2.8.3 Uolezi wa Kijamii....95
4.2.8.4 Uolezi wa Nafsi....99
4.2.9 Matumizi ya Vitenzi vya Kitambuzi....100
4.3 Muhtasari wa Sura....104
SURA YA TANO....105
MATUMIZI YA NDUNI ZA KISINTAKSIA KATIKA KUCHIMUZA MAUDHUI YA DINI NA MAMLAKA KATIKA RIWAYA TEULE....105
5.0 Utangulizi....105
5.1 Usambamba....105
5.1.1 Mbinu ya Anafora (Pia Epanafora)....106
5.1.2 Epifora....123
5.1.3 Tanakuzi....126
5.1.4 Muundogeu/muundopindu (Chiasmus)....131
5.1.5 Matumizi ya mbinu ya mjalizo/asindeto....133
5.1.6 Usambamba Kiusawe....135
5.1.7 Mgeuko wa polepole (Gradation)....145
5.1.8 Udondoshaji....150
5.1.8.1 Udondoshaji katika uanzaji kati (In medias res)....152
5.1.9 Uorodheshaji....154
5.2 Matumizi ya Kauli ya Kutendwa....158
5.3 Muhtasari wa Sura....161
SURA YA SITA....162
MATUMIZI YA TAMATHALI ZA USEMI KAMA MBINU ZA KIMTINDO KATIKA UCHIMUZI WA MASUALA YA DINI NA MAMLAKA KATIKA RIWAYA TEULE....162
6.0 Utangulizi....162
6.1 Tamathali za Usemi Zilizotumika katika Riwaya Teule....163
6.1.1 Sitiari....163
6.1.2 Tashbihi....194
6.1.3 Tashihisi....206
6.1.4 Kinaya....213
6.1.5 Kejeli....226

6.1.6 Chuku 234
6.1.7 Maswali ya Balagha 237
6.1.8 Haipofora 240
6.1.9 Dokezo 242
6.1.10 Matumizi ya Majina kama Ishara 244
6.1.10.1 Mbinu ya Majazi 244
6.1.10.1.1 Matumizi ya Aptronimu 245
6.1.10.1.1.1 Aptronimu katika Riwaya ya *Paradiso* 245
6.1.10.1.1.2 Aptronimu katika Riwaya ya *Nguvu ya Sala* 247
6.1.10.1.1.3 Aptronimu katika Riwaya ya *Asali Chungu* 248
6.1.10.1.1.4 Aptronimu katika Riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* 250
6.1.10.2 Matumizi ya Toponimu 251
6.1.10.3 Majina ya Magari 254
6.2 Muhtasari wa Sura 257
SURA YA SABA 258
MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI 258
7.1 Muhtasari wa Utafiti 258
7.2 Mahitimisho ya Utafiti 258
7.2.1 Uteuzi wa Kileksika kama Nduni ya Kimtindo katika Kuchimuza Maudhui katika Riwaya Teule 259
7.2.2 Matumizi ya Nduni za Kisintaksia katika Kuchimuza Maudhui katika Riwaya Teule 262
7.2.3 Matumizi ya tamathali za usemi kama mbinu za kimtindo katika kuchimuza maudhui katika riwaya teule 265
7.3 Mchango wa Utafiti Huu 267
7.4 Hitimisho 268
7.5 Mapendekezo 269
MAREJELEO 270
VIAMBATISHO 279
Kiambatisho 1: Madondoo ya Data kutoka *Paradiso* 279
Kiambatisho 2: Madondoo ya Data kutoka *Nguvu ya sala* 291
Kiambatisho 3: Madondoo ya Data kutoka *Asali Chungu* 297
Kiambatisho 4: Madondoo ya Data kutoka *Kasri ya Mwinyi Fuad* 305
Kiambatisho 5: Cheti cha Plagiarism 312

VIJELEZI VYA ISTILAHI

Dini	1. Imani inayohusiana na mambo ya kiroho kwamba kuna muumba ambaye aliuumba ulimwengu huu na kwamba ndiye mtawala wa kila kilichomo. 2. Mfumo fulani wa imani hii na njia ya kuabudu, kusali na kuheshimu/kutii huyo muumba kama vile Ukristo, Uislamu, Uyahudi, na kadhalika.
Elimumitindo	Taaluma inayochunguza kazi za kifasihi kwa misingi ya kiisimu.
Isimu	Taaluma ya ufafanuzi, uchambuzi na uchanganuzi wa lugha kwa kutumia mbinu za kisayansi.
Kabaila	Tajiri aliye na majumba na ardhi za kupangisha kwa faida yake binafsi au za watu wachache.
Kasri	Jumba kubwa la fahari
Kileksika	Kuhusiana na sehemu ya sarufi iliyo na taarifa zote za maneno
Kisintaksia	Kuhusiana na utanzu wa sarufi unaojishughulisha na uchanganuzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake.
Mamlaka	Amri au uwezo wa juu wa kuongozea mambo, shirika au shughuli fulani.
Matini	Kifungu cha diskosi chenye urefu wowote na ambacho ni semwa.
Mtindo	Jinsi mtunzi wa kazi ya kisanaa anavyotumia lugha kujieleza.
Nduni	Sifa maalum ya kitu.
Paradiso	Mahali patakatifu ambapo panaaminiwa kuwa waumini wanaofuata amri za mwenyezi Mungu na kuacha makatazo yake

wataishi kwa raha baada ya kufufuliwa na kulipwa kwa matendo yao.

Tamathali ya usemi Fungu la maneno au hata neno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine.

Uajinabishaji Hali ya kukifanya kipengele fulani, hasa cha kilugha ya kifasihi, kijitokeze wazi kikilinganishwa na lugha ya kawaida.

Uchimuzi Njia ya kuvifanya vipengele fulani vya mtindo vijitokeze.

Ujumi Sifa za uzuri na urembo katika fasihi na sanaa kwa jumla.

Ukiushi Uvunjaji kimaksudi wa kaida za matumizi ya lugha ili kubuni njia mpya za kujieleza

Uolezi Unajumuisha vipengele vya kiisimu vinavyotambulisha virejeleo kwa kuzingatia hali iliyopo ya usemaji

Usambamba Mbinu ya kuyarudia maneno fulani au maana fulani kwa muundo mwingine tofauti.

SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Sura hii inabainisha misingi ya utafiti huu. Inaelezea usuli wa utafiti na suala la utafiti. Pia, inaweka wazi malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, pamoja na umuhimu wa utafiti huu.

1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

1.1.1 Maelezo mafupi tangulizi kuhusu elimumitindo

Elimumitindo ni mkabala mmojawapo wa kiisimu unaotumiwa kuzichanganua kazi za kifasihi. Kwa mujibu wa Candria (2019), kwa vile lugha ni kipengele cha msingi cha fasihi, elimumitindo, kama taaluma inayochunguza lugha ina mamlaka au uwezo wa kuchunguza kazi za kifasihi. Elimumitindo ni uchunguzi na ufafanuzi wa matini kwa mkabala wa kiisimu (Short, 2013). Uchunguzi wa kimtindo unahusisha maelezo ya kiisimu na fasiri ya miundo ya kiisimu kwa njia wazi iwezekanavyo.

Kwa mujibu wa Short (2013), kazi za awali zilijihusisha sana na kujaribu kueleza mtindo wa mwandishi, lakini katika miaka kumi na mitano (kabla ya mwaka wa toleo lake la 2013), juhudi kubwa ya uchambuzi wa kiisimu imekuwa katika kujaribu kuelewa uhusiano kati ya matini ya kifasihi, kwa upande mmoja, jinsi tunavyoielewa, na jinsi tunavyoathiriwa na matini hiyo, kuliko kuangalia mtindo wa mwandishi. Huu ni mkabala wa kitaamuli, tofauti na mkabala wa kitakwimu ambao unalenga kulinganisha mitindo ya waandishi kwa kutumia takwimu.

Ingawa kimsingi kazi zinazochunguzwa katika elimumitindo ni za kifasihi au kazi zenye sifa za kiujumi, taaluma hii imepanuka ambapo sasa kazi zinazochunguzwa ni

pamoja na kazi ambazo si za kifasihi. Hii ni kwa sababu matumizi ya lugha kwa kawaida huwa yanahusisha utofauti kwa njia moja au nyingine.

Tunaunga mkono maoni ya Leech (2008) kwamba elimumitindo ichukuliwe kama taaluma inayohusisha uwanja wa isimu na uwanja wa fasihi ambapo kuna mwingiliano kati ya taaluma hizi mbili. Huo ndio mwelekeo tunaoufuatilia katika utafiti huu.

Kama tulivyotaja hapo awali, elimumitindo ilijikita sana katika kutambua mtindo wa mwandishi. Huu ulikuwa ni mkabala wa kuangalia mtindo kama "mtu". Iliaminika kwamba mchunguzi angeweza kuisoma kazi fulani akaamua kwamba kazi hiyo imeandikwa na mtunzi fulani. Lakini msimamo huo ulipoteza nguvu kwa vile ulizingatia zaidi mwandishi wala siyo kazi iliyoandikwa, yaani matini yenyewe. Kwa hivyo, kulizuka mikabala mingine iliyozingatia matini na msomaji, kama vile elimumitindo ya kijinsia, elimumitindo ya kitambuzi, elimumitindo ya kikopasi, na mingineyo.

1.1.2 Uchunguzi Kimtindo wa Fasihi ya Kiswahili

Zipo tafiti kadhaa ambazo zimefanywa kuhusu kazi za kifasihi za Kiswahili kimtindo katika kiwango cha uzamili na cha uzamifu. Hata hivyo, kuna haja utafiti zaidi katika uwanja huu ambao unaendelea kukua, hasa kubainisha taratibu za kufanyia uchunguzi.

Katika uchunguzi wa kimtindo wa kazi za Kiswahili, Kitsao (1975) ameweka msingi wa uchunguzi wa aina hiyo. Uchunguzi wake unaonyesha jinsi uchanganuzi wa kimtindo wa kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili unaweza kufanywa kwa kuzingatia vipengele vya kileksika, kisarufi, na kisemantiki. Mchango wa Kitsao katika uchunguzi wa kazi za fasihi ya Kiswahili kimtindo unadhihirika tunapozingatia kwamba alifanya utafiti wake wakati ambapo mbinu za uchunguzi wa aina hii zilikuwa bado changa. Anaweza kuangaliwa kama mtangulizi wa utafiti wa kimtindo wa kazi za fasihi ya

Kiswahili. Kwa hivyo, ingawa kazi yake itakuwa na mapungufu, kama zilivyo kazi zozote za kiutafiti, bado hii ni kazi muhimu rejelezi kwa uchunguzi wa kimtindo.

Katika tasnifu yake ya uzamifu, Kitsao (1982) amefanya uchanganuzi wa kimtindo wa kazi za tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiswahili (ushairi, tamthilia na riwaya) akitumia mkabala wa kitakwimu ambapo anazingatia vipengele vya msamiati, sarufi na semantiki. Anakisia kwamba katika utafiti wake hakuzingatia sana kipengele cha semantiki kwa vile vipimo vya kitakwimu vilikuwa bado vinahitaji kuendelezwa ili kuweza kushughulikia ngazi hii ya matini vya kutosha. Kuhusu riwaya amezingatia hasa jinsi mdafao wa nduni za kiisimu unavyozitofautisha matini tofauti mintarafu waandishi wa matini hizo. Pia, anaangazia jinsi mdafao huo wa nduni za kila kipengele cha lugha, kama vile urefu wa sentensi, kategoria za kileksika na idadi ya silabi unavyoathiri usomekaji wa matini mahsusi.

Ingawa uchunguzi wa kitakwimu unaweza kuitofautisha mitindo ya matini mbalimbali, kipengele cha maudhui kimeachwa nyuma na uchunguzi wa kitakwimu wa Kitsao (1982). Badala yake yeye anaeleza kwamba aliamua kukishughulikia kipengele hicho kwa kutumia uchanganuzi wa kijadi wa kifasihi. Hii inaashiria udhaifu wa mkabala wa kitakwimu katika kuchunguza kipengele cha maudhui katika riwaya – kwa mujibu wa Kitsao.

Mtafiti mwingine mtangulizi ambaye amefanya uchunguzi wa kimtindo wa kazi za Kiswahili ni Kazungu (1982). Kazungu anachunguza ukiushi na uchimuzi wa kazi kutoka tanzu tatu za fasihi ya Kiswahili: riwaya, shairi na tamthilia. Uchunguzi wake ulikuwa katika kiwango cha uzamili. Kazungu hashughulikii suala maalum, ila anafanya uchanganuzi wa jumla tu wa vipengele vya lugha katika kazi alizoziteua. Amezingatia viwango vya kileksika, kigrafolojia, kisintaksia na kisemantiki. Huu ni

uchunguzi muhimu sana unaochangia taaluma ya elimumitindo katika Kiswahili. Hata hivyo, uchunguzi wa Kazungu unakosa kina ambacho kingemsaidia msomaji kupata uelewa mpana wa uchambuzi wa kimtindo. Tena hafuatilii suala au masuala fulani mahsusi ambayo yanahusiana na jamii kwa njia ya moja kwa moja. Hivyo, kuna haja ya kuchambua kazi za fasihi ya Kiswahili kimtindo kwa kina zaidi.

Naye Michira, katika tasnifu yake ya uzamili (1993), anachanganua lugha ya wachuuzi na lugha ya matangazo ya kibiashara redioni kimtindo. Michira analenga "kudhihirisha upekee wa kila aina ya lugha hizi pamoja na uhusiano kati yao; kati yao na aina nyingine za matumizi ya lugha." Kazi hii ni mchango kwa uchunguzi wa kimtindo katika Kiswahili, ila katika uchunguzi wa kimtindo wa siku hizi kinachosisitizwa zaidi sio kutofautisha mitindo, bali kuchunguza ubunifu wa kiisimu wa mwandishi katika kuwasilisha maudhui yake. Kwa hivyo, kinachosisitizwa ni jinsi mwandishi anavyowasilisha maudhui katika kazi yake, pamoja na kile kinachowasilishwa, yaani maudhui au ujumbe.

Tena, Michira (2018) alichapisha makala *A Stylistic Analysis of John Habwe's Pendo La Karaha* (uchanganuzi wa kimtindo wa riwaya ya John Habwe *Pendo La Karaha*) ambamo amezingatia viwango vitatu vya uchunguzi kimtindo yaani, kiwango cha kileksika, kiwango cha kisintakia na kiwango cha kisemantiki. Hii ni makala inayotoa taarifa muhimu ya kimtindo, ingawa ni makala ya jarida. Michira pia anatenganisha mbinu za usambamba, anafora na tanakuzi, wakati ambapo tunachukulia anafora na tanakuzi kama aina za usambamba.

Wasike (2020) katika tasnifu yake ya uzamifu anachunguza mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika kazi za kifasihi, akizingatia kielelezo cha tanzu teule za fasihi andishi mkiwemo riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Wasike ameegemeza utafiti

wake kwenye kipengele kimoja cha mtindo peke yake: tamathali za usemi. Hakuzingatia vipengele vingine vya kimtindo kama vile msamiati na sintaksia. Vipengele vya kileksika na kisintaksia ni muhimu sana katika kupata kuelewa zaidi dhana husika za utafiti. Katika utafiti wetu tunazingatia vipengele vyote vitatu.

Kimgung (2021) anachunguza mitindo ya uhalisia mazingaombwe katika riwaya teule za Kiswahili kama nyenzo za mivurugo katika jamii. Anaangazia namna mitindo inavyowakilisha mivurugo na mitafaruku ya kijamii katika riwaya ya Kiswahili ya kimazingaombwe. Kwa kweli, uchunguzi wake haudhihirishi nduni za kimtindo, ingawa neno "mitindo" limetajwa katika mada ya tasnifu yake.

Ni bayana kuwa tafiti za kimtindo za kazi za Kiswahili hazionyeshi uchunguzi mpana wa vipengele vya uchanganuzi wa kimtindo. Hivi ni vipengele muhimu katika uchanganuzi wa kimtindo. Vipengele hivi vimetambulishwa na wanamitindo Leech na Short (2007) katika orodha yao ya vipengele vya kiisimu na kimtindo vinavyofaa kuzingatiwa katika uchunguzi wa kimtindo.

Tafiti tulizozirejelea haziangazii masuala ya masuala ya dini na mamlaka. Masuala haya yanahusisha masuala mengine ndani yake kama vile uongozi, tamaa ya pesa na mali, migogoro katika jamii, masuala ya jinsia na familia, na ugawanaji wa rasilimali. Ni muhimu kuyachunguza masuala haya kwa mkabala wa kimtindo ili kuyafafanua na kuyafanya yaeleweke. Hii ni njia mojawapo inayoweza kuboresha mahusiano kati ya wanajamii. Hili ni pengo tunalolishughulikia katika utafiti wetu wa kimtindo.

1.2 Suala la Utafiti

Ingawa masuala ibuka mbalimbali yamechunguzwa kimtindo katika tafiti za fasihi ya Kiswahili, kuna pengo la kitaaluma kuhusiana na namna masuala ya dini na mamlaka yanavyojengwa na kuwasilishwa kimtindo katika riwaya za Kiswahili. Tafiti za

kimtindo zilizotangulia kama za Wasike (2021) na Kimgung (2021) zimejikita zaidi katika masuala ya UKIMWI, pamoja na mitafaruku katika kijamii.

Riwaya kama *Paradiso*, *Nguvu ya Sala*, *Asali Chungu*, na *Kasri ya Mwinyi Fuad* zinaakisi mwingiliano mpana kati ya masuala ya kiuchumi, matamanio ya mamlaka, na misimamo ya kidini, lakini mwingiliano huu haujafafanuliwa kimakini kwa kutumia mkabala wa kimtindo unaohusisha viwango vya leksia, sintaksia na semantiki.

Kwa hivyo, mwanzo wa tatizo unatokana na ukosefu wa uchambuzi wa kina unaoonyesha jinsi mbinu za kimtindo zinavyojitokeza katika kujenga na kuwakilisha dhamira za dini na mamlaka katika riwaya hizi. Kukosekana kwa mchango huo kunazuia uelewa mpana wa namna fasihi inavyoakisi, kukosoa au kuendeleza mifumo ya mamlaka na imani katika jamii za Afrika chini ya Jangwa la Sahara.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

(i) Kufafanua jinsi uteuzi wa kileksika unavyojitokeza kama nduni ya kimtindo katika kuchimuza masuala ya dini na mamlaka katika riwaya teule.

(ii) Kuchanganua matumizi ya nduni za kisintaksia katika kuchimuza maudhui ya dini na mamlaka katika riwaya teule.

(iii) Kuhakiki matumizi ya tamathali za usemi kama mbinu za kimtindo katika uchimuzi wa masuala ya dini na mamlaka katika riwaya teule.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

(i) Nduni za kileksika zimetumiwaje kimtindo ili kusawiri maudhui ya dini na mamlaka katika riwaya teule?

(ii) Nduni za mtindo za kisintaksia zimetumiwaje katika riwaya teule ili kusawiri maudhui ya dini na mamlaka?

(iii) Waandishi wa riwaya teule za Kiswahili wamezitumiaje tamathali za usemi ili kuwasilisha masuala ya dini na mamlaka katika riwaya zao?

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Mtafiti aliichagua mada hii kwa sababu zifuatazo:

Katika mapitio ya maandishi ya awali, mtafiti aligundua kwamba taratibu na mbinu ambazo zinazingatia ubunifu wa kiisimu kuliko mtindo wa mwandishi hazijabainishwa katika Kiswahili. Kwa hivyo, mtafiti aliona kwamba kuna haja ya kuchangia taaluma ya elimumitindo, kwa kuziweka taratibu hizo bayana.

Masuala ya dini na mamlaka ni ya muhimu sana kwa vile yanahusu maisha ya kila siku ya wanajamii, hasa katika jamii za Kiafrika. Riwaya tulizoziteua zinaangazia masuala ibuka mbalimbali ndani ya vipengele vya dini na mamlaka. Ni muhimu kuyachunguza masuala haya kwa sababu wanajamii wanaathiriwa pakubwa kwa njia mbalimbali na masuala haya.

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika utanzu wa riwaya ya Kiswahili. Tulichunguza kimtindo masuala ya dini na mamlaka katika riwaya teule za *Paradiso* ya John Habwe (2005), *Nguvu ya Sala* ya Wamitila (1999), *Asali Chungu* ya Said Ahmed Mohamed (1977), na

Kasri ya Mwinyi Fuad ya Shafi Adam Shafi (1977). Riwaya hizi zimeteuliwa kimaksudi kwa mujibu wa masuala tunayoyachunguza, yaani dini na mamlaka. Masuala haya yamechaguliwa kwa sababu yanagusa maisha ya kawaida ya wanajamii, hasa kiuchumi na kijamii.

Riwaya tulizoziteua zimeandikwa na waandishi Wakenya (*Paradiso* na *Nguvu ya Sala*) pamoja na Watanzania (*Asali Chungu* na *Kasri ya Mwinyi Fuad*). Kipindi cha uandishi wa riwaya hizi ni kuanzia mwaka 1977 hadi 2005.

Katika utafiti huu tulizichanganua riwaya tukiongozwa hasa na viwango vya kiisimu vifuatavyo:

(i) Kiwango cha kileksika

(ii) Kiwango cha kisintaksia

(iii) Kiwango cha kisemantiki (tamathali za usemi)

Viwango hivi vimependekezwa na Leech na Short (2007) katika orodha yao ya vipengele vya uchanganuzi wa kimtindo. Tulitumia orodha hiyo kufanyia uchunguzi huu kwa sababu orodha hiyo ni pana. Hata hivyo, tulikiacha nje kipengele cha mshikamano kwenye orodha hiyo kwa sababu ya mawanda ya utafiti huu. Tena tumeigeuza kidogo orodha ya Leech na Short kwa kuingiza nduni za kimtindo ambazo hazitajwi katika orodha hiyo, lakini ambazo zinabainika katika riwaya teule, mintarafu uchimuzi wa maudhui kuhusu dini na mamlaka.

Katika utafiti huu tulilenga mtindo wa riwaya kwa mujibu wa ubunifu wa kiisimu uliobainika katika kazi husika kuliko kuangalia usuli wa mwandishi. Ili kutekeleza hili, riwaya zilizoteuliwa ni zile zilizozingatia masuala husika.

Utafiti huu ulikuwa ni wa kidawati ambapo tulijikita katika kuzisoma kwa makini riwaya husika na kuyateua madondoo mahsusi ya data kutoka katika riwaya hizo, tukiongozwa na malengo ya utafiti huu, pamoja na Nadharia ya Uchimuzi. Mtandao ulitufaa sana katika mapitio ya maandishi.

Tuliitumia nadharia hii kama msingi wa kukusanyia madondoo ya data yenye nduni za kiisimu zilizochimuzwa mintarafu maudhui. Tulizingatia mihimili ya nadharia hii: ukiushi na usambamba.

Mkabala wa utafiti huu ni wa kitaamuli. Huu ni mkabala unaoegemea mbinu za kimaelezo wala sio mbinu za kitakwimu. Tulitumia mkabala wa kitaamuli kwa sababu data tuliyoikusanya haikuwa kwa njia ya takwimu. Tulitambulisha ruwaza za kimtindo ambazo zilibainika katika riwaya husika, kisha tukafasiri jinsi ruwaza hizo zilivyotumika katika kujenga maana na tena kutoa maudhui mbalimbali kuhusu dini na mamlaka.

1.7 Umuhimu wa Utafiti huu

Utafiti huu umebainisha jinsi mwandishi anavyochimuza ujumbe kwa kutumia mbinu za kileksika, kisintaksia na kisemantiki. Mbinu zilizojadiliwa zinawasaidia wasomaji, waandishi chipukizi, wahakiki, walimu wa fasihi, na wanafunzi katika kusimbua maana iliyomo katika matini za riwaya. Wanafunzi wanaweza wakaiga uandishi bora lakini pia wakajifunza mafunzo fulani kutokana na kazi ya kifasihi.

Uchanganuzi huu wa kimtindo wa matini za kifasihi utasaidia kuonyesha jinsi taaluma hii ya elimumitindo inavyosaidia katika kuzielewa kazi za kifasihi pamoja na jinsi ya kuzifafanua na kuzitathmini. Ingawa isimu si sehemu ya lazima katika uhakiki wa kifasihi, inaweza kumsaidia mchambuzi wa kazi husika ya kifasihi kuwa na uelewa bora

zaidi wa matini. Uchanganuzi wa kazi za kifasihi kwa misingi ya kiisimu unaweka njia mbadala ya kuzichunguza kazi hizo.

Mbinu ambazo zilitumika katika kuzichunguza kazi za utanzu wa riwaya zitaweza pia kutumika katika kuchunguza kazi za tanzu nyingine za fasihi kama vile tamthilia na ushairi, pale zinapofaa. Mbinu za kimtindo zinaweza pia kutumika katika kuchunguza na kuzielewa kazi zisizo za kifasihi.

Taaluma ya elimumitindo ni kipengele muhimu cha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha – hasa sarufi. Hii ni kwa sababu uchanganuzi wa kazi za kifasihi kiisimu hurejelea muundo wa lugha husika. Hivyo, utafiti huu utasaidia katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha.

Utafiti huu utachochea tafiti nyingine katika uwanja huu na pia utakuza mjadala wa kitaaluma. Utafiti wenyewe utakuwa ni rejeleo kwa wasomi wanaolenga kufanya utafiti husika.

1.8 Muhtasari wa Sura

Sura hii imebainisha misingi ya utafiti. Katika sura hii tumezungumzia usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, malengo na maswali yaliyoongoza utafiti huu. Halafu tumeeleza sababu za kuchagua mada ya utafiti wetu, tena tukaonyesha upeo wa utafiti na hatimaye kuangazia umuhimu wa utafiti huu. Maelezo haya yanaiwekea msingi sura inayofuata kwa kubainisha suala linalochunguzwa pamoja na malengo ya uchunguzi huo. Sura inayofuata ni ya mapitio ya maandishi ambayo pia inabainisha kiunzi cha nadharia. Vilevile tumebainisha pengo lililozibwa na utafiti huu.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.0 Utangulizi

Sura ya kwanza imeweka misingi ya utafiti ambapo usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti na umuhimu wa utafiti yamebainishwa. Katika sehemu hii tunahakiki maandishi kuhusu mada ya utafiti huu. Tunapitia maandishi kuhusu tafiti za kimtindo katika Kiswahili na kubainisha pengo katika tafiti hizo ambalo utafiti wetu umeshughulikia. Pengo hilo ndilo lililopelekea masuala yaliyochunguzwa katika utafiti wetu. Sehemu hii pia inabainisha kiunzi cha nadharia iliyoongoza utafiti huu. Kiunzi hiki kinaenda sambamba na orodha ya vipengele vya uchanganuzi wa kimtindo ya Leech na Short (2007).

2.1 Tafiti Tangulizi za Kimtindo katika Kiswahili

Kuna mikabala mbalimbali ya kuzichunguza kazi za fasihi. Elimumitindo ni mkabala mmojawapo wa mikabala hiyo. Zipo tafiti za kimtindo za kiuzamilifu ambazo zimefanywa zikiangazia tanzu mahsusi za fasihi, pamoja na masuala mbalimbali.

Katika uchunguzi wa kimtindo wa kazi za fasihi ya Kiswahili, Kitsao (1975) anazichanganua na kuzilinganisha kazi anuwai za kinathari mkiwemo barua, madondoo kutoka katika magazeti ya Kiswahili, hadithi fupi, riwaya pamoja na tamthilia. Anakiri kwamba uchunguzi wake wa kazi za kinathari ni wa kiutangulizi kwa vile uchunguzi wa awali ulizingatia zaidi kazi za kishairi. Anasema kwamba uchunguzi alioufanya unaweza kuangaliwa kama “uchunguzi wa kisasa – uchunguzi ambao unahusisha kazi anuwai, mkiwemo hata matini za kinathari za Kiswahili.”

Kitsao anaeleza kwamba kwa vile hakukuwa na kiunzi cha uchanganuzi wa kimtindo wakati alipofanya uchunguzi wake, aliamua kutumia kile cha Crystal na Davy (1969) kilichokusudiwa hasa kuchanganua Kiingereza cha kimaongezi. Anasema kwamba ilibidi akifanyie mageuzi kiunzi hicho ili kimwezeshe kuzichanganua kazi za kinathari za Kiswahili. Anataja vipengele vya lugha vinavyochunguzwa kwa kutumia kiunzi hicho: fonetiki/grafetiki, fonolojia/grafolojia, semantiki, sarufi na msamiati. Kati ya vipengele hivi, Kitsao anateua vipengele vitatu: semantiki, sarufi na msamiati, na uchunguzi wake umezingatia utaratibu huo, yaani anaanza na uchambuzi wa kisemantiki, kuelekea uchambuzi wa kimsamiati. Kwa mujibu wa Kitsao, ngazi hizo za kisemantiki, kisintaksia na kimsamiati zinahusisha zile nduni za kiisimu ambazo zinavuta nadhari katika kazi za kinathari, na hizi ndizo zinaonyesha kile ambacho elimumitindo inachunguza.

Uchunguzi huu wa Kitaso (1975) unaufaa sana uchunguzi wa kimtindo wa kazi za Kiswahili, hasa uchunguzi wetu ambao unaangazia riwaya. Ngazi za uchunguzi wa kimtindo za kisemantiki, kisintaksia na kimsamiati zinamwezesha mtafiti kufanya uchunguzi mpana wa kimtindo kwa njia ya ukusanyaji wa data pamoja na uchanganuzi wa kimtindo wenyewe. Hii ni kwa sababu ngazi hizi zinagusia vipengele muhimu vya muundo wa lugha ambavyo vinabainika katika kazi za kimaandishi. Kwa jumla, utafiti wetu umezingatia ngazi tatu za uchanganuzi alizozizingatia Kitsao isipokuwa baadhi ya vipengele vidogovidogo ndani ya ngazi hizo. Hii ni kwa sababu ya mapungufu mbalimbali yanayobainika katika kiunzi alichokitumia, pamoja na ufafanuzi wake kuhusu kazi za kinathari alizozichanganua.

Mojawapo ya mapungufu katika kazi ya Kitsao (1975) ni katika uchunguzi wa ngazi ya kisemantiki ambao hauko bayana. Anachanganya vipengele mbalimbali vya matumizi

ya lugha bila kuvihusisha na kipengele cha maana katika kazi husika. Kwa mfano, ingawa ni vizuri anarejelea baadhi ya tamathali za usemi kama vile sitiari, tashbihi, na ishara, anazungumzia vipengele vingine vya lugha bila kuvihusisha na kipengele cha maana. Kwa mfano, katika uchunguzi wake anahusisha uakifishi, usemi halisi na usemi wa taarifa, pamoja na kauli za kimazungumzo. Hii inaufanya uchunguzi wake kukosa muwala katika baadhi ya sehemu.

Kuhusu ngazi ya kisintaksia, Kitsao (1975) anatoa kauli ambazo zingehitaji ushahidi wa kitakwimu. Kwa mfano, anaposema kwamba kazi fulani inatumia sentensi ndefu au sentensi fupi, si wazi anatumia kigezo kipi kuziainisha sentensi kama fupi au ndefu. Hii ni tofauti na Michira (1993) ambaye anatoa idadi ya maneno yanayojenga urefu wa sentensi. Anasema kwamba kwa mujibu wa kazi aliyoifanya, sentensi fupi ina maneno yasiyopita sita; sentensi ya wastani ina maneno yasiyopita kumi na matano; na anaichukulia sentensi ndefu kuwa na maneno zaidi ya kumi na matano. Hata hivyo, Michira haelezi chanzo cha idadi hizi. Pia, Kitsao anapotofautisha matini mbili kwa kusema kwamba moja inatumia sentensi kamili na nyingine inatumia sentensi zisizo kamili, habainishi idadi ya sentensi zilizo kamili na zile zisizo kamili. Hii inakifanya kigezo cha kutumia takwimu bila kuzingatia kaida maalum kiwe na mushkili.

Vipengele vya kimsamiati anavyovirejelea Kitsao ni vichache mno. Kipengele cha kimsamiati ndicho hakifafanuliwa kwa kina katika kazi yake. Katika ngazi ya kimsamiati anachunguza msamiati wa kimazungumzo, msamiati rasmi, msamiati wa Kiswahili, msamiati mkopo. Pia, anachunguza kuchanganya msimbo na kubadilisha msimbo pamoja na simo. Uainishaji huu wa msamiati unaufaa uchunguzi wa kimtindo. Hata hivyo, Kitsao hakuuhusisha na mtindo wala kufafanua kwa kina uamilifu wa aina

hizo za msamiati. Anaishia kutaja tu aina hizo za msamiati na kutoa mifano kutoka kazi husika bila kuzihusisha na mtindo.

Katika tasnifu yake ya uzamifu, Kitsao (1982) anatumia mkabala wa kitakwimu kuzifafanua kazi anuwai za tanzu tatu za fasihi yaani ushairi, riwaya na tamthilia. Tofauti na utafiti wa Kitsao, utafiti wetu unalenga kazi za riwaya peke yake. Kwa hivyo, tulizingatia uchambuzi wa Kitsao kuhusu kazi za riwaya za Kiswahili katika tasnifu yake. Kitsao anazichambua riwaya sita za Kiswahili: *Utubora Mkulima* ya Shaaban Robert (1968), *Mzimu wa Watu wa Kale* ya Mohamed Said Abdulla (1960), *Nyota ya Rehema* ya Mohamed Said Mohamed (1976), *Kichwamaji* ya Kezilahabi (1974), *Ukiwa* ya Katama Mkangi (1975), na *Simu ya Kufa* ya Faraji Katalambulla (1965). Kuhusu uchambuzi wa kitakwimu wa riwaya hizo, Kitsao amezingatia vipengele vya aina za usemi (usemi halisi na usemi wa taarifa), urefu wa sentesni, uchangamani wa sentensi, idadi ya vishazi katika sentensi, kategoria za maneno, idadi ya silabi katika kila neno, na matumizi ya viakifishi.

Uchanganuzi alioufanya Kitsao (1982) ulilenga mdafao wa nduni za kiisimu kama msingi wa kuzitofautisha matini teule. Uwasilishaji wake wa data za kitakwimu umefanywa kwa kutumia grafu na pai chati. Akitumia mbinu hizo za kitakwimu, Kitsao anafanikiwa katika kuzibainisha sifa maalum za kila matini kutoka kila riwaya ambazo (sifa) zinaashiria mtindo wa kila mwandishi. Uchunguzi huu unatoa umaizi anuwai kuhusu riwaya, mintarafu mtindo. Unaonyesha jinsi takwimu zinavyoweza kuchangia katika uchanganuzi wa kazi za fasihi za Kiswahili. Kitsao alifanya kazi yake kabla enzi ya mahesabu ya kompyuta ambayo inawezesha uchunguzi wa kikopasi. Kwa hivyo, anafaa kupongezwa kwa jitihada hiyo. Lakini, ingawa uchunguzi huu ni wa muhimu kuhusu suala la mtindo katika riwaya za Kiswahili, unazingatia zaidi takwimu na

umuhimu wa mdafao wa nduni za kimtindo kuliko suala la maudhui. Mara nyingi waandishi wa riwaya huwa wanaandika kazi za kifasihi wakilenga zaidi kuwasilisha ujumbe fulani kwa msomaji au hadhira kuliko kudhihirisha tu matumizi yao ya lugha. Kwa mujibu wa kauli hii, utafiti wetu unatofautiana na utafiti wa Kitsao kwa vile utafiti wetu unazingatia mwambatano kati ya matumizi ya lugha na maudhui yanayotolewa na mwandishi katika kazi yake kupitia kwa ubunifu wake wa lugha.

Ingawa uchunguzi wa kitakwimu wa Kitsao unatupatia maarifa fulani kuhusu matumizi ya lugha katika riwaya husika, na unatufunza mengi kuhusu vipengele mbalimbali vya lugha vilivyochunguzwa, usampulishaji wake wa madondoo anayoyazingatia kufanyia uchanganuzi na kutoa mahitimisho kuhusu sifa za kimtindo za riwaya teule unazua wasiwasi fulani kuhusu mahitimisho hayo. Kitsao anakiri kwamba sampuli anazozitumia huenda zisitoe picha ya jumla kuhusu riwaya nzima. Kwa mfano, kuhusu urefu wa sentensi, anazingatia madondoo ya sentensi mia tano (500) za kwanza katika kila riwaya. Hatuelezwi hii ni asilimia gani ya jumla ya sentensi katika riwaya. Pia, hatuelezwi jinsi sampuli au vipimo vingine kama vile kategoria za maneno, idadi ya silabi na idadi ya viakifishi ilivyoteuliwa. Si dhahiri ikiwa sampuli anazozitoa Kitsao ni sampuli wakilishi za wango katika riwaya nzima.

Mkabala wa kitakwimu, ambao unahitaji kaida. Maandishi hayaonyeshi kaida za Kiswahili kama vile kaida ya urefu au ufupi wa sentensi au idadi ya silabi katika maneno marefu au maneno mafupi. Kitsao anatoa kauli kwamba vitenzi vya Kiswahili huwa ni virefu kuliko nomino zake (yaani huwa na silabi nyingi zaidi), kitu ambacho ni dhahiri kwa vile ni wazi kwamba kitenzi cha Kiswahili husheheni mofimu kadhaa, na wakati mwingine huweza hata kusimama kama sentensi, pale ambapo kiima hakijitokezi katika muundo wa nje. Kwa hivyo, kauli kwamba vitenzi vya Kiswahili ni virefu kuliko

nomino haitoi taarifa mpya au yenye umaizi, ila ni taarifa ambayo tayari inajulikana. Utafiti wetu ulitumia mkabala wa kimaelezo ili kuepukana na changamoto ya ukosefu wa kaida za kitakwimu katika Kiswahili. Mkabala wa kimaelezo unafaa utafiti huu kwa vile unalenga kufafanua uchimuzi alioutumia mwandishi katika kuibua maudhui.

Kazungu (1983) anachunguza ukiushi na uchimuzi katika matini teule za fasihi ya Kiswahili. Anateua kazi mojamoja ya kifasihi kutoka katika kila utanzu – riwaya, tamthilia na ushairi. Kazungu amefanya kazi nzuri ya kuziangazia kazi hizo teule kimtindo kwa kuchunguza mtindo wake kileksika, kisintaksia na kisemantiki. Hata hivyo, hakuchanganua vipengele vya kimtindo kwa kina, labda kwa sababu ya upeo na mipaka ya kazi yake. Kuhusu riwaya ya *Asali Chungu* ya Said Ahmed Mohamed (1978), Kazungu ametumia sampuli ya tungo chache chache kutoka katika riwaya nzima.

Michira (1993) anachanganua mitindo ya lugha ya wachuuzi katika soko la Gikomba na lugha ya matangazo ya kibiashara redioni. Kazi yake ni ya uzamili. Naye pia anachunguza vipengele vya kileksika, kisarufi na kisemantiki vya matini. Hata hivyo, tofauti na uchunguzi wetu, uchunguzi alioufanya Michira hauhusu matini za kifasihi. Kazi hii ya Michira ni mchango mkubwa katika uchunguzi wa kimtindo wa matini za Kiswahili. Ni nguzo muhimu kwa watafiti wa kazi za kimtindo. Michira anatambulisha sentensi fupi na sentensi ndefu na anatoa idadi ya maneno ya kila aina hizo za sentensi. Tena anaeleza athari ya kimtindo ya aina hizo za sentensi. Kileksika, anachunguza vipengele kama vile msamiati mkopo, msamiati mwepesi, na michuuko. Ingawa vipengele vya kimaana (kisemantiki na kipragmatiki) havikujitokeza bayana katika kazi yake, anazingatia tamathali za usemi pamoja na viziada lugha kama vile nyimbo, kucheza, mavazi na ishara za kuchekesha. Sawa na kazi ya Kitsao (1975), baadhi ya

kauli anazozitoa Michira kuhusu vipengele mahsusi zingehitaji ushahidi wa kitakwimu. Tofauti na utafiti wa Michira, utafiti wetu unazingatia nduni za kiisimu zilizochimuzwa, sio tu vipengele mbalimbali vya kiisimu kwa jumla.

Onchangu (2013) anachanganua mtindo katika riwaya na hadithi fupi za Clara Momanyi. Kazi yake ni ya uzamili, na ni mchango katika uchanganuzi wa kimtindo wa kazi za kifasihi za Kiswahili. Anatoa mifano ya tungo ambazo anadai kwamba zimekiushwa lakini haonyeshi jinsi ukiushi huo unavyojidhihirisha. Baadhi ya mifano anayoitoa ni tungo za kawaida tu. Ni tungo ambazo hazikuchimuzwa kwa njia yoyote. Katika maelezo yake kuhusu sentensi ndefu na fupi, haonyeshi kigezo alichokitumia kuamua ipi ni sentensi ndefu au ipi ni fupi. Tunaona kwamba baadhi ya vipengele vya kimtindo alivyovitumia angeviacha tu kama havikujidhihirisha katika kazi za kifasihi anazozichanganua.

Silavwe (2016) amefanya utafiti kuhusu mtindo katika riwaya ya *Majaliwa* ya Edwin Semzaba. Silavwe amezingatia tamathali za usemi, matumizi ya nyimbo, hadithi, na matumizi ya uhalisia mazingaombwe. Huo ndio upeo wa utafiti wake. Hivyo, utafiti wake haukuzingatia vipengele vya isimu, hasa vya kileksika na vya kisintaksia, ambavyo ni vya muhimu sana katika uchunguzi wa kimtindo.

Wasike (2020) katika tasnifu yake uzamifu anachunguza mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika kazi za kifasihi, akizingatia kielelezo cha tanzu teule za fasihi andishi mkiwemo riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Uchunguzi alioufanya Wasike ulizingatia tamathali za usemi. Kwa hivyo, hii ni kazi inayotoa mwanga kuhusu kipengele hiki cha matumizi ya lugha (tamathali za usemi). Lakini suala la mtindo halijitokezi bayana katika kazi yake. Pamoja na kipengele cha tamathali za usemi, utafiti

wetu ulichunguza pia vipengele vya kileksika na kisintaksia, kwa kutumia Nadharia ya Uchimuzi.

Naye Rayya (2002) alifanya uchunguzi wa kimtindo kuhusu nyimbo za harusi za Mombasa. Utafiti wake vilevile ni wa kiwango cha uzamifu. Rayya ameangazia vipengele kadhaa vya kiisimu vya kifonolojia, kileksika, kisintaksia, kisemantiki pamoja na viziada-lugha. Tofauti na uchunguzi wa Rayya, uchunguzi wetu unashughulikia utanzu wa riwaya. Pia, badala ya kuchunguza kiwango cha kisemantiki kwa jumla, tunateua kipengele cha tamathali za usemi, ambazo Rayya na Kazungu (1983) wanazichunguza ndani ya sura kuhusu semantiki. Kipengele cha semantiki ni kipana sana na kinaingiliana sana na vipengele vya kileksika na kisintaksia.

Naye Kimgung (2021) anachunguza mitindo ya uhalisia mazingaombwe katika riwaya teule za Kiswahili kama nyenzo za mivurugo katika jamii, yaani namna mitindo inavyowakilisha mivurugo na mitafaruku ya kijamii katika riwaya ya Kiswahili ya kimazingaombwe. Tasnifu yake haizingatii vipengele mahsusi vya kimtindo, ila imeangazia kipengele cha umazingaombwe kiujumla na jinsi kinavyowakilisha masuala anayoyaangazia.

Kwa jumla, kuna tafiti kadhaa ambazo zimefanywa kwa kuzingatia hasa ukiushi katika tamathali za usemi zilizotumiwa na mwandishi husika. Baadhi ya watafiti wamehusisha pia vigezo vingine kama vile kigezo cha kileksika, kigezo cha kisintaksia na kigezo cha kifonolojia. Hata hivyo, katika tafiti kadhaa, masuala ya dini na mamlaka hayajachunguzwa kimtindo. Aidha, tafiti hizo hazikutumia Nadharia ya Uchimuzi kama msingi wa uchanganuzi wa vipengele mahsusi vya kiisimu. Hii ndiyo nadharia inayoongoza utafiti wetu.

2.2 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uchimuzi. Tulitumia nadharia hiyo kulingana na mkabala wa uchunguzi wa kimtindo tunaoutumia, yaani ufafanuzi wa kiisimu wa nduni za kimtindo katika kazi husika za kifasihi, ukiambatana na fasiri ya nduni zilizotambuliwa.

Culpeper (2014) anasema kwamba Nadharia ya Uchimuzi ilianzishwa katika elimumitindo ya kifasihi ili kushughulikia masuala ya ufasiri wa kifasihi. Hii ni kwa sababu ni muhimu kueleza uamilifu wa nduni za kiisimu zilizochimuzwa.

Kwa mujibu wa Kipacha na Jilala (2021), "maendeleo katika taaluma ya uchanganuzi lugha kwenye karne ya ishirini yamesababisha elimumitindo kuja juu kama taaluma mojawapo yenye nadharia yake mahsusi ya mchomozo. Madhumuni ya nadharia hiyo ya elimumitindo ni kubaini vipengele vya lugha katika matini na kuibua umuhimu wake katika kuchanganua matini." Wanachomaanisha waandishi hawa ni kwamba Nadharia ya Uchimuzi (wao wanatumia istilahi 'mchomozo') inatumika katika kutambua vipengele vya lugha ambavyo vimechimuzwa na pia kujaribu kubaini jinsi vipengele hivyo vilivyochimuzwa vinavyohusika katika uwasilishaji wa ujumbe wa mwandishi. Jilala na Kipacha wanasema kuwa swali analotakiwa kulijibu mchambuzi ni hili: Ni nini dhamira ya mwandishi au msimuliaji kuchomoza vipengele husika vya lugha.

2.2.1 Nadharia ya Uchimuzi

Nadharia ya Uchimuzi iliasisiwa na wanaisimu wa Tapo la Prague katika karne ya ishirini. Nadharia hii ililenga kuweka uhusiano kati ya viwango vya maumbo ya lugha na maana za matini, jambo ambalo lilimwezesha msomaji kusimbua ujumbe wa mwandishi. Wanaisimu hawa walipinga mkabala wa wahakiki wa kifasihi unaozingatia zaidi mwandishi katika kuielewa fasihi. Wao walipendelea mkabala wa kuichunguza

lugha ya matini kulingana na athari za kisaikolojia za matumizi ya miundo husika ya lugha.

Neno “foregrounding” (uchimuzi) ni tafsiri ya neno “actualisace” ambalo lilitumiwa mara ya kwanza na mwanaisimu wa Czechoslovakia, Jan Mukarovsky. Kwa mujibu wa Peer na Hakemulder (2006), uchimuzi unarejelea mbinu za kiisimu, yaani ukiushi na usambamba, ambazo zinatumika katika matini za kifasihi kiuamilifu. Mbinu hizi zinaongeza uwezo wa matini wa kujenga maana na wakati huo huo zinaweza kumwathiri msomaji kiujumi. Kwa mujibu wa Leech (1969), ubunifu wa mtunzi inadhihirisha ukiushi wake wa ruwaza zilizokubalika, na kama kanuni ya kawaida, mtu yeyote anayekusudia kuchunguza umuhimu na thamani ya kazi ya kisanaa ni lazima azingatie zaidi kipengele cha mvuto na mshangao kuliko ruwaza ya moja kwa moja. Ukiushi wa kaida za kiisimu na kaida nyingine zilizokubalika umepewa jina ‘uchimuzi’.

Baldick (2008) anasema kwamba uchimuzi ni njia ya kukifanya kipengele fulani cha matini kijitokeze zaidi kuliko vipengele vingine vya matini. Kwa mujibu wa Kipacha na Jilala (2021), uchimuzi husababisha taharuki na ustaajabisho. Kadiri mwandishi anavyochomoza vipengele vya kiisimu katika uandishi wa kifasihi, ndivyo wasomaji wanavyoshtushwa na kuwa makini na suala linalochomozwa. Hii inawasaidia wasomaji kujaribu kujenga maana ya kile kinachowasilishwa na mwandishi au kupata ujumbe wa mwandishi.

Boyne (2009) anasisitiza kwamba miundo ya sentensi iliyokiuka kanuni za lugha au iliyochomoza inasaidia katika kuifanya dunia ya kubuni ijitokeze na hivyo kumsaidia msomaji kuijenga dunia hiyo pia. Mathalan miundo ya kisintaksia inayoonekana kama kwamba imevurugika katika riwaya inaweza kutumika kuakisi vurugu na uharibifu

katika dunia ya riwaya. Kulingana na Boyne, utawala kiufundi (unaofanywa na mwandishi) wa miundo ya kawaida ya sentensi za lugha unamshtua msomaji ili afikie fasiri inayokusudiwa na mwandishi na pia kusaidia katika kuakisi maudhui na mandhari ya riwaya.

Arnold (kama anavyorejelewa na Menialo, 2020) anaamini kwamba uchimuzi unasisitiza vivuli vya maana, na kwa kumfanya msomaji azingatie sehemu fulani za matini, unamsaidia kuona uhusiano kati ya mawazo na umuhimu wa picha mahsusi pamoja na matukio ili aweze kufasiri matini nzima.

Ufasiri unaozingatia vipengele vya ukiushi na usambamba unaweza kufanywa katika viwango vyote vya lugha – fonolojia, grafolojia, mofolojia, leksika, sintaksia, semantiki na pragmatiki.

Kwa hiyo, uchimuzi ni njia ya kujengea maana na toni ya mwandishi wala siyo kitu ambacho kimeongezewa tu katika lugha ya kazi ya kifasihi kama pambo, ingawa suala la ujumi pia ni muhimu katika fasihi. Uchimuzi ni aina ya ujumi unaosheheni ujumbe wa mwandishi.

Nadharia ya Uchimuzi ilimsaidia mtafiti kukusanya data kwa kuzingatia vifungu vya matini vyenye nduni za lugha zilizochimuzwa. Inamsaidia pia kuchanganua data hiyo kwa kuzingatia ruwaza na mahusiano katika nduni za lugha zilizochimuzwa. Nadharia hii ilikidhi malengo ya utafiti huu kwa vile inabainisha uchimuzi katika viwango vya uchanganuzi wa lugha – kileksika, kisintaksia na kisemantiki. Viwango hivi ndivyo vinavyoshughulikiwa katika malengo ya utafiti huu.

2.2.1.1 Asili ya Nadharia ya Uchimuzi

Van Peer na Hakemulder (2006) wanaeleza kwamba ingawa Nadharia ya Uchimuzi iliasisiwa na wanaisimu wa Tapo la Prague, wao sio walioigundua dhana ya uchimuzi. Uchimuzi ulitokana na maendeleo ya kihistoria ya mawazo ambayo yalianzishwa na wanamuundo wa Urusi, hasa wale ambao walikuwa na uhusiano na mbinu ya uajinabishaji ambayo ilipendekezwa na Viktor Shklovsky. Kulingana na Shklovsky, madhumuni ya sanaa ni kuvifanya vitu visiwe vyenye kujulikana ili viweze kutazamwa upya. Kwa mujibu wa Shklovsky na wanamuundo wenzake, mbinu zinazotumiwa na waandishi hazitumiwi kwa lengo la kuifanya kazi ya kifasihi ipendeze tu bali mbinu hizo zina uamilifu mahsusi. Hivyo, dhana ya uchimuzi ni ya kinadharia pia, ambayo baadaye ilipelekwa katika nchi za kimagharibi na wasomi kama Roman Jakobson, Felix Vodicka, na Rene Wellek.

Nao Jeffries na McIntyre (2010) wanaeleza kwamba uchimuzi ndiyo njia ya utendekaji wa uajinabishaji. Uajinabishaji ndio utaratibu uliochukuliwa kuwa sifa moja kuu ya lugha ya kifasihi. Uajinabishaji unaelezwa kuwa ni njia ya kuzuia usomaji haraka wa matini kwa kuionyesha dunia katika njia nyingine isiyo ya kawaida. Waandishi hawa wanasema kwamba kumekuwa na mjadala mkali kuhusu sifa zinazoibainisha lugha ya kifasihi. Ilichukuliwa kwamba uchimuzi ndio ulioitambulisha lugha ya kifasihi. Lakini iligunduliwa kwamba uchimuzi haupatikani katika kazi za kifasihi peke yake ila unapatikana katika kazi au maandishi ambayo si ya kifasihi. Hata hivyo, uchimuzi unapatikana zaidi katika matini za kifasihi, hasa ushairi. Uchimuzi huenda bado ndiyo nguzo kuu ya uchanganuzi wa kimtindo (Leech, 1970, akirejelewa na Jeffries na McIntyre, 2010)

Nadharia ya Uchimuzi iliboreshwa na wanaelimumitindo wa Kiingereza, hasa Geoffrey Leech (1969). Hata hivyo, asili ya nadharia hii ni kazi ya Aristotle, mwanasalsafa wa Kiyunani. Aristotle alisisitiza ukweli kwamba matini ya kifasihi inaundwa kutokana na kanuni maalum, na hivyo, katika mchakato huu, mbinu za ukiushi na usambamba zinakuwa na dhima muhimu.

Nadharia hii imetumiwa na waandishi wa riwaya teule kama nyenzo ya kuwasilishia maudhui ya dini na maamlaka. Inasaidia kumwelekeza msomaji kuzingatia zaidi nduni za lugha ambazo zimechimuza maudhui hayo..

2.2.1.2 Mihimili ya Nadharia ya Uchimuzi

Mihimili ya Nadharia ya Uchimuzi ni ifuatayo:

(i) Ukiushi

(ii) Usambamba

Kwa jumla, ukiushi unaashiria kuchepuka kwa kaida za lugha wakati ambapo usambamba unaashiria kwenda sambamba na kaida za lugha lakini kwa njia ambayo miundo iliyotumika imechomozwa. Hizi ndizo kanuni kuu mbili zinazotumiwa kuunda ruwaza za miundo ya lugha kwa njia ambayo miundo hiyo inachimuzwa kisaikolojia akilini mwa wasomaji, yaani zinakuwa na athari kwa utambuzi wa msomaji.

2.2.1.2.1 Ukiushi

Ukiushi unarejelea uvunjaji kimaksudi wa kanuni za matumizi ya lugha na matarajio ya msomaji, yaani ni upotoshaji wa kimaksudi wa kaida za lugha katika viwango mbalimbali vya lugha kama vile msamiati, sarufi, maumbo sauti, grafolojia, na kadhalika.

Jeffries na McIntyre (2010) wanaeleza kwamba ukiushi ni sifa ya kawaida hasa ya mtindo wa kishairi, ingawa unapatikana sana pia katika tanzu na aina nyingine za matini. Pia, wanasema kuwa dhana inayosema kwamba ushairi huvunja kanuni si jipya.

Sehemu za lugha zilizokiuka kanuni za lugha hutambulika zaidi na huwa na umuhimu fulani katika matini. Humpa msomaji fununu ya maana iliyokusudiwa na mtunzi. Humfanya msomaji ajaribu kutambua umuhimu wa sehemu hizo, yaani kujaribu kufasiri maana ya miundo ya lugha inayochimuzwa kwa njia ya ukiushi. Nduni ya kiisimu au ya kifasihi inatambulika zaidi kwa mujibu wa kaida fulani. Kaida ya kiisimu ni mazoea katika kusema au kuandika. Kwa kutumia kielelezo cha picha, nduni zilizochimuzwa zinakuwa katika sehemu ya mbele (zimejitokeza zaidi) wakati ambapo nduni ambazo hazikuchimuzwa zinakuwa katika sehemu ya nyuma (Kipacha na Jilala, 2021).

Kwa kuifanya lugha isiwe ya kawaida, msomaji hukawiza usomaji ili msomaji aweze kujishughulisha na matini akijaribu kuielewa. Kwa njia hiyo, ujumbe utaweza kumfikia msomaji. Kwa mujibu wa Awonuga na wenzake (2018), uchanganuzi wa matini za kifasihi kimtindo haufai kuharakishwa ikiwa lengo la matini hiyo ni kupata athari tarajiwa kwa msomaji. Anasema pia kwamba madhumuni ya sanaa ni kuifanya lugha isiwe ya kawaida, na kwa njia hiyo kumfanya msomaji atumie juhudi zaidi za kiakili ili kujaribu kuelewa kusudi la kimawasiliano la mwandishi.

Ukiushi ni sifa mojawapo kuu ya kazi za kifasihi, kwa vile ni njia mojawapo ya kuitofautisha lugha ya kifasihi na lugha isiyo ya kifasihi. Hata hivyo, utafiti umeonyesha kwamba ni vigumu kutofautisha lugha ya kawaida na lugha ya kifasihi. Hii ni kwa sababu maandishi kama vile matangazo au hotuba yanaweza kuhusisha

ukiushi. Hata hivyo, inaaminika kwamba kazi za kifasihi huonyesha sifa hii zaidi kuliko maandishi mengine. Ni njia mojawapo ya mwandishi kutumia lugha kiubunifu.

Leech na Short (2007) wanatofautisha kati ya viwango vitatu vya ukiushi. Kiwango cha kwanza ni ukiushi wa msingi ambapo matini hukiuka kaida za lugha kwa jumla. Kiwango cha pili ni ukiushi usio wa msingi ambapo matini hukiuka kaida za muundo wa kifasihi hasa. Kiwango cha tatu ni ukiushi unaovunja kaida zilizomo ndani ya matini. Kwa mujibu wa Jeffries na MacIntyre (2010), mbinu za kisintaksia zinazotumika katika mtindo wa kifasihi ni mifano ya uchimuzi kwa njia ya ukiushi wa kaida zilizomo ndani ya lugha. Katika utafiti huu tunazingatia ukiushi wa kiwango cha kwanza – yaani ukiushi wa kimsingi ambapo matini hukiuka kaida za lugha kwa ujumla. Tunazingatia aina hii ya ukiushi kwa sababu kiwango hiki ni kipana zaidi kuliko viwango vingine vilivyotajwa.

Ukiushi unaweza kubainishwa kimaelezo au kitakwimu kwa kuzingatia idadi ya vitenzi, viunganishi, viwakilishi au idadi ya vijenzi vinginevyo katika kazi nzima (Kipacha na Jilala, 2021). Hata hivyo, Kipacha na Jilala hawaelezei ukiushi unaobainishwa kimaelezo. Utafiti huu unalijaza pengo hili kwa kuonyesha kwamba ukiushi unaweza kubainishwa kimaelezo kwa kurejelea na kufafanua mbinu za kiisimu zinazodhihirisha ukiushi, yaani kwa kueleza jinsi zinavyojitokeza, pamoja na umuhimu wa matumizi yake.

2.2.1.2.2 Usambamba

Usambamba, kwa upande mwingine unahusisha miundo ambayo imejirudia na ambayo inaweza kulinganuliwa na miundo isiyo sambamba. Kwa mujibu wa Mbatiah (2001) usambamba ni mbinu ya utunzi inayotumia ulinganifu wa kimuundo wa sehemu mbili za usemi ambazo zina ukinzani kimaana. Anasema kwamba usambamba unaweza

kutumiwa katika sentensi moja na pia miongoni mwa sentensi kadhaa. Mbinu ya usambamba inaurutubisha usemi kimaana na kuupa msisitizo. Naye Wamitila (2003) anaeleza kwamba usambamba ni mbinu inayotumiwa katika kazi za kifasihi ambapo msanii anayarudia maneno fulani au maana fulani kwa muundo mwingine tofauti. Pia anasema kwamba urudiaji huu unaweza kuwa katika viwango tofauti vya kisintaksia kama vile katika virai, vishazi, au sentensi.

Kwa mujibu wa Jeffries na McIntyre (2010) usambamba unaweza kujitokeza katika viwango tofauti vya muundo wa kiisimu – kisintaksia, kifonolojia na kisemantiki. Nao Kipacha na Jilala (2021) wanaeleza kuwa katika usambamba, kunajitokeza urari au uradidi katika miundo ya silabi, maneno, virai au sentensi. Wanasema kwamba mojawapo ya sehemu kuu ya usambamba ni takriri na kwamba matini za ushairi, matangazo na hotuba zaweza kuwa na vipengele vya usambamba.

Kuhusu namna ya kufasiri miundo sambamba, Leech (1969, kama alivyorejelewa na Jeffries na McIntyre, 2010) anaeleza kwamba matumizi ya usambamba yanahusisha uhusiano wa ulinganifu kati ya vifungu vilivyo sambamba. Katika kufasiri vifungu sambamba vinavyojitokeza, mchunguzi anazingatia uhusiano wa nje kati ya vifungu hivyo.

Gregoriou (2014) anaeleza kwamba vifungu katika matini vinaweza kuwa sambamba kisemantiki na pia kisintaksia. Anasema kuwa urudiaji wa maana unaweza kuelezwa kama usambamba wa kisemantiki, wakati ambapo urudiaji wa maneno yenyewe unajulikana kama usambamba wa kileksika. Kwa mujibu wa mwandishi huyu, miundo sambamba ina uwezo sio tu wa kuchimuza sehemu za matini lakini pia kutufanya tutafute maana sambamba au pia maana mlinganuo. Urudiaji wa miundo unawafanya wasomaji kujaribu kutafuta mahusiano ya kimaana kati ya jozi ya miundo sambamba.

2.2.1.3 Mshikamano wa Uchimuzi

Kulingana na Leech (2008) nduni ambazo zimechimuzwa huwa zinahusiana zenyewe kwa upande mmoja na pia huwa zinahusiana na matini nzima. Kwa mfano kunakuwa na mshikamano wa kileksika kati ya faridi za kileksika zilizorudiwarudiwa katika sehemu tofauti za matini na uteuzi wa faridi ambazo zina uhusiano wa kisemantiki. Uchimuzi wa nduni fulani za kiisimu unahusiana na maana ya matini kwa jumla, yaani kunakuwa na ulinganifu wa kisemantiki. Leech anasema kwamba tunaweza kupata ruwaza fulani ambayo imezagaa katika matini nzima. Huu pia unakuwa ni uchimuzi wa aina fulani ambao Leech anauita "uchimuzi ulioenea" (Tafsiri yetu), yaani "extended foregrounding". Mahusiano ya mshikamano yanasaidia katika kutoa fununu ambazo zinaweza kutumiwa katika fasiri. Kwa hiyo, anachotueleza Leech ni kwamba kunakuwa na mchakato wa kufasiri nduni moja moja ambao hatimaye unapelekea fasiri ya jumla, yaani fasiri inayotokana na mkusanyiko wa fasiri kadhaa ndogo ndogo.

Katika utafiti huu, dhana hii ya mshikamano wa uchimuzi ilikuwa ya muhimu kwa sababu ilitusaidia katika fasiri ya miundo kiushi na miundo sambamba ambayo inaonyesha ulinganifu wa kisemantiki katika matini tulizozichanganua.

2.3 Pengo la Utafiti

Ingawa tafiti za awali zimechambua kazi za riwaya za Kiswahili kimtindo hakuna utafiti uliangazia jinsi waandishi wanavyochimuza maudhui ya dini na mamlaka katika riwaya ya Kiswahili. Utafiti wetu unashughulikia pengo hilo. Ndani ya masuala haya, riwaya husika zinasawiri maudhui kama vile ufisadi, unyanyasaji wa kijinsia, ukosefu wa ajira, tamaa ya pesa na mali, na uhalifu mijini. Haya ni masuala ibuka katika jamii mbalimbali ambayo yanafaa kujadiliwa. Uchanganuzi wa kimtindo wa unaweza kubainisha jinsi maudhui haya yanavyochimuzwa na waandishi kileksika, kisarufi na kisemantiki.

2.4 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii tumepitia na kuhakiki maandishi kuhusu mada ya utafiti huu. Tumepitia baadhi ya tafiti za kimtindo katika Kiswahili na kubainisha pengo lililopo katika tafiti hizo, ambalo utafiti huu umeshughulikia. Sura hii pia imebainisha nadharia iliyoongoza utafiti huu pamoja na mihimili ya nadharia hiyo. Sura inayofuata inafafanua mbinu za utafiti tulizozitumia kutekelezea utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia sura hii tulipitia maandishi kuhusu mada ya utafiti huu na kubainisha pengo katika tafiti za awali ambalo utafiti huu unashughulikia. Pia, tulieleza nadharia iliyoongoza utafiti huu pamoja na mihimili ya nadharia hiyo. Katika sura hii tunafafanua mbinu zilizotumika katika utafiti huu, yaani eneo la utafiti, muundo wa utafiti, wango wa utafiti, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, vifaa vya utafiti, na jinsi data ilivyochanganuliwa.

3.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulikuwa ni wa mezani ambapo mtafiti alipitia vitabu, majarida, na makala mbalimbali kutoka kwenye mtandao kuhusu mada ya utafiti. Riwaya zifuatazo ndizo zilizokuwa vyanzo vya data ya utafiti huu: *Paradiso* ya John Habwe (2005), *Nguvu ya Sala* ya Kyallo Wadi Wamitila (1999), *Asali Chungu* ya Said Ahmed Mohamed (1977) na *Kasri ya Mwinyi Fuad* ya Shafi Adam Shafi (1978). Tulitumia mtandao ili kupata maandishi mbalimbali yanayohusu mada ya utafiti huu, pamoja na nadharia ambayo ilituongoza katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data.

3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia muundo wa usanifu kifani ambapo masuala mahsusi ya dini na mamlaka yalichunguzwa katika riwaya teule ili kubainisha mbinu za kiisimu wanazozitumia waandishi kujenga maana au kuwasilisha masuala mbalimbali. Utafiti huu uliozingatia usomaji wa maandishi ili kukusanya data.

Mtafiti alikusanya data kutoka katika riwaya teule kwa kulenga madondoo yenye nduni husika za kimtindo zilizochimuzwa, mintarafu masuala ya dini na mamlaka (sampuli

ya madondoo yaliyochanganuliwa imeambatishwa). Nduni hizo ziliandikwa kwa kuzichapa kwenye kompyuta. Kisha zilitolewa maelezo ya kiisimu ambayo baadaye yalihusianishwa na jinsi nduni hizo zilivyotumiwa na mwandishi kujenga maana au kutoa maudhui fulani.Tulizingatia viwango vya uchunguzi vya kileksika, kisintaksia na kisemantiki (tamathali za usemi).

Mkabala wa utafiti huu ni wa kitaamuli. Hii inamaanisha kwamba data iliyokusanywa na kuchanganuliwa haikuwa ya kitakwimu. Kilichosisitizwa ni maelezo. Mtafiti alipata taarifa ya kina kuhusu masuala ya dini na mamlaka, kisha akatambua ruwaza, mienendo na mahusiano katika tungo zilizochimuzwa kwa mujibu wa masuala hayo. Halafu, alitoa fasiri ya ruwaza, mienendo na mahusiano hayo, yaani uamilifu wake katika matini, mintarafu ujenzi wa maudhui ya dini na mamlaka katika riwaya mahsusi.

3.3 Wango wa Utafiti

Utafiti huu ulihusisha ukusanyaji na uchanganuzi wa data kutoka katika riwaya nne za Kiswahili zilizotajwa katika sehemu 3.1.

3.4 Sampuli na Usampulishaji

Katika sehemu hii tunabainisha sampuli ya riwaya teule pamoja na madondoo yaliyoteuliwa kutoka katika riwaya hizo mintarafu masuala ya dini na mamlaka na Nadharia ya Uchimuzi.

Utafiti huu ulilenga kuchunguza nduni za kimtindo zilizobainika katika data iliyokusanywa kutoka riwaya teule za Kiswahili. Tuliziteua riwaya nne za Kiswahili ambazo zimeangazia masuala hayo na zimetajwa katika sehemu 3.1.. Uteuzi huu ulifanywa kimaksudi, yaani tuliziteua riwaya kwa mujibu wa masuala ya dini na mamlaka ambayo tuliyachunguza kimtindo.

Kwa vile tulilenga kuchunguza masuala ya dini na mamlaka katika riwaya teule, na sio masuala mengine katika riwaya hizo, tuliisoma kila riwaya na kuteua madondoo kwa mujibu wa Nadharia ya Uchimuzi, yaani tungo zilizochimuzwa kileksika, kisintaksia na kisemantiki (kitamathali). Orodha ya kategoria za kiisimu na kimtindo ya Leech na Short (2007) ilitufaa katika kubainisha ngazi hizo za uchimuzi ambazo zinaenda sambamba na malengo ya utafiti wetu. Madondoo yaliyoteuliwa yameambatishwa.

3.5 Ukusanyaji wa Data

Data ilikusanywa kutoka katika riwaya zilizoteuliwa. Data hiyo ilikusanywa kwa kuzingatia vipengele vitatu katika Orodha ya Kategoria za Kiisimu na Kimtindo ya Leech na Short (2007) vifuatavyo:

i. Kategoria za kileksika
ii. Kategoria za kisarufi
iii. Tamathali za usemi

Vipengele hivi vinaakisi hali ya lugha kama mfumo wa msimbo wenye viwango vya kileksika, kisarufi na kimaana. Orodha hii ilitusaidia kukusanya data kwa utaratibu na kwa mapana. Hata hivyo, tulivifanyia mageuzi baadhi ya vipengele kwenye orodha hiyo ili vikidhi mahitaji ya utafiti wetu. Tulifanya hivyo kwa kuzingatia nduni za kiisimu ambazo hazikutajwa katika orodha hiyo lakini ambazo zilibainika katika riwaya teule. Leech na Short (2007) wanapendekeza kwamba orodha hiyo itumike kulingana na mahitaji ya utafiti husika, wala sio kama kanuni zisizobadilika.

Tulizingatia tungo ambazo zimechimuzwa kileksika, kisintaksia pamoja na kisemantiki (tamathali za usemi) katika riwaya teule. Tungo ambazo hazikuchimuzwa kwa mujibu wa ngazi hizo za kiisimu na tena zile ambazo hazikuhusu masuala ya dini na mamlaka hazikuzingatiwa.

3.5.1 Mbinu za Kukusanya Data

Data ambayo ilitumika katika uchunguzi huu ilikusanywa bila kutumia njia ya kielektroniki. Hii ni kwa sababu riwaya ambazo tulizichanganua hazipatikani katika umbo la kielekroniki. Kwa hiyo, katika utafiti huu mtafiti aliisoma kila riwaya kwa makini sana huku akiteua madondoo yaliyohusiana na kipengele cha kimtindo kilichochunguzwa kwa mujibu wa masuala ya dini na mamlaka. Kwa vile mtafiti alitoa madondoo yaliyohusiana na masuala mahususi ya dini na mamlaka peke yake, aliweza kupitia riwaya nzima akitafuta tungo mbalimbali ambazo zimechimuzwa kwa mujibu wa masuala hayo. Mtafiti aliziwekea rangi ya kusisitiza tungo zilizochimuzwa, kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu.

3.6 Vifaa vya Utafiti

Mtafiti alitumia kalamu za kusisitizia kuzibainisha tungo zilizochimuzwa katika riwaya husika. Tena, alitumia kalamu kuandika ufafanuzi kuhusu tungo zilizochimuzwa kando kando kwenye kurasa za maandishi ya riwaya kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu. Tungo ziliteuliwa kwa kuzingatia ujuzi wa kiisimu na wa kifasihi wa mtafiti. Kisha, mtafiti alitumia kompyuta kuyachapa yale madondoo yenye tungo zilizosisitizwa kwa kalamu ya kusisitizia.

3.7 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa riwaya ulifanywa mintarafu malengo ya utafiti ambayo yanawiana na orodha ya kategoria za kiisimu na kimtindo ya Leech na Short (2007), yaani tulichanganua kipengele cha kileksika kwanza, halafu tukachanganua kipengele cha kisintaksia, na hatimaye tukachanganua kipengele cha tamathali za usemi.

Data ya utafiti huu ilichanganuliwa kitaamuli. Tulitumia uchanganuzi wa kidhamira ambao ulihusisha kuzitambulisha ruwaza na mienendo mbalimbali katika madondoo ya

data, mintarafu vipengele vya kileksika, kisintaksia na kitamathali. Tulizifafanua kiisimu nduni zilizochimuzwa katika riwaya teule tukizingatia malengo ya utafiti huu. Kisha tulizifasiri nduni zilizotambuliwa kwa kuzingatia umuhimu na uamilifu wa uchimuzi wa nduni hizo katika kuibua masuala ya dini na mamlaka katika riwaya teule. Mchakato huu unaweza kuchukuliwa kama ni mwambatano wa kauli za kiisimu na zile za kiuamilifu (Leech, 2008). Fasiri ilifanywa kwa kutumia ujuzi na ubunifu wa mtafiti kulingana na ushahidi wa kiisimu uliobainika katika maelezo ya kiisimu. Katika fasiri tulihusisha mbinu kutoka taaluma za semantiki na pragmatiki. Kwa mfano, vipengele vya kisemantiki vya maana ya moja kwa moja na maana iliyodokezwa vilitumika katika kubainisha maana inayojengwa katika tungo husika ambayo (tungo) imechimuzwa. Pia, tulizingatia pendekezo la Leech (2008) la msomaji kuweza kufikia fasiri kwa kutumia udadisi, utambuzi, na ubunifu. Hii inafanywa kwa kuhusisha ujuzi wa kiisimu wa msomaji na ujuzi ulimwengu halisi. Ufahamu unaotokana na mpango wa ulimwengu halisi uliomo akilini mwa msomaji unamsaidia msomaji kujenga ulimwengu wa kubuniwa na kwa njia hiyo, msomaji huweza kuelewa kuelewa anachokisema mwandishi kwa mujibu wa ufahamu huo. Mahitimisho yalifanywa kuhusu ufafanuzi, umuhimu na uamilifu wa tungo husika mintarafu ya masuala mahsusi yaliyowasilishwa.

3.8 Maadili ya Kiutafiti

Katika utafiti huu, maadili ya kiutafiti yalizingatiwa mkiwemo yafuatayo:

Uchanganuzi wa data pamoja na fasiri ya ruwaza na mienendo iliyojitokeza katika data yalifanywa bila upendeleo wowote wa mtafiti. Mahitimisho ya utafiti yalitokana na uchanganuzi wa data kutoka riwaya teule, siyo yale aliyoyapendelea mtafiti.

Ili kuhakikisha uaminifu wa mahitimisho ya utafiti, mtafiti alizingatia kanuni ya utafiti wa kisayansi inayosema kwamba mbinu zilizotumika katika utafiti ziwe wazi ili ziweze kutumiwa upya na mtafiti mwingine kuthibitisha mahitimisho ya utafiti.

Madondoo kutoka kwenye riwaya teule ambayo yemetumiwa kama vyanzo vya data katika utafiti huu yalinakiliwa neno kwa neno ili kufaa matakwa ya mtafiti. Baada ya kuchapwa, mtafiti aliyahariri vizuri ili kuhakikisha kwamba ni sahihi kabisa na hakuna mabadiliko yoyote ambayo yamejitokeza. Hii ni kwa sababu mabadiliko kwenye vyanzo vya data yanaweza kuufanya utafiti kutokuwa wa kuaminika,

3.9 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii tumebainisha mbinu zilizotumika katika kukusanya na kuchanganua data na hivyo kutekeleza malengo na kuyajibu maswali ya utafiti huu. Tumebainisha eneo la utafiti, muundo wa utafiti, wango wa utafiti, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, vifaa vya utafiti na pia utaratibu wa kuichanganua data. Tena, tumeonyesha jinsi suala la etikeli lilivyozingatiwa katika utafiti huu. Sura hii inaweka msingi wa sura inayofuata ya uchanganuzi wa data kwa kuonyessha utaratibu wa kufikia malengo ya utafiti huu. Katika sura inayofuata tunawasilisha na kuichanganua data ya utafiti huu kwa mujibu wa malengo.

SURA YA NNE

UTEUZI WA KILEKSIKA KAMA NDUNI YA KIMTINDO KATIKA KUCHIMUZA MAUDHUI YA DINI NA MAMLAKA KATIKA RIWAYA TEULE

4.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, tumeeleza mbinu za utafiti tulizozitumia katika kutekeleza malengo ya utafiti huu. Sura hii inalenga kutimiza lengo la kwanza kwa kufafanua nduni za kileksika zilizotumiwa na waandishi wa riwaya teule ili kusawiri maudhui. Mbinu za kileksika tunazozichanganua ni pamoja na urudiaji, visawe, kinyume, utohozi, uhamishaji wa nomino kutoka ngeli moja hadi nyingine, msamiati wa kitathmini, na vitenzi vya kitambuzi. Tunazichunguza nduni za kileksika zilizochimuzwa kiisimu katika riwaya teule kwa ajili ya kutoa maudhui mbalimbali kuhusu dini na mamlaka.

4.1 Maelezo ya Riwaya Teule

Katika sehemu hii tunalenga kutoa taarifa ya jumla kuhusu riwaya teule, yaani kumtambulisha mwandishi wa kila riwaya, pamoja na kile ambacho anaangazia katika riwaya yake.

4.1.1 Riwaya ya *Paradiso* ya John Hamu Habwe (2005)

Paradiso ni riwaya inayodhihirisha kinaya ambapo viongozi wa kidini (wachungaji) pamoja na baadhi ya waumini wamejenga paradiso yao hapa duniani, ingawa lengo lao (kijuujuu) ni kwenda paradiso ya baadaye. Kweli kinzani ni kwamba paradiso waliyoijenga hapa duniani inawafanya washindwe kwenda paradiso ya baadaye. Paradiso ya duniani imejaa tabia hasi – hasa tamaa ya pesa – ambayo ni chimbuko la tabia nyingine hasi kama vile wivu, chuki, ufisadi, na hata ulanguzi wa madawa ya kulevya.

Kwa sababu ya tamaa ya pesa na mali, viongozi wa dini wanashindana. Ushindani huu unapelekea mfarakano kati yao, waumini wao, pamoja na makanisa menza. Hii ni kinyume kabisa na mafundisho ya Kikristo kuhusu kanisa la pamoja la Kristo. Ni kinaya kwamba viongozi hawa, ambao hata baadhi wanajipa cheo cha uaskofu hawafuati mfano uliowekwa na Kristo mwenyewe ambaye hakulenga kumiliki pesa na mali. Hili linadhihirisha kuwa kuna unafiki mwingi. Viongozi hao wanadai kwamba wanamfuata Kristo lakini vitendo vyao vinaonyesha kwamba hawamfuati, bali wanafuata maisha ya anasa ya hapa duniani; wanajenga paradiso yao hapa duniani.

Habwe anaandika kuhusu uhalisia unaodhihirika katika maisha ya jamii anayoiangazia. Anayasawiri maisha katika nchi ya Kenya. Mandhari yaliyoangaziwa ni jiji la Nairobi na mtaa duni wa Kibera, jiji la Mombasa, pamoja na sehemu ya mashambani ya Budalangi.

Mwandishi anaangazia nafasi ya dini katika maisha ya wanajamii. Raia wengi ni maskini na wanaliangalia kanisa kama asasi inayoweza kuwasuluhishia matatizo yao ya kila siku kama vile magonjwa na ufukara. Wengi wanajaa makanisani wakiwa na matumaini makubwa ya kuondolewa shida zao kupitia kwa sala na miujiza. Hata hivyo. viongozi wa dini wanatumia fursa hii (ya watu kukimbilia makanisani) kujitajirisha, kupitia kwa kukusanya zaka, fungu la kumi, na matoleo mengine.

Mwandishi amemtumia mhusika Michael kama mchungaji kielelezo au Mkristo mwema kwa jumla. Mwandishi amemtumia mhusika huyu kwa ajili ya kulinganua tabia zake na zile za wachungaji wanafiki. Wakati ambapo wachungaji wengine wana tamaa ya pesa na mali, Michael analenga kuiga mfano wa Yesu kwa kutokuwa na tamaa hiyo. Hakimbilii maisha ya utajiri wa nyumba, ardhi, magari, na wanawake. Hata hivyo, kama mwanadamu, Michael pia anateleza na kuingia katika dhambi kwa kufanya

vitendo visivyo vya kimaadili. Licha ya kuteleza, Michael anarekebisha mwenendo wake na kurudi kwenye njia nyoofu ya Kikristo. Hii inadhihirisha hali ya kawaida ya mabadiliko maishani ambapo mwema anaweza akabadilika akawa mui, na mui akawa mwema. Inaonyesha kwamba kila binadamu ana udhaifu fulani.

Motifu kuu ya riwaya hii ni nafasi ya dini katika maisha ya watu katika masuala ya kiuchumi na kisiasa.

4.1.2 Riwaya ya *Nguvu ya Sala* ya Kyallo Wadi Wamitila (2003)

Katika riwaya ya *Nguvu ya Sala*, Wamitila anaangazia "nguvu ya sala" au uwezo wa maombi kukabiliana na masuala ya msingi katika jamii kama vile ukosefu wa ajira, gharama ya maisha, mabadiliko katika jamii, pamoja na suala la jinsia ambalo ndilo amelisisitiza zaidi katika riwaya yake. Anachunguza nafasi ya mwanamke katika jamii na jinsi anavyokandamizwa. Katika riwaya hii, Wamitila anauliza swali kwa njia isiyo ya moja kwa moja: Je, nguvu ya sala au imani katika Mungu ina uwezo wa kukabiliana na changamoto za maisha zinazowakabili wanajamii?

Riwaya hii imesimuliwa katika nafsi mbili: nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu. Usimulizi wa nafsi ya kwanza unamhusu mhusika Susan Ngunze, bintiye Richard Ngunze. Kupitia kwa mhusika huyu, mtunzi anawasilisha maudhui kwamba sala peke yake haiwezi kusuluhisha mengi ya matatizo yanayowakumba wanajamii. Yeye anaona kwamba mfumo wa jamii lazima ubadilike. Usimulizi wa nafsi ya tatu unamhusisha mhusika mkuu Richard – baba yake Susan Ngunze. Tofauti na binti yake Susan, Richard ni mhusika mwenye imani kwamba sala ndiyo njia pekee inayofaa kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazomkabili mwanajamii. Richard ni mmenyu. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), mmenyu ni "mtu ambaye ana mapendeleo makubwa ya umenyu au usafi na usahihi katika matumizi fulani katika mtindo." Richard ana msimamo mkali

kuhusu dini na kwa hivyo ni mkali sana kwa mke na watoto wake katika kuhakikisha kwamba msimamo wake unatekelezwa. Ana ubinafsi mwingi kwa kujifikiria mwenyewe kama Mkristo mwenye familia ambayo ni kielelezo cha maisha ya kikristo.

Usimulizi huu wa nafsi mbili unalenga kuonyesha uhusiano kati ya mienendo ya wahusika wawili inayohitilafiana. Usimulizi wa nafsi ya kwanza wa Susan unamfanya msomaji kumhurumia Susan kuliko baba yake ambaye anawasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu. Kwa vile katika riwaya hii Susan anawakilisha jinsia ya kike, anatudhihirishia jinsi mwanamke anavyonyanyaswa katika jamii na kumhukumu mwanamume anayemnyanyasa. Richard ndiye anayewakilisha jinsia ya kiume. Msingi wa msimamo wetu ni kwamba ingawa anwani ya riwaya hii ni *Nguvu ya Sala*, suala la jinsia ndilo limepewa kipaumbele na mwandishi katika riwaya hii. Mwanamke amesawiriwa kama mtu anayekandamizwa katika jamii, na ukandamizaji huu unafanyika katika mazingira ya dini. Lakini kizazi cha Susan kinawakilisha mabadiliko katika jamii yanayokuja ambapo mwanamke atapata uhuru.

4.1.3 Riwaya ya *Asali Chungu* ya Said Ahmed Mohamed (1978)

Asali Chungu ni riwaya ya kwanza ya mwandishi Said Ahmed Mohamed. Riwaya hii inayamulika maisha katika jamii ambayo haitajwi, ila tunaweza kukisia jamii hiyo tukizingatia usuli wa mwandishi. Mwandishi huyo alizaliwa katika kisiwa cha Unguja na anaelezea sherehe muhimu ya kisiwa hiki ya kukoga mwaka. Hivyo, inaaminika kwamba mwandishi anayamulika maisha katika kipindi baada ya ukoloni. Ukoloni umezalisha hali ya matabaka ambapo kuna tabaka la wenye nacho wakiwakilishwa na wahusika kama Zuberi, mke wake Amina, na Wahindi. Kwa upande mwingine, kuna tabaka la wasio nacho likiwakilishwa na wahusika kama Dude, Semeni, Bi Pili, Mzee Shabaan Supu, na wengineo. Makabaila wanawanyanyasa na kuwanyonya wasio nacho.

Mhusika Zuberi, kwa mfano, anafaidika kutokana na nafasi yake katika serikali kama Mkuu wa Walaya. Anafanya kila anachotaka bila kuhofia adhabu yoyote. Kwa mfano, anambaka msichana mdogo Semeni, mtumishi wake wa nyumbani. Ng'ombe wake wanaiharibu mimea ya wanawake jirani bila yeye kujali. Tena anatumia umiliki wake wa ardhi kuwanyanyasa mafukara kama Mzee Omari, ambaye hana ardhi yoyote na ni lazima aitegemee ile ya Zuberi ili kulisha familia yake.

Wananchi ni wanyonge. Wanamlalamikia Zuberi ambaye ndiye amesababisha dhiki yao. Wanyonge wanatangamana na wenye mamlaka: mtawala na mtawaliwa; mwenye ardhi na mpangaji; mwenye nyumba na mtumishi. Hakuna matumaini kwamba hali hii itabadilika.

Tofauti na nafasi aliyo nayo Zuberi, vijana (wakiwakilishwa na mhusika Dude) wanazunguka mjini wakitafuta kazi. Watu kama Dude wanafanya kazi duni sana ili waweze kujikimu. Ukosefu huu wa ajira ndio unaowafanya vijana kama Dude na Bushiri kuanguka katika mtego wa mapenzi na wanawake kama Amina ambaye anatumia pesa na mali yake kujipatia mapenzi na vijana. Vijana, ambao ni wanyonge sana kiuchumi, inabidi wafanye kazi yoyote ile. Hivyo, ni rahisi kwa Amina kuwanasa.

Riwaya ya *Asali Chungu* inaelezea pia uozo uliopo katika jamii. Zuberi ni mbakaji, na anatumia nafasi yake kufanya mapenzi na wasichana wadogo ambao analetewa na Binti Daudi. Naye Bi Amina, mkewe Zuberi, si mwaminifu kwa mume wake. Kwa hiyo, mume huku na mke huku – wote wakiwa na ashiki kubwa. Dude, mtoto anayezaliwa kutokana na kitendo cha Zuberi kumbaka Semeni baadaye anafanya mapenzi na Amina. Kisha anamwoa Shemsa na tena kumtia mimba Latifa, mdogo wake Shemsa. Kitendo cha Zuberi kuiramba asali kinakuwa na athari kubwa kwake. Anapoyagundua yote ambayo yamekuwa yakifanyika kati ya Dude (ambaye Zuberi sasa anajua ni mtoto

wake) na mkewe Amina na pia Shemsa na Latifa, anahisi uchungu mkubwa na kujutia yote aliyoyafanya. Anakuwa mnyonge sana, ambaye anaona kwamba labda akitubu na kutenda mema, Mungu huenda akamsamehe.

Mwishoni mwa riwaya tunaona mapinduzi yakifanyika ghafla. Wakulima wamechoka na hali ya kukandamizwa. Maskini wanadai haki yao na wanatekeleza maafa kama vile kuichoma nyumba ya Mzee Zuberi na Bi Amina. Hili linaashiria mwisho wa umwinyi, na mwanzo wa jamii mpya (au ujamaa) yenye usawa na haki kwa kila mtu. Hatimaye, asali inageuka kuwa chungu kwa Zuberi na makabaila wenzake. Vitendo vya Zuberi vya kuwanyanyasa wanyonge vinamletea majuto makubwa.

4.1.4 Riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* ya Shafi Adam Shafi (1978)

Riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* inasawiri mvutano kati ya wenye mamlaka, ambao ni makabaila kwa upande mmoja na wanyonge, ambao ni watumishi pamoja na wakulima kwenye ardhi ya mabwana shamba.

Mabwana shamba wanawanyanyasa watumishi wa nyumbani pamoja na wakulima wasio na ardhi. Watumishi wa nyumbani wanafanya kazi kubwa bila malipo. Hali yao ya maisha ni mbovu sana. Maisha yao ni kama ya wanyama. Pia, wananchi wengi hawana ardhi. Ardhi hiyo iko mikononi mwa mabwana shamba ambao wanaitumia kujinufaisha kiuchumi na kuishi maisha ya starehe wakati ambapo hali ya uchumi ya wakulima ni mbaya sana.

Lakini, mwishowe wanyonge wanaungana na kuipindua serikali inayowanyanyasa. Baada ya serikali kupinduliwa, maisha ya mabwana shamba walioitegemea serikali kudumisha hadhi yao yanakuwa matatani. Wanapoteza sehemu kubwa sana ya mashamba yao pamoja na baadhi ya mali waliyoipata kutokana na umiliki wa mashamba haya. Fuad, mmojawapo wa mabwana shamba hawa, anajikuta sasa ni

mnyonge sana. Hana la kufanya. Hana mamlaka tena. Badala ya kunyenyekewa na wanamapinduzi, yeye sasa ndiye anayewanyenyekea kupita kiasi. Hili linaashiria kwamba mnyonge akiazimia anaweza kubadilisha hali yake. Unyonge sio majaliwa yake kama mhusika Kijakazi anavyoamini.

4.2 Uteuzi wa Kileksika kama Nduni ya Kimtindo katika Usawiri wa Maudhui ya Dini na Mamlaka katika Riwaya Teule

Katika sehemu hii tunaangazia namna ambavyo mbinu mbalimbali za kileksika zimetumiwa na waandishi wa riwaya za *Paradiso, Nguvu ya Sala*, *Asali Chungu*, na *Kasri ya Mwinyi Fuad* zimetumiwa na waandishi kuashiria maudhui ya dini na mamlaka. Mbinu hizi ni pamoja na visawe, vinyume, urudiaji, uhamishaji wa nomino kutoka ngeli moja hadi nyingine, udunishaji, utohozi, urudiaji, na matumizi ya msamiati wa kitathmini.

4.2.1 Matumizi ya Visawe

Habwe (2005) ametumia visawe 'paradiso' na 'ahera' katika riwaya yake ili kujenga maudhui ya tamaa ya pesa na mali miongoni mwa wachungaji. Badala ya wachungaji kulenga paradiso ya baadaye kwa kufanya vitendo adilifu, wanalenga paradiso ya hapa duniani, yaani maisha ya utajiri mkubwa. Licha ya kwamba wachungaji wana haki ya kutajirika, wanatumia mbinu zisizofaa kupata pesa kwa mfano kusisitiza kiasi cha matoleo kanisani na hata kulangua madawa ya kulevya. Hii ni kinyume na maisha ya Yesu ambaye wachungaji hawa wanadai kumfuata lakini ambaye hakuwa na mali.

1. Lakini leo alitaka waelewe kanuni muhimu ya injili. Nayo ni kujitayarisha katika ulimwengu kwa **maisha ya ahera**.
   (Habwe, 2005, Ukur. 56)

2. Michael **aliishi Paradiso** na baadaye angeishi katika **Paradiso nyingine**.
   (Habwe, 2005, Ukur. 142)

3. Kuvaa kwao na kutembea kwao kulionyesha kuwa **wao waliishi ahera**.
(Habwe, 2005, Ukur. 130)

4. Ahera walikoishi **walihodhi mapesa**, **nyumba** za kukodisha na **magari** mtawalia. **Kula kwao** kulidhihirisha pia kuwa ni kwa juu.
(Habwe, 2005, Ukur. 130)

Katika madondoo ya 1 – 4 mwandishi anatumia visawe 'paradiso' na 'ahera' au 'maisha ya ahera' kuchimuza maudhui ya dini. Anaonyesha jinsi wahungaji wanavyojenga paradiso ya hapa duniani kwa tamaa ya vitu vya dunia badala ya kujiepusha na tamaa hiyo ili kwenda paradiso ya halisi.

Jambo la muhimu ni mtu kujaribu kujitayarishia maisha ya ahera au paradiso ya baadaye kwa kufanya mambo anayoyapenda Mungu. Awali, Mchungaji Michael anajaribu kufuata kanuni hiyo, na anawashauri waumini wengine kuifuata. Lakini baadaye naye anavutwa na mambo ya paradiso ya hapa duniani. Dondoo la 2 linatuonyesha kwamba hata Michael, ambaye amechorwa kama mchungaji kielelezo anaanza kuishi katika paradiso ya hapa duniani. Lakini anatarajia pia kuishi katika paradiso ya baadaye, kitu ambacho hakiwezekani, kwa vile paradiso ya hapa duniani ina mambo yanayomzuia mtu kwenda paradiso ya baadaye. Mambo ya paradiso ya hapa duniani yametajwa katika dondoo la 3 na la 4, yaani kuvaa na kutembea, kuhodhi pesa, nyumba, na magari. Mambo haya yanaonyesha tamaa ya vitu vya dunia, "ambayo Bwana Yesu alisema tusiwe nayo" (Habwe, 2005, Ukur. 77). Hili ndilo jambo analojaribu kudhihirisha mwandishi, yaani tamaa ya vitu vya dunia ambayo inapelekea vitendo visivyo vya kimaadili. Mwandishi anausawiri unafiki uliopo ambapo wachungaji kama Michael hawatekelezi yale wanayoyahubiri makanisani.

Mwandishi wa *Paradiso* pia anatumia visawe kuibua maudhui ya tamaa ya pesa. Askofu Joshua na mkewe Lona wanapofariki inagundulika kwamba walikuwa na pesa nyingi benkini.

5. Akaunti zao zilifura kwa **darahima**.
(Habwe, 2005, Ukur. 134)

Mwandishi ametumia neno **'darahima'** badala ya neno la kawaida 'pesa'. Uteuzi huu wa leksimu 'darahima' umefanywa ili kuchimuza faridi hiyo na kuonyesha kiasi cha utajiri wa wachungaji Joshua na mkewe Lona. Matumizi ya neno 'pesa' yasingekuwa na athari ya kuvuta nadhari ya msomaji. Tena, matumizi ya neno lisilo la kawaida yanamfanya msomaji kuliangalia neno hilo kwa makini na kuzingatia kile ambacho mwandishi anajaribu kuwasilisha. Akaunti za askofu na mkewe kufura kwa darahima ni kitu kilicho tofauti na mafundisho ya Kikristo, ambayo hayasisitizi utajiri, na badala yake yanasisitiza unyenyekevu katika hali zote. Joshua na mkewe wanatafuta utajiri ambao utawapa mamlaka makubwa katika maamuzi yao.

Mwandishi anadhihirisha jinsi ambavyo wachungaji wanatumia rasilimali za kanisa kwa ajili ya manufaa yao. Kwa mfano, kuwapeleka watoto wa Askofu Joshua shuleni sasa umekuwa kama 'mradi' wa kanisa.

6. Moja katika **miradi** ya pale kanisani ni kuwabwaga na kuwazoa kutoka shuleni **wana** wa mchungaji.
(Habwe, 2005, Ukur. 213)

Mwandishi anatumia neno '**wana**' badala ya neno lililozoeleka 'watoto'. Kwa njia hii, mwandishi amelichimuza neno 'wana' ili kumwathiri msomaji kuhusu tabia hiyo ya mchungaji kuwatwika waumini jukumu la kupeleka wanawe na kuwachukua kutoka shuleni. Matumizi ya neno 'wana' badala ya neno 'watoto' yanamfanya msomaji alenge tendo hilo lisilo la haki la kuwafanya waumini wabebe mzigo wa gharama za

kuwapeleka watoto wa mchungaji shuleni na tena kuwachukua kutoka huko. Uchimuzi wa neno 'wana' unasaidia kuonyesha mamlaka waliyo nayo wachungaji kanisani kwa kuwawekea waumini mzigo ambao waumini hao hawezi kuukataa. Hii ni kwa sababu waumini hawana mamlaka kanisani.

Matumizi mengine ya visawe katika riwaya teule tunayaona pale ambapo mwandishi wa *Nguvu ya Sala* anawasilisha mawazo ya mhusika Richard Ngunze kuhusu kukosekana kwa ubinadamu miongoni mwa wakazi wa jiji la Nairobi. Anawaita 'makatili' au 'magombe' watu wanaompiga kijana ambaye ameiba kibogosho cha mwanamke fulani.

7. Labda maisha ya mjini **yaliwanyang'anya** binadamu chembe za huruma zilizobakia, **wameshapokwa** hisia zote za kibinadamu na kubakia makatili au magombe ambayo yalikuwa tayari kumkumta pembe yeyote aliyepita mbele yao bila ya kuwazia lolote.

   *(*Wamitila, 1999, Ukur. 118**)**

Mwandishi anachimuza ubinafsi wa wakazi wa jiji la Nairobi kupitia kwa visawe: '**yalivyowanyang'anya**' na '**wameshapokwa.**' Visawe hivi vinaonyesha kwamba ugumu wa maisha una nguvu fulani ya kuwafanya wakazi wa jiji la Nairobi wapoteze utu. Wengi wao hawana uwezo wa kiuchumi. Ni kama kwamba wakazi hawa wamepoteza uwezo wa kudhibiti vitendo vyao. Kuna nguvu fulani inayowasukuma kufanya vitendo vya kikatili. Changamoto hii, kwa mujibu wa Susan, haiwezi kukabiliwa kwa njia ya nguvu ya sala peke yake.

Kwa mujibu wa Susan, babake hajajua kwamba kuna mabadiliko katika maisha ya kisasa. Susan anaona kwamba baba yake anang'ang'ania mkabala wa nguvu ya sala ambao haufai tena katika kukabiliana na changamoto za maisha ya jijini Nairobi.

8. Kwa kiasi kikubwa nilihisi kuwa baba alishindwa kulielewa hili kutokana na namna **alivyotopea** na **kubobea** katika imani yake.

> Kwake kilichokuwa muhimu ni kuyafuata mafundisho ya dini na kuithamini nguvu ya sala.
>
> *(*Wamitila, 1999, Ukur. 71**)**

Susan anasisitiza kwamba mambo yamebadilika, na jamii inafaa kwenda na wakati. Anatambua kwamba baba yake "**ametopea** na **kubobea"** katika imani yake. Mwandishi ametumia visawe '**kutopea**' na '**kubobea**' kama njia ya kuchimuza jinsi Richard anavyoshikilia mwelekeo wa dini kusuluhishia kila changamoto ya maisha. Ni vigumu sana kumshawishi mtu ambaye ametopea na kubobea katika imani kubadilisha msimamo wake.

Kupitia kwa matumizi ya visawe, Wamitila pia anagusia suala la jinsia kwa kuonyesha jinsi ambavyo mwanamke anakandamizwa na utamaduni wa jamii yake. Inabidi akae nyumbani na kufanya shughuli za nyumbani wiki nzima.

9. Mary alikuwa **mama wa nyumbani.**

   (Habwe, 2005, Ukur. **5**)

10. Mary Kasiva alikuwa **mke wa nyumbani** alishughulika na kazi za nyumbani wiki nzima, kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi. Siku ya Jumapili alijiunga na mumewe kwenda kanisani. Hiyo ilishakuwa ratiba yake sasa na wala hakuwa na hiari tena.

    (Wamitila, 1999, Ukur. 178)

Katika madondoo ya 9 na 10, tunaona kwamba mwandishi anamrejelea Mary Kasiva kwa kutumia visawe '**mama wa nyumbani**' na tena '**mke wa nyumbani**'. Visawe hivi vinajitokeza katika kurasa tofauti za riwaya: awali kabisa katika sura ya pili, na baadaye sana katika sura ya ishirini na tano. Matumizi ya visawe hivi yanaonyesha jinsi ambavyo mwandishi anazingatia hali ya mwanamke ya kukaa na kufanya shughuli za nyumbani tu. Ni kama kwamba mwandishi anarudia kauli ileile, na hii inavuta nadhari ya msomaji ambaye atatambua kwamba kuna ujumbe ambao mwandishi anamwasilishia kutokana na msisitizo wa visawe. Mwandishi anaonyesha kwamba si

haki mwanamke kufungiwa nyumbani kwa shughuli kadhaa. Hali hii inatuonyesha jinsi ambavyo mwanamke hana mamlaka hata katika mazingira ya dini ambayo inasisitiza haki kwa binadamu wote.

Mwandishi wa riwaya ya *Asali Chungu* ametumia visawe kuwasilisha maudhui ya matumizi yasiyofaa ya mamlaka ambapo DC, Bwana Zuberi, anatumia ofisi yake kama mahali pa kufanyia vitendo vya kimapenzi na wasichana, wakati ambapo wanawake wanyonge wanaotafuta huduma ya umma kutoka kwake wanaambiwa wasubiri. Tofauti na wanawake ambao sababu zao za kutaka kuonana na Bwana DC zimeelezwa, hatujui kwa nini hasa wasichana wanataka kumwona Bwana Zuberi, ila maelezo ya msimulizi kuhusu wasichana hawa wakati wakitoka ofisini mwa Zuberi ndiyo yanatuonyesha kwamba wameitiwa sababu za kimapenzi. Wasichana hawa wana ruhusa ya kuingia ofisini mwa Zuberi moja kwa moja, wakati ambapo wanawake wakongwe wanatakiwa kusubiri.

11. Katikati ya bao, **jana-jike** lenye jirim la kiboko linatia gati wenzake huku linapuma.

    …na aghalabu watu watakaopata nafasi hiyo ni kama **huyu kimwana** aliye ndani sasa hivi. Bahati ni ya warembo na wenye sura zao!

    (Mohamed, 1977, Ukur. **8**)

12. Muda mrefu ukapita – hata huko, katikati ya kukata tamaa, mlango wa ofisini ukafunguliwa. **Kijanajali** kimoja kikadhihiri, macho kupekupe; haya za kujitia zimemvaa; damu mashavuni imemwiva; mabaka mawili ya damu iliyojikusanya yanaonyesha dhahiri chini ya shingo yake ya mbuni; na nywele zimetimka.

    (Mohamed, 1977, Ukur. 4)

Mwandishi ametumia majina mbalimbali kuwaelezea wasichana hawa ambao wanaingia ofisini mwa Zuberi moja kwa moja: **jana-jike**, **kimwana**, **kijanajali**. Kwa kutumia visawe vya majina anayowapachika wasichana hawa, mwandishi anawachimuza na kulinganisha jinsi wanavyotendewa katika ofisi hiyo, tofauti na jinsi

wanawake wazee wasiojiweza wanavyotendewa. 'Warembo wenye sura zao' ndio wana bahati ya kuonana na Bwana DC. Majina 'kimwana', 'kijanajali', na 'jana-jike' yanalenga kumfanya msomaji awe makini kuzingatia uchu wa Zuberi kwa wasichana ambao kiumri, yeye angekuwa baba yao. Wanalolifanya ndani ofisini limedokezwa kwa njia ya maelezo ya mwonekano wao wanapotoka ofisini mwa Zuberi. Kuhusu 'kijanajali' kimoja kinachotoka ofisini mwa Zuberi, mwandishi anaeleza: "macho kupekupe; haya za kujitia zimemvaa; damu mashavuni imemwiva; … nywele zimetimka." Maelezo haya yanaashiria vitendo vya kimapenzi kati ya Zuberi na wasichana hawa ofisini mwake. Badala ya kuwasaidia wanawake wakongwe, Zuberi anatumia nafasi yake kama DC kuingia katika mahusiano ya kimapenzi hata ofisini mwake.

Fasiri kwamba Zuberi anaingia katika vitendo vya kimapenzi na wasichana wanaoingia ofisini mwake inatokana na hulka ya Zuberi kwa jumla. Tunaona kwamba anawanyanyasa wafanyakazi wake wa kike. Maelezo kuhusu wafanyakazi wasichana wanaofanya kazi katika jumba la Zuberi yanatuonyesha kuwa ni mwanamume mwenye ashiki nyingi. Wasichana wafanyakazi wanne wanaamua kulala pamoja baada ya "tukio fulani". Kulingana na maelezo kuhusu hulka ya Zuberi, ni dhahiri kwamba Zuberi anaingia katika vyumba vya wafanyakazi wasichana, hasa tukizingatia jinsi anavyotumia hila kuingia katika chumba cha msichana Semeni, (ambaye tunaambiwa ni **kigoli**) na kumbaka. Pia tunaambiwa kwamba kazi mojawapo ya Biti Daudi (mwanamke anayesimamia shughuli katika jumba la Bwana Zuberi) ni "kumteremshia Zuberi mabibi kemkem". Maelezo haya yote kumhusu Zuberi yanaashiria kwamba wasichana wanaoingia ofisini mwa Zuberi wanaingizwa katika vitendo vya kimapenzi na Zuberi. Zuberi anatumia mamlaka yake kufanya anavyotaka kwa kuwaingiza wasichana wadogo na wanyonge katika vitendo vya kimapenzi.

Mbinu hii ya matumizi ya visawe kurejelea au kuelezea kitu kile kile au mtu yule yule imetumiwa vilevile kumrejelea Zuberi. Katika kummulika mtu ambaye anawanyanyasa wanawake wanaolima kwenye shamba lake, mwandishi ametumia misamiati mbalimbali ili kuonyesha hisia za wanyonge kuhusu wale wenye mamlaka.

13. [Bi Pili] anachacharika baoni, tayari kumvunjia mbarika **Bwana DC**. ….
Wote wamekuja kwa dhamiri moja tu – kuonana na **bwana!**
Wengine …. Wamepanda gari na kushuka hapo kwa tamaa kuwa angalau '**Bwana Mkubwa'** atawatazama kwa jicho la rehema.
(Mohamed, 1977, Ukur. 1)

14. Wanyama wa **bwana huyu** walifungwa kondeni mwangu….
Shoti wameulaula muhogo wangu na migomba yote.
Basi nd'o nimekuja kwa **huyu bwana**.
Nawe unatarajia nini kwa **bwana huyu**?
Shtakia Mungu dada kuliko kumshtakia **kiumbe huyu**…
(Mohamed, 1977, Kur. 2-3)

15. Lawama na malalamiko juu ya matendo ya **Bwana Zuberi** yakaendelea.
(Mohamed, 1977, Ukur. 4)

Katika madondoo ya 13 - 15, Zuberi anarejelewa kwa majina mbalimbali ya kupachika: '**Bwana DC**', '**Bwana**', '**Bwana Mkubwa**', '**bwana huyu**', '**huyu bwana**', pamoja na '**Bwana Zuberi**'. Cheo cha Zuberi ni bayana. Yeye ni DC, yaani, *District Commissioner*. Lakini, mbali na kuitwa 'Bwana DC', hata neno 'bwana' peke yake limetumika kumrejelea. Pia anaitwa 'bwana mkubwa'. Msisitizo wa neno 'bwana' pia unaashiria hisia na mtazamo wa hao wanawake ambao wamekuja kumwona Zuberi. Baadhi ya matumizi ya majina anayopachikwa Zuberi yanaonyesha tathmini hasi kutoka kwa wanawake waliokuja kumwona kuhusu shida zao. Kwa kusema 'bwana huyu' au 'huyu bwana', wanawake hao wanajitenga na Zuberi kiuolezo. Hawataki kumrejelea kwa jina. Wote wanakubaliana kuhusu mtu anayewatesa. Hivyo, wanatumia kirejeshi 'huyu', yaani mtu ambaye amehusika na shida inayowakabili. Hata bibi

mmoja anampachika DC jina '**kiumbe huyu**'. Kwa kumwita '**kiumbe huyu'** wanawake wanampunguzia ubinadamu na kumwonyesha kama mtu asiye na hisia za utu. Hii ni kwa sababu ya muktadha wa hali mbaya ya kimaisha ya wanawake ambao wamekuja kumlalamikia 'kiumbe huyu.' Sifa hii ya Zuberi ya kutenda kinyama tunaiona wakati akielekea kwenye chumba cha Semeni kumnajisi. Amefunga matambara miguuni ili asisikike. Msimuliaji anatuelezea kwamba katika hali hiyo Zuberi alikuwa: '**hayawani**' kesha kazi!' na kwamba 'Yu tayari kukamilisha unyama wake' (Mohamed, 1977, Ukur. 9). Zuberi ni Bwana DC, lakini tena ni 'kiumbe huyu' au hayawani; mtu ambaye anatenda unyama.

Usawe umetumiwa pia katika kurejelea maudhui ya majaliwa katika riwaya ya *Paradiso* pamoja na riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Majaliwa yanaashiria kwamba mwanadamu hana mamlaka kuhusu kuzaliwa kwake wala mstakabali wake. Katika riwaya ya *Paradiso* tunaona kwamba mhusika Apondi (mama yake Michael) anatambua jambo hili. Anasema, "Lakini hesabu ya mtu anayo Maulana katika kufi yake. Mtu mwenyewe hajui. Mara ananyakuliwa kama mwizi" (Habwe, 2005, Ukur. 89). Maudhui ya majaliwa yamesisitizwa katika mkusanyiko wa vitenzi-jina ambavyo vinataja hatua tatu muhimu katika maisha ya binadamu.

16. Moyo wake [Michael] lakini ulikumbuka maisha yana hatua tatu:
    kuja, **kuoa** na **kuondoka**.
    (Habwe, 2005, Ukur. 90)

17. Mungu ndiye anayefahamu **kuja**, **kuweko** na hata **kutoka**.
    (Habwe, 2005, Ukur.96)

Katika dondoo la 16, mwandishi anarejelea hatua tatu katika maisha ya binadamu: '**kuja**', '**kuoa**' na '**kuondoka**' (Habwe, 2005, Ukur. 90). Katika dondoo la 17 anatumia leksimu '**kuja**', '**kuweko**' na '**kutoka**.' Isipokuwa leksimu ya 'kuja' ambayo imerudiwa katika tungo zote mbili, leksimu zilizobaki zimetumika kama visawe, yaani

ametumia ‘kuoa’ kama kisawe cha ‘kuweko’ (katika muktadha wa madondoo haya), na ‘kuondoka’ kama kisawe cha ‘kutoka’. Katika dondoo hilo hilo anasema ‘na hata kutoka’. Hapa mwandishi anamaanisha kwamba binadamu ajue kwamba Mungu anadhibiti kila kitu, mkiwemo mwisho wa maisha yake, yaani Mungu anadhibiti maisha ya mtu kikamilifu, na kwa hiyo binadamu asijidanganye akifikiri kwamba yeye ndiye anayedhibiti maisha yake, na ajue kwamba maisha yake yana mwisho. Lakini tunamwona mhusika Lona ambaye anadhibiti karibu kila kitu ila “kuna kitu kimoja tu hakukidhibiti nacho ni wakati na ahadi yake kwa Bwana” (Habwe, 2005, Ukur. 131). Hii inamaanisha kwamba mamlaka aliyo nayo mwanadamu yana kikomo. Mungu ndiye aliye na mamlaka zaidi. Mwandishi anatoa funzo kwa binadamu kutojikweza sana wakati anapotangamana na binadamu wenzake.

Mwandishi ametumia visawe ili kusisisitiza kwamba maisha hayadumu. Binadamu anakuwepo hapa duniani kwa muda tu, halafu ni lazima apaondoke. Ingawa mwandishi ametumia neno ‘kuoa’ ambalo linarejelea jinsia ya kiume peke yake, inaweza kuchukuliwa kwamba mwandishi anazungumzia hata mwanamke, au kasahau kutumia neno ‘kuolewa’ kurejelea jinsia ya kike. Fasiri hii inatokana na jinsi ambavyo mwandishi amejaribu kumwendeleza mhusika mwanamke katika riwaya hii. Katika madondoo haya mwandishi ametumia neno lile lile ‘kuja’, badala ya ‘kuzaliwa’ ili liambatane na leksimu zinazofuata na kuendeleza hoja ya mabadiliko katika maisha na kutodumu kwa maisha ya mwanadamu.

4.2.2 Matumizi ya Vinyume

Msamiati kinyume ni msamiati unaohusisha maneno yanayokinzana kimaana. Hii ni njia ya kufafanua faridi ambazo zinaingia katika unyume huo. Sifa za faridi moja zinalinganuliwa na sifa za faridi nyingine.

Waandishi wametumia msamiati kinyume unaoonyesha pengo la kiuchumi lililopo kati ya matajiri na mafukara. Miongoni mwa mali wanazozimiliki wachungaji na watu wengine wenye nacho ni nyumba au makazi ya kifahari. Makazi haya ni ishara ya mamlaka makubwa. Makazi ya matajiri yanalinganuliwa kileksika na makazi ya watu maskini na wanyonge.

18. Nyumba yake Joshua ni **ya kisasa** si kama **kibanda alichokaa hapo Kibera**. Kibanda hicho …hakikumstahili hasa alipopandishwa na kuwa Askofu Mkuu.
(Habwe, 2005, Ukur. 43)

19. Waliachana usiku ule. Amuko akaelekea **Mountain View** naye Michael akaenda katika **kibanda chake Kibera**.
(Habwe, 2005, Ukur. 42)

20. Kwa mbali **uliwazukia ukuta** wa manjano uliozunguka **maskani ya Bwana na Bibi Zuberi**.
(Mohamed, 1977, Ukur. 94)

21. Palikuwa na vyumba vingi vidogovidogo vilivyojipanga sturi moja **kule mabandani**. Mabanda yenyewe yalikuwa yamekamatana na jumba kubwa [la Zuberi] …
(Mohamed, 1977, Ukur. 9)

Katika riwaya ya *Paradiso* mwandishi anaonyesha vile nyumba ya Askofu Joshua ni ya kifahari, tofauti na "kibanda alichokaa hapo Kibera." Katika riwaya ya *Asali Chungu* tunaona kuwa maskani ya Bwana na Bibi Zuberi ni jumba kubwa lililozungukwa na ukuta. Maskani haya pia yamelinganuliwa na maskani ya wafanyakazi wake ambao wanakaa mabandani.. Hali hii ni sawa na ile tunayoiona katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* ambapo kabaila Fuad anaishi katika kasri, wakati ambapo wafanyakazi wake kama vile Vuai na Kijakazi wanakaa katika mabanda. Kibanda cha Kijakazi hata kiko nyuma ya banda la ng'ombe.

22. Usiku ule Vuai alirejea nyumbani amechoka… Hakusimama popote ila alifululiza **bandani kwake** kwenda kupumzika.
(Shafi, 1978, Ukur. 33)

23. Kijakazi aliondoka bandani humo …alikwenda zake chumbani kwake nyuma ya **banda hilo** [la ng'ombe]…
(Shafi, 1978, Ukur. 88)

Kama inavyodhihirika katika madondoo haya, makazi ya wanyonge yaliyopo nje ya majumba ya makabaila ni mabovu sana. Wanaishi katika mabanda tu. Hata ng'ombe wa Fuad pia wanakaa kwenye mabanda. Tofauti kati ya msamiati uliotumika kuelezea makazi ya matajiri na makazi ya mafukara unalenga kulichimuza tatizo la pengo lililopo kati ya matajiri na mafukara. Raia wengi ni maskini wanaoishi maisha duni kabisa, wakati ambapo matajiri wanaishi maisha ya starehe. Hakuna usawa.

4.2.3 Mbinu ya Kuhamisha Nomino kutoka Ngeli Moja Hadi Ngeli Nyingine

Kama njia ya kuwasilisha maudhui yao, baadhi ya waandishi wamehamisha nomino kutoka ngeli moja hadi nyingine. Uhamishaji unaotokea sio wa kawaida au ule ambao umezoeleka na kukubalika katika Kiswahili. Kwa hiyo, waandishi kuhamisha nomino hadi ngeli nyingine ni ukiushi unaouchimuza ujumbe fulani. Msomaji anajaribu kufasiri sababu za uhamishaji huo.

24. Ahera walikoishi walihodhi **mapesa**, nyumba za kukodisha na magari mtawalia. Kula kwao kulidhihirisha pia kuwa ni kwa juu.
(Habwe, 2005, Ukur. 130)

25. Si muhimu ujana au ubichi wake; muhimu ni **mipesa** yake ambayo ndiyo tegemeo lako, au sivyo?
(Mohamed, 1977, Ukur. 92)

26. Majuto; majuto sina. Nina wasiwasi tu kukosa yale **mapesa** yake ambayo hata wewe uliniasa kuyang'ang'ania. Lakini sasa nakwambia kwa dhati: nimechoka kununuliwa.
(Mohamed, 1977, Ukur. 118)

Waandishi wameihamisha nomino 'pesa' ambayo ni nomino ya ngeli ya 9/10 hadi kwenye ngeli ya 6 (**mapesa**) na tena kwenye ngeli ya 4 (**mipesa**) ili kudhihirisha pengo

kati ya uwezo na utajiri (wa Amina) kwa upande mmoja, na unyonge wa kifedha wa watu kama Bushiri, Dude, na vijana wengine maskini. Uhamishaji huu na msisitizo wa pesa unaonyesha uwezo na mamlaka yanavyotokana na kumiliki pesa nyingi. Akitumia pesa zake, Amina anawanunua vijana kwa maslahi yake anavyotaka.

Pesa zimesababisha ubinafsi mwingi. Katika riwaya ya *Paradiso* tunaona jinsi ambavyo Askofu Joshua na Kasisi Lona "walihodhi **mapesa**" na vitu vingine. Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 2013) 'kuhodhi' ni kurundika bidhaa au mali. Wachungaji hawa wamezipa pesa kipaumbele, sio ufalme wa Mungu. Wanatumia mbinu kadhaa kujipatia pesa mkiwemo kulangua madawa, kuanzisha miradi kadha ya kanisa, na kukusanya zaka na matoleo mengine kwa hila.

Said Ahmed Mohamed amelihamisha neno 'pesa' hadi kwenye ngeli tofauti kwa kuziwekea viambishi vya ngeli hizo, yaani kiambishi cha ngeli ya nne **mi-** katika '**mipesa**' na kiambishi cha ngeli ya 6 **ma-** katika '**mapesa**'. Hii ni njia anayoitumia mwandishi kuichimuza dhana ya 'pesa' na msimamo wake kuhusu uwezo unaotokana na umiliki wa pesa nyingi. Kwa mujibu wa Bi Mwanakweli, mhusika katika riwaya ya *Asali Chungu* 'ukiwa na pesa una kila kitu' (Mohamed, 1977, Ukur. 107). Huo ndio uwezo alio nao Bi Amina. Ana pesa, na anaonekana kuwa na kila kitu, kwa vile anaweza kujipatia chochote anachotaka. Naye Dude anatafuta pesa tu kutoka kwa Bi Amina.

Uhamishaji wa nomino kutoka ngeli moja hadi ngeli nyingine katika riwaya ya *Asali Chungu* umetumiwa kuashiria ufukara na unyonge walio nao raia wengi.

27. "Baada ya kuhakikisha hilo, Kabore akapeperukia chumba chengine…" Waliokuwepo walimshindikiza Kabore kwa macho – wakashuhudia **mkanzu** wake….
(Mohamed, 1977, Ukur. **4**)

Katika dondoo la 27, mwandishi ametumia neno ‘mkanzu’ (nomino ya ngeli ya 3) ambayo mwandishi ameihamisha kutoka ngeli ya 9 (kanzu) kwa kuiwekea kiambishi cha ngeli ya 3 ‘**m**’. Uhamishaji huu umefanywa kimaksudi ili kudhihihisha kinaya kilichopo ambapo Kabore, tarishi ambaye ni mnyonge, anahusika katika kuwanyanyasa wanyonge wenzake. Yeye anajiona kama sehemu ya mfumo wa mamlaka ya serikali, lakini kusema kweli yeye ni mnyonge kabisa. Neno ‘**mkanzu**’ linadhihirisha unyonge wake, ingawa yeye hajitambui kama mnyonge. Neno ‘**mkanzu**’ limetumika kuwasilisha hisia hasi walizo nazo wanawake (waliokuja kumlalamikia Zuberi) kumhusu tarishi huyu Kabore. Wanawake hawaoni tu, ila ‘wanashuhudia’ **‘mkanzu**’wa Kabore. ‘Wakashuhudia’ ni neno ambalo limetumiwa kisitiari kudhihirisha hali ya ufukara ya Kabore. Kabore anahusika katika unyanyasaji wa wanawake unaofanywa na Zuberi, lakini naye pia anaweza akaangaliwa kama mwathirika anayetumiwa tu na mwenye mamlaka – Zuberi. Naye Kabore anatafuta riziki tu. Kwa mtazamo wao, wanawake wanaona kwamba Kabore ni kama mtumwa wa DC.

Katika kuonyesha kiasi cha ufukara unaowakabili raia wengi, mwandishi Said Ahmed Mohamed pia anatuonyesha hali ya vitu wanavyovimiliki raia wanyonge. Akiwa anaelekea kukutana na Bushiri Dude anashuhudia ufukara wa watu wa kawaida. Anakutana na mchukuzi mmoja – jirani yake – ambaye anaburura ‘**mparapata**’ wake wenye shehena ya mizigo:

28. Dude alimwangalia yule mchukuzi aliyemsalimu. Kwenye kibao cha nyuma cha huo **mbaiskeli wake**, palikuwa pamefungwa ndizi mbivu, ndizi mbichi… mtu angalistaajabu mchukuzi huyo aliwezaje kuburura **baiskeli hiyo** bila kupinduka nayo… Dude alimwangalia yule jirani yake kwa muda jinsi alivyokuwa akichapuka huku kailalia mbele baiskeli yake, na nyuma, yale mararu ya suruali na shati lake yanapeperuka.

(Mohamed, 1977, Ukur. 73)

Baiskeli anayoiburura mchukuzi huyo imeelezwa kwa lugha hasi. Ni '**mparapata**' au '**mbaiskeli**' tu. Tunapata picha ya baiskeli iliyochakaa. Tofauti na watu kama Zuberi na Amina wenye uwezo mkubwa wa pesa na mali ambao unadhihirika katika umiliki wa magari na mashamba makubwa, watu kama Dude na wachukuzi, kama huyu anayeelezwa katika dondoo la 28, karibu hawana chochote. Watu hawa hawana uwezo wa kifedha wa kununua magari. Lakini zaidi ya hilo, hata baiskeli ya mchukuzi huyu ni '**mparapata**' au '**mbaiskeli**' tu. Gharama ya magari imewashinda wanyonge; hata gharama ya baiskeli mpya hawaiwezi. Mwandishi ameihamisha nomino 'baiskeli' kutoka ngeli yake ya kawaida yaani ngeli ya 9 hadi kwenye ngeli ya 3, sawa na anavyoihamisha nomino 'kanzu' kutoka ngeli ya 9/10 hadi kwenye ngeli ya 3. Ufukara wa mchukuzi umesisitizwa pia katika maelezo mengine yanayoambatana na uhamishaji wa nomino. Mchukuzi amevaa 'mararu ya suruali'. Maelezo kuhusu mavazi na mali ya watu wanyonge kama Dude, Kabore na wachukuzi – yote yanadhihirisha ufukara mkubwa wa watu wengi wa kawaida.

4.2.4 Udunishaji

Waandishi wa riwaya teule pia wametumia nomino mahsusi za ngeli ya 7/8 zinazoonyesha udogo kimaksudi ili kuwasilisha ujumbe fulani. Hii inadhihirika katika madondoo yafuatayo:

29. Yule **kijana** …. Alimsihi Mungu wake amnusuru na hujuma za wastaarabu hawa waliokuwa wanatishia kumwua kwa sababu ya kunyakua **kibogosho** cha mwanamke mmoja mnene ambacho hakikuwa na chochote ila karatasi za shashi zilizokuwa na kamasi na **vitaulo vya *stayfree***.
(Wamitila, 1999, Ukur. 115)

30. Siku hizi zilionekana kama za mwisho kweli maana maradhi, ufukara, mizozo na ukosefu wa kanisa ni baadhi ya **vijisababu** vilivyosukuma watu kanisani.
(Habwe, 2005, Ukur. 52)

31. Michael alishangaa ni kwa jinsi gani matanga yamekuwa **kisababu** cha kujipatia pesa.
(Habwe, 2005, Ukur. 95)

Katika dondoo la 29, mwandishi anazungumzia uhalifu na kiasi cha ukatili jijini Nairobi. Kuna kisa cha kijana fulani anayeuawa na umati wa watu kwa sababu ya kunyakua kibogosho cha mwanamke mmoja. Mwandishi ametumia msamiati unaoonyesha kwamba kitendo cha kumuua kijana ambaye ameiba hakifai. Ametumia neno '**kibogosho**' na '**vitaulo vya *stayfree***' – nomino ambazo zinaonyesha kwamba kitu kilichoibwa si cha muhimu sana, kikilinganishwa na kitendo cha kumuua kijana huyo. Wamitila ametumia nomino hiyo **'kibogosho**' kimaksudi. Ingawa Kihore na wenzake (2003) wanatambua kwamba uainishaji wa ngeli kisemantiki una utata, wanakubali kwamba kuna "dhana za jumlajumla zinazojitokeza katika baadhi ya nomino za ngeli mbalimbali." Kuhusu nomino za ngeli ya 7 wanaeleza kuwa nomino za ngeli hii ni majina ya "vitu vya kawaida kwa jumla, vitu visivyo na thamani…. Katika ngeli hizi huingizwa pia nomino zinazohusu watu au wanyama ambao ama wanadharauliwa kutokana na udogo wao…." Kwa hivyo, matumizi ya nomino 'kibogosho' katika muktadha huu yanaashiria kwamba haifai kijana huyu kuuawa kwa sababu ya kuiba kitu kisicho cha thamani kama kibogosho ambacho hata "hakikuwa na chochote ila karatasi za shashi … na vitaulo vya *stayfree*. Hata neno "**vitaulo**" ni nomino ambayo pia inaashiria vitu visivyo vya muhimu sana. Hata wanaomuua wanatambua kwamba huyu ni '**kijana**' au '**kitoto**' tu. Nomino hizo mbili ('kijana' au 'kitoto') pia ni za ngeli ya 7 katika uainishaji wa kimofolojia. Matumizi ya nomino hizi za watu wanaochukuliwa kuwa hawajapevuka kiumri yanasisitiza ule ukatili anaotendewa kijana aliyeiba kibogosho tu.

Mwandishi ametumia nomino za ngeli ya 7 kimaksudi kwa njia ya kulinganua kitendo cha ukatili cha kumuua kijana na kitu kilichoibwa. Hakuna usawa au haki, kwa vile

adhabu ya kumuua mtu hailingani kabisa na thamani ya kitu kilichoibwa, ingawa hii haimaanishi kwamba ingekuwa sawa kumuua kijana huyo kama angeiba kitu cha thamani zaidi kama vile gari. Matumizi ya nomino hizo ya ngeli ya 7 ni kwa ajili ya uchimuzi wa ukatili unaotendeka na shida ya gharama ya maisha jijini Nairobi. Lakini nomino 'vitaulo' inatokana na mchakato wa kimofolojia wa udogeshaji ambapo nomino za ngeli nyingine, huongezewa kiambishi 'ki' au viambishi 'ki' na 'ji' au kiambishi cha wingi "vi" cha ngeli ya 8 ili kuziingiza nomino hizo katika ngeli ya 7/8.

Katika riwaya ya *Paradiso* (Dondoo 30) tunaona jinsi ambavyo mwandishi anadogesha neno 'sababu' kwa kuliwekea viambishi "ki" na "ji" na kuunda nomino '**vijisababu**' katika tungo 'vijisababu vilivyowasukuma watu kanisani'. Hapa mwandishi ametumia viambishi 'ki' na 'ji' kama njia ya kuzidunisha sababu watu wanazozitoa za kwenda kanisani. Mwandishi anafanya hivyo ili kuonyesha kwamba sababu hizo hazina uzito sana au sio za maana au za msingi. 'Vijisababu' vinavyowasukuma watu kanisani ni pamoja na maradhi, ufukara, mizozo na ukosefu wa kanisa. Mwandishi anaeleza kwamba baadhi ya waumini wanakwenda kanisani 'kutupa wakati' tu, sio kwa ajili ya kusikiliza neno la Bwana.

Hata hivyo, katika riwaya hiyo hiyo ya *Paradiso* (Dondoo la 31) nomino "**kisababu**" pia imetumika. Nomino hii imetumika kurejelea kitendo cha Wakristo wa Budalangi kuomba pesa na chakula kutoka kwa wafiwa, yaani Michael na baba yake Mango. Mchungaji Michael anakiona kitendo hicho kama 'kisababu' cha kujipatia pesa, yaani sio sababu hasa, ila ni kama kisingizio tu. Hii inamaanisha kwamba njia zote mbili: kuambisha "**ki**" peke yake au "**kiji-**" kwenye nomino 'sababu' (au nomino nyingine kama hiyo) zinawezekana.

Kwa njia ya ulinganuzi, hata yule mwanamke ambaye kibogosho chake kimenyakuliwa ni mnene. Hapa mwandishi analinganua umbo la mlalamishi (**mwanamke mnene**) na umri wa mtoto aliyeiba kuonyesha jinsi ambavyo mtoto yule ameonewa na mtu anayemshinda sana kiumri na kiumbo, lakini ambaye hana huruma kwake (mtoto huyo). Hata umati unatambua kwamba hiki ni kitoto tu: "**Kitoto** kama hiki kimejifunzia wizi wapi?" Unene wa mwanamke mlalamishi umetumiwa kusisitizia hali ya kutokuwepo ulinganifu kati ya tendo la kuiba na adhabu ya kuua. Ukosefu wa huruma yoyote kwa kitoto hiki unadhihirisha kile ambacho mwandishi anajaribu kukiwasilisha; yaani ikiwa watu wako radhi kumuua mtoto tu, hiyo inaonyesha kiasi cha ukosefu wa huruma miongoni mwa wakazi wa jiji la Nairobi.

Kwa mujibu wa Richard Ngunze, ukatili huu ni uasi wa binadamu, yaani binadamu kuiacha njia ya Bwana. Richard anaona kwamba kinachohitajika katika kukabiliana na vitendo kama hivyo ni nguvu ya sala. Lakini, binti yake Susan ana mtazamo kwamba huu ni mfumo wa maisha. Sio kwamba watu wameasi, ila hali ngumu ya maisha ya jijini Nairobi ndiyo imewabadilisha, wakawa hawana huruma – 'hayawani' au 'magombe', kama Richard anavyowachukulia.

4.2.5 Utohozi

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) utohozi ni kulichukua neno kutoka lugha moja na kulipa matamshi na mwendelezo wa lugha pokezi. Hii ni njia mojawapo ya kuunda msamiati. Kwa upande mwingine, Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013) inaeleza kwamba kutohoa neno ni kubadilisha matamshi au tahajia ya neno la lugha ya kigeni ili lilingane na matamshi au tahajia ya lugha ya kienyeji.

Istilahi ambazo zimetoholewa zinafungamana na ujumbe ambao mwandishi anaazimia kuutoa. Waandishi wamezitumia istilahi hizo kimaksudi. Kupitia kwa mbinu ya

utohozi, Habwe anatoa maudhui kwamba mchungaji anatarajiwa kuwa mfano bora kwa jamii. Awali, Michael anafanya vitendo vinavyomfurahisha Bwana, vitendo ambavyo kwa kweli vitamsaidia kwenda paradiso ya baadaye. Anafuata msingi wa injili unaosisitiza kwamba muumini asiwe na tamaa ya vitu vya dunia. Katika mtazamo wa baba yake, mtoto wake Michael amehitimu kikristo na anaweza kwenda paradiso moja kwa moja.

> 32. Mango aliona kuingia paradiso yatakuwa mapenzi ya Bwana Yesu. Michael alikuwa na **pasipoti** ya moja kwa moja. (Habwe, 2005, Ukur. 141)

Katika dondoo la 32, neno 'pasipoti' limetoholewa kutoka neno la Kiingereza "passport" ambacho ni kibali cha serikali kwa mwananchi kinachomtambulisha wakati anaposafiri kwenda nchi zingine. Kwa hiyo, tunaona kuwa Michael ana kibali cha kwenda paradiso moja kwa moja, tofauti na wachungaji wengine. Lakini kinachosisitizwa na mwandishi, na ambacho ndicho lengo lake la kuandika riwaya ya *Paradiso* ni kwamba mwenye 'pasipoti' ya kwenda paradiso ni yule ambaye amejiepusha na vitendo visivyo vya kimaadili ambavyo vinamzuia mtu kwenda paradiso. Kwa njia hii, mwandishi anajaribu kupiga vita vitendo visivyo vya kimaadili katika jamii.

Katika riwaya ya *Nguvu ya Sala*, mwandishi ametumia neno 'pasta', ambalo limetoholewa kutokana na neno la Kingereza 'pastor' yaani mchungaji. Huu ni uteuzi unaofaa kuchunguzwa, kwa vile mwandishi ameamua kutohoa neno kutoka katika lugha nyingine, wakati ambapo neno la Kiswahili lipo. Mwandishi ametumia neno pasta wakati akizungumzia ukali wa Richard kwa watoto wake. Ukali wa Richard unalinganuliwa na upole wa rafiki yake Nichodemus, baba yake Bathsheba, ambaye si pasta.

> 33. Babake Bathsheba alikuwa Mkristo. Hakuwa **pasta** kama babangu ila alikuwa mzee wa kanisa na wala sidhani kama alikuwa mkali kama alivyokuwa baba. Labda siku moja angekuwa mkali; siku ambayo angekuwa **pasta**.
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 16)

Mwandishi anaonyesha kinaya ambapo, Richard, ambaye ni pasta, ni mkali zaidi kuliko Mkristo wa kawaida, wakati ambapo hali ingekuwa ni kinyume chake. Richard anataka awe ni Mkristo asiye na doa au mkamilifu (mmenyu), ilhali hilo haliwezekani kwa binadamu. Kwa vile matarajio yake hayawezi kutimizwa kwa sababu ya jinsi alivyoumbwa binadamu, hali hiyo inapelekea ukali wake wa kila mara kwa wanafamilia wake kwa sababu ya chochote anachokiona ni kosa kubwa. Neno 'pasta' pia limerudiwa mara mbili kama njia ya kulichimuza ili kumfanya msomaji azingatie kinaya kilichopo ambapo mtu ambaye ni pasta hana tabia inayotarajiwa kwa mtu wa mwito huo. Ni njia ya kuzimulika tabia za Richard ambazo haziendani na hulka ya mtu ambaye angekuwa pasta wa kweli. Mwandishi hatumii neno la Kiswahili 'mchungaji' kwa vile lingesikika la kawaida, kuliko neno 'pasta' ambalo ndilo limezoeleka zaidi miongoni mwa watu, kurejelea wachungaji wa dhehebu la kipentekosti.

4.2.6 Urudiaji Kileksika

Wamitila (2003) anaeleza kwamba urudiaji ni hali ya kulisema jambo mara kadha wa kadha na kimsingi hukusudiwa kuhakikisha kuwa msomaji anayakumbuka mambo fulani. Anasema kwamba urudiaji ni mbinu mojawapo ya uradidi. Pia, anafafanua kuwa inawezekana mwandishi akautumia urudiaji kama njia ya kulisisitiza au kuliweka jambo fulani wazi.

Kwa mujibu wa Mbatiah (2001), uradidi ni njia bora ya kulisisitiza jambo fulani na ni dhana muhimu katika uhakiki wa kimtindo. Mbinu ya urudiaji wa leksimu imetumika sana katika riwaya zote teule. Mbinu hii ni njia kuu ya kusisitizia jambo au maudhui.

Urudiaji ni njia ya kuimarisha ujumbe unaowasilishwa akilini mwa msomaji. Pia, urudiaji unaleta mshikamano katika kazi ya kifasihi.

Urudiaji unaonyesha kwamba mwandishi anafikiria sana jambo analolizungumzia kwa vile kwa kurudia, anadhihirisha mhemko mkubwa kuhusu jambo hilo. Kwa hiyo, urudiaji ni kiashiria muhimu ambacho msomaji anaweza kukitumia kutambua ujumbe, mtazamo, pamoja na kusudi la mwandishi la kutunga kazi fulani.

Akitumia mbinu ya urudiaji, mwandishi wa riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* anaendeleza motifu ya majaliwa katika riwaya hiyo. Mnyonge pamoja na mwenye mamlaka wote wanaamini kwamba hali zao zinatokana na majaliwa.

34. Sikiliza Mkongwe mwanangu, hayo ndiyo **majaaliwa** yangu. Kuna wengi Bwana Mungu **amewajaalia** na kuwatukuza mabwana wakubwa na wengi **amewajaalia** umaskini. Lazima ufahamu Mkongwe kama kila mtu ana **majaaliwa** yake. Hivyo ndivyo ulimwengu.
(Shafi, 1978, Ukur. 70)

35. Lakini ukitazama hayo ni kweli. Hawa mabwana shamba wanatutesa sana lakini hatuna la kufanya. Ndio **tulivyojaaliwa.**
(Shafi, 1978, Ukur. 26)

36. Sikiliza Bin Malik… hawa watwana wasikushughulishe akili yako; wa moja havai mbili. Wao **washajaaliwa** kuwa nyuma, watakuwa nyuma maisha yao.
(Shafi, 1978, Ukur. 35)

Kuna wafanyakazi katika mashamba ya mabwana shamba ambao wanaamini kwamba wao wamejaliwa unyonge, na mabwana shamba wamejaliwa kuwa na mamlaka. Kijakazi, pamoja na mfanyakazi mwingine aliyetajwa katika ni baadhi ya wafanyakazi wenye msimamo huu. Dhana hii ya majaliwa inaendelezwa na wenye mamlaka ambao ni watawala pamoja na mabwana shamba. Kulingana nao, jamii ina matabaka ambayo ndiyo mpango wa asili wa Mungu. Wao wanaona kwamba hata wale wa tabaka la chini la wanyonge wamekubali hali yao ya unyonge na uduni. Hata hivyo, kuna pia

wafanyakazi wengine ambao wana mwamko. Wao hawaamini kwamba unyonge wao ni majaliwa. Mfano wa wafanyakazi hawa ni Mkongwe, mfanyakazi mwenza wa Kijakazi. Mkongwe anaamini kwamba “hivyo sivyo ulimwengu wa leo ulivyo”, yaani hakuna aliyejaliwa umaskini na unyonge (Shafi, 1978, Ukur. 70).

Ingawa wenye mamlaka kiuchumi na kisiasa wanafikiri kwamba wanyonge wameikubali “nafasi yao”, wanatumia nguvu za vyombo vya usalama kuhakikisha kwamba wanyonge wanabaki katika nafasi yao duni, na wao wenye mamlaka wanabaki katika nafasi yao ya kupendelewa mpaka wanyonge wanapoungana na kutambua kwamba wanaweza kuiondoa hali hii inayowadunisha.

Hata hivyo, wafanyakazi wasioamini kwamba kuna wale waliojaliwa na kutukuzwa wanafanya uamuzi wa kuipinga dhana hiyo. Wanashirikiana na kuipindua serikali na kuleta mabadiliko makubwa ambapo rasilimali muhimu ya ardhi inagawiwa wakulima wote kwa usawa. Mfumo unaowanyonya wanauondoa. Wanamapinduzi sasa ndio wanaochukua mamlaka. Aliyekuwa mwenye nguvu na mamlaka (mabwana shamba na watawala) sasa ndio wanaogeuka wanyonge kabisa. Mabadiliko haya yanaidengua kabisa dhana ya majaliwa. Udenguzi huu unaonyesha kwamba kila mtu ana mamlaka fulani, pindi anapoamua kubadilisha mawazo yake na kuamini kwamba anaweza kufanya mabadiliko makubwa katika maisha yake.

Kupitia kwa mbinu ya urudiaji, waandishi wa riwaya teule wameibua maudhui ya msamaha. Msamaha ni nguzo muhimu katika Ukristo. Hii inadhihirika tukichunguza riwaya ya *Paradiso.*

37. [Mwenyezi Mungu] **anaposamehe husamehe** kabisa. Hakumbuki hata moja **alilosamehe**. ‘Ni wakati gani mtu anapaswa **kusamehe**?’ aliwaza. Labda anapomwomba Maulana ampe nguvu ya **kusamehe** na uwezo wa kudumisha **msamaha huo**.
(Habwe, 2005, Ukur. 209)

> 38. "Lakini **ulisamehe**?" wazo la kwanza lilikuja juu.
> **Ulisamehe** kwa nini una fundo bado?
> … Alikubali ni vizuri **kumsamehe** mwenzako kwani nawe hujui utakosa nini. Nawe ukikosa utahitaji **msamaha** kwani katika dunia hapana asekosa.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 210)

Katika madondoo ya 37 na 38, tunamwona mhusika Lydia akiona shida kumsamehe rafiki yake Patricia ambaye amemwingilia kwenye ndoa yake na Michael. Mwandishi ameibua maudhui kuhusu suala hili muhimu la msamaha katika Ukristo, kwa kurudiarudia neno '**samehe**' au '**msamaha**'. Kauli mbalimbali zimetolewa kuhusu msamaha na tena msamaha wa kweli. Ni wakati gani mtu anapaswa kusamehe? Ujumbe ni kwamba ukimsamehe mtu usiendelee kuwa na fundo moyoni, yaani ukimsamehe, umsamehe kabisa. Ni vizuri kumsamehe mwenzako kwani na wewe huenda ukakosea na ukahitaji msamaha. Lydia anatambua kwamba duniani hakuna asiyekosa. Kwa hiyo, mwandishi amechimuza ujumbe huu kuhusu umuhimu wa msamaha kwa kurudiarudia neno '**kusamehe**' au '**msamaha**'. Ingawa kwa kawaida kurudiarudia huku kungemchosha msomaji, msisitizo wa aina hii unamfanya msomaji akumbuke na azingatie ujumbe muhimu kuhusu 'msamaha' wa kweli. Msamaha ni njia mojawapo ya kudumisha amani katika mahusiano ya mtu na mtu na tena katika jamii nzima, kwa vile hasira na chuki vinaweza kuleta madhara makubwa katika jamii. Hii ni dhima mojawapo ya dini anayoiangazia Habwe katika riwaya ya *Paradiso*. Hata hivyo, katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* tunaona jinsi ambavyo Richard, ambaye ameokoka, anashindwa kumsamehe mkewe Mary Kasiva kwa kuzaa mtoto ambaye si wake.

Urudiaji pia umetumiwa kuibua maudhui kuhusu mahusiano ya kijinsia. Katika riwaya ya *Paradiso* mwanamke amerejelewa kwa njia hasi na baadhi ya wahusika. Baada ya kutengana na Lona, Bwana Mganga, aliyekuwa mumewe anawachukia wanawake kabisa. Anachukulia kwamba wanawake wote ni wabaya.

> 39. Bwana Mganga hakutaka tena kuoa mke mwingine. Aliwaona **wanawake** kama vinyonga. Walibadilika kulingana na mazingira. Alipofikiria kuwa mama yake ni **mwanamke** pia ilimsikitisha. Kwani alikosa imani nao wote! Pale alipofanya kazi alikuwa na shida ya kutengana na **wanawake**. Ni kama kila **mwanamke** aliyemwona alikuwa kama Lona. Bosi wake alikuwa **mwanamke**. Lakini alikuwa mpole na msikivu. Mganga hakutaka kumsikiliza sana.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 71)

Fikira ya wanaume kama Mganga inatokana na wao kujiona kama wenye mamlaka kiasilia, wakimchukulia mwanamke kama kiumbe dhaifu. Ndio maana mwandishi anataja kwamba bosi wake Mganga alikuwa mwanamke. Mganga anawakilisha wanaume wenye mtazamo hasi kuhusu wanawake. Mganga anawachukia wanawake kwa sababu ya kuvunjwa moyo na mwanamke mmoja. Anajumlisha kwa kukosa imani na wanawake wote. Kwa njia ya kuonyesha msimamo mkali wa Mganga (na wanaume kama yeye), mwandishi amerudiarudia neno '**mwanamke**' au wingi wake '**wanawake**' mara kadhaa. Msimamo wa Mganga ni mkali mno kiasi kwamba anajutia kuzaliwa na mwanamke, kitu ambacho ni cha kimaumbile. Kwa kumsawiri mhusika huyu akiwa na msimamo kama huu, ni kama kwamba mwandishi anataka kuonyesha udhaifu wa fikira kama hiyo ya mtu kujutia kuzaliwa na mwanamke, kwani angezaliwa na jinsia ipi? Ni kama anapinga maumbile.

Kupitia mbinu hii ya urudiaji, mwandishi pia ameibua maudhui kuhusu jinsi utamaduni unavyomkandamiza mwanamke. Katika tamaduni mbalimbali, mwanamke ndiye anayewajibika kuhusu nidhamu ya watoto, hasa wasichana. Ni dhahiri katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* kwamba Mary Kasiva amefungwa na matarajio haya. Anaona kwamba yeye ndiye anawajibika kuwashauri binti zake kuhusu matarajio ya jamii na utamaduni wa jamii hiyo kuhusu mtoto wa kike. Mume wake (Richard) ni mkali sana, na anamtia hofu, kwa vile yeye Richard ni pasta ambaye analenga kuwa na familia ya Kikristo isiyo

na doa. Anamkandamiza sana mkewe kiasi kwamba mwanamke huyo anahofia madhara kumfika akipatikana lawamani na mume wake. Hofu hii anaionyesha hata mbele ya binti zake.

40. "Utamweleza nini **babako**? aliniuliza mama.
(Wamitila, 1999, Ukur. 22)

41. "**Babako** akijua atasema nini?" aliuliza mama.
"Hamna ubaya lakini **babako** hapendelei mambo hayo," alisema mama hatimaye.
"Mwanangu **babako** anahofu kusemwa na watu. Kumbuka ni kiongozi wa kanisa. Je, watu watamfikiria nini wakisikia watoto wake wa kike hulala nje?" alieleza mama.
(Wamitila, 1999, Ukur. 186)

42. "Usifanye tendo kama hilo bila ya ruhusa ya **babako**," alisema akimwelekezea Roselyn.
(Wamitila, 1999, Ukur. 187)

Katika mazungumzo haya neno **babako** limerudiwarudiwa ili kuonyesha jinsi ambavyo mwanamke hana mamlaka katika familia. Ingawa Mary haoni shida kuhusu binti yake Roseyn kwenda matembezini, anamwambia binti yake kwamba asifanye hivyo bila ya ruhusa ya baba yake kwa vile babake ndiye atasemwa. Mary anatumia nafsi ya tatu kuonyesha kwamba yeye hana mamlaka yoyote kuhusu kuwakubalia mabinti zake kwenda matembezini. Badala ya kusema 'watu watatufikiria nini' (kama wazazi) au 'watu watanifikiria nini', anasema 'watu watamfikiria nini', kana kwamba yeye siye mzazi pia. Ni kama kwamba watoto ni wa baba (mwanamume). Richard anachukulia kwamba yeye ndiye sura ya familia yake ya Kikristo isiyo na doa. Hali hii inatuonyesha makutano kati ya jinsia, dini, utamaduni na mamlaka.

Neno '**babako**' limerudiwarudiwa katika sehemu nyingine ya riwaya hii ili kudhihirisha ubinafsi wa Richard. Richard Ngunze amesawiriwa kama mtu mwenye ubinafsi mwingi. Ingawa yeye anasisitiza umuhimu wa 'nguvu ya sala' au mafundisho ya Biblia, ameonyeshwa kuwa ni mtu anayejifikiria zaidi. Hii inadhihirika wakati binti

yake Susan anapowaaga wazazi wake akiwa anaondoka kwenda kujiunga na shule ya sekondari.

> 43. "Kumbuka huko utakutana na wasichana wa kila aina," alieleza mama.
> "Jitunze vizuri mwanangu ili **usiniaibishe mimi**," alisema baba.
> "Mm! mwanangu jitahidi **usimwaibishe babako**," alisisitiza mama.
> "Kuwa kielelezo kizuri na kumbuka kuwa jamii nzima ime***ni***kodolea macho **mimi babako**!" alimalizia baba.
> (Wamitila, 1999, Ukur. 61)

Katika dondoo la 43, tunaona kwamba mama ndiye anayetangulia kutoa mawaidha kwa binti yake, kabla ya baba kuingilia kati. Lakini, hata kama wazazi wote wawili wanatoa ushauri, Richard anatoa kauli zinazomrejelea yeye peke yake, kwa msisitizo fulani. Badala ya kusema tu **usiniaibishe** tu au hata usituaibishe, Richard anasisitiza umuhimu wake kama kiongozi wa familia kwa kuongezea neno '**mimi**', ambalo lisingehitajika katika muktadha huu. Tena anasema: 'jamii nzima imenikodolea macho '**mimi babako**'. Haya ni maelezo ya ziada yanayothibitisha ubinafsi wake. Ingawa mama ndiye anayetangulia kutoa ushauri kwa binti yake, hana budi kusisitiza tu maneno ya mume wake (baba yake Susan) ambaye anaonyesha dhahiri kuwa yeye ndiye ana mamlaka kuhusu binti zake kuliko mama yao. Richard anataka kauli yake ndiyo ipenyeze zaidi. Hivyo, mama naye hana budi kusisitiza maneno ya mumewe kwa kusema: "usimwaibishe **babako**" kwa vile mumewe amejitokeza kwa nguvu ya maneno ya kusisitiza mamlaka yake kama baba, na kiongozi wa familia. Katika tamaduni mbalimbali, baba ndiye anayetambulika kama kiongozi wa familia. Hata hivyo, katika nyumba ya Richard, kuna karatasi lililobandikwa ukutani lenye maneno yanayomtaja Kristo kama kiongozi wa nyumba hiyo. Hii inamaanisha kwamba, kusema kweli, katika kaya yenye msingi wa Kikristo, Kristo ndiye kiongozi halisi wa kaya hiyo.

Ingawa katika dondoo hili la 37 neno ‘**babako**’ limerudiwa mara mbili, tunaona kwamba katika muundo wa ndani neno hili limerudiwa mara tatu, kwa vile limeashiriwa katika maneno ya Richard anaposema: “usiniaibishe mimi.” Katika muundo wa ndani tungo hiyo ni: “usiniaibishe mimi [**babako]**.” Lakini katika tungo hii, neno hili ‘babako’ limedondoshwa, labda kwa kusudi la kusisitiza neno ‘mimi’ ambalo linakuwa mwishoni mwa kauli ya Richard. Kulifanya neno ‘mimi’ lije mwishoni mwa kauli ya Richard kunasisitiza ubinafsi wake, na mamlaka yake kama mwanamume na tena baba. Tunajua kwamba neno hilo limedondoshwa kwa vile mke wake analitumia katika jibu lake anaposema: “usimwaibishe **babako**.” Hivyo, urudiaji unaweza ukaashiriwa tu katika muundo wa nje.

Msimamo wetu kuhusu urudiaji wa neno ‘babako’ unaungwa mkono na mtazamio anaoutumia mwandishi kuhusu wahusika hawa wawili. Mama anasisitiza tu maneno ya mumewe: “…usimwaibishe babako,” **alisisitiza** mama. Ingawa kuna kauli zingine zinazotolewa na wahusika ambazo hatukuzinukuu kwa vile tulilenga mbinu ya urudiaji, tunaona kwamba mama ndiye anayeanzisha mazungumzo haya ya kumshauri binti yao. Baba anafuata tu mkondo kwa kuchangia, kusisitiza au hata kumkata mama kauli. Ingawa mama ndiye anayeanzisha juhudi hii ya kutoa mawaidha kwa Susan, baba ndiye anayetaka anajipa kipaumbele, kwa kuonyesha mamlaka yake kama mwanamume. Ndiye anayehitimisha mazungumzo haya ya mawaidha, ingawa siye anayeyaanzisha: “…kumbuka kuwa jamii nzima imenikodolea macho ***mimi babako***!” **alimalizia** baba. Hapa tunaona jinsi mwandishi anavyoangazia suala la jinsia. Anamwimarisha mhusika wa kike (Mary Kasiva) kama mtu anayewajibika zaidi kwa kuanzisha mazungumzo haya muhimu, na mume wake anafuatilia tu kwa kuchangia yale ambayo mama anasema. Mwandishi anadhihirisha taasubi ya kiume aliyo nayo Richard kwa vile anavyopenyeza mazungumzo na kuonyesha udume wake kama mtu mwenye mamlaka

zaidi katika familia. Mwanamke amesawiriwa kama kiumbe mnyonge kwenye familia anayeonewa na mwanamume.

Wamitila ametumia urudiaji kuonyesha uwezo wa mwanamke. Anachangia harakati za mwanamke za kujikomboa na kutafuta usawa. Tofauti na mhusika Mary Kasiva, ambaye ni mke tu wa nyumbani, binti yake Susan na wanafunzi wenzake wa kike wanawakilisha mwamko mpya wa mwanamke anayejiendeleza kimasomo. Kwa hivyo, tunaona jinsi mwandishi alivyowaimarisha wanawake kupitia mbinu ya urudiaji. Hili linadhihirika tukichunguza mawazo ya Susan:

44. Nilikuwa na tamaa ya kufuzu na kuingia chuo kikuu mwakani. **Hamna** msichana yeyote ambaye alishajiunga na chuo kikuu kutoka kijiji cha Misombe.

Sio wasichana peke yao hata wavulana pia; **hamna** hata mmoja aliyewahi kujiunga na chuo kikuu.
(Wamitila, 1999, Ukur. 119**)**

45. Fauka ya kusimuliana visa na vitushi mbalimbali tulijadili masuala fulani kuhusu Fasihi. Hili ndilo somo nililolipenda sana, **hamna** mwanafunzi aliyenishinda katika darasa letu. Somo lililonitatiza ni somo la Hisabati. **Hamna** aliyemshinda Kate katika somo hili.
(Wamitila, 1999, Ukur. 123**)**

Katika madondoo haya, mwandishi anarudiarudia kitenzi kanushi '**hamna**' ili kuchimuza uwezo wa wasichana – kimasomo. Anawapiku wasichana na wavulana na kujiunga na chuo kikuu. Kwa kusema kwamba, "sio wasichana peke yao hata wavulana" mwandishi anasisitiza uwezo wa msichana huyu, kwa vile inaonekana kwamba kwa kawaida wavulana ndio huonyeshwa kuwa na uwezo zaidi kimasomo kuliko wasichana. Mwandishi anaonyesha uwezo wa msichana mwingine, Kate, katika masomo. Wakati ambapo Susan anawashinda wasichana wote katika somo la fasihi, Kate anawashinda katika somo la Hisabati. Haya ni masomo ambayo huchukuliwa

kuwa ni magumu. Kwa kuonyesha uwezo wa wasichana hawa wa kufanya vizuri katika masomo ‘magumu’, mwandishi anamwimarisha mhusika wa kike na kwa njia fulani kumpa mamlaka.

Maudhui ya ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana, upendeleo, na ufisadi ni masuala yanayoangaziwa katika riwaya teule kupitia kwa mbinu ya urudiaji wa leksimu. Katika riwaya ya *Asali Chungu* tunawaona vijana Dude na Bushiri ambao wanaishi maisha mabovu kwa sababu ya kukosa ajira. Vijana hawa ni “miongoni mwa maelfu ya vijana wanaotafuta kazi na hatimaye kuzurura ovyo majiani na kuhunika.” Kazi anayoipata Dude ni ile ya ‘kupara magondi’ kwa Shaaban Supu. Mwandishi amelimulika tatizo hili la ukosefu wa kazi kwa kurudiarudia neno ‘kazi’.

> 46. Kukosa **kazi** kulikuwa kwingi kuliko kupata, na hata kama kijana mmoja alipata, ilikuwa **kazi** ya kuosha vyombo, kupika au kufagiafagia kwa Wahindi; au pengine iliwabidi wawe wapagazi au wapara samaki Forodha ya Papa. **Kazi** hizi hakuna iliyomfaa Dude, ingawa kwa uhitaji aliokuwa nao hangezionea taabu kama angezipata. Kwa hivyo akawa mmoja wa wale vijana waliobaki kuzurura wanatafuta **kazi**, mpaka siku moja akakata tamaa.
> (Mohamed, 1977, Ukur. 65)

Urudiaji wa leksimu ‘kazi’ katika dondoo la 46 umetumiwa na mwandishi kuzijenga kauli mbalimbali kuhusiana na tatizo hili la ukosefu wa kazi. Kuna kauli inayotaja shida yenyewe, yaani ukosefu wa kazi. Kauli nyingine inataja kazi duni zinazopatikana kwa vijana wanaotafuta ajira. Kauli ya tatu inataja kwamba hata hizo kazi duni hazipatikani. Kauli ya mwisho inataja hali ya vijana kukata tamaa kwa sababu ya kukosa kazi.

Zaidi ya tatizo la ukosefu wa kazi, kuna upendeleo wa ndugu katika ofisi ya Leba wanapowaajiri watu. Ofisa wa Leba, ambaye anahusika na shughuli ya kuwatia watu kazini ni Baniani anayewapendelea jamaa zake wa Kihindi.

> 47. Mara nyingi aliwatia kazini jamaa zake wa Kihindi au yeyote aliyeweza kumpa tonge.” **Kazi** njema zikawa za mabwana na matajiri; kina Dude mara nyingi wakiangukia utopasi. Na hata

> hizo za utopasi, huweza kupita mwaka mzima mtu anakwenda akirudi bila kupata lolote, ila kuwaona wale waliokuja mwisho wanatoka ofisini na furaha, wamekwisha pata **kazi**.
> (Mohamed, 1977, Ukur. 66)

Katika dondoo hili, neno kazi linajitokeza pia, na limerudiwa mara mbili. Maudhui yanayojitokeza kuhusiana na urudiaji huu ni upendeleo uliopo katika kuzigawa zile kazi chache zinazopatikana. Ofisa wa Leba anayezigawa kazi hizi ambaye ni Baniani anazigawa kazi kwa jamaa zake wa Kihindi. Pia kuna maudhui ya ufisadi ambapo wanaomhonga Baniani ndio wanaopata kazi. Akina Dude wanaachwa wakizurura kutokana na kutokuwa na hata pesa za kumhonga huyo Baniani kwa sababu hawana kipato chochote, na ndio maana wanatafuta kazi.

Hali ya ukosefu wa ajira ni mbaya sana kiasi kwamba hata kazi za utopasi. Vijana kushindwa kupata hata kazi ya utopasi, na wengine kutoa hongo (imedokezwa) na kufurahi kwa kuzipata kazi za aina hiyo ni kinaya kwa vile kazi kama hizo ni duni sana, sio kazi za kushindaniwa. Ni kinaya kinachoonyesha kuwa tatizo hili la ukosefu wa ajira kwa vijana ni kubwa sana nchini. Ukosefu wa ajira unapelekea matatizo mengine kama vile uhalifu, kutumia nguvu, na unyonyaji.

Upendeleo wa Wahindi katika kuwatia watu kazini unamfanya Dude akate tamaa na kumhujumu Mukri, kitendo kinachomfanya afungwe miaka miwili na kumwacha Mukri akiendelea "kugawa kazi kwa aliowapenda…" (Mohamed, 1977, Ukur. 66). Anapoachiliwa kutoka gerezani, Dude anakuwa mtu ambaye amekata tamaa zaidi kuhusu kupata kazi.

48. "Hisia zake za ulimwengu… zimebadilika sana. Sasa moyo wake umehodhi chuki… Hatamani **kazi** kwa mtu yeyote zaidi ya ile [**kazi**] ya kupara magondi kwa Shabaani Supu."

    Kazi! **Kazi** gani itakayotafutwa tena na Dude? Labda sasa **kazi** imtafute yeye. Lau kama Bushiri anamwita yeye kwa **kazi**, basi

> angeliweza kuifikiria **kazi** hiyo; maana imemjia, hakuiendea. **Kazi** kwa wanyonge kama yeye, na lile darasa lake la sita alilomaliza?
> (Mohamed, 1977, Ukur. 67)

Dondoo la 48 linaelezea hali ya kukata tamaa kabisa inayowakumba vijana kwa sababu ya kushindwa kupata kazi za maana. Hali kama hiyo inawaweka vijana katika hali ya kuweza kudhuriwa na watu wengine. Inamfanya Dude awe tayari kuingia katika mtego wa watu kama Bibi Amina, ambao wanawatafuta vijana kama Dude wa kuwafurahisha kimapenzi. Kwa hivyo, Bushiri anapomjia na pendekezo la kazi, Dude yuko radhi tu kuifanya kazi hiyo bila kusita, mradi kazi hiyo inampatia riziki.

Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* tunapata maudhui ya unyonyaji wa wafanyakazi wanyonge. Wafanyakazi kama Kijakazi wanafanyishwa kazi nyingi sana bila hata kupumzika. Msisitizo wa kazi tunauona pale ambapo msichana mwingine (Mkongwe) analetwa kuja kufanya kazi pamoja na Kijakazi.

49. **Kazi** aliyokuwa nayo Mkongwe hapo shambani kwa Fuad ilikuwa ni kushirikiana na Kijakazi katika **kazi** zake. Kwa hakika hakuajiriwa ili amsaidie Kijakazi na kupunguza mzigo wa **kazi** nyingi alizokuwa nazo, bali kuwa pamoja naye ili **kazi** ifanyike kwa wingi zaidi.

    Kazi za Kijakazi zilikuwa kama kawaida, moja baada ya moja bila mapumziko.

50. Kijakazi mbona unafanya **kazi** namna hii? Hivi utajiua kwa **kazi**. Halafu unapata faida gani hasa kujivunja kwa **kazi** namna hii? Mkongwe aliuliza.

    (Shafi, 1978, Ukur. 17)

Katika madondoo haya, neno **'kazi'** limerudiwarudiwa kama njia ya kusisitiza jinsi watumishi wa Fuad wanavyofanya kazi kipunda. Wanafanya kazi moja baada ya nyingine, bila kupumzika. Hii ni kwa manufaa ya kabaila Fuad ambaye hawajali hata kidogo.

Tunaona jinsi ambavyo mnyonge anavyochangia unyonyaji wake na kabaila. Ingawa Mkongwe anautambua unyonyaji huu, Kijakazi anachukulia kwamba kufanyishwa kazi namna hiyo ni majaliwa yake.

> 51. "Siku zote nimekuwa hivi! Sasa hata sihisi kama ninafanya **kazi** kwa sababu nimelemaa kufanya **kazi** namna hii," Kijakazi alijibu.
> (Shafi, 1978, Ukur. 18)

Hapa tunaona kwamba mnyonge ameizoea hali yake ya unyonge na hatambui kwamba ananyonywa na bwana shamba, hata kama mtumishi mwenzake anajaribu kumwelezea kuhusu unyonyaji huo. Mkongwe anamwelezea Kijakazi jinsi ambavyo Fuad ni "mwizi wa nguvu za watu." Ni kinaya kwamba kinachomfurahisha mnyonge ni kusifiwa na kabaila kwa kufanya kazi nyingi kipunda. Kijakazi hatambui jinsi wafanyakazi wanavyonyonywa na bwana shamba Fuad. Unyonyaji huo anautambua baadaye sana wakati akili yake inapoanza kufikiria hali yake. Mwishoni anautambua unyonyaji huo na anabadilika kabisa kimawazo.

Shafi Adam Shafi ametumia mbinu ya urudiaji kusawiri maudhui ya mabadiliko ambapo aliyekuwa mnyonge amebadilika na kutambua unyonge wake. Kijakazi anaanza kubadilika anapotambua kwamba mambo yameanza kubadilika nchini, na Fuad hana mamlaka kama aliyokuwa nayo awali. Anakataa kuzitii amri za Fuad, ambaye anashangazwa na kile ambacho kimetokea – kwamba Kijakazi anathubutu kukataa kutii amri zake. Tofauti kati ya hali ya awali na mabadiliko ambayo yanatokea inaashiriwa na urudiaji wa neno '**leo**.'

> 52. "Unasema nini?" **Leo** wewe unakataa kutii amri yangu," Fuad alimkaripia Kijakazi…
>
> "Ama **leo** Kijakazi umefurutu ada! Wewe **leo** unathubutu kuvunja amri yangu na kunieleza maneno kama hayo? Hujapata hata siku moja kufanya utovu wa adabu kama hii **leo**! **Leo** ng'ombe wewe unathubutu kuniasi?
> "Mimi… sitopiga magoti tena mbele yako," alisema Kijakazi…

> **Leo** Kijakazi aliazimia kweli na makelele ya Fuad hayakumshtua hata kidogo.
> "Zaidi ya miaka hamsini sasa umekuwa shambani hapa pamoja na sisi… **Leo** hii unata…
> Fuad aliona **leo** kweli imemdhihiri na Kijakazi si wa kuchezewa tena.
> (Shafi, 1978, Kur. 90 - 93)

Neno '**leo**' limerudiwarudiwa mara kadhaa kuakisi mabadiliko ambayo yanatokea nchini. Neno 'leo' linaashiria mwamko kwa mnyonge ambaye anatambua kwamba naye sasa ana mamlaka fulani. Mnyonge wa awali (Kijakazi) hata anathubutu kumwambia mkubwa wake (Fuad) amkande miguu, yaani bwana amkande mtumwa miguu. Mwandishi anaelezea mabadiliko haya ambapo mwenye mamlaka (Fuad) amepoteza mamlaka yake, na ndio anaanza kung'amua hali mpya iliyopo sasa.

Wanyonge wanafanya mapinduzi ya serikali na kuwapokonya mabwana shamba mamlaka. Fuad, mtu ambaye awali alikuwa na mamlaka makubwa sasa ni mnyonge kabisa. Anajikuta hana la kufanya kuhusu mabadiliko yanayoendelea nchini. Wanamapinduzi sasa wanakuja kwake na kufanya wanavyotaka, na yeye hawezi kuwazuia.

53. **Pale pale** watu walitoka na kumwacha Fuad amekaa **pale** ukumbini. Alibakia **pale pale** juu ya kiti amepigwa na bumbuazi hajui la kufanya. Hamaki zilikuwa zimemjaa lakini alizidiwa nguvu. Usiku ulikuwa umekwisha ingia na Fuad aliwasha karabai na baadaye akarejea **pale pale** alipokuwa amekaa juu ya kiti.
    (Shafi, 1978, Ukur. Kur. 79 - 80)

Katika dondoo hili, urudiaji wa fungu la maneno '**pale pale'** unaonyesha unyonge anaouhisi Fuad, baada ya kupoteza mamlaka yake kwa kunyang'anywa ardhi yake. Baada ya kunyang'anywa ardhi yake, Fuad anakaa pale ukumbini mwake akiwa amezidiwa na nguvu na hajui la kufanya. Wanamapinduzi wanapoondoka anabakia tu pale ukumbini. Fungu la maneno '**pale pale**' limetumiwa kuashiria hali ya Fuad ya kukwama kabisa. Baada ya kupoteza ardhi yake na kuambiwa kulima mwenyewe Fuad

sasa amekwama kabisa. Aliyekuwa bwana shamba kuambiwa kulima mwenyewe ni mageuzi makubwa ambayo Fuad hawezi kuyavumilia. Aliyekuwa na mamlaka sasa hana mamlaka yoyote. Hii inaashiria kwamba mamlaka hayadumu. Mwenye mamlaka anaweza akayapoteza; naye mnyonge anaweza akapata mamlaka.

Mwandishi wa riwaya ya *Paradiso* anaangazia tatizo la wachungaji kutokuwa mfano mzuri kwa jamii. Jambo hili linadhihirika katika mienendo ya wachungaji hawa. Kuna visa vya mapenzi nje ya ndoa miongoni mwa wachungaji. Mhusika mmoja anayetajwa ni Kasisi Lona, mkewe Askofu Joshua. Joshua anawazia maneno ya binti yake Nice kumwambia kuwa yeye siye baba yake:

> 54. **Labda** ni kweli. **Labda** si kweli. Ni nani ajuaye? **Labda** mamake anajua. **Labda** ndiye aliyemweleza. **Labda** mtoto anaropokwa.
> (Habwe, 2005, Ukur. 86)

Nice kumwambia Askofu kwamba yeye siye baba yake inaashiria kuwa Lona hakuwa mwaminifu. Wasiwasi wa Joshua unadhihirika katika matumizi ya kielezi '**labda**'. Lakini fikira inamjia kwamba huenda Nice alikuwa anaropokwa tu. Hapo nyuma Joshua anamwambia Lona kwamba Nice si mtoto mdogo wa miaka minne. Kwa hiyo maneno yake Nice ni ya kuchukulia kwa makini. Katika dondoo la 108, inatajwa dhahiri kwamba wote (mke na mume) walikuwa sio waaminifu. Kwa hiyo, kuna uwezekano mkubwa kwamba maneno ya Nice ni ya kweli. Hii ni ithibati kuwa Lona, anafanya uzinzi. Tena hii inaashiria kwamba kauli ya mhubiri katika *Nguvu ya Sala* kwamba uzinzi ni miongoni mwa vitendo visivyo vya kimaadili ambavyo vimekithiri katika jamii ni ya kweli. Mhubiri anasema,"Uzinzi umeongezeka …" (Wamitila, 1999, Ukur. 153). Waandishi wawili (John Habwe na Kyallo Wadi Wamitila), ambao wanaandika kuhusu jamii ileile (Kenya) inaonekana wanawiana katika ujumbe wao kuhusu vitendo vya kimapenzi visivyo vya kimaadili. Vitendo vya wachungaji visivyo vya kimaadili

vinaenda kinyume na mafundisho ya dini ya Kikristo. Vinaonyesha jinsi ambavyo wameshindwa kuidhibiti mienendo yao.

Mwandishi amewaumba kimaksudi baadhi ya wahusika wa kike wakiwa na mamlaka. Mfano ni mhusika Lona ambaye anashikilia nafasi ya ukasisi katika kanisa la New Jerusalem. Lona ana ushawishi katika maamuzi muhimu kanisani. Ni kama kwamba anadhibiti kila kitu katika kanisa hilo:

55. Lona sasa ndiye **aliyedhibiti** mamlaka ya New Jerusalem.
(Habwe, 2005, Ukur. 120)

56. Hakuna tena kilichomtisha Lona. Tayari **amemdhibiti** mumewe. **Alidhibiti** uchumi. **Aliwadhibiti** waumini. Sasa **alidhibiti** siasa za nchi. Maana hata rais wa nchi alimfahamu. Si muhali kumwona akitumika siku za holidei akiomba au kama amekaa na wakubwa wa serikali huku kajipamba lile joho… Hata kama Lona **alidhibiti** kila kitu, kuna kitu kimoja tu **hakukidhibiti** nacho ni wakati na ahadi yake kwa Bwana.
(Habwe, 2005, Ukur. 131)

Mwandishi amerudiarudia neno '**dhibiti**' kusisitiza mamlaka aliyo nayo Lona. Anadhibiti mamlaka katika kanisa, anamdhibiti mume wake, na anadhibiti uchumi, waumini, na hata siasa za nchi. Huyu ni bibi anayejua anachokitaka na anakitafuta na kukipata. Yuko tayari kufanya lolote ili kudhibiti vitu vinavyotimiza maslahi yake. Hii ndiyo sababu anaenda kwa mganga wa kienyeji ambaye anampa dawa ya kumfanya mume wake awe zuzu, ili aweze kumdhibiti zaidi.

Lona anajipenyeza kwenye siasa za kitaifa ili awe na ushawishi huko pia. Uhusiano wake na wanasiasa unamletea manufaa kwa njia ya misaada ya pesa kwa kanisa, cheo na umaarufu kwa vile yeye ndiye anayeitwa kutoa sala katika "siku za holidei". Kwa jumla, tunamwona mhusika mwanamke ambaye amepewa uwezo mamlaka makubwa kuliko wanaume wengi. Hata hivyo, mwandishi anaelekea kuonya watu kama Lona kwamba mtu hawezi kudhibiti kila kitu, kwani hawezi kudhibiti wakati na ahadi kwa

Bwana. Lona anakumbushwa kufikiria ahera ya baadaye. Siku moja, wakati akisoma Biblia anaulizwa swali: *"NI NANI ATAKAYEKAA HEMANI MWA BWANA?" (*Habwe, 2005, Ukur. 130). Mwandishi amelichimuza swali hili kigrafolojia kwa kuliandika katika herufi kubwa. Mwandishi anatueleza kwamba *Lona alijitathmini akaona hawezi hata chembe* (msisitizo wa herufi mlazo ni wa mwandishi). Hiki ni kinaya kwa vile viongozi wa kidini ndio wangekuwa katika msitari wa mbele kwenda ahera ya baadaye. Lakini badala ya viongozi hawa kulenga ahera, wao wanalenga ahera ya hapa duniani, kwa kudhibiti vitu vya dunia. Kwa hivyo, tunajifunza kwamba mamlaka ya binadamu yana kikomo, tofauti na mamlaka ya Mungu. Mwandishi anataka wenye mamlaka wakumbuke jambo hilo.

Mwandishi wa *Paradiso* pia anaibua maaudhui ya tamaa ya uongozi na mamlaka miongoni mwa wachungaji. Mchungaji Boribori, binamu yake Askofu Joshua, anaona kwamba hana mamlaka na ushawishi katika kanisa la New Jerusalem. Mamlaka na udhibiti vimeshikiliwa na Lona na mumewe, Askofu Joshua. Kwa hiyo, ili naye awe na mamlaka, anapanga kuanzisha kanisa lake mwenyewe, akalidhibiti. Neno 'dhibiti' limetumika katika taarifa kuhusu kusudi la Boribori:

57. Fununu zilisambazwa na wadhabidhabina kuwa Boribori angefungua kanisa lake ili naye **akalidhibiti**, atoe wa kutoa na kuchomeka humo ndani wa kuchomeka.
(Habwe, 2005, Ukur. 137)

Ni wazi kwamba baadhi ya makanisa yanaanzishwa sio kwa misingi ya injili ila kwa misingi ya utashi wa mamlaka. Kusudi la Boribori la kutaka mamlaka limeonyeshwa kwa matumizi ya neno '**ili**.' Hii inaashiria kwamba dini inatumiwa kama njia ya kupata mamlaka. Boribori anataka kuwa na udhibiti kamili ambapo sasa ataweza kufanya anachotaka. Kwa vile yeye ni mchungaji anayependa mali, inaonekana kwamba lengo lake ni kudhibiti pesa za kanisa.

Katika riwaya ya *Paradiso*, urudiaji umetumika kuonyesha jinsi ambavyo makanisa ya kiprotestanti yameacha msingi wa kutafuta paradiso ya baadaye na badala yake makanisa hayo yanakuwa na mikakati ya kuingiza pesa zaidi tu. Kutokana na ongezeko la idadi ya waumini wanaotafuta masuluhisho kwa changamoto za maisha yao, ibada kadhaa katika kanisa la New Jerusalem sasa zinapangwa:

> 58. Kanisa la new Jerusalem liliendelea kukua. Sasa hivi lilkuwa na washiriki elfu tano waliohudhuria **ibada** tatu mbalimbali. **Ibada** ya saa kumi na mbili… **ibada** ya saa tano… **ibada** ya saa saba.
> (Habwe, 2005, Kur. 42 - 43)

Mwandishi amerudiarudia neno **ibada** kwa njia ya kuliwekea mkazo ili msomaji ahisi wingi wa ibada katika kanisa la New Jerusalem. Msomaji anahisi kwamba ibada kadhaa zinapangwa. Dondoo la 58 linaonyesha jinsi makanisa yanavyozidisha kipato kutokana na ibada hizi. Lakini ibada hizi kadhaa hazipangwi kwa ajili ya kueneza injili na kuwawezesha kondoo (yaani waumini) kufika paradiso ya baadaye, bali ni njia ya kuingiza matoleo au pesa zaidi. Ni ishara ya tamaa ya pesa ambayo mwandishi anaikemea.

4.2.7 Matumizi ya Msamiati wa Kitathmini

Katika kipengele hiki tunachunguza msamiati uliotumiwa na waandishi ambao unaonyesha mitazamo yao kuhusu wahusika. Tukizingatia mtazamo wa msimulizi na wahusika wengine tunapata maudhui mbalimbali kuhusu dini na mamlaka. Mtazamo huu unaweza kuwa chanya au hasi.

Akitumia msamiati wa kitathmini, Habwe anasawiri maudhui ya utashi wa madaraka miongoni mwa wachungaji. Boribori ni miongoni mwa wachungaji ambaye analenga kufungua kanisa lake ili akalidhibiti mwenyewe. Hili linadhihirika katika dondoo la 57, ambalo limekwisharejelewa katika sehemu 4.2.5.

> [57] Fununu zilisambazwa na wadhabidhabina kuwa Boribori angefungua kanisa lake ili naye akalidhibiti, **atoe** wa kutoa na **kuchomeka** humo ndani wa kuchomeka.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 137)

Katika dondoo la 57, tunaona jinsi ambavyo mwandishi ametumia msamiati hasi anaposema: [Mchungaji Boribori] "**…atoe… na kuchomeka**." Hapa tunapata picha ya mchungaji ambaye anafanya uamuzi kulingana na matakwa yake, siyo nia ya kuendeleza injili. Neno "**kuchomeka**" linaashiria kulazimisha tu, siyo kwa sababu kitu kinafaa. Boribori anataka kudhibiti mamlaka ya kanisa ili afanye atakavyo yeye; atoe na kuchomeka amtakaye katika nyadhifa mbalimbali kanisani. Akiwa na mamlaka hayo, waumini wataogopa kumpinga kuhusu jambo lolote. Kwa kutumia msamiati huu hasi, mwandishi anaonyesha kwamba yeye hakubaliani na mpango wa Boribori unaoonyesha tamaa ya uongozi na madaraka, badala ya kufikiria huduma ya injili kwa waumini na jamii kwa jumla.

Kupitia kwa msamiati wa kitathmini katika riwaya ya *Paradiso* suala la injili ya utajiri linachimuzwa. Makanisa mengi, badala ya kusisitiza mabadiliko ya mienendo ya watu, yanasisitiza utajiri, kinyume na mfano ulioonyeshwa na Kristo, kwa vile yeye hakuwa na mali yoyote (Habwe, 2005, Ukur. 44).

59. **Sasa** injili **iliyovuma** New Jerusalem ilikuwa ya maendeleo ya kiuchumi.

    Askofu Joshua **alikashifu** mtu yeyote aliyeendelea kuja kanisani na Mungu Baba hajampa **gari** au kumzawadisha **kana kwamba** injili na utajiri ni mambo yaliyofungamana.

60. **Yeyote** aliyetaka utajiri wa haraka **alikimbilia** injili.

    (Habwe, 2005, Ukur. 220)

Katika madondoo ya 59 na 60 mwandishi anatuonyesha mtazamo wake kuhusu injili ya maendeleo. Anafanya hivi kupitia kwa msamiati na kauli mbalimbali. Katika dondoo la 59, mwandishi anatumia neno '**sasa**' kuonyesha kwamba awali injili haikuhubiriwa

kwa lengo la kujiendeleza kiuchumi. Kitenzi '**iliyovuma**' kinatumika kurejelea iliyoshika kas katika kanisa la New Jerusalem**.** Anatumia kitenzi hicho '**iliyovuma**', kisitiari badala ya kusema '**iliyohubiriwa'** ili kuchimuza jambo analolizungumzia. Injili sasa inanadiwa na wachungaji kama bidhaa kwa lengo la kujitajirisha. Msomaji anaweza akalinganisha jinsi injili sasa inavyohubiriwa na picha aliyo nayo akilini ya jinsi upepo unavyovuma. Mfuatano wa kielezi **sasa,** kitenzi **iliyovuma** na kauli hizo kuhusishwa na injili ya maendeleo ya kiuchumi unaonyesha kwamba mwandishi hakubaliani na injili ya aina hii. Kwa njia fulani anasema kwamba injili ya namna hii ambayo sasa inasisitiza utajiri haitampeleka mtu ahera au paradiso ya baadaye. Mwandishi anakemea utashi wa pesa na mali miongoni mwa wanajamii na hasa viongozi wa dini.

Kwa watu maskini katika sehemu hiyo ya Kibera, inaonekana kuwa wao wanaona kwamba hii ndiyo injili itakayowatoa katika umaskini. Maneno 'wanakimbilia injili', yanachimuza msimamo wa mwandishi kwamba yeye hakubaliani na injili hiyo, kwa vile watu wanakimbilia mali, sio injili ya kweli ya kuboresha mienendo ya wanajamii. Mtazamo wa mwandishi unadhihirika katika matumizi ya maneno '**yeyote**', '**wa haraka**' na '**alikimbilia**.' Neno '**yeyote'** katika muktadha huu linaashiria kitu kisicho cha muhimu sana kwa vile kinapatikana kwa kila mtu. Kanisa si mahali pa kutafutia mali. Mwandishi pia anarejelea **utajiri wa haraka.** Watu wanataka utajiri wa haraka, sio ule unaotokana na jitihada na subira. Maneno 'utajiri wa haraka' yana uhasi, kwa vile katika jamii nyingi, kinachosisitizwa ni juhudi na subira. Aidha, matumizi ya kitenzi '**alikimbilia**' pia yanaashiria uhasi kwa vile kile kinachokimbiliwa sicho kinachofaa kwa Mkristo. Hivyo, kitenzi 'alikimbilia' kimetumiwa kwa njia hasi ili kuonyesha kinyume cha jinsi mambo yanavyofaa kuwa.

Mtazamo dhahiri wa mwandishi kuhusu injili ya utajiri wa magari na zawadi nyingine ambazo wahubiri wanasisitiza Mungu anawatakia waumini wawe nazo unaonekana pale mwandishi anapotoa maelezo haya: '**kana kwamba injili na utajiri ni mambo yaliyofungamana**' (Dondoo 56). Kauli hii ambayo ni ishara ya mwandishi kujipenyeza katika masimulizi na kutoa maoni yake. Msimamo wake unadhihirika kwa maneno yake mwenyewe. Yeye anaona kwamba injili na utajiri si mambo yanayofungamana. Watu wanaenda makanisani kutafuta pesa na mali, sio kulisikiliza neno la Bwana. Huu ni unafiki.

Inabainika kuwa mali zile pesa ambazo wachungaji wanadai ni zawadi kutoka kwa Mungu, kusema kweli ni mapato yanayotokana na na hila, pamoja na tamaa yao. Askofu Joshua na mkewe, Kasisi Lona Bosire wanayadhibiti masuala yote ya kifedha katika kanisa la New Jerusalem. Mwandishi anatumia msamiati unaodhihirisha mtazamo wake kuhusu tabia hii ya wachungaji hawa.

61. **Askofu Joshua** na **kasisi Lona Bosire** walipokea **misaada yote** wakaiweka katika akaunti zao **kwa niaba ya kanisa** la New Jerusalem.

    Mapato yaliyotoka katika miradi ya kanisa…pia yalimiminika katika **fuko lao**.

    (Habwe, 2005, Ukur. 130)

Msamiati unaoonyesha mtazamo hasi wa mwandishi kuhusu vitendo vya Askofu Joshua na mkewe Joshua ni maneno '**misaada yote**', '**yalimiminika**' na '**fuko lao'.** Maneno haya yote yanaashiria tamaa waliyo nayo wachungaji hawa. Askofu Joshua na mkewe Lona Bosire wanapokea misaada kutoka kwa wanasiasa wanaokuja kanisani New Jerusalem. Wanasiasa hao wanakuja kuombewa ili mipango yao ya kisiasa ifanikiwe. Misaada hii inatolewa kwa ajili ya miradi ya kanisa. Askofu Joshua na mkewe wanaiweka misaada hii, pamoja na mapato kutoka katika miradi ya kanisa katika '**fuko**

lao’. Mwandishi anatumia kirai ‘**fuko lao**’ ili kuchimuza kiwango cha tamaa ya pesa walicho nacho wachungaji hawa. Neno ‘fuko’ linatokana na ukuzaji wa neno ‘mfuko’. Ukuzaji huu unalifanya neno ‘fuko’ lidhihirishe kwamba kiasi cha pesa kinachochukuliwa ni kikubwa sana. Kiwango hiki kinadhihirisha tamaa kubwa ya pesa. Kwa hivyo, tunaona kwamba utajiri ambao wachungaji wanadai kwamba unatoka kwa Mungu kusema kweli unatokana na hila zao.

Mwandishi Habwe (2005) katika riwaya ya *Paradiso* amechimuza vyeo na majina ya wachungaji wanaohusika katika udanganyifu au unafiki. Ametumia msamiati unaodhihirisha mtazamo wake. Ili kuonyesha kwamba wachungaji ndio wanaohusika na tabia hasi anazozizungumzia. Mwandishi anasisitiza vyeo vya kidini vya wanaofaidika na misaada kutoka kwa wanasiasa. Hapa mwandishi amechimuza vyeo na majina yao. Katika sehemu zingine za riwaya, Lona harejelewi kwa cheo cha “kasisi”. Mwandishi amemchimuza kwa kulitaja jina lake0= kamili: Lona Bosire, wakati ambapo katika sehemu zingine za riwaya anaitwa Lona tu. Badala ya kusema **Askofu Joshua** na **mkewe Lona,** mwandishi anarejelea cheo chake Lona pia. Hii ni kwa sababu Lona, kwa mujibu wa hulka yake, ameweza kushindania nafasi ya kudhibiti mambo ya kanisa. Si mke wa askofu tu, bali naye pia ni kasisi katika kanisa hilo. Vyeo hivi vinampa fursa ya kujitajirisha na hivyo kuwadhibiti waumini na wanajamii kwa jumla.

Vitenzi vyenye kuonyesha mtazamio wa wahusika vimetumiwa kutoa maudhui kuhusu masuala ya kijinsia. Katika riwaya ya *Paradiso*, wahusika wa hulka mbalimbali wametumiwa kuwakilisha mitazamo tofauti kuhusu mahusiano ya kijinsia. Kuna wahusika ambao wanaonyesha kuwa ni sawa kumdhibiti mwanamke ilhali kuna

wahusika wengine wa kike ambao wako huru na wana mamlaka katika familia na masuala ya jamii.

62. Salome **hakuzuiliwa** na Kyalo kwenda New Jerusalem.
(Habwe, 2005, Ukur. 70)

63. Hata vile vikao vya nyumbani vya sala ambavyo alisema **viliharibu wanawake** sasa **alimkubali mkewe kuvishiriki**.
(Habwe, 2005, Ukur. 71)

Madondoo ya 62 na 63 yanaonyesha jinsi ambavyo mwanamume ana mamlaka juu ya mwanamke katika jamii anayoisawiri mwandishi. Kyalo anamdhibiti mkewe Salome. Mke anapenda mambo ya kanisa, lakini mumewe hataki kabisa mambo ya kanisa. Yeye (Kyalo) ndiye anayeamua ama Salome aende au asiende kanisani. Pia mwanamke lazima apate idhini ya mume wake ili kushiriki vikao vya nyumbani vya wanawake. Vitenzi vilivyotumika vinaonyesha mamlaka aliyo nayo mwanamume katika ndoa. Salome '**hakuzuiliwa**' na Kyalo kwenda kanisani. Kitenzi '**hakuzuiliwa**' kimekanushwa. Hii inamfanya msomaji kuchunguza uyakinishi wa kitenzi hiki, yaani Salome '**alizuiliwa**' na mume wake Kyalo. Kitenzi 'hakuzuiliwa' kinaashiria kwamba Kyalo ana mamlaka ya kumzuia mkewe Salome.

Dharau ya mwanamume kwa mwanamke inabainika katika mtazamo wa Kyalo. Kwa kufikiria kuwa vikao vya nyumbani vya sala '**viliharibu wanawake**', Kyalo anaonyesha kwamba mwanamke hana uwezo wa kuamua kati ya zuri na baya, kana kwamba yeye ni mtoto, ambaye anahitaji kusaidiwa kuamua kati ya zuri na baya. Kauli 'viliwaharibu wanawake' inaonyesha taasubi ya kiume. Wanawake ni watu wazima wenye uwezo na haki ya kujiamulia.

Katika dondoo la 10, maelezo yanayotolewa na mwandishi kuhusu hali ya mwanamke kukaa nyumbani tu yanaonyesha msimamo wake. Msimulizi anatumia msamiati ambao unaonyesha kuwa mwanamke huyu (Mary Kasiva) ni kama mtumwa, ambaye

amefungiwa nyumbani ili afanye shughuli za nyumbani tu. Mwandishi anasema kuwa Kasiva alishughulika na kazi za nyumbani '**wiki nzima**'. Anaongezea ufafanuzi kwamba hii '**ilishakuwa ratiba**' ya mwanamke huyu, tena kwa msisitizo zaidi: kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi. Kwa kutumia neno '**ilishakuwa**', mwandishi anaonyesha hali ya kukatisha tamaa ya Mary. Hii inalenga kumfanya msomaji amhurumie mwanamke huyu. Mtazamo wa msimuliaji ni wa kumhurumia au kumsikitikia Mary na wanawake walio katika hali kama hii kwa jumla. Neno '**ratiba**' pia linaonyesha jinsi ambavyo mwanamke amefungwa kiwakati na shughuli za nyumbani.

Hata hivyo, baadhi ya wanawake wenyewe wanaendeleza fikira kwamba mwanamume ana mamlaka kuliko mwanamke. Katika riwaya ya *Paradiso*, msimamo huu unaendelezwa na wahusika wawili wanawake, yaani Patricia na Lydia. Wao wanaona ni sawa kushughulika na mapishi, wakati ambapo Michael (mwanamume) amekaa tu akisoma gazeti.

64. Usiwasumbue watu tutapika wenyewe. Sisi ni **wanawake ati**.
(Habwe, 2005, Ukur. 98)

Ni dhahiri kwamba Lydia anaamini kuwa mwanamume "hawezi" kupika. Jamii imewafundisha kwamba kupika ni jukumu la mwanamke, na kwamba huu ni mpango wa Mungu, kama Lydia anavyoeleza: "Ndio maana Mungu akatuumba wawili wawili, wawili wawili maana kila mmoja ana jukumu lake. Langu huliwezi na lako siliwezi" (Habwe, 2005, Ukur. 100). Lydia anahalalisha msimamo wake kwa kumrejelea Mungu kama mwenye kugawa majukumu kwa kila jinsia. Tena anasema: '**sisi ni wanawake ati**.' Hii ina maana kwamba wamekubali jukumu hili la kupika, ambalo jamii imempa mwanamke, sio maumbile yake. Neno "ati" linaashiria kwamba wanawake hawa wamekubali kwamba hali hii ni ya kawaida. Hii inamaanisha kwamba wakati mwingine

mwanamke mwenyewe anahalalisha tofauti na mahusiano ya kimamlaka kati ya jinsia ya kike na ya kiume zilizopo katika jamii.

Lydia na Patricia wanatoa kauli nyingine ambazo zinaonyesha itikadi waliyo nayo kuhusu nafasi ya mwanamke kama kiumbe dhaifu katika jamii:

> 65. Mbona Mungu **inasemekana** aliumba mwanamke kwa ubavu wa mwanamume?" Patricia **alidai**.
>
> "Lakini **mahali kwingi** katika Biblia mwanamke **ameitwa** kiumbe dhaifu," Patricia aliuliza tena.
>
> "Biblia **imeeleza waziwazi** kuwa mwanamke ni kiumbe dhaifu," Lydia alisema.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 101)

Katika dondoo la 65, mwandishi ametumia msamiati unaoashiria mzungumzaji kutokuwa na hakika. Vitenzi '**inasemekana'** na '**alidai**' vinaonyesha kuwa kuna uwezekano wa maelezo kwamba Mungu alimuumba mwanamke kutoka katika ubavu wa mwanamke kutokuwa kweli. Patricia anasisitiza kuwa katika Biblia mwanamke ameitwa kiumbe duni. Naye Lydia anaendeleza mawazo hayo hayo ya rafiki yake Patricia kwa kuchangia kwamba Biblia inaeleza '**waziwazi**' kuwa mwanamke ni kiumbe duni. Neno 'waziwazi' linaashiria kuwa mzungumzaji ana uhakika kabisa kuhusu analolisema. Inaonekana kwamba wanawake hawa kimsingi hawaungi mkono hali ya kutokuwepo usawa, ila wanaona kwamba inabidi wafuate mkondo kwa vile kulingana na wao, Biblia imehalalisha hali ya kutokuwepo usawa. Mwandishi anadhihirisha jinsi mwanamke anavyokwamiza ukombozi wake mwenyewe kwa kuendeleza dhana kwamba Mungu mwenyewe ndiye ameuweka mpango ambapo kihadhi, mwanamke yuko nyuma ya mwanamume.

Naye mwanamume anaonyesha kuridhika na hali ya mambo kuhusu jinsia ambayo imempendelea yeye. Mwandishi amemtumia mhusika Michael kusawiri jambo hili:

66. Michael aliangalia wale wanawake walivyofanya mle ndani akakinai kuwa kazi ya nyumbani walikuwa **washenga kwayo**.
(Habwe, 2005, Ukur. 99)

67. Nyinyi naona mu **mafundi wa kupika** sana," Michael alisema **akitabasamu**.
(Habwe, 2005, Ukur. 100)

Hali kadhalika, Michael anaona kwamba Lydia na Patricia walikuwa '**washenga**' au '**mafundi wa kupika**'. Shughuli hii anaiangalia kama mtazamaji tu, kama kwamba haimhusu. Anatumia kauli hizo huku '**akitabasamu**'. Hapa mwandishi anatuonyesha mwanamume anayefurahia hadhi yake ya kupikiwa na mwanamke. Ingawa kusingekuwa na shida yoyote Michael kupikiwa na Patricia na Lydia, muktadha na maneno anayoyatumia mwandishi yana toni inayoonyesha kwamba mwandishi hafurahii jinsi mwanamume anavyochukulia kwamba ni haki yake kupikiwa na wanawake. Pia, msimulizi anaonyesha kwamba si sawa mwanamume kufikiri kwamba yeye hawezi kupika au kusaidia katika shughuli zingine katika upishi.

Ili kuchimuza ujumbe wake kuhusu suala la jinsia na majukumu ya nyumbani, mwandishi anamwonyesha mwanamume akisoma gazeti wakati wanawake wanashughulika kupika jikoni. Gazeti analolisoma Michael ni gazeti la ***Victory***, jina ambalo mwandishi ameliteua kimaksudi ili kuchimuza maudhui yake ya mamlaka ya mwanamume juu ya mwanamke:

68. Lydia na Patricia waliandaa meza. Michael aliacha kusoma **gazeti la *Victory*** akajongea mezani na kuanza kula.
(Habwe, 2005, Ukur. 100)

Hata baada ya kupika, Lydia na Patricia ndio wanaoandaa meza. Michael (mwanamume) bado anasoma gazeti. Hashughuliki na lolote. Yote yanafanywa na wanawake. Mara tu baada ya wanawake kuandaa meza, mwanamume (Michael) ambaye hajashughulika na lolote katika kukiandaa chakula anajongea mezani na kuanza

kula mara moja. Mwanamke anashughulika kupika lakini mwanamume ndiye anayetangulia kula. Mwandishi anataja pia kwamba Michael alikuwa akisoma gazeti la ***Victory***. Mwandishi amelitumia jina hili la gazeti kimaksudi kuonyesha "ushindi" wa jinsia ya kiume dhidi ya jinsia ya kike. Kwa hivyo, kwa mujibu wa muktadha wa matumizi yake, jina la gazeti hilo halikuteuliwa kisadfa. Hii ni ishara ya mamlaka aliyo nayo mwanamume katika jamii ukimlinganisha na mwanamke. Toni anayoitumia mwandishi inaonyesha kutofurahishwa na hali hii ya mambo. Hii ni kwa sababu tunaona mlinganuo ambapo mwanamume ndiye 'mshindi', ingawa mwanamke ndiye ameshughulika kuandaa chakula.

Jambo hili la mwanamume kusoma gazeti wakati mwanamke anashughulika jikoni (kwa vile jamii inasema kwamba mwanamume hapiki au hafanyi shughuli za jikoni) tunaliona pia katika riwaya ya Wamitila ya *Nguvu ya Sala*.

> 69. Baba alikuwa ameketi kwenye baraza ya nyumba nilipotokeza. Alikuwa **akisomasoma gazeti**… Niliingia nyumbani… kisha nikatoka kuelekea **jikoni alikokuwa mama**.
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 121)

Tunamwona mwanamume mwingine akiburudika kwa kusoma gazeti wakati mwanamke akishughulika jikoni. Mwandishi ametumia faridi ya 'gazeti' kuonyesha jinsi ambavyo kuna tofauti ya kimamlaka katika jamii kati ya mwanamume na mwanamke. Tunamwona Susan akifululiza moja kwa moja hadi kwa mama yake. Susan anaposema, "…nikatoka kuelekea **jikoni alikokuwa mama**," maneno hayo yana maana fulani. Susan hasemi "kuelekea kwa mama aliyekuwa jikoni," bali anasema "…kuelekea jikoni **alikokuwa** mama." Kitenzi 'alikokuwa" kinasisitiza mahali ukitofautisha na mahali alikokuwa baba. Pia, Susan anaeleza kuwa baba yake alikuwa '**akisomasoma**' gazeti. Wakati ambapo baba 'anasomasoma gazeti' mama yake

"**anashughulika kuviosha vyombo**" na "akiviinamia vyombo alivyokuwa anaosha" (Wamitila, 1999, Ukur. 121). Susan hasemi kwamba baba yake alikuwa 'akisoma' gazeti, bali alikuwa '**akisomasoma**' gazeti, wakati ambapo mama '**akiviinamia**' vyombo alivyokuwa anaosha. Hii inaashiria kwamba mama anafanya shughuli ya maana na kwa umakini ukimlinganisha na baba ambaye hafanyi shughuli ya maana ila 'kusomasoma' gazeti tu, yaani kusoma bila kuwa makini. Kwa namna fulani, dondoo hili linaonyesha jinsi ambavyo mwanamke anavyodunishwa katika jamii kwa kumwonyesha kama chombo cha kufanya kazi, lakini wakati huo huo hali hii inamdunisha mwanamume kwa kumwonyesha kama mtu ambaye hafanyi shughuli ya maana.

Ingawa mhusika Michael ametumiwa na mwandishi kumwakilisha mwanamume anayefurahia hadhi yake akilinganishwa na mwanamke. Michael ana imani kwamba Mungu anapendelea usawa wa kijinsia. Anasema: "Huo usawa [wa kijinsia miongoni mwa watoto] ndio Mungu alioutaka" (Habwe, 2005, Ukur. 101). Wazo hili la Mchungaji Michael (mwanamume) ni kinyume na mawazo ya Patricia na Lydia (wanawake) kwamba mwanamke ni kiumbe dhaifu kwa vile 'inasemekana' aliumbwa kutokana na ubavu wa mwanamume.

Hata hivyo, maoni ya Lydia na Patricia yanaelekea kukanushwa na mhusika mwingine wa kike – Lona. Lona ameonyeshwa kama mwanamke mwenye msimamo, ambaye anaweza kujiamulia atakacho. Anamkataa Mganga, ambaye inabidi aondoke pale nyumbani.

70. Mume wa awali wa Lona, Bw. Mganga, alipaondoka pale nyumbani bila chuki yoyote. **Alielewa** kila mwanamke ana haki ya kupenda aliyemtaka.

(Habwe, 2005, Ukur. 71)

Mganga anaamua kuondoka kwa hiari kuliko kubishana na Lona. Hii inamaanisha kwamba mwanamke ana uwezo wa kujiamulia kuolewa na anayempenda ni jambo ambalo halina ubishi wowote. Ni ukweli dhahiri ambao inabidi wanaohusika kulielewa.

Katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* pia mhusika wa kike amekuzwa kupitia kwa msamiati unaotumiwa katika kumwelezea. Ingawa inaonekana kwamba mwanamume ana mamlaka makubwa kuliko mwanamke katika jamii, mwandishi anaonyesha kwamba kuna upande mwingine wa hali hii ambapo mwanamke naye ana mamlaka kwa njia zisisokuwa wazi.

> 71. Alikuwepo Masaku aliyekuwa mwanamume. Masaku alikuwa na sifa za ajabu ajabu. Mwalimu alitueleza kuwa shujaa huyo aliacha nyayo zake juu ya jabali fulani **karibu na mlima karibu na mji wa Machakos.**
> Alikuwepo **shujaa mwingine wa kike**. Alikuwa na **uwezo** wa kutabiri mambo. **Aliweza** kutabiri majanga ambayo yangeisibu jamii. Huyu alizikwa katika pango fulani **karibu na kijiji chetu**.
> (Wamitila, 1999, Ukur. 9)

Hapa tunamwona msimulizi akitumia msamiati unaoashiria msimamo wake kuhusu mashujaa wa jinsia zote mbili. Amehakikisha kwamba mashujaa ni wa jinsia zote mbili. Shujaa mwanamke na shujaa mwanamume wote wawili wana uwezo fulani, ila tunajulishwa kuwa shujaa mwanamume (Masaku) alikuwa na "**sifa za ajabu ajabu.**" Kwa upande mwingine, uwezo wa shujaa wa kike umeelezwa ni wa kutabiri mambo. ambayo yangeisibu jamii. Kuna msisitizo fulani wa uwezo wa shujaa wa kike: 'alikuwa na uwezo.' Pia, 'aliweza kutabiri'. Hii inamfanya shujaa mwanamke awe wa muhimu sana kwa jamii. Tofauti na ufafanuzi tunaoupata kuhusu shujaa mwanamke, inasemekana kuwa shujaa mwanamume alikuwa na 'sifa za ajabu ajabu'. Mwandishi hatoi mfano wa sifa hizo. Kwa kuzielezea sifa za shujaa huyo kama za 'ajabu ajabu' mwandishi amemdunisha kwa vile sifa za ajabu ajabu hazieleweki bayana na inaonekana si za muhimu. Tena, wakati ambapo shujaa mwanamke amezikwa "**karibu**

na kijiji chetu", shujaa mwanamume alizikwa "**karibu na mlima karibu na mji wa Machakos"**, yaani mbali na kijiji. Shujaa mwanamke amepewa sifa ya "ukaribu", wakati ambapo shujaa wa kiume amepewa sifa ya "umbali". Ni kama kwamba shujaa mwanamke anafungamana zaidi na jamii husika kuliko shujaa wa kiume. Kwa hiyo, tunaona kwamba mwandishi amemwinua mwanamke kwa kuchimuza sifa zake, na kumdunisha mwanamume kimaksudi kwa kutotaja umuhimu wake katika jamii. Uimarishaji wa mhusika wa kike ndiyo mojawapo ya motifu kuu katika riwaya hii ya Wamitila. Kwa hiyo, tunamwangalia mwandishi huyo kama mtetezi wa mwanamke katika jamii.

Katika riwaya ya *Paradiso*, mwandishi amesawiri maudhui ya mwema kuwa mui. Hili linadhihirishwa na mhusika Mchungaji Michael. Awali Michael anasawiriwa kama mhusika mwema; mchungaji ambaye ni kielelezo kwa wachungaji wengine. Hata hivyo, baadaye anateleza na kuacha njia ya kwenda paradiso ya baadaye. Akaanza kujenga paradiso yake ya hapa duniani kwa kufanya mambo maovu kama vile mapenzi nje ya ndoa pamoja na kukimbilia pesa na mali. Mabadiliko haya yanamfanya asiwe kielelezo kwa wengine. Mabadiliko katika imani yake yanadhihirika pia kisitiari katika maumbile yake.

72. **Kasisi** Michael **aliendelea kushuka kitambi**.
(Habwe, 2005, Ukur. 160)

Kitambi mara nyingi huhusishwa na utajiri. Ni ishara kwamba mtu ana uwezo wa kuhimili gharama ya vyakula na vinywaji ambavyo si vizuri kwa afya lakini ambavyo ni ghali kwa maskini. Tukichunguza msamiati uliotumika katika kauli tunaona kwamba mwandishi ana mtazamo hasi kumhusu mchungaji Michael. Kitambi si ishara ya afya nzuri, ingawa katika jamii mbalimbali inachukuliwa kama (ishara) ya "mwenye nacho". Msimulizi anaposema kuwa [Michael] '**aliendelea kushuka kitambi'**, anaashiria

kwamba maumbile ya Mchungaji Michael yanaendelea kubadilika na kuharibika. Kisitiari, kushuka kitambi ni ishara ya maporomoko yake kimaadili. Hata mwandishi anachimuza cheo chake cha ukasisi kwa kumwita "Kasisi Michael" ili kumkumbusha msomaji kwamba mtu anayelengwa au anayezungumziwa ni kasisi. Katika sehemu zingine za riwaya mwandishi hamrejelei kama "Kasisi Michael". Mwandishi anataka kuhusisha matarajio kuhusu mtu mwenye hadhi ya ukasisi katika jamii na maumbile na tabia ya Michael ya sasa. Mwandishi anataka msomaji azingatie jinsi ambavyo mchungaji huyo anaendelea kuiacha njia ya Bwana.

Katika riwaya ya *Paradiso,* Habwe (2005) ameangazia suala la unyonyaji wa waumini unaofanywa na wachungaji. Wachungaji wanasisitiza zaka na matoleo mengine kanisani kwa ajili ya manufaa yao. Mbinu mbalimbali zinatumiwa kuhakikisha kwamba waumini wanatoa zaka hiyo. Haya yanadhihirika katika dondoo lifuatalo:

> 73. Tangazo jingine ndugu zangu na dada zangu katika Yesu ni kwamba matoleo yenu yamepungua. Kitabu cha Malaki kinasema **matoleo ni lazima** kwa waumini. Matoleo **yapaswa** kuwa mazuri. Baadhi yenu mnaleta kanisani masazo ya *supermarket,* yaani *change*. **Si ruhusa** kuleta shilingi moja kanisani au hata shilingi kumi…
> …**ni haramu** kucheza muziki katika vyombo hivyo **ikiwa hukuchangia**.
>
> Kuanzia Jumapili ijayo, vifuko vya sadaka vitakuwa kule mbele na kila mmoja **atapaswa** kupeleka zaka yake kila mtu akimwona. Mara minong'ono ikazuka kanisani… Hajui kuna watu wengine hawana pa kutoa **hiyo zaka**. Hata kula hawawezi kula. Tena hizo pesa si **wanazila wao**…
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 54)

Lugha inayotumiwa kanisani kuwafanya waumini watoe zaka ni ya masharti. Ili kuwatawala waumini kwa hila kwa ajili ya kuwafanya watoe zaka na matoleo mengine, mtangazaji anawatolea nukuu kutoka katika Biblia. Nukuu hiyo inalenga kuwafanya waumini wajilaumu kwa kukiuka amri ya Mungu. Viongozi wa kanisa wanateua vifungu kutoka katika Biblia ambavyo vinahimiza utoaji wa matoleo. Lugha

iliyotumika kwenye nukuu hiyo ni ya masharti: "…matoleo **ni lazima** kwa waumini." Hii ina maana kwamba hakuna hiari kwa muumini ila kutoa matoleo hayo.

Kauli nyingine ambazo zinaonyesha kwamba waumini wanalazimishwa kutoa zaka ni kwamba matoleo '**yanapaswa** kuwa mazuri… **Si ruhusa** kuleta….' Tena mtangazaji anasema, '**ni haramu**' kucheza muziki katika vyombo ikiwa muumini hakuchangia. Pia, kila muumini '**atapaswa**' kuipeleka zaka yake mbele kanisani kila mtu akimwona. Katika kutumia tungo hizi za masharti, mwandishi anaonyesha jinsi kanisa linavyowashurutisha waumini kutoa matoleo bila kufikiria hali zao. Kuna matumizi ya mamlaka kanisani yanayohusisha hila ya kunukuu Biblia na kauli nyingine kali zinazolenga kuwafanya waumini wajilaumu kwa kutotoa matoleo "mazuri", yaani mengi. Kinaya ni kwamba lugha ya masharti kama hii haifai kutumiwa kanisani. Lugha inayotarajiwa kutumiwa kanisani ni ile ya upole na unyenyekevu.

Mzee mmoja katika kanisa la New Jerusalem anateta kuwa pesa zinazokusanywa kanisani 'wanazila wao', yaani viongozi wa kanisa. Kauli ya mzee muumini huyu inatufanya tuhisi jinsi waumini wanavyohisi kuwa wametengwa. Wanahisi kwamba wananyonywa tu na viongozi wa kanisa.

Akitumia mbinu ya kileksika ya msamiati wa kitathmini, mwandishi wa *Nguvu ya Sala* anaangazia suala la mabadiliko kwa upana kwa kuzingatia jinsi ambavyo nguvu ya sala haiwezi kutegemewa kukabiliana na changamoto za maisha zinazowakumba watu. Susan na dada yake Roselyn, kinyume na baba yao, wanatambua kwamba dunia imebadilika na inahitaji mkabala mpya, siyo mkabala wa nguvu ya sala tena.

74. Kwa kiasi kikubwa imani hiyo **ilishampofua** na kumfanya **ashindwe** kuuangalia uhalisi.
    (Wamitila, 1999, Ukur. 71)

Vitenzi '**ilishampofua**' na '**ashindwe**'vinaonyesha tathmini hasi ya Susan kuhusu baba yake. Mtoto anaona uhalisi ambao baba 'anashindwa' kuuona. Vitenzi vyote viwili vya kitathmini vinamwonyesha Richard kama mtu ambaye hana uwezo wa kuona uhalisi. Hapa tunaona jinsi mwandishi anavyomwimarisha mhusika wa kike kwa kumpa uwezo fulani ambao mwanamume hana. Wanaomtathmini na kuona kwamba amepungukiwa kimawazo ni mabinti zake. Richard amesawiriwa kama mtu ambaye hajui kwamba dunia inabadilika, na kinachompofua, kulingana na mabinti zake ni dini, hasa imani yake katika "nguvu ya sala."

4.2.8 Matumizi ya Uolezi

Kwa mujibu wa Kahigi (2019) uolezi unajumlisha vipengele vya kiisimu vinavyotambulisha virejeleo kwa kuzingatia hali iliyopo ya usemaji. Vigezo vya uolezi ni *fasi/eneo* na *wakati* kuhusiana na msemaji na hali ya ushiriki. Kahigi anaorodhesha aina tano za uolezi, yaani uolezi wa nafsi, uolezi wa fasi/eneo, uolezi wa wakati, uolezi wa kijamii na uolezi kilongo. Kati ya aina hizo za uolezi, utafiti huu unahusika na aina tatu: uolezi fasi, uolezi wakati na uolezi wa kijamii ambazo ndizo aina zinazodhihirika katika riwaya zilizochunguzwa, mintarafu ya masuala ya dini na mamlaka.

4.2.8.1 Uolezi wa Fasi

Katika riwaya ya *Paradiso* tunaona uolezi wa fasi ukitumika kutuonyesha ufarakano, chuki na ugomvi uliopo kati ya wahubiri na makanisa yao. Huu ni ugomvi tunaouona hata katika makanisa ya siku hizi.

> 75. Tonje alifungua kanisa **lake** mwenyewe. Yeye na babake hawaonani uso kwa uso. Kila mmoja yuko na mambo **yake**," Zuhra alieleza.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 45)

Kupitia kwa mhusika Zuhra (mkewe Mango) ambaye ni Mwislamu, tunapata maelezo kuhusu mivutano iliyopo kati ya wachungaji, wakiwakilishwa na wahusika Tonje na

baba yake. Kwa vile Zuhra ni Mwislamu, tunaangalia suala hili kupitia kwa mtazamo wake kama mtu ambaye hahusiki moja kwa moja katika shughuli za makanisa. Mwandishi analenga kutupatia msimamo wa mhusika ambao unaaminika kwa vile yeye anayaangalia mambo ya makanisa kama mtu asiyehusika nayo. Mhubiri Tonje na baba yake hawasikilizani. Kila mmoja anataka kuongoza kanisa lake. Mwandishi ametumia msamiati unaotuonyesha mfarakano huu. Vibainishi vimilikishi '**lake**' na '**yake**' vinatuonyesha pengo lililopo kati ya mtoto na baba yake, watu ambao kijamii na kidini wanatarajiwa kuwa na umoja wa mzazi na mwana, badala ya kutoonana uso kwa uso. Badala ya dini kutumiwa kuimarisha umoja, imetumika kuleta utengano. Kwa njia fulani dini ina mamlaka ya kutenganisha watu.

Uolezi wa fasi umetumika pia kuonyesha matabaka katika jamii. Kuna tabaka la mabwana na tabaka la watwana. Fuad, ambaye ni wa tabaka la kibwana, anamlalamikia Bwana Marjebi, ambaye ni wa tabaka lile lile kuhusu wafanyakazi wa tabaka la kitwana.

76. "… Bwana Marjebi … nataka unieleze khasa, mana'ke **hawa…**"
Fuad alisita kidogo na kumtazama Bwana Marjebi huku akitafuta neno la kusema, "**ng'ombe hawa**, nisamehe…lakini sina vingine vyovyote vya kuwaita ila hivyo – **hawa** siku hizi wamekuwa hata hawaogopi."
(Shafi, 1978, Ukur. 35)

Matabaka ni ya kimamlaka. Tabaka la juu linakuwa na mamlaka kuliko tabaka la chini. Tofauti hii inadhihirika katika lugha inayotumika. Fuad anawazungumzia wakulima na wafanyakazi kwenye shamba lake kwa kutumia neno 'hawa' badala ya kusema 'wafanyakazi wangu'. Kwa vile hawajarejelewa kabla, Marjebi anashindwa kujua ni nani hasa Fuad anaowazungumzia. Fuad anawazungumzia kama kwamba wako hapo karibu kutokana na hisia zake kuwahusu. Ni kama kwamba kitaswira anawaona. Hata hivyo, kitabaka na kihadhi wako mbali. Hapa tunaona uolezi wa fasi ukitumiwa kuakisi uolezi wa kijamii. Isitoshe, kwa kuwaita 'ng'ombe', Fuad anaonyesha kwamba

hawathamini kama binadamu wenzake. Hali hii inadhihirisha uolezi wa kijamii ambapo yeye binadamu anajitenga na wale anaowaona kama wanyama. Inadhihirisha mamlaka aliyo nayo yanayotokana na nafasi yake kama kabaila.

Mtunzi wa *Paradiso* pia pia anatumia uolezi wa fasi kuzungumzia suala la jinsia ambapo kuna jambo la upendeleo kwa mwanamume katika jamii. Katika dondoo la 66, tunapata msamiati unaodhihirisha jinsi mwanamume anavyoridhika na hali ya kupendelewa katika jamii. Tunalirejelea dondoo hilo kwa mujibu wa mbinu ya uolezi wa fasi (Sehemu 4.2.8.1).

> [66] Michael aliangalia **wale wanawake** walivyofanya **mle ndani** akakinai kuwa kazi ya nyumbani walikuwa washenga kwayo.
> (Habwe, 2005, Ukur. 99)

Msimulizi anasema Michael aliwaangalia '**wale wanawake**,**'** badala ya kutumia majina ya wanawake hao, yaani badala ya kusema Lydia na Patricia, kwa vile anawajua vizuri sana. Hapa jinsi yao, na namna wanavyoangaliwa na mwanamume kama watu wa jinsi hiyo, imechimuzwa. Zaidi ya hayo, mwandishi anasema '**walivyofanya mle ndani**', sio 'walivyokuwa wakipika jikoni', kwa vile ni dhahiri walikuwa wakipika. Matumizi ya '**walivyofanya mle ndani'** inamfanya mwanamume kutenganishwa zaidi na shughuli ya kupika, kama kwamba wanawake hawa walikuwa wakifanya kitu ambacho alikiona ni cha ajabu. Hali hii inaonyesha mamlaka aliyo nayo mwanamume katika jamii ambapo yeye anakaa akisoma magazeti wakati akipikiwa chakula. Fikira za Michael kama mchungaji hazimwonyeshi kama Mkristo anayezingatia usawa wa binadamu.

4.2.8.2 Uolezi wakati

Uolezi wakati umetumiwa katika riwaya ya *Paradiso* kuelezea mabadiliko katika madhumuni ya watu kwenda kanisani. Vilevile Zuhra anatusaidia kuelewa mabadiliko yanayotokea katika jamii mintarafu ya dini ya Kikristo. Zuhra anasema:

> 77. Wajua **siku hizi** mwanangu watu wanatafuta kunako miujiza. Yaani mahali ambapo matatizo yao ya kiuchumi, kijamii yanaweza kutatuliwa…
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 46)

Kirai '**siku hizi'** kinatuonyesha kwamba kumetokea mabadiliko katika mtazamo wa watu kuhusu dhima ya kanisa. Tofauti na siku za awali, watu sasa wanakwenda kanisani kutafuta miujiza au utatuzi wa matatizo yao ya kiuchumi. Watu wengi wa sehemu ya Kibera ni maskini na hawana rasilimali za kuwatoa kwenye ufukara. Kwa hiyo, wanaona kwamba makanisa yanaweza yakawasaidia kuondoa hali yao ngumu. Wachungaji kadhaa nao wameanzisha makanisa katika sehemu hiyo wakijua kwamba watu wanatafuta suluhisho la hapo hapo, yaani miujiza. Kanisa linatazamwa kama nyenzo ya kutatulia matatizo, sio kuabudu Mungu. Watu wanaliona kanisa kama asasi yenye uwezo mkubwa wa kutatua matatizo ambayo yamewashinda. Hivyo, ni kama kuna ubadilishanaji ambapo mwenye shida anatoa kile kidogo alicho nacho, akitarajia kwamba shida yake itaondolewa na mchungaji kupitia kwa miujiza. Ni kama kwamba wachungaji wanauza miujiza kwa mafukara.

4.2.8.3 Uolezi wa Kijamii

Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, uolezi wa kijamii unadhihirika tunapoangalia jinsi ambavyo wanamapinduzi na wafanyakazi wanavyomkata Fuad jina kwa kutotanguliza jina 'bwana' baada ya yeye kupoteza mamlaka yake. Wafanyakazi kumwita Fuad 'bwana' ni ishara mojawapo ya mamlaka aliyo nayo Fuad kama bwana shamba. Wafanyakazi wote na wakulima ni lazima watangulize jina 'bwana'

wanapozungumza naye au wanapomrejelea bwana shamba huyu. Lakini, kama ishara ya mapinduzi yanayoendelea nchini, watwana na wakulima wa Fuad wanaacha kumwita ‘bwana’. Vuai, mkulima mmojawapo katika shamba la Fuad anamjibu Fuad kwa ujeuri bila kutumia jina ‘bwana’:

> 78. “Wewe! Wewe! Mimi nakutafuta wewe tokea saa ile!” alianza Fuad huku akimwelekezea [Vuai] kidole chake…
>
> Juzi ulikuwa unatoka wapi?
> “Mkutano,” alijibu Vuai **bila ya kumwita Fuad ‘Bwana’** kama ilivyo kawaida yao.
> (Shafi, 1978, Ukur. 27)

Vuai anajua kwamba baada ya serikali ya kisultan kuangushwa, mabwana shamba hawana mamlaka tena. Kwa hivyo, hamwogopi tena Fuad. Matumizi ya jina ‘bwana’ yanaashiria pengo la kihadhi lililopo kati ya mabwana shamba na wafanyakazi. Mabwana shamba wamekuwa katika tabaka la juu, ilhali wafanyakazi wamekuwa katika tabaka la chini.

Naye Kijakazi, ambaye amekuwa anafikiri kwamba utumwa ni majaliwa yake, hatimaye anagoma kwa kukataa kumwita Fuad ‘bwana’ na kutii amri zake. Baada ya kumwogopa sana na kumtii Fuad kwa muda mrefu, anaamua kumkata Fuad jina kwa kumjibu bila kutumia jina ‘bwana’ baada ya kutambua kwamba Fuad amepoteza mamlaka yake. Kama ishara ya kugoma kwake, Kijakazi anakataa kutii agizo la Fuad la kumvua viatu:

> 79. **Sikiliza Fuad,** mimi nitakufanyia kila utakalo… lakini sitopiga magoti tena kukuvua viatu… Kwa hasira, Kijakazi alimwambia Fuad, ikiwa ndiyo **mara yake ya kwanza kumkata jina**, yaani kumwita jina lake **bila kutanguliza ‘bwana**’.
> (Shafi, 1978, Ukur. 90)
>
> 80. **Sikiliza Fuad!** Nakwambia wazi, baada ya leo – nakwambia tena – baada ya leo, **sitokubali** kukutumikia utumwa wa namna yoyote!
> (Shafi, 1978, Ukur. 94)

Utiifu na hofu ya Kijakazi kwa Fuad havipo tena. Kukataa kumwita Fuad 'bwana' ni ishara kwamba mnyonge ameanza kumgeukia mwenye nguvu kwa kukataa uhusiano wa bwana na mtumwa. Kijakazi anatupilia mbali jina la hadhi 'bwana.' mara kadhaa kuonyesha kwamba amefanya hivyo kimaksudi ili Fuad atambue kwamba 'ubwana' wake umeisha. Kwa hivyo, Kijakazi anapokataa kumwita Fuad 'bwana', anadhihirisha uolezi wa kijamii, ambapo pengo la kihadhi kati yake na Fuad halipo tena.

Nao wanamapinduzi wanajua kwamba siku za ubwana wa mabwana shamba zimeisha. Kwa hivyo, wanapokuja kwa Fuad, hawamchukulii na kumheshimu kama bwana shamba. Wanamrejelea bila kutumia jina 'bwana'. Badala yake, Fuad ndiye anayemwita mwanamapinduzi 'bwana.'

81. "Nafikiri unaelewa kuhusu sheria mpya ya ardhi?"…

    "Naam! Nimeisikia **Bwana**!" Fuad alijibu, wakati umemgeukia na sasa naye anajua kuita '**Bwana.**'
    (Shafi, 1978, Kur. 54 -55)

82. Baada ya kufika tu gari hilo, alishuka mtu mmoja na kumwuliza Kijakazi, "**Fuad tumemkuta**?"

    "**Bwana**? Si... sijui, ngojea nikatazame ndani," Kijakazi alijibu.
    ...mara [Fuad] **alitoka nje mbio.**
    Nipo! **Nipo Bwana!** Je, mnataka kuonana na mimi? Fuad aliuliza …
    (Shafi, 1978, Ukur. 95)

Wanamapinduzi wanauliza: "Fuad tumemkuta?" kama kwamba Fuad ni mtu wa kawaida tu kama wao, badala ya kusema "**Bwana Fuad tumemkuta**?" au "**Bwana tumemkuta**?" Kulingana na wao Fuad sasa siye bwana tena, ila kwa Kijakazi ambaye kwa sasa bado anamheshimu na kumwogopa sana Fuad. Lakini katika kuwajibu, Kijakazi anatumia jina 'bwana', kama kwamba anawakosoa wanamapinduzi kwa kuashiria kwamba Fuad anaitwa 'bwana', siyo 'Fuad' tu.

Mapinduzi ambapo mabwana shamba wamepoteza ardhi na mamlaka yao yameakisiwa katika lugha. Awali, Fuad ndiye anayeitwa 'bwana' lakini baada ya mapinduzi, yeye sasa ndiye anayewaita wanamapinduzi 'bwana', kama tunavyoona katika madondoo 78 na 79. Wakati huu Fuad ndiye mnyonge, Kwanza anasema **'Nipo! Nipo Bwana'**. Hii inamaanisha kwamba yeye anajua kuwa mtu anayekuzidi mamlaka ni lazima kumwita 'bwana', kama ambavyo wafanyakazi wake wamekuwa wakimwita yeye. Mwandishi anapenyeza masimulizi kwa kumwelezea msomaji mabadiliko ambayo yametokea. Anasema: "wakati umemgeukia Fuad na sasa naye anajua kuita 'bwana'."

Mnyonge anaamini kuwa yeye hafai kuonyeshwa heshima yoyote. Hili linadhihirika tukimwangalia mhusika Kijakazi. Wakati anapomwita Fuad, yeye anasisitiza jina 'bwana'. Lakini yeye [Kijakazi] anapoitwa 'bibi' na Mkongwe, anashtuka. Anajiona kama mtu asiye na thamani, yaani mtumwa tu ambaye amejaliwa huo utumwa. Ingawa anawaheshimu sana mabwana shamba yeye anaona hafai heshima yoyote.

83. "Hivyo **Bi Kijakazi** utaendelea kufanya kazi namna hii mpaka lini?" Mkongwe alimwuliza.

    Kijakazi alishtuka kwani hajapata kuitwa **bibi** hata siku moja maishani mwake. Bibi aliyemjua yeye duniani ni **Bibi Maimuna** tu ambaye alifariki zamani.
    Unasemaje vile? **Umeniita Bibi**? Tafadhali usiniite hivyo; mimi ni **Kijakazi tu**."

    (Shafi, 1978, Ukur. 97)

Kwa mtazamo wa Kijakazi wanaoitwa 'mabibi' ni wale wenye mamlaka makubwa, kama vile Bibi Maimuna. Wanyonge kama yeye hawafai kuwa 'bibi'. Yeye anajiona kama mtu duni. Hapa tunamwona mnyonge ambaye hatambui kwamba hata naye, ingawa ni mtumishi, anafaa heshima. Inamaanisha kwamba mnyonge mwenyewe ndiye anayejidunisha hata mbele ya mnyonge mwenzake. Kwa Mkongwe, Kijakazi ni mtu mwenye heshima yake, hasa kwa mujibu wa umri wake. Hapa tunaona uolezi wa kijamii ulioshiriwa na tofauti kati ya matabaka. Wakati ambapo ni kawaida Maimuna, ambaye

ni mtu wa tabaka la juu kuitwa 'bibi', mtu wa tabaka la chini anajiona kama mtu asiyefaa cheo hicho. Mnyonge mwenyewe anaendeleza mahusiano ya kimamlaka ya aina hii.

Hali hii inalingana na ile tunayoiona katika riwaya ya *Asali Chungu* ambapo mnyonge (Dude) anaona kwamba matajiri ndio wanaostahili kucheka, sio wanyonge. Kwa hiyo, mnyonge mwenyewe anajidunisha na kuendeleza unyonge wake.

> [101] Dude hufikiria furaha wanayokuwa nayo matajiri. **Wao ndio** wenye furaha ya kweli; **Ndio** wanaojua kucheka. **Wao ndio** wanaostahili kicheko.
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 77)

Hali ya wanyonge kama Kijakazi na Dude inaonyesha kwamba mnyonge mwenyewe ameathirika kiasi kwamba kiolezi, yeye anajiona kama mtu ambaye yuko katika hadhi ya chini, wakati ambapo mabwana shamba au makabaila wako katika hadhi ya juu.

4.2.8.4 Uolezi wa Nafsi

Uolezi wa nafsi unadhihirika tukizingatia namna wanamapinduzi wanavyozungumza na Fuad. Wao sasa ndio wanaomwambia Fuad la kufanya, kuhusu mali iliyokuwa yake, yaani ardhi na magari. Uolezi wa nafsi unaonyesha tofauti ya kimamlaka:

84. Basi sisi tumekuja **kukujuvya** kwamba… **inakupasa ujue** kwamba … sasa **unaweza** kuendelea na kazi zako mpaka **tutakapokuletea** taarifa nyingine," alieleza yule mtu.

    "Nimesikia, Bwana! **Nimesikia**!"

    (Shafi, 1978, Kur. 54 -55)

85. Nakumbuka! Nakumbuka vizuri! Sielewi, **Bwana**, na itakuwa vizuri **ukinifahamisha**!

    (Shafi, 1978, Ukur. 55)

86. Si muhimu ikiwa **wewe** unaunga mkono au huungi mkono, **sisi** tumekuja kukwambia tu…

    (Shafi, 1978, Ukur. 59)

Katika madondoo ya 84 – 86 tunaona jinsi ambavyo hadhi ya Fuad imeshuka sana kutokana na mapinduzi ambayo yametokea ambapo wanamapinduzi wamechukua hatamu za uongozi wa serikali. Fuad, ambaye alidekezwa tangu utotoni mwake hajui jinsi ya kukabiliana na hali hii ngumu. Amezoea anasa tu. Yeye si mtu shupavu. Anawaogopa sana wanamapinduzi na kwa hivyo anatumia lugha ya kujidunisha sana. Uolezi wa nafsi unadhihirika katika maneno ya Fuad na maneno ya wanamapinduzi. Pengo kubwa la kimamlaka kati ya makundi haya mawili linadhihirika katika maneno ya wanamapinduzi. Tunapata mtazamio wao katika kauli mbalimbali wanazozitumia. Vitenzi '**kukujuvya**', '**inakupasa**', '**unaweza**' na '**tutakapokuletea**' vinamfanya msomaji ayaangalie yanayoendelea akiwa kwenye upande wa wanamapinduzi ambao sasa ndio wenye mamlaka wakiwa wanamwambia mnyonge Fuad la kufanya. Uolezi wa nafsi pia unabainika katika matumizi ya viwakilishi '**wewe**' na '**sisi**' ambavyo katika muktadha huu pia vinaonyesha pengo la kimamlaka lililopo kati ya aliyekuwa bwana shamba na wanamapinduzi ambao sasa ndio wana mamlaka.

Kwa upande mwingine, Fuad anaonyesha kutambua mamlaka waliyo nayo wanamapinduzi. Kauli zake zinazosisitiza nafsi ya kwanza, yaani '**nimesikia'** na '**ukinifahamisha'** zinaonyesha mtu aliye tayari kutii maagizo. Vitenzi vyote viwili vinaashiria kupokea. Fuad 'amesikia' na pia atatii maagizo 'akifahamishwa'. Wenye mamlaka watasema, na lake ni kusikia na kutii.

4.2.9 Matumizi ya Vitenzi vya Kitambuzi

Mbinu nyingine ya kileksika ambayo imetumiwa na waandishi wa riwaya teule ni matumizi ya vitenzi vya kitambuzi. Hivi ni vitenzi vinavyoonyesha michakato ya kiakili kama vile 'jua', 'elewa', 'fahamu', na 'ng'amua.' Matumizi ya vitenzi vya kitambuzi

yanatusaidia kuelewa tabia na mienendo ya wahusika, pamoja na maudhui yanayowasilishwa.

Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* tunaona mabadiliko ambapo Kijakazi ambaye hatambui haki zake, baadaye anang'amua kwamba wakati wote amekuwa akinyonywa na kabaila Fuad na kwamba sasa ni wakati wa kuzikata nyuzi za uhusiano huo wa kitumwa.

> 87. Mengi yaliyomjia kichwani usiku ule… Kwa mara ya kwanza **alifikiri** namna alivyopoteza maisha yake shambani pale… **Alifikiri** namna alivyomlea Fuad… hadi anampopoa kwa mateke…
>
> Kidogo kidogo **fikira** za Kijakazi **zilianza kufanya kazi**:
> "Kweli mimi ni maskini, mtu wa chini, sina mbele wala nyuma lakini hata ile heshima ya uzee hanipi….
> Kidogo kidogo… [Kijakazi] **Alianza kuona** kwamba utiifu wake wote aliokuwa nao kwa Fuad haungemsaidia chochote. **Alihisi** kuwa alivyozidisha utiifu wake ndivyo Fuad alivyozidi kiburi chake na kwa sababu hii **aliona** wakati umefika wa kumpa Fuad ukweli wake.
>
> (Shafi, 1978, Ukur. 83)

Kijakazi anapitia mabadiliko ya kimsingi ambapo fikira zake ndio 'zinaanza kufanya kazi'. Mabadiliko haya sio ya ghafla, bali yanatokea pole pole akilini mwake. Mwandishi ametumia vitenzi vya kitambuzi kuonyesha mchakato huu wa mabadiliko anaoupitia Kijakazi. Mwandishi anatumia kauli '**alifikiri'**, '**fikira zake zilianza kufanya kazi**', 'alianza **kuona**', '**alihisi** kuwa', na '**aliona**' kuonyesha jinsi mabadiliko yanavyoanza kutokea katika akili ya Kijakazi. Mabadiliko haya ndiyo yanayomtayarishia mapinduzi anayoyafanya katika ngazi yake kwa kukataa kuzifuata tena amri za Fuad. Ingawa Mkongwe amemshauri mara kadhaa kuhusu unyonyaji anaofanyiwa, Kijakazi hang'amui hili mpaka mchakato wa kitambuzi unapotokea akilini mwake. Akaanza kuwa mtu anayetathmini mambo, siye mtu anayefuata tu

maagizo ya kabaila. Fikira yake ya awali kwamba hali aliyomo ni majaliwa inatoweka. Mwandishi anasisitiza mchakato huu zaidi:

> 88. Haukupita muda **akang'amua** kuwa utiifu wake... ulikuwa hauna maana kwa Fuad.
>
> **Fikira za Kijakazi** zilizidi kubadilika. Alizidi **kuona** wazi kwamba maisha yake yote aliyapoteza pale kwa… **Alizidi kuamini** kwamba siku zote alikuwa akijidanganya…
>
> (Shafi, 1978, Ukur. 89)

Kauli zenye vitenzi vya kitambuzi katika dondoo hili zinadhihirisha jinsi ambavyo mnyonge anaendelea kubadilika kwa kutambua jinsi ambavyo amekuwa akinyonywa mwenye mamlaka. Kauli '**Fikira za Kijakazi zilizidi kubadilika**' inaashiria mchakato wa kufikiri. Kitenzi cha utambuzi '**aliamini**' kinaonyesha kuwa Kijakazi sasa ana hakika kuhusu yale ambayo alikuwa ameanza kuyahisi.

Suala la msamaha pamoja na mamlaka waliyo nayo wachungaji limegusiwa kupitia mbinu ya kileksika ya vitenzi vya kitambuzi. Askofu Joshua anaambiwa habari ya uongo na mke wake Lona kwamba mchungaji Boribori amemnyanyasa kimapenzi. Badala ya kuthibitisha ukweli wa habari hiyo, Joshua anataka kuchukulia sheria mikononi mwake.

> 89. [Joshua] alikwenda katika chumba cha kulala akashika bastola yake.…. **Aliona** ni vizuri kama atamwadhibu [Boribori] mwenyewe.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 139)

Kitenzi cha utambuzi '**aliona**' katika dondoo hili kinaonyesha jinsi ambavyo Joshua anajitwalia mamlaka ya Mungu ya kuadhibu binadamu mwenzake. Askofu Joshua ana utajiri na mamlaka makubwa kiasi kwamba anahofia usalama wake. Kwa hivyo, anamiliki bastola, ambayo yuko tayari kuitumia wakati wowote. Badala ya kumwacha Mungu akamwadhibu Boribori yeye (Joshua) '**aliona**' akamwadhibu Boribori mwenyewe, siyo kuzungumza naye, kumwombea au kumsamehe.

Kuhusu uwezo wa kifedha walio nao wachungaji tunaona maamuzi wanayoyafanya kulingana na uwezo huo. Mojawapo ya maamuzi hayo ni kuwapeleka watoto wao katika shule na vyuo vya bei, ambavyo wanyonge (waumini walio wengi katika makanisa ya wachungaji) hawawezi kuhimili gharama yake.

90. Wanawe wawili wa kike walisomea Chuo Kikuu cha Daystar kwa hiyo **aliona** asiwadhiki sana kwa kukaa Kibera.
(Habwe, 2005, Ukur. 43)

Kitenzi cha kitambuzi **'aliona'** kinatumiwa kubainisha mchakato wa uamuzi wa mchungaji Joshua wa kuwapekeleka watoto wake katika chuo cha kifahari. Kitenzi hicho kinaonyeshaa kwamba alifikiria vizuri kabla ya kuchukua uamuzi huo. Toni ya mwandishi ya kutopendelea uamuzi huo inabainika katika muktadha wa matumizi ya kitenzi hicho 'aliona'. Watoto wa mchungaji wanasomea katika vyuo vya bei ya juu wakati ambapo watoto wa watu wa kawaida (waumini katika makanisa ya wachungaji hao) hawana uwezo wa kifedha wa kuwapeleka watoto wao katika vyuo hivyo. Pia, mafundisho ya Kikristo hayasisitizi utajiri. Watoto wa waumini maskini wanaona dhiki, wakati ambapo yeye Joshua anaona 'asiwadhiki' watoto wake, kama kwamba anawadekeza.

Uwezo unaotokana na umiliki wa fedha na mali unadhihirika katika mawazo ya Amuko, Mkristo tajiri mmojawapo aliyekuja katika kanisa la New Jerusalem kuombewa na Mchungaji Michael.

91. Kitu kimoja **aliamini** ni kuwa atampigia ahsante yule kijana maskini, Michael.
Aliamua ampe moja katika magari yake.
Alifikiria ampe lile gari la *Peugeot*.
(Habwe, 2005, Ukur. 47)

Vitenzi vya kitambuzi vilivyotumika katika dondoo vinaashiria uwezo anaouhisi Amuko, ukilinganishwa na uwezo wa mchungaji Michael. Huu ni uwezo unaotokana

na ukwasi mkubwa wa Amuko, ingawa ukwasi huu unatokana na ufisadi anaoufanya serikalini. Mchakato wa uamuzi wa Amuko unaodhihirika katika matumizi ya vitenzi vya kitambuzi vifuatavyo: '**aliamini**', '**aliamua**' na '**alifikiria**'. Haoni haja ya kumuuliza Michael ikiwa atakubali kupokea zawadi ya gari au zawadi nyingine yoyote. Kitenzi '**aliamini**' kinaonyesha kuwa hana wasiwasi wowote kuhusu uwezo wake pamoja na hitaji la yule anayetaka kumpa zawadi. Halafu anaamua kumpa Michael gari kwa vile uwezo anao. Hata ni gari mojawapo tu kati ya magari kadha anayoyamiliki. Kinachomsumbua tu ni kuchagua ampe gari lipi kati ya magari yake.

4.3 Muhtasari wa Sura

Sura hii imeangazia uteuzi wa kileksika kama kipengele cha kimtindo katika kusawiri na kuchimuza maudhui kuhusu dini na mamlaka katika riwaya teule za Kiswahili. Mbinu za kileksika mbalimbali zimeangaziwa, kama vile matumizi ya visawe, matumizi ya kinyume, urudiaji, kuhamisha nomino kutoka ngeli moja hadi nyingine, msamiati wa kitathmini, na msamiati unaoonyesha uolezi. Kwa mujibu wa data, mbinu iliyotumiwa na waandishi wote ni urudiaji. Hii ni kwa sababu urudiaji ni mbinu muhimu ya kusisitizia ujumbe na kuhakikisha kwamba unakumbukika. Uchambuzi wa data umeonyesha kwamba riwaya ya *Paradiso* ya Habwe (2005) ndiyo imedhihirisha mbinu zote za kileksika isipokuwa mbinu ya uhamishaji katika riwaya yake ya *Paradiso*. Tofauti na riwaya nyingine, riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad,* haikuzingatia sana mbinu za kileksika ili kusawiri maudhui kuhusu mamlaka. Isipokuwa urudiaji, uolezi na kauli chache zinazoonyesha vitenzi vya kitambuzi, mwandishi wa riwaya hii hakutumia mbinu zingine za kileksika katika kutoa ujumbe wake. Sura inayofuata inachunguza nduni za kisintaksia zilizotumiwa kimtindo katika riwaya teule za Kiswahili ili kusawiri maudhui ya dini na mamlaka.

SURA YA TANO

MATUMIZI YA NDUNI ZA KISINTAKSIA KATIKA KUCHIMUZA MAUDHUI YA DINI NA MAMLAKA KATIKA RIWAYA TEULE

5.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeangazia uteuzi wa kileksika kama kipengele cha kimtindo katika kusawiri maudhui kuhusu dini na mamlaka katika riwaya teule. Mbinu kadhaa za kileksika, mkiwemo matumizi ya visawe, matumizi ya kinyume, urudiaji, kuhamisha nomino kutoka ngeli moja hadi nyingine, na kadhalika ziliangaziwa. Katika sura hii tunashughulikia lengo la pili la utafiti huu kwa kuchanganua nduni za kisintaksia zinazotumiwa kimtindo katika riwaya teule za Kiswahili ili kusawiri maudhui. Mbinu za kisintaksia tulizozizingatia ni za kiusambamba, pamoja na mbinu ya matumizi ya kauli ya kutendwa, ambayo inadhihirisha ukiushi. Mbinu za kiusambamba zilizobainika katika riwaya ni zifuatazo: anafora, epifora, tanakuzi, muundogeu, mjalizo, usambamba kiusawe, mgeuko wa polepole, urudiaji, udondoshaji, na uorodheshaji.

5.1 Usambamba

Dhana hii ilifasiliwa katika sehemu 2.3.1.2.2. Usambamba unahusisha ulinganifu wa kimuundo wa sehemu mbili za usemi ambazo zina ukinzani kimaana. Katika matumizi ya usambamba msanii anayarudia maneno au maana fulani katika vipashio tofauti vya kisintaksia – virai, vishazi, au sentensi.

Mbinu mbalimbali za kiusambamba zimetumiwa na waandishi wa riwaya teule tulizochanganua ili kuibua maudhui mbalimbali. Miongoni mwa mbinu hizi ni pamoja na anafora, epifora, mjalizo na uorodheshaji.

5.1.1 Mbinu ya Anafora (Pia Epanafora)

Wamitila (2003) anaeleza kwamba anafora ni mbinu ya kibalagha au kiusemi ambayo inahusisha kurudia neno au kundi la maneno katika vishazi au sentensi zinazofuatana. Ni aina mojawapo ya usambamba. Naye Michira (2018) anaelekea kukubaliana na maelezo ya Wamitila anapofafanua kwamba anafora ni mbinu ya kibalagha ambapo neno, au mfuatano wa maneno unarudiwa mwanzoni mwa sentensi, vishazi au virai vinavyofuatana. Mfuatano huo unaunda ruwaza yenye ridhimu pamoja na msisitizo unaotokana na urudiaji. Mbinu hii imetumiwa na waandishi wa riwaya za utafiti huu kuwasilishia maudhui mbalimbali.

Katika riwaya ya *Paradiso*, mbinu ya anafora imetumiwa kuibua maudhui ya wivu, chuki na ufarakano katika makanisa ya kiprotestanti. Migogoro katika makanisa na baina ya makanisa imesababishwa na tamaa na ulafi wa vitu vya dunia. Viongozi wa makanisa wanashindania uongozi kwa sababu ya zaka na matoleo kutoka kwa waumini. Badala ya kusikilizana kama ndugu wa Kikristo wachungaji na baadhi ya waumini wao wanaamua kutengana.

> 92. **Kundi la Michael** lilisisitiza kuna uhuru wa kukaa hali **kundi la Joshua** lilitaka liondoke. **Kundi la Joshua** lilidai kuwa ndilo lenye haki tu kuwepo katika jengo hili.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 76)

Migogoro iliyomo ndani ya kanisa imesisitizwa na urudiaji wa kirai '**kundi la…**', ambacho kimerudiwa mara tatu. Urudiaji huu ni njia ya kusisitiza mgawanyiko uliopo kati ya wachungaji, hasa Michael na Joshua. Urudiaji huu katika vishazi viwili vinavyounda sentensi ya kwanza tayari unachimuza suala la mgawanyiko. Urudiaji huu ungeweza kuepukika ikiwa mwandishi angedondosha nomino 'kundi' na badala yake akatumia kiwakilishi chake 'lile', yaani kwa kusema: '**Kundi la Michael** lilisisitiza kuna uhuru wa kukaa ilhali ***lile la*** Joshua lilitaka liondoke.' Hii ni kwa sababu msomaji

anajua tayari kwamba kinachozungumziwa ni makundi, kwa vile sehemu ya kiima ‘kundi la’ imekwishatajwa. Kwa hiyo, mwandishi anaporudia kirai ‘**kundi la…’** mara ya tatu, kwa njia fulani, anakiuka kanuni ya ikitisadi katika lugha ambayo inasisitiza matumizi ya kiwakilishi katika tungo inayofuata, pale ambapo nomino kiima tayari inajulikana. Urudiaji wa kirai ‘kundi la …’ mwanzoni mwa kishazi cha tatu mfululizo ndiko kunakomshtua msomaji na kumfanya azingatie suala linalozungumziwa, yaani kanisa kujitenga katika makundi, kitu ambacho ni kinyume na msingi wa kanisa la Kristo. Waumini sasa wamejitenga katika makambi ya viongozi wao. Askofu Joshua hataki kabisa Michael (mhubiri mwenzake) aendelee kuhudumu katika kanisa lao la New Jerusalem, ingawa Michael yuko radhi kutafuta suluhisho la hali hii. Kanisa linashindwa kuwa mfano kwa jamii kuhusu jinsi ya kushirikiana, kuwa na umoja, kutafuta njia za kuridhiana, pamoja na kuepukana na tamaa ya vitu vya dunia ambayo ndiyo hasa chanzo cha migogoro na ufarakano katika jamii. Mwandishi anaeleza bayana kwamba mgawanyiko katika kanisa unatokana na wachungaji kujitafutia riziki (Habwe, 2005, Ukur. 220).

Katika riwaya ya *Paradiso,* Habwe anazungumzia kanisa kielelezo. Hili tunalipata kupitia kwa maneno ya mhusika Michael, ambaye ni mhusika kielelezo.

> 93. Michael alikuwa na maono ya kanisa la Yesu. Kanisa hili si la kuvunjikavunjika kama amiba. **Ni kanisa la** umoja. **Kanisa la** msamaha. **Kanisa la** utekelezaji na kutumaini mwisho. … KANISA LA PARADISO.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 225)

Kanisa ambalo ni kielelezo analoonyeshwa Michael katika maono limetolewa sifa kwa njia ya usambamba wa kianafora. Maneno “**kanisa la**” yamerudiwarudiwa mara tatu. Maneno hayo yanafuatwa na sifa chanya ambazo mchungaji Michael anaona zinafaa kuwa ndizo zinazolitambulisha kanisa la Yesu au kanisa la paradiso. Sifa hizo ni

'umoja', 'msamaha', pamoja na 'utekelezaji na matumaini.' Vifungu '**la** umoja', '**la** msamaha', na '**la** utekelezaji na kutumaini' ni virai vihusishi vinavyofanya kazi kama vivumishi vya nomino 'kanisa'. Kwa vile kazi ya kivumishi ni kuelezea nomino, tunaona jinsi ambavyo mwandishi anatumia urudiaji wa tungo zinazofanya kazi kama vivumishi kianafora ili kuchimuza ujumbe wake. Nomino inayoelezewa ni 'kanisa'.. Zaidi ya hayo, mwandishi anachimuza maneno 'kanisa la paradiso' kigrafolojia kwa kutumia herufi kubwa ili kuakisi anwani ya riwaya yake. Mwandishi anatoa maudhui kwamba tofauti na kanisa kielelezo la Yesu, makanisa mengi yanafanya kinyume na sifa hizo zilizotajwa.

Hwandishi wa *Paradiso* pia anaelezea nafasi ya kanisa maishani mwa waumini. Wakati ambapo baadhi wanakwenda kanisani kutafuta injili ya kweli, wengine wanakwenda kanisani wa sababu zisizo za kidini.

94. Kibera nzima Jumapili ilikuwa kama uwanja wa disko. **Kunao** waliofanya ya shari. Pia, **kunao** waliofanya ya shwari. **Kunao** ambao makanisa yalikuwa kama vyama vya ushirika kwamba mtu akifa aweze kufanyiwa mchango wa kusafirishwa nyumbani. **Kulikuwa na makanisa ambapo** watu walikwenda kutupa wakati kwa sababu ya uvunjifu. **Mengine yalikuwa ni mahali pa kwenda kama mazoea** bila kuwepo na sababu maalum. Bethany lakini kilikuwa mfano wa kilima cha Zayuni ambapo mtu angeweza kutafuta toba na suluhu ya kweli kwa Bwana.
(Habwe, 2005, Ukur. 113)

Katika dondoo hili, mwandishi ametumia mbinu ya anafora kulinganua sifa hasi na sifa chanya katika makanisa ambapo kuna waumini waliofuatilia msingi hasa wa kwenda kanisani, yaani waliofanya ya shwari. Bethany inatajwa kama kanisa lililozingatia msingi wa Ukristo. Lakini sifa hasi ndizo ambazo zimezingatiwa hasa na mwandishi. Anaeleza kwamba baadhi ya makanisa yalitumiwa kama vyama vya ushirika, mengine yalitumiwa kama mahali pa kupotezea wakati, na mengine yalikuwa mahali pa kwenda

kama mazoea tu. Kuna kinaya kwamba, ingawa makanisa katika eneo la Kibera ni mengi sana, mengi ya makanisa haya hayazingatii msingi wa Ukristo.

Mbinu ya anafora pia imetumiwa kuibua maudhui ya ufisadi. Ingawa riwaya ya *Paradiso* imeangazia mambo yanayoendelea makanisani hasa, tunaona jinsi mwandishi anavyogusia uhusiano kati ya makanisa na watu wanaotoka katika asasi zingine nje ya kanisa. Mathalan, kanisa huyamulika maovu yanayoendelea katika jamii. Mwandishi ameangazia suala la ufisadi na jinsi watu fisadi wanavyoleta pesa au mali kanisani. Tunamwona mhusika Amuko akitumia ufisadi kujitajirisha. Kutokana na ufisadi, sasa ana magari na "nyumba ambazo hazihesabiki", ambazo pia zinamwingizia kipato.Kipato kikubwa ni msingi wa mamlaka ya kudhibiti mambo mbalimbali maishani. Amuko hayuko tayari kuiacha paradiso yake ya hapa duniani ili kumtumikia Mungu.

95. **Ataacha vipi** ulevi? **Ataacha vipi** wapenzi wake wa kike? **Ataacha vipi** ufisadi wake wa ofisini ambao ndio umemletea magari kochokocho aliyo nayo na nyumba ambazo hazihesabiki.
(Habwe, 2005, Ukur. 41)

Katika dondoo mwandishi anarudiarudia kirai "**ataacha vipi"** mwanzoni mwa kila kishazi. Kauli hiyo imefuatwa na faridi ambazo zina uhusiano fulani kwa vile zote ni hasi, yaani ulevi, wapenzi wa kike, na ufisadi. Mwandishi anatumia urudiaji wa kianafora kukemea mambo hayo. Kila kishazi chenye kirai kinachorudiwarudiwa kinajitokeza kama swali la balagha. Hii inaonyesha hisia za mtunzi kuhusu mambo yanayozungumziwa. Faridi hizi zote ni vitendo ambavyo jamii inavikemea. Lakini, tofauti na vishazi viwili vya kwanza ambavyo ni sentensi sahili, tungo ya tatu kwenye mfuatano wa vishazi ni sentensi changamani yenye kishazi huru na kishazi kitegemezi. Mwandishi angesema tu "Ataacha vipi ufisadi?" ili muundo wa kishazi hiki ulingane

na muundo wa vishazi vya awali. Kusudi la mwandishi kubadilisha muundo katika kishazi cha tatu ni kulisisitiza suala la ufisadi kupitia kwa maelezo ya ziada. Inaonekana kwamba, tofauti na vitendo vingine visivyo vya kimaadili ambavyo amevitaja (ulevi na wapenzi wa kike), mwandishi anaona kwamba ufisadi ndio una athari kubwa kwa jamii kuliko vitendo hivyo. Muundo wa ndani wa kishazi kitegemezi "ambao [ufisadi] ndio umemletea magari kochokocho aliyo nayo na nyumba ambazo hazihesabiki" ni "Ufisadi ndio umemletea [Amuko] magari kochokocho aliyo nayo na nyumba ambazo hazihesabiki." Sentensi hiyo kwenye muundo wa ndani inasisitiza maudhui ya ufisadi, na mhusika Amuko ametumiwa kuwasilisha maudhui haya. Tena, tunaona baadhi ya vitu ambavyo Amuko amevipata kutokana na ufisadi – kama vile magari – vinatolewa kwa makanisa kama zawadi. Nguvu ya umiliki wa vitu hivi inamdhibiti Amuko. Anaona shida kuviacha.

Akitumia mbinu ya anafora, mwandishi wa riwaya ya *Paradiso* ameibua maudhui ya rushwa, mauaji na udanganyifu katika jamii. Suala la ulaghai limesisitizwa na mwandishi katika sehemu zingine mbalimbali za riwaya hii. Katika dondoo lifuatalo, tunapata vishazi vitatu ambavyo vyote vimejitokeza kama maswali ya balagha.

96. **Ni wangapi** walao rushwa? **Ni wangapi** wauao? **Ni wangapi** wadanganyao?"

(Habwe, 2005, Ukur. 130)

Dondoo la 96 linawasilisha mawazo ya Lona, ambayo yametolewa kianafora katika sentensi tatu zenye muundo unaolingana. Sentensi zote tatu ni changamani, zenye kishazi huru na kishazi kitegemezi. Kishazi kitegemezi kinataja vitendo visivyo vya kimaadili wanavyofanya baadhi ya Wakristo anaowarejelea Lona. Lakini nomino inayowarejelea Wakristo hao imedondoshwa. Hata hivyo muktadha unaashiria kwamba ni Wakristo wanaofanya vitendo visivyo vya kimaadili vinavyotajwa kiusambamba

katika sentensi hizo. Sentensi zote tatu ni maswali ya balagha kwa vile yanaonyesha fikira nzito za mhusika Lona. Anajaribu kuhalalisha msingi wa mwenendo wake kwamba, kwa vile wengine wanafanya vitendo hivyo visivyo vya kimaadili, hamna ubaya naye akishiriki katika kuvifanya.

Matumizi ya muundo wa sentensi unaolingana yanaashiria ulinganifu wa uzito wa faridi zinazotajwa. Kwa kuvitaja vitendo visivyo vya kimaadili katika sentensi tatu zinazolingana kimuundo, mwandishi anaashiria kwamba vitendo vyote vitatu vina uzito unaolingana. Usawe fulani wa kisemantiki umeashiriwa kati ya vitendo hivyo vitatu: kula rushwa, kuua na kudanganya. Ni vitendo vibaya sana ambavyo kila Mkristo anafaa kuepukana navyo. Kusudi la mwandishi la kuvitaja vitendo hivi katika sentensi tatu tofauti kiusambamba ni kuvichimuza. Anataka msomaji ahisi uzito wa kila kitendo kinachofanywa na Wakristo, na tena jinsi kasisi Lona anavyojaribu kujipa moyo kuhusu vitendo vyake visivyo vya kimaadili pia.

Mwandishi wa riwaya ya *Paradiso* anasawiri maudhui ya unafiki miongoni mwa wachungaji. Lona anajifanya kama Mkristo anayetaka kwenda paradiso ya baadaye, wakati ambapo anaendelea kujenga paradiso yake hapa duniani kwa kufanya chochote kile, mkiwemo vitendo vilivyotajwa katika dondoo la 96, yaani kula rushwa, kuua au kudanganya. Mwandishi anatoa maoni yake kuhusu hali hii kwa kutueleza kwamba “Lona na mumewe walipoteza nadhiri yao ya ndani; nadhiri ambayo ingewaongoza kutenda wema na kuendesha neno la Bwana” (Habwe, 2005, Ukur. 131).

Habwe pia anasawiri maudhui ya tamaa na utashi wa mali unaodhihirishwa na wachungaji. Amefanya hivi kwa kutofautisha tabia ya wachungaji hawa na mwenendo wa Yesu. Wakati ambapo wahubiri wengine kama Joshua na Boribori wana tamaa ya

mali za dunia, wahubiri wengine, kama vile Michael (angalau kabla hajateleza) hawajali sana mali.

97. [Michael] alitaka kuwa kama Yesu… [Yesu] **Hakuwa na** kwake. **Hakuwa na** gari. **Hakuwa na** mke. **Hakuwa na** nyumba.
(Habwe, 2005, Ukur. 44)

Katika dondoo la 97, tunaona kishazi cha kwanza ambapo kauli inayotaja hoja kuu inayomwonyesha Yesu kama mfano kwa Wakristo wote imetangulizwa. Kauli hiyo inafuatwa na vishazi huru vinne – vyote vyenye muundo sawa. Hii inaashiria ulinganifu wa ujumbe katika vishazi hivi vinne. Baada ya kirai '**hakuwa na…**' kinachorudiwarudiwa, kumetajwa vitu ambavyo Yesu hakuwa navyo. Hii inaonyesha kwamba vitu hivyo si vya msingi kwa Mkristo kwa vile hata Yesu hakuwa navyo. Katika *Paradiso* inadhihirika kuwa, kinyume na mfano huu wa Yesu, Wakristo wengi, hata wachungaji, wanavipa vitu hivi kipaumbele. Ni dhahiri kwamba anayetaka kuwa Mkristo wa kweli ni lazima afuate mfano wa Yesu. Njia mojawapo ya kuwa Mkristo mwema ni kutovitamani vitu vilivyotajwa. Mtu kujiita Mkristo wakati ambapo hafuati mfano wa Yesu inakuwa ni kinaya.

Kwa kuvitaja vitu ambavyo Yesu hakuwa navyo katika vishazi tofauti, badala ya kuviorodhesha, mwandishi anavichimuza. Kama angeviorodhesha tu vitu hivyo, yaani akasema tu: "Yesu hakuwa na kwake, gari, mke, na nyumba", msomaji asingeihisi ile athari ya msisitizo unaotokana na upangaji wa kiusambamba. Kwa kuvitaja vitu hivyo kimoja baada ya kingine katika sentensi fupifupi kianafora, msisitizo wa kila faridi unabainika. Ni dhahiri kwamba mwandishi anakiuka kanuni za lugha kwa kuziweka faridi katika sentensi. Mwandishi anafanya uchaguzi kimaksudi kutumia muundo uliokiuka kanuni ya lugha ya kutorudiarudia vitu ambavyo vingetajwa katika orodha tu.

Mbinu ya anafora imetumiwa katika riwaya ya *Paradiso* kuangazia jinsi kazi ya Mungu ilivyo. Ni kazi ambayo si nyepesi, inayohitaji mtu kujitoa mhanga.

> 98. …lakini hivyo ndivyo ilivyo kazi ya Mungu. **Ina** milima. **Ina** mabonde. **Ina** vilio. **Ina** vicheko.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 68)

Dondoo hili linaonyesha dhahiri kwamba kazi ya Mungu ina changamoto lakini inafurahisha. Mwandishi ametumia mbinu ya usambamba kuonyesha hali hizi mbili kwa njia ya kutaja kila hali na kinyume chake: milima inawakilisha changamoto katika kuifanya kazi ya Mungu. Nayo mabonde (kinyume cha milima katika mkutadha huu) yanawakilisha wepesi. Vilio vinawakilisha hali isiyo na furaha, na vicheko vinawakilisha furaha iliyomo katika kuifanya kazi ya Mungu. Anayefanya kazi ya Mungu ni lazima awe tayari kwa hali hizi mbili ikiwa anataka kufika paradiso ya baadaye. Michael yuko tayari kumfanyia Mungu kazi katika hali yoyote, wakati ambapo watu kama Amuko wanaona shida kumfanyia Mungu kazi.

Mbinu ya anafora imetumiwa pia na mwandishi wa riwaya ya *Asali Chungu* kuwasilisha maudhui ya unyonge na kukata tamaa miongoni mwa raia fukara. Katika sura ya kwanza ya riwaya hii tunaona hali ya kukatisha tamaa ya wanawake, mkiwemo wakongwe, ambao wamekuja kumwona Bwana DC kuhusu matatizo yao, ambayo chanzo chake (matatizo hayo) ni yeye mwenyewe. Hiki ni kinaya. Toni ya kukata tamaa inadhihirika katika mazungumzo ya wanawake hawa:

> 99. Nawe unataraji nini kwa bwana huyu?
> **Pana la** kutaraji bibi we. **Pana la** kuja tukirudi tu, angalau kudanganya roho…
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 3)

Mwandishi anatumia mbinu ya usambamba wa kianafora ili kuonyesha unyonge ukikabiliana na mamlaka. Sentensi ya swali inatangulia vishazi vyenye maneno yaliyorudiwa kiusambamba. Sentensi hiyo inajitokeza kama swali na inaweka msingi

wa toni ya hali ya wanawake ambao wamekuja kumwona Bwana DC. Swali hilo linaonyesha kuwa hakuna matarajio yoyote. Jibu lenyewe linapatikana ndani ya swali kwa vile toni ya swali tayari inaonyesha kwamba hakuna la kutaraji kwa Bwana Zuberi, mtu asiyemjali mnyonge. Hata hivyo, mwanamke mmoja anatoa jibu la swali hilo kiusambamba katika vishazi viwili vinavyotangulia kwa kutumia kirai "**pana la…**" Ingawa vishazi vyote viwili vinavyofuatana vinatangulia kwa kirai hicho, kiundani taarifa iliyomo katika vishazi hivyo inakinzana. Kijuujuu, kishazi cha kwanza kinataja kwamba kuna matarajio. Lakini kishazi cha pili kinaonyesha kwamba hakuna matumaini, kwa vile mwanamke anayejibu anaonyesha kwamba kuja kumwona Zuberi ni kama kudanganya roho tu. Kwa hivyo, usambamba hapa umetumiwa kudhihirisha hali hiyo ya kweli kinzani ambayo inahusisha kinaya.

Hali nyingine inayotuonyesha mahusiano kati ya wenye mamlaka na wanyonge katika *Asali Chungu* ni pale Biti Daudi anapotumia mbinu hii ya anafora katika kujaribu kumshawishi msichana Semeni akubali kufanya mapenzi na Zuberi. Lengo mojawapo la mbinu ya usambamba katika balagha ni kumshawishi msikilizaji au msomaji.

> 100. **Kuna** walionunuliwa nyumba mama [**kuna**] waliofuliwa vyombo vya dhahabu kochokocho; **kuna** walioandikiwa vikataa na mashamba ya fahari; **kuna** wanaovaa na kubadili; [**kuna**] wanaotumia maisha yao bila ya kujua pesa inaingia wapi inatokea wapi. Nini basi? … iweje mama, bwana kama huyu kakutaka wewe usimjamili? Huoni kwamba unajiharibia hivyo? Eee mwana, unajivunjia riziki zako we!
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 17)

Katika nukuu hii, tungo sambamba zote zinaanza na kitenzi '**kuna**', ingawa katika tungo ya pili na ya tano kitenzi hicho 'kuna' kimedondoshwa. Mwandishi anakidondosha kitenzi hiki ili ageuze muundo wa tungo kidogo, asije akamchosha msomaji. Nomino kiima 'watu' pia imedondoshwa kwa vile muktadha unaonyesha kuwa mwandishi anazungumzia watu, sio viumbe wengine. Neno linadondoshwa pale

ambapo inatarajiwa kwamba msomaji anaweza kutabiri neno lililokusudiwa, hata kama halikutajwa. Kitenzi 'kuna' kinafuatwa na kishazi kitegemezi cha urejeshi katika tungo za kianafora. Kishazi hiki kitegemezi kingebebwa na nomino ambayo haikutajwa. Kishazi hiki kinafanya kazi kama kivumishi. Kazi ya kivumishi ni kutoa sifa za kitu. Kwa hiyo, kwa kurudia tungo zinazofanya kazi kama vivumishi, msemaji anasisitiza ujumbe wake, yaani manufaa ambayo yatamjia Semeni akikubali kufanya mapenzi na Zuberi. Isitoshe, vishazi hivyo vilivyobebwa vinaonyesha uwezo wa kifedha alio nao Zuberi. Anatumia uwezo huu kujipatia mapenzi na wasichana wadogo akina Semeni. Semeni ni fukara kabisa, hana chochote, na Biti Daudi anamtajia yale yote ambayo hangeweza kuyapata, lakini ambayo sasa yanawezekana pindi akikubali kufanya mapenzi na Zuberi.

Unyonge unaotokana na ufukara umedhihirishwa pia tukimwangalia mhusika Mzee 'Kheri Karibu' katika riwaya ya *Asali Chungu*. Huyu ni mzee mlemavu wa macho, masikio na miguu. Anapata riziki kwa kuombaomba tu mbele ya msikiti. Kheri Karibu ana tabia ya kucheka kila mara, kitu kinachomshangaza Dude, kwa vile yeye haoni namna mzee huyo anavyoweza kuendelea kucheka wakati ambapo yuko katika hali ya kusikitisha. Dude anaona kwamba matajiri ndio wana sababu ya kucheka.

> 101. Dude hufikiria furaha wanayokuwa nayo matajiri. **Wao ndio** wenye furaha ya kweli; [**Wao**] **ndio** wanaojua kucheka. **Wao ndio** wanaostahili kicheko.
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 77)

Katika dondoo, tunaona jinsi ambavyo mwandishi ameangazia pengo lililopo kati ya wenye nacho na wasio nacho katika jamii. Kwa kutumia mbinu ya anafora, mwandishi anaonyesha jinsi ambavyo matajiri wana kila kitu kinachowawezesha kuwa na furaha na hivyo kucheka. Faridi zilizoonyeshwa baada ya kifungu '**wao ndio**' zinadhihirisha kinaya, mwandishi anaposema kwamba matajiri ndio wana 'furaha ya kweli',

‘wanaojua kucheka’ na tena’wanaostahili kucheka’. Fikira hizi za Dude zinatokana na kuvunjika moyo kwa sababu ya hali yake ya ufukara pamoja na ya watu wengine wenye ufukara kama yeye. Maneno ya Dude yanaashiria kwamba kicheko hakiambatani na mtu maskini, kwani ni nini kitakachomfanya acheke wakati ambapo ana shida ya kiuchumi? Kwa upande mwingine, tajiri anaonyeshwa kama mtu ambaye ana sababu ya kucheka kwa vile ana pesa na mali; hana shida ya kiuchumi. Lakini hii si kweli, kwa vile tunaona jinsi ambavyo tajiri Zuberi anaona huzuni kubwa kwa yaliyomfika – uzee na ugonjwa, pamoja na kujutia kumbaka Semeni na matokeo ya kitendo hicho. Ingawa bado ni tajiri, hana sababu ya kucheka. Anahuzunika tu, hata kama aliyoyafanya nyuma dhidi ya mnyonge yalikuwa yanampa furaha kubwa.

Said Ahmed Mohamed (1978) anasawiri maudhui ya kikomo cha uwezo wa pesa na mali. Hii inadhihirika tunapoona jinsi mhusika Amina – bibi mwenye pesa na mali – anavyoshindwa kuizuia ndoa kati ya Dude (aliyekuwa mpenzi wake) na Shemsa, binti yake. Anafikiri kwamba kauli yake moja tu ‘Shemsa haolewi na Dude’ itatosha. Lakini anagundua kwamba mwenye mamlaka ya kweli kuhusu watoto ni mumewe Zuberi, yaani baba ya watoto wake.

> 102. **Leo ati** Amina anashindwa na la kufanya. **Leo ati** anaogopa watu kujua siri yake. **Leo ati** yeye na Biti Daudi wake wanachelea aibu na fedheha…
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 152)

Mwandishi ametumia mbinu ya anafora kuonyesha vile ambavyo aliyekuwa na mamlaka sasa amekuwa mnyonge. Awali, Amina na Biti Daudi wangeweza kupanga na kufanikiwa kutekeleza lolote. Lakini sasa mambo yamebadilika na wao sasa ni wanyonge. Mwandishi amerudiarudia kifungu elezi “**leo ati**” mwanzoni mwa vishazi vitatu vinavyofuatana. Maneno hayo yanaleta hisia za mshangao kuhusu mabadiliko yaliyotokea ambapo mabibi hawa wawili, ambao awali hawakushindwa katika mpango

wao wowote, sasa nao wanaweza kushindwa kutekeleza jambo. Baada ya kifungu elezi "**leo ati**" mwandishi anatuelezea hulka ya Amina na mshauri wake Biti Daudi. Vishazi viwili vya kwanza vinamsawiri Amina kama mtu ambaye hashindwi katika mipango yake. Katika kishazi cha pili, ameelezwa kama mtu ambaye haogopi watu kumsema. Kishazi cha tatu kinawazungumzia kwa pamoja Amina na Biti Daudi. Wanaelezwa kama mabibi wasioona aibu na fedheha. Lakini, kuna usawe fulani wa kisemantiki kati ya kishazi cha pili na kishazi cha tatu ambapo kishazi kinamtaja Amina kama mtu asiyeogopa siri zake kujulikana; na kishazi cha tatu kinamwelezea kama mtu asiyeona aibu. Huu ni msisitizo ambao unamfanya msomaji amchunguze mhusika huyu kwa makini. Inabainika kwamba Amina amekuwa akifanya mapenzi na kijana mdogo Dude bila kuchelea kusemwa na watu. Hii ni kutokana na yeye kujihisi mwenye uwezo mkubwa wa pesa na mali.

Jambo la unyonyaji wa wanyonge limegusiwa katika riwaya za *Asali Chungu* na *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Katika riwaya ya *Asali Chungu* tunaona jinsi ambavyo Bi Elisi, Bi Mwanakweli, Bi Mkasi na wafanyakazi wengine wananyonywa na kabaila Zuberi. Aidha, katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* tunaona jinsi mhusika Kijakazi, ambaye ni mtumishi wa nyumbani, anavyonyonywa na mabwana shamba:

> 103. …kawaida yake ni ile ya uchovu, ya mtu aliyechakaa, mwenye mikono iliyojaa visuguru na visigino vya miguu vilivyolika kwa kwenda, **si** mvua, **si** jua; **si** usiku **si** mchana, kazi hazikumwisha Kijakazi.
>
> (Shafi, 1978, Ukur. 2**)**

Tunamwona Kijakazi, msichana aliyezaliwa katika ufukara, akitarajiwa kufanya kazi wakati wote. Mwandishi anaonyesha kwamba msichana huyu anafanya kazi bila kupumzika. Kutopumzika kwa Kijakazi kumeakisiwa katika lugha anayoitumia mwandishi. Mwandishi anatumia virai vinne mfululizo. Vyote vinaanza na neno

kanushi ‘**si**’. Baada ya neno hilo kunafuata nomino zinazorejelea hali ya hewa, kisha zile zinazorejelea wakati. Badala ya kusema tu “Kijakazi alifanya kazi bila kupumzika katika hali yoyote na wakati wowote”, mwandishi anarudiarudia kauli ili msomaji ahisi kwa kweli msichana huyu anatendewa ukatili. Kwa hiyo, mwandishi anatumia njia ya anafora ili kuchimuza ujumbe wake kwa msomaji.

Baadhi ya wafanyakazi wa mabwana shamba wanazijua haki zao na wanatambua jinsi wanavyonyonywa na mabwana shamba hao. Mmojawapo wa hawa ni Mkongwe, mfanyakazi mwenzake Kijakazi. Tofauti na Kijakazi, Mkongwe hayuko tayari kufanya kazi kitumwa. Anatambua kwamba bwana shamba Fuad hawajali wafanyakazi wanyonge hata kidogo.

> 104. Nimechoka kutumwa na kusumbuliwa na Fuad. Mtu huyu **hana** wema wala ihsani. **Hana** fadhili, ni mtovu wa adabu.
> (Shafi, 1978, Ukur. 68)

Kama ilivyo katika tungo nyingi za kianafora, tunapata tungo ya kwanza ambayo inatangulia tungo zilizopangwa kianafora. Katika dondoo la 104, sentensi ya kwanza inatanguliza kauli ya hali iliyopo. Kisha tunapata sentensi mbili ambamo kitenzi kanushi ‘**hana**’ kimerudiwa mara mbili. Katika tungo ya kwanza, kiima cha kimuundo, yaani kwa mujibu wa mpangilio wa vipashio ni ‘Mkongwe’, ingawa kiima cha kimantiki, yaani mtendaji ni ‘Fuad’. Fuad ndiye anayemtuma na kumsumbua Mkongwe. Iingawa kiima hicho cha kimantiki kinajulikana tayari (yaani Fuad), tunaona katika kishazi cha kwanza kwenye mpangilio wa kianafora mwandishi anatanguliza kirai nomino ‘**mtu huyu**’ ambacho kingedondoshwa; yaani sentensi ya pili ingeanza na kirai kitenzi ‘hana wema” tu. ‘Mtu huyu’ ni Fuad, ambaye jina lake linajitokeza mwishoni mwa sentensi iliyotangulia. Pia, muundo wa ndani wa tungo “**hana** wema wala ihsani” ni sentensi mbili zinazounda sentensi ambatani: “[Fuad] **hana** wema *wala*

[Fuad **hana]** ihsani". Kwa hivyo, hata kama katika muundo wa nje, neno '**hana**' linajitokeza mara mbili, kwa kweli neno hilo linajitokeza mara tatu, tukizingatia muundo wa ndani wa sentensi.

Katika sentensi ya tatu kiima (Fuad au 'mtu huyu') kimedondoshwa kabisa kwa vile kimekwisharejelewa mara mbili. Tungo ya tatu, ingekuwa ni sentensi ambatani, yaani "Hana fadhili na ni mtovu wa adabu. Lakini badala ya kiunganishi 'na' au alama ya nukta mkato, tunapata alama ya mkato. Si dhahiri kama mwandishi ametumia alama ya mkato badala ya kiunganishi au alama ya nukta mkato kimaksudi au kama ni kosa la kiuakifishi. Hata hivyo, matokeo ya matumizi ya alama ya mkato katika tungo hiyo ni kuongeza kasi katika usomaji wa tungo zinazotaja sifa ambazo Fuad hana. Pia, tungo hiyo ya tatu ina muundo tofauti ambapo badala ya kuendeleza mbinu ya anafora kwa kusema '**hana adabu**', mwandishi sasa anatumia kitenzi kishirikishi 'ni'. Kama mwandishi angeendeleza muundo wa awali tungepata vishazi vinne vinavyolingana: [Fuad] **hana** wema. **Hana** ihsani. **Hana** fadhili. **Hana** adabu. Lakini mwandishi hakuamua kuvipanga vishazi namna hiyo. Hata hivyo, ingawa tungo ya tatu katika mpangilio wa kianafora katika dondoo la 104 ni tofauti kimuundo, bado inaendeleza ujumbe uliotajwa katika tungo za kianafora zilizoitangulia. Matumizi ya mbinu ya anafora ni kusisitiza sifa ambazo bwana shamba Fuad hana. Kuna ulinganifu kisemantiki kati ya sifa hizi. Zinamjenga Fuad kama mtu ambaye hana utu.

Shafi Adam Shafi anatuonyesha jinsi ambavyo mnyonge anaweza kujikwamiza katika unyonge wake kwa kumthamini mtu ambaye hamthamini yeye mnyonge. Kijakazi ni mfanyakazi ambaye amejikwamiza kwenye utumwa. Kinyume na wafanyakazi wenzake, Kijakazi anamwona Fuad kama mtu mwema na bado ana lengo la

kumfurahisha kwa kumfanyia kazi zaidi. Kijakazi bado anaamini kwamba utumwa ni majaliwa yake. Mwandishi anaeleza msimamo huu wa Kijakazi:

> 105. Kwa Kijakazi, Fuad alikuwa ni mtu aliyetimilia; **hakuna** mwenye heshima na adabu kumshinda yeye**, hakuna** mzuri wa kumshinda yeye; **hana** dosari hata kidogo.
> (Shafi, 1978, Ukur. 72)

Sentensi tangulizi inayotoa kauli ya jumla kumhusu Fuad: ni mtu aliyetimilia – kwa mujibu wa Kijakazi. Lakini sifa hizi zimetolewa kupitia kwa ukanushi, kwa kumlinganisha Fuad na watu wengine. Badala ya kusema tu "Fuad ni mtu mwenye heshima na adabu, na ni mzuri kuwashinda wote", mwandishi ametumia njia isiyo ya moja kwa moja kwa kurejelea sifa ambazo watu wengine wanazikosa. Huu ni uchimuzi unaolenga kumfanya msomaji azingatie kweli kinzani, kwa vile, katika muktadha wa riwaya, tunaona kwamba Fuad hana zile sifa ambazo Kijakazi anampa. Ingawa kuna tungo mbili zenye urudiaji wa kianafora ambapo kitenzi '**hakuna**' kimerudiwa mwanzoni mwa kishazi cha pili na cha tatu, kishazi kinachofuata vishazi hivyo kina muundo tofauti. Kitenzi kilichotumika mwanzoni mwa kishazi hicho kinamrejelea Fuad moja kwa moja kwa kuikanusha sifa hasi ambayo Fuad angekuwa nayo. Kimsingi, kuna ulinganifu wa kisemantiki kati ya tungo '**hana dosari hata kidogo'** na tungo iliyotangulia tungo za kianafora**,** yaani "**Fuad ni mtu aliyetimilia**." Lakini, hata kama Kijakazi anaonekana kama mjinga kwa kumsifu mtu ambaye anamdhulumu, huenda hii inatokana na unyonge alionao ambao ulianzia utotoni. Alizaliwa katika mazingira ya utumwa na hajatambua kwamba wakati umebadilika na mabwana shamba hawana mamlaka makubwa kama ilivyokuwa awali.

Hatimaye Kijakazi anang'amua unyonge wake na dhuluma ya Fuad ambaye awali Kijakazi anamsifu kama mtu asiye na dosari. Anaanza kubadilika. Mwandishi anaonyesha kwamba mabadiliko ni kitu cha kawaida maishani:

106. “Nimechoka, nimechoka roho yangu na utumwa huu usiokuwa na malipo wala hisani; wewe **huna** haya wala **hujui** vibaya, **huna** heshima na wala **hujui** unajiona nani.
(Shafi, 1978, Ukur. 90)

Mbinu ya usambamba wa kianafora imetumiwa kubainisha sifa hasi za Fuad. Hapa Kijakazi sasa anamwona Fuad kama mtu asiyetimilia: hana haya, hajui vibaya na hana heshima. Katika dondoo hilo la 103, tunapata tungo mbili zinazofuatana kianafora zenye kitenzi kinachorudiwarudiwa mwanzoni mwa kila kishazi. Lakini kishazi cha mwisho kina muundo tofauti. Hii inaashiria uamilifu tofauti wa kishazi hicho. Kishazi hicho kinakamilisha zile fikira ambazo msemaji amezitoa awali. Kwa mfano, katika dondoo hili, Kijakazi anakamilisha kauli yake kwa fikira inayojitokeza kwa njia ya swali analojiuliza mwenyewe. Kwa njia ya anafora, Fuad sasa anaelezwa kama mtu mwenye sifa hasi. Fuad hamheshimu Kijakazi kwa vile anamwona kama mtumwa tu, mtu asiye na chochote.

Mabadiliko yanatokea kwa upande wa mnyonge na kwa upande wa mwenye mamlaka vilevile. Kijakazi anatambua kwamba hakuna haja ya kuendelea kumtumikia bwana shamba kama mtumwa. Naye Fuad vile vile anatambua kwamba mambo yamebadilika na ameyapoteza mamlaka aliyokuwa nayo. Kwa hivyo, Fuad, badala ya kutumia lugha kali ya matusi kwa Kijakazi, kama alivyozoea kufanya awali, sasa anatumia lugha ya upole kwa aliyekuwa mtumwa wake.

107. Mara Fuad alikuja matao ya chini na kuanza kuzungumza na Kijakazi kwa upole. “Sikiliza Kijakazi, sharti ujue kama sisi tunakuona kama **wewe ni** mmoja wetu ndani ya nyumba hii, **wewe ni** kama bibi yangu, [**wewe**] **ni** sawasawa na ye yote katika ukoo wangu. **Wewe** wakati wote ulikuwa mtumishi mtiifu. Kijakazi sharti ufahamu kwamba **wewe ni** kama mzee wangu kwani **wewe ndiye** uliyenilea. …nami nakwambia waziwazi kama **wewe** umekuwa kama mama yangu wa pili.”
(Shafi, 1978, Ukur. 67)

Kwanza kabisa tunaambiwa kwamba Fuad "**alikuja matao ya chini**" (kitu ambacho alikuwa hajawahi kukifanya), halafu akaanza kuzungumza na Kijakazi. Kama ilivyobainishwa awali, usambamba ni njia ya ushawishi. Kwa hivyo, tunaona kwamba kijalizo kinachofuata kitenzi kishirikishi katika tungo zote zinazoanza kwa njia ya kianafora ni kauli zinazolenga kumshawishi Kijakazi asimwache (Fuad). Kauli hizo zote zina uamilifu wa kumsifu Kijakazi. Uchimuzi unaofanywa kwa kutumia vitenzi vishirikishi unasaidia kuzibainisha kauli hizo, kwa vile zinajitokeza kama vijalizo katika kila kirai kinachohusika katika usambamba. Fuad anakuja matao ya chini baada ya mamlaka aliyokuwa nayo awali kudhoofishwa na wanamapinduzi. Awali 'anambwekea' Kijakazi, lakini sasa anatumia lugha ya kushawishi iliyopangwa kianafora.

Mabadiliko ambapo mabwana shamba wamepoteza mali zao na kuwa wanyonge kabisa yameangaziwa pia na mwandishi. Baada ya serikali ya kisultani kupinduliwa, mabwana shamba wanajikuta hawana hatua yoyote wanayoweza kuchukua kuyazuia mabadiliko yanayotokea. Hii inadhihirika tukimwangalia mhusika Fuad:

> 108. Fuad **hakuwa na** la kufanya. **Hakuwa na** njia yoyote ya kuyazuia yaliyokuwa yakitokea. Kila siku alisikia matangazo ya mapinduzi katika redio, matangazo ya kuchukuliwa mali za mabepari, kudhibiti biashara ya nje na ndani… kuzuia kabisa unyonyaji wa mabepari na mabwana shamba. Yeye **hakuwa na** la kusema isipokuwa kulaani na kutukana tu na hayo hayakumsaidia chochote.
>
> (Shafi, 1978, Ukur. 57)

Kupitia kwa mbinu ya anafora tunaona kwamba Fuad ni mwathirika wa mapinduzi yanayotokea ambapo aliyekuwa na mamlaka sasa hana mamlaka hayo tena. Virai vitenzi vya ukanushi "**hakuwa na…**" vinaonyesha uwezo wote ambao Fuad amepokonywa. Hana la kufanya; hana njia ya kuyazuia yanayotokea. Katika dondoo la 108, tunaona kwamba kuna ruwaza ambapo virai vinavyorudiwa viko katika vishazi

viwili vya kwanza. Lakini baada ya hapo kuna maelezo mengine kabla ya kirai kingine chenye muundo sawa na virai vya awali vya kianafora kujitokeza, yaani "**hakuwa na la kusema**". Kirai hiki ambacho kimetenganishwa na virai vingine vya awali kwa maelezo kina uamilifu ule ule wa kusisitiza unyonge alio nao Fuad na kuhitimisha ujumbe wa mwandishi kuhusu hali hii.

5.1.2 Epifora

Epifora ni urudiaji wa neno mwishoni mwa vishazi au sentensi zinazofuatana. Ni tofauti na urudiaji wa kianafora ambao unatokea mwanzoni mwa vishazi au sentensi. Mbinu ya epifora imedhihirika katika tungo chache katika riwaya tunazozichunguza.

Katika *Kasri ya Mwinyi Fuad*, mwandishi anadhihirisha uwezo mkubwa walio nao mabwana shamba. Uwezo huu unatokana na umiliki wa ardhi kubwa ambayo inawaletea kipato kikubwa. Katika riwaya hiyo, tunamwona bwana shamba Fuad akifurahia uwezo mkubwa alio nao, ambao ni kinyume na unyonge mkubwa wa raia walio wengi.

> 109. Gari lilikwenda mjini abiria akiwa Fuad peke yake. Hakuzungumza na dereva wake njia nzima. Fikra mbalimbali zilikuwa zikimwendea kichwani mwake. Alifikiri ulwa **aliokuwa nao**, pesa **alizokuwa nazo,** amri **aliyokuwa nayo** kwa wapagazi wake wote shambani kwake.
>
> Lakini halafu zilimjia fikra kwamba juu ya yote hayo alikuwa hastarehe kama anavyotaka yeye.
>
> (Shafi, 1978, Ukur. 24)

Vitu vinavyomfanya Fuad ahisi uwezo mkubwa vimetangulia kirai kinachorejelea umiliki wa vitu hivyo, ambacho kinarudiwarudiwa mwishoni mwa vishazi vilivyo katika mpangilio wa kiusambamba. Kurudiarudia kirai huku kunajenga ridhimu fulani ambayo inaleta mvuto kwa msomaji. Uwezo unaotokana na umiliki huo ndicho kitu ambacho kimesisitizwa. Vitu anavyovimiliki Fuad ni **ulwa**, **pesa**, na **amri**. Katika

kishazi cha mwisho katika urudiaji wa kiepifora, kuna maelezo ambayo yameongezewa. Mwandishi angesema tu ‘a**mri aliyokuwa nayo**’, muundo ambao ungekuwa sawa na muundo wa vishazi vilivyotangulia. Badala yake, tunaona kuwa maelezo yameongezewa, yaani tunajulishwa kuwa amri aliyokuwa nayo ni ‘kwa wapagazi wake wote shambani kwake.’ Maelezo haya yameongezewa kwa ajili ya msisitizo. Mwandishi anasisitiza uwezo wa Fuad wa kuwaamuru wapagazi wake. Pia, kwenye maelezo yenyewe kuna msisitizo kwa njia ya uziada fulani. Badala ya kusema, ‘kwa wapagazi wake wote’, mwandishi anaongezea kirai ‘shambani kwake’, wakati ambapo tunajua kwamba muktadha ni shamba lake. Sababu ya kuongezea maneno ‘shambani kwake’ yaweza kuwa pia ni kusisitiza kiwango cha mamlaka yake kwa njia ya umiliki wa shamba pamoja na wapagazi.

Bila viambishi rejeshi, vishazi hivyo tegemezi vingeweza kusimama kama vishazi huru, yaani kila kimoja kikawa sentensi: “**Ulwa alikuwa nao**. **Pesa alikuwa nazo**. **Amri alikuwa nayo**”. Ingawa mbinu hii pia inawezekana katika kazi za fasihi, mwandishi anaamua kutumia mbinu inayoleta kasi na ridhimu fulani katika maelezo yake, yaani kwa kutumia urejeshi na alama ya mkato. Msomaji akiwa anasoma anaihisi ridhimu na kasi hii pamoja na faridi zilizotajwa kwa mfululizo. Pia, mwandishi angeweza kuviorodhesha tu vitu anavyovimiliki Fuad kwa kusema: pesa, ulwa, na amri aliyokuwa nayo. Hii ingekuwa tungo ya kawaida isiyochimuzwa ambayo isingemvuta msomaji. Kwa hivyo, zaidi ya kutoa maudhui, mbinu ya usambamba ina dhima ya kiujumi, yaani kutoa masimulizi kwa njia inayomvuta msomaji. Anapovutwa anajaribu pia kutambua kile ambacho mwandishi analenga kusema, yaani maudhui au ujumbe wa mwandishi.

Mbinu ya epifora vilevile inaendeleza maudhui ya mabadiliko katika riwaya ambapo mwenye mamlaka (Fuad) anapoteza mamlaka yake na kuwa mnyonge. Mabadiliko

haya ni kamili kabisa kwa vile tunamwona aliyekuwa bwana sasa akimbembeleza mtumwa wake. Amegeuka na kuwa mtu anayehitaji usaidizi wa aliyekuwa mtumwa wake.

> 110. Zaidi ya miaka hamsini sasa umekuwa shambani hapa **pamoja na sisi**, mvua, jua, **tuko pamoja** hapa, shida, raha almuradi **tuko pamoja**.
>
> (Shafi, 1978, Ukur. 91)

Katika urudiaji unaodhihirika katika dondoo la 110, virai vimerudiwa mara tatu. Lakini kirai cha kwanza katika urudiaji huo kina muundo tofauti na virai vile vingine viwili vinavyokifuata. Wakati ambapo kirai cha kwanza kwenye mfuatano wa kiepifora ni "**pamoja na sisi**", kirai kingine kinachorudiwa ni "**tuko pamoja**". Hata hivyo, hii ni kawaida kwa vile mbinu ya usambamba inahusisha ulinganifu wa miundo, sio ulinganifu kamili wa kila neno. Kinachosisitizwa katika urudiaji huu ni matumizi ya mbinu hii kwa kusudi la kushawishi ambapo mwandishi anasisitiza maneno yanayorudiwarudiwa mwishoni mwa vishazi. Maneno hayo yanatumiwa kusisitiza zaidi kauli zinazotangulia kirai. Maneno hayo ni 'shambani hapa', 'mvua, jua' na 'shida', pamoja na 'raha'. Matumizi ya faridi hizi kadhaa yanaakisi hisia na hali ya kukata tamaa aliyo nayo Fuad, mtu ambaye hapo awali alikuwa anawaamuru wafanyakazi kama alivyotaka.

Habwe (2005) pia ameitumia mbinu ya epifora katika riwaya yake ya *Paradiso* kuibua maudhui ya wazazi kutokuwa mfano mzuri kwa watoto wao mintarafu uaminifu katika ndoa. 129

> 111. Kwa kweli vitendo vya mzazi huwa mfano mwema kwa wana. Yeye Joshua **hakuwa mwaminifu**. Wala Lona **hakuwa mwaminifu**.
>
> (Habwe, 2005, Ukur.)

Tunaona jinsi ambavyo wachungaji wameshindwa kuwa waaminifu katika ndoa. Lona anahusika katika mapenzi nje ya ndoa; mume wake Joshua naye vilevile, jambo ambalo limesisitizwa kwa urudiaji wa kiarifu katika sentensi mbili zinazofuatana. Pia, badala ya kutumia sentensi moja kwa kusema Joshua na Lona au Joshua na mkewe hawakuwa waaminifu, mwandishi anamwelezea kila mhusika kivyake, yaani kila mhusika ni kiima katika sentensi kinachoelezwa kwa kiarifu, badala ya wahusika hao kuunda kiima kimoja na kuelezwa kwa kiarifu kimoja. Kwa kuwaelezea wahusika hawa katika sentensi mbili, mwandishi anachimuza ile taarifa kuu inayowahusu, yaani hawakuwa waaminifu katika ndoa. Mwandishi anammulika kila mhusika kivyake, na anataka msomaji atambue kwamba kila mmojawao hakuwa mwaminifu.

5.1.3 Tanakuzi

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) tanakuzi inarejelea misemo inayoelekea kupingana na kuwa na maana tofauti. Ni mbinu mojawapo katika balagha. Ni mbinu inayoyaweka sambamba maneno au mawazo kinyume. Mlinganuo kati ya maneno au mawazo husika huleta msisitizo fulani. Michira (2018) anasema kuwa tanakuzi ni mbinu ya kuyaweka kwa makusudi maneno, miundo ya kisarufi (virai, vishazi au sentensi) au mawazo kinyume ili kuonyesha au kusisitiza hitilafu za asili katika maisha.

Kwa kutumia usambamba aina ya tanakuzi, Habwe (2005) katika riwaya yake ya *Paradiso* ameangazia tatizo la ulanguzi wa madawa katika makanisa, kama ishara kwamba hili ni tatizo katika jamii kwa jumla. Walanguzi wanakusudia kujipatia pesa za haraka.

112. **Waumini wengine** walipofanya bidii katika sala **wengine** wakalangua madawa. **Waumini wengine** walipoufuata uso wa Bwana, wenzao **wengine** waliuza bangi katika mataifa ya nje ili kupata dola.

(Habwe, 2005, Ukur. 208)

Mbinu ya tanakuzi imetumiwa kuvibainisha vikundi viwili katika kanisa: kikundi kinachofanya mambo yanayofaa, na kikundi kinachofanya mambo yasiyofaa. Wakati Wakristo wenye mwenendo unaofaa wanapofanya bidii katika sala na kufuata uso wa Bwana, wenzao wasio na mwenendo unaofaa wanalangua madawa. Tofauti kati ya makundi hayo mawili zimewekwa katika jozi mbili, na kila jozi inahusisha tabaini, yaani kila mwenendo mzuri unalinganishwa kiutanakuzi na mwenendo mbaya. Hata hivyo, badala ya kuipanga pamoja mienendo chanya na mienendo hasi katika makundi tofauti mwandishi anaamua kuzipanga aina hizo mbili za mienendo katika jozi mbili ili kusisitiza mlinganuo katika mienendo. Mlinganuo huu ni mfano wa hitilafu za asili katika maisha anazozizungumzia Michira (2018), kwa vile katika maisha huwa kuna watu wenye mienendo inayofaa na wale wenye mienendo isiyofaa. Tanakuzi ni mbinu ya kawaida inayotumiwa katika ubainishaji wa faridi. Sifa mbaya zinaeleweka zaidi zikilinganuliwa na zile nzuri.

Mbinu ya kitanakuzi imetumiwa na mwandishi kulimulika suala la ulanguzi wa madawa katika jamii. Tatizo ni kubwa sana kiasi kwamba hata kanisa limeathirika, wakati ambapo taasisi hii ndiyo ingekuwa msitari wa mbele katika kupigana dhidi ya tatizo hili. Hiki ni kinaya. Msingi wa ulanguzi huu ni tamaa ya pesa. Tamaa ya pesa na mali ni motifu ambayo Habwe ameiangazia katika riwaya yake. Ili kulimulika tatizo hili, mwandishi anatumia mienendo chanya kama kinyume cha mienendo hasi ya ulanguzi wa madawa.

Habwe (2005) anasisitiza suala la imani ya kweli kwa kutumia mbinu za kisintaksia pia. Analinganua makundi mawili katika makanisa: wale wanaokwenda kanisani kwa ajili ya kuabudu Mungu kwa kweli, na wale ambao wanakwenda kanisani kwa maslahi yao, hasa kutafuta riziki au maisha. Kanisa linatumiwa kama nyenzo tu ya kutafutia mali,

siyo tena mahali pa kurekebishia mienendo, kama njia ya kujitayarishia paradiso ya baadaye.

> 113. Hivyo ndivyo madhabahu ya Mungu yalivyokuwa siku hizi. Kulikuwa na **wale waliomwabudu Mungu kwa haki na ukweli** lakini **wengine walitumia madhabahu kama nyenzo** ya kutafuta maisha.
> (Habwe, 2005, Ukur. 208)

Akizungumzia makundi mawili ya waumini mwandishi anatumia sentensi mbili katika mpangilio wa kitanakuzi ambapo moja ni kinyume cha nyingine, zikiunganishwa na kiunganishi 'lakini'. Kiunganishi hicho ndicho kinachobainisha mbinu ya tanakuzi iliyotumiwa na mwandishi. Matamko katika sentensi mbili zilizounganishwa katika dondoo la 113 yanakinzana katika ujumbe wake. Kinyume kilichopo hakipatikani katika maana za kisemantiki za maneno yaliyotumiwa, bali ni cha kimantiki.

Lakini mwandishi anaonyesha kwamba mali wakati mwingine inaweza ikakosa maana, na hivyo si vizuri Mkristo hasa kuikimbilia. Kuna wakati ambapo inaweza ikakosa maana. Ili kudhihirisha jambo hili, Habwe amemtumia mhusika Boribori kama mfano. Boribori amehodhi mali, na kweli anaishi katika paradiso ya hapa duniani. Lakini anaposhikwa na kufungwa gerezani mali yake inapoteza maana kwake.

> 114. Nyumba hii Boribori ameihama sasa. **Hakuihama kwa hiari, amehama kwa lazima**. **Amehama kwa ajili ya hadaa**. Sasa Boribori analala mto uliochanika.
> (Habwe, 2005, Ukur. 222)

Baada ya kauli tangulizi ambayo inatoa dokezo kuhusu hali mpya aliyomo mchungaji Boribori, mwandishi anatumia mbinu ya tanakuzi katika vishazi vinavyofuata. Tanakuzi hii inatokana na mfuatano wa kishazi kanushi na kishazi yakinishi. Hata hivyo, taarifa iliyomo katika kishazi kanushi na ile iliyomo katika kishazi yakinishi kinachokifuata inalingana kisemantiki, yaani kuna usawe fulani. Hii ni kwa sababu

tamko “hakuihama kwa hiari” inalingana kisemantiki na tamko “amehama kwa lazima”. Matamko yote mawili yanarejelea kulazimika au kutokuwa na hiari. Halafu kishazi kingine kinachofuata ambapo neno ‘amehama’ limerudiwa kinatoa sababu ya Boribori kulazimika kuihama nyumba yake ya starehe na kwenda kuishi katika mahali duni gerezani. Kwa hiyo, mbinu ya tanakuzi imetumiwa kuonyesha mabadiliko ambapo mwenye uwezo mkubwa wa kifedha anaupoteza uwezo huo.

Kuna unafiki mwingi unaodhihirishwa ndani ya Kanisa. Njia mojawapo anayoitumia mwandishi kuusawiri ni kupitia mbinu ya usambamba wa kitanakuzi.

115. Kila uchao **matendo yake yakawa** baidi na usemi wake.
Ubaya wake ukawa fufufu na **wema ukawa** mchache.
(Habwe, 2005, Ukur. 131)

Mhusika mmojawapo aliyetumiwa kuwasilishia maudhui kuhusu unafiki ni Lona. Lona anadai kuwa anafanya kazi ya Mungu, wakati ambapo, kusema kweli anaendeleza sana mambo ya kidunia. Mwandishi anatumia matamko yanayokinzana katika vishazi tofauti. Katika sentensi ya kwanza ya dondoo la 115 vifungu vinavyokinzana ni virai ‘matendo yake’ na ‘usemi wake’ ambapo kirai kihusishi ‘baidi na’ ndicho kimetumiwa kuonyesha ukinzani kati ya maneno ya Lona na matendo yake, yaani anayoyasema siyo anayoyatenda. Huo ni unafiki. Sentensi ya pili katika dondoo hilo ni sentensi ambatani yenye vishazi huru viwili vilivyounganishwa kwa kiunganishi ‘na’. Vishazi hivi pia vinakinzana ambapo ubaya wa Lona unalinganishwa na wema wake na inadhihirika kwamba ubaya wake ndio mwingi kuliko wema wake. Kwa jumla, tunaona jinsi ambavyo mbinu ya tanakuzi imetumiwa kumjenga mhusika Lona, kama Mkristo mnafiki, na tena mtu asiye mwema. Lakini la msingi zaidi ni ujenzi wa maudhui ya unafiki miongoni mwa Wakristo ambao mwandishi anaukemea.

Habwe anazungumzia hali ambapo wahubiri wamezingatia sana mapato ya pesa kuliko injili na hivyo wakalifanya kanisa kuwa kama biashara.

> 116. Uaskofu uligeuka na kuwa **sio huduma** tena kwa Bwana lakini **kazi**. Kazi ya mshahara wa mwisho wa mwezi.
> (Habwe, 2005, Ukur. 67)

Katika matumizi ya tanakuzi katika dondoo la 116, mwandishi anatumia kiunganishi ‘lakini’ kuonyesha hali ya utofauti uliopo kati ya matarajio ya jinsi mambo yalivyo kuhusu huduma ya Bwana na jinsi yanavyotakiwa kuwa. Katika matumizi ya mbinu ya tanakuzi, kuna udondoshaji wa vipashio. Muundo wa ndani wa sentensi hiyo ungekuwa: “**Uaskofu uligeuka na kuwa sio huduma tena kwa Bwana** lakini **[uaskofu uligeuka kuwa] kazi**.” Kwa hiyo, tunaona kwamba katika sentensi hiyo ya kwanza katika dondoo kuna sentensi iliyomezwa au inayobebwa na sentensi kuu. Udondoshaji huu unalenga kuepuka urudiaji, kwa vile faridi zinazozungumziwa tayari zinajulikana. Udondoshaji pia unaleta kasi katika usomaji wa tungo mintarafu muundo wa sentensi. Pia unamwezesha mwandishi kusisitiza neno ‘**kazi**’, kwa vile baada ya kiunganishi, badala ya kupata hiyo sentensi iliyomezwa tunapata neno ‘kazi’ moja kwa moja.

Pia, mwandishi amebadilisha mpangilio wa vipashio katika sentensi yenye tanakuzi. Sentensi yenyewe ingekuwa “Uaskofu uligeuka na kuwa kazi, sio huduma tena kwa Bwana.” Muundo huu ungekuwa ni wa kawaida sana, usiochimuzwa. Lakini mwandishi analenga kuchimuza ujumbe wake kuhusu uaskofu kutokuwa huduma kwa Bwana. Kwa hiyo, zaidi ya kiunganishi ‘lakini’ tanakuzi inaweza kujengwa kwa kubadilisha vipashio, kwa kusudi la kuchimuza ujumbe fulani katika riwaya, kwa mujibu wa kipashio ambacho kimechimuzwa.

Mbinu ya tanakuzi imetumiwa katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* kuuchimuza udhaifu wa mhusika mwanamume, katika jitihada za mwandishi za kumwimarisha mhusika wa kike. Richard, mwanamume ambaye ni mkali sana nyumbani, akisisitiza umuhimu wa kuzingatia mienendo anayoiona kama ndiyo ya kikristo, amesawiriwa kama mwoga. Kinyume na ukali wake, Richard anamwogopa sana nyoka na anasisitiza kuwa anamchukia kiumbe huyo kwa sababu ndiye (kiumbe) aliyekuwa chanzo cha uasi. Lakini binti yake, kinyume na baba yake, anasema kwamba hamwogopi nyoka hasa.

> 117. **Sikumwogopa nyoka** kwa kuwa alikuwa na uwezo wa kuua. **Nilimwogopa** kutokana na maelezo ya baba aliyemchukia mnyama huyo. Alituambia mara nyingi kuwa huyo ndiye aliyekuwa chanzo cha uasi wa binadamu katika bustani ya Edeni…
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 46)

Hulka za mtoto (Susan) na baba yake Richard au mwanamume zinalinganuliwa. Susan haogopi hatari ya kuuliwa na nyoka bali anamwogopa kwa sababu ya maelezo ya kidini ya baba yake kumhusu nyoka. Kinyume na Susan, baba yake anaogopa hatari ya nyoka. Hili linadhihirika tukiangalia jinsi hofu inavyomvaa anapokabiliana na nyoka (madondoo 132 na 133). Kwa hivyo, kwa kutumia mbinu ya tanakuzi, mwandishi anamkuza mhusika wa kike na kumdunisha mhusika wa kiume. Hii ni motifu ya mwandishi katika riwaya yake ya *Nguvu ya Sala*. Inaonekana kwamba Wamitila, ni mtetezi wa haki za mwanamke katika jamii.

5.1.4 Muundogeu/muundopindu (Chiasmus)

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), muundogeu au muundopindu (yaani *chiasmus*) ni mbinu ya kibalagha iliyotumiwa kuelezea mtindo wa kugeuza au kupindua miundo katika ruwaza ya AB:BA. Naye Wales (2014) anaeleza kwamba asili ya neno ‘chiasmus’ ni Kiyunani na ni istilahi katika balagha inayotumiwa kuelezea tungo inayohusisha urudiaji wa maneno au elementi kwa mpinduo.

Mbinu ya muundogeu haijitokezi sana katika riwaya teule. Lakini katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* Wamitila ameitumia kuwasilishia maudhui ya mambo kuzoroteka duniani:

> 118. [Richard] aliyapitisha matamko mbalimbali [ya mhubiri] katika akili yake.
> "Ulimwengu umejaa uchafu wa kila aina…"
> "Watu wamegeuka makatili…"
> "Uzinzi umeongezeka…"
> **"Amani hamna… Hamna tena amani…"**
> (Wamitila, 1999, Ukur. 153)

Katika tungo "A**mani hamna… Hamna tena amani…**", mwandishi anapindua mpangilio wa vipashio. Katika kipashio "Amani hamna" mwandishi anaanza na nomino 'amani' ambayo ndiyo inakuwa kiima, ikifuatwa na kiarifu kinachotawaliwa na kitenzi 'hamna'. Halafu mwandishi anapindua mpangilio huu ambapo katika tungo "Hamna tena amani …" anaanza na kitenzi kama kijenzi cha msingi cha kiarifu. Baada ya kitenzi tunapata kielezi 'tena', kisha nomino yambwa, yaani 'amani'. Hata hivyo, katika muundo wa ndani, nomino. 'amani' ndiyo yambwa katika tungo zote mbili – kimantiki. Kusudi la upinduzi huu wa kimuundo ni kuchimuza taarifa kwamba mambo duniani yameharibika kiasi kwamba hata amani imekosekana kabisa.

Kijuujuu, tungo "Amani hamna … Mm … Hamna tena amani …" inahusisha uziada, kwa vile ingetosha mwandishi kusema tu: "Hamna amani tena." Lakini lengo la mwandishi la kutumia muundogeu katika muktadha huu ni kusisitiza kauli yake. Muundogeu huu unajitokeza mwishoni mwa orodha ya mambo mengine mengi ambayo yamekwenda kombo au ambayo ni mabaya katika jamii – ukatili, uzinzi, mimba zisizotakikana, na mengineyo. Msisitizo huo katika muundogeu unabainika zaidi hasa mwandishi anapoongezea kielezi 'tena' katika kishazi cha pili katika muundogeu. Toni ya mhubiri ni ile ya kukata tamaa kuhusu mambo yanayoendelea duniani.

5.1.5 Matumizi ya mbinu ya mjalizo/asindeto

Mbatiah (2001) anaeleza kuwa asindeto ni kunga ya mtunzi ambapo viunganishi hudondoshwa katika tamko ili kuleta wekevu na kasi ya masimulizi au maelezo. Anaonyesha kwamba mbinu hii inaweza pia kuitwa 'mjalizo.' Istilahi 'asindeto' inatokana na utohozi wa neno la Kiingereza *asyndeton*. Mbatiah pia anasema kwamba mbinu hii inatumiwa kuleta ridhimu katika maandishi.

Akitumia mbinu ya mjalizo, mwandishi wa riwaya ya *Paradiso* anazungumzia tabia ambazo mtu anayetaka kumfanyia Bwana kazi anafaa kutokuwa nazo. Mchungaji Michael ni mmmojawapo wa wale ambao wameazimia kumfanyia Bwana kazi.

> 119. [Michael] ...yeye alijikaza ili asimame na kumfanyia Bwana kazi **bila ujanja**, **bila ghilba.**
> (Habwe, 2005, Ukur. 66)

Katika dondoo la 119, mwandishi ametumia mbinu ya mjalizo kwa kudondosha kiunganishi 'na' ambacho kingewekwa kati ya virai 'bila ujanja' na 'bila ghiliba.' Tena kwa kutumia kiunganishi 'na', neno 'bila' katika kirai 'bila ghilba' lisingehitajika, kwa vile ni urudiaji usiohitajika. Kwa hivyo tungepata tungo: "bila ujanja na ghilba." Hata faridi 'ujanja' na 'ghilba' zina usawe fulani, ingawa usawe huo si kamili. Kwa kuziweka faridi hizo katika virai tofauti na kurudia kihusishi 'bila', mwandishi anachimuza suala la ujanja katika makanisa, wakati ambapo makanisa ndiyo yanafaa kupambana dhidi ya tabia hiyo.

Habwe (2005) anaangazia suala la migogoro katika makanisa. Hakuna umoja katika kanisa, tofauti na mafundisho ya Bwana, ambaye ndiye kiongozi wa kanisa. Hiki ni kinaya, kwa vile kanisa linafanya kinyume na mafundisho ya Kristo, na bila Kristo hakuna Ukristo, na hakuna kanisa.

> 120. [Michael] aliona kanisa la Bwana likisambaratika **kila siku**, **kila mwezi**, **kila mwaka**.
> (Habwe, 2005, Ukur. 77)

Mwandishi ametumia mbinu ya mjalizo kusisitiza kiasi cha msambaratiko katika kanisa. Amefanya hivi kwa kuonyesha kiasi cha kuongezeka kwa msambaratiko kiwakati. Mjalizo umetumika kwa kudondosha kiunganishi 'na' kati ya faridi mbili za mwisho. Kwa kawaida, mfuatano ungekuwa "**kila siku**, **kila mwezi** na **kila mwaka**." Kwa kudondosha kiunganishi 'na', mwandishi analenga kuongeza kasi na ridhimu katika usomaji wa tungo hiyo. Hii ni kwa sababu za kiujumi na tena kumfanya msomaji azingatie ujumbe unaowasilishwa.

Kulingana na mchungaji Michael, migogoro kanisani inatokana na ushindani kwa ajili ya vitu vya dunia. Ushindani huu unatokana na ulafi na tamaa ya vitu hivi.

> 121. Kisa na maana ni nini?" Michael aliwaza. **Ushindani**, **ulafi** wa vitu vya dunia hii. **Tamaa** ambayo Bwana Yesu alisema tusiwe nayo.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 77)

Katika kuelezea hali ya tamaa na ushindani, mwandishi anafuatanisha faridi mbili bila kiunganishi 'na' ambacho kwa kawaida huwekwa kati ya faridi mbili zilizoorodheshwa. Mwandishi anataja faridi mbili, halafu anaweka kituo mwishoni mwa faridi hizo kama kwamba tungo hiyo yenye nomino mbili ni sentensi, yaani: "**Ushindani**, **ulafi** wa vitu vya dunia hii." Lakini kwa vile haina sehemu ya kiarifu, tungo hiyo si sentensi, ila inadhihirisha usambamba aina ya mjalizo. Kisha, tungo inayofuata tungo hiyo ni kishazi kitegemezi ambacho pia kimewekewa kituo kama kwamba ni sentensi. Kishazi hiki kingeambatanishwa na kishazi cha awali kwa alama ya kistari kirefu. Badala ya kufanya hivyo mwandishi anakifanya kishazi hicho kitegemezi kisimame kama sentensi. Hata hivyo, tungo kama hizi ni za kawaida katika kazi za kifasihi. Hii ni njia ya usisitizaji. Tungo hiyo inayoanza na neno "tamaa" inahitimisha yale ambayo mwandishi ameyazungumzia katika kishazi cha awali.

Matumizi ya tungo hizi ambazo si sentensi kamili lakini ambazo zimewekewa kituo kama kwamba ni sentensi kamili ni njia mojawapo ya ukiushi ambao unachimuza ujumbe wa mwandishi. Kwa sababu ya pesa nyingi zinazoingia kanisani kunazuka migogoro. Ushindani hauko kwenye kulieneza neno la Mungu, bali ni kwa ajili ya vitu vya dunia ambavyo Yesu alisema wasiwe navyo. Mkristo kufanya yale ambayo Yesu ameyakataza ni kinaya. Mwandishi analenga kuikemea tabia ya ulafi, tamaa na chuki katika jamii. Anataka kuonyesha kwamba mambo haya yapo, hata katika asasi ambamo yasingetarajiwa. Ikiwa yanaweza kutokea katika asasi kama kanisa, hii inaonyesha kwamba tabia hizi ni tatizo kubwa katika jamii ambalo linapelekea kukosekana kwa amani na labda maendeleo katika jamii.

5.1.6 Usambamba Kiusawe

Inaonekana kwamba mienendo isiyofaa ya wahubiri imewakinaisha baadhi ya wanajamii kuhusu mambo ya dini, kiasi kwamba baadhi wanaamini kuwa dini haina thamani yoyote katika maisha yao. Hili linabainika tukimwangalia mhusika Kyalo katika riwaya ya *Paradiso*. Huyu ni mhusika ambaye hataki kabisa kujihusisha na mambo ya dini.

> 122. Kyalo hakuwa kama mkewe. **Hakupenda** masuala ya dini. Tangu alipozaliwa **hakuwa** amekwenda kanisani. **Hakuona** haja yoyote ya kujidhiki na sala ndefu ambazo zilichosha. **Hakupenda** hasa sala za kelele. Aliona kuwa mke wake alikuwa mjinga kwa kujishughulisha na hadaa za wahubiri**.**
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 49)

Kupitia kwa usambamba, mwandishi anabainisha hali ya baadhi ya watu kutopenda mambo ya dini. Usambamba uliopo katika dondoo la 122 unabainishwa kupitia kwa urudiaji wa vitenzi kanushi: "**hakupenda, hakuwa, hakuona**". Vitenzi hivyo kanushi ni tofauti kisemantiki lakini usawe kati yake unatokana na ukanushaji na kuazimia kwa mhusika. Inaonekana kwamba kuna watu ambao wamepoteza imani kuhusu masuala ya

kanisa kwa vile, ingawa kuna sala ndefu na kelele makanisani wakati wa ibada, bado makanisa yanafaa kuwa mfano wa kuigwa kwa wanajamii. Lakini yanayoendelea humo yanawakinaisha watu kama Kyalo.

Maudhui kuhusu watu kutopendezwa na unafiki wa wachungaji na mienendo ya makanisa kwa jumla yamewasilishwa kupitia kwa mhusika mwingine. Lydia, ambaye baadaye anaolewa na mchungaji Michael.

> 123. **Vitendo vya dini vilimuudhi**. **Kelele na vurumai vilishtadi kanisani**. Huko walitafuta pepo lakini huko ndiko walikokugeuza na kukufanya Jehanamu kwa **vitendo**, **tamaa** na **utashi wa dunia**.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 97)

Kuna ulinganifu katika kauli zinazoonyesha msimamo wa Lydia kuhusu makanisa ya kiprotestanti. Kauli zote mbili zinakamilishana. Ni fikira mbili kuhusu msimamo wa Lydia. "Vitendo vya dini" na "kelele na vurumai" ni virai ambavyo vinafanya kazi karibu ile ile. Kirai kinachotangulia hakitoi taarifa mahsusi, ila kinatoa hisia ya jumla. Kirai kinachofuata kinaonyesha sababu mahsusi za kuchukizwa kwa Lydia, yaani kelele na vurumai kwenye makanisa.

Sawasawa na mawazo ya Kyalo, mawazo ya Lydia kuhusu makanisa vilevile yanabainisha unafiki katika makanisa ambapo, ingawa waumini, hasa wachungaji, wanaomba kwa kelele, mienendo yao imejaa tamaa ya vitu vya dunia. Hili ndilo jambo linalowaudhi Lydia na Kyalo hasa.

Usambamba wa kiusawe umetumika pia katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* kuwasilisha maudhui kwamba mambo mengi katika jamii yameenda kombo. Mhubiri mmoja katika *Uhuru Park*, ambaye mhusika Richard anamsikiliza, anazungumzia vitendo visivyo vya kimaadili na matukio mengine katika jamii nchini Kenya na kwingineko duniani.

124. "**Ulimwengu umejaa uchafu** wa kila aina …"
"**Watu wamegeuka makatili** …"
"**Uzinzi umeongezeka** …"
"**Uzinzi na ukahaba unazengea**."
"Matatizo ya ajira; ehh, **matatizo ya kazi yameongezeka**."
"Mimba zisizotakikana, matokeo ya hila za Lusiferi. Unyama wa binadamu … Msisahau Vietnam na kwingineko."
(Wamitila, 1999, Ukur.153**)**

Kauli za mhubiri zimepangwa kishairi. Hii inaleta mshikamano kati ya mistari iliyotumika, pamoja na ridhimu fulani. Upangaji huu unazifanya kauli za mhubiri kukumbukika kwa msomaji. Haya ni matumizi ya lugha kwa sababu za kibalagha. Lugha ya kibalagha hulenga kuziathiri hisia za msikilizaji au msomaji.

Katika upangaji huu wa kishairi, mwandihsi anabainisha ni wapi vitendo visivyo vya kimaadili vinapatikana, yaani ulimwenguni (msitari wa kwanza), na miongoni mwa watu (msitari wa pili). Nomino zinazoashiria mambo yaliyo kombo zimejitokeza katika nafasi ya yambwa. Katika mistari inayofuata, nomino zinazorejelea matukio, mienendo na vitendo visivyo vya kimaadili ndizo zinazotangulia katika kila msitari. Hii ni njia ya kuzisisitiza nomino hizo – yaani kwa kuziweka katika nafasi ile ile (mwanzoni mwa kila msitari).

Katika msitari wa sita na wa saba mwandishi ametumia virai nomino tu ambapo neno kuu ni nomino inayotaja vitendo visivyo vya kimaadili. Kwa vile kwenye mistari inayotangulia mwandishi anaonyesha kwamba tabia na mienendo mibaya imeongezeka, anadondosha kiarifu katika mistari ya sita na saba. Mwandishi anadondosha kiarifu ili msomaji aweze kuzingatia tabia na vitendo visivyo vya kimaadili vinavyoongezeka. Kudondosha kiarifu pia kunaziwezesha tungo kusomeka kwa kasi zaidi kwa vile faridi zilizotajwa zinasikika kama orodha.

Katika kishazi "Msisahau Vietnam na kwingineko" msemaji anadokeza tu vita katika nchi hiyo vilivyotokana na Marekani kuishambulia Vietnam. Anaashiria vitendo vya kinyama vilivyofanywa katika vita hivyo.

Mwandishi anazungumzia ugumu wa maisha jijini Nairobi, ambao umewakatisha vijana tamaa. Unawafanya vijana kuchukua hatua ambazo wasingechukua. Tunaona hili tunapozingatia mhusika Richard Ngunze. Maisha jijini humu yamemshinda kwa sababu ya kutokuwa na rasilimali za kifedha. Tatizo hili linatokana na ukosefu wa ajira unaowakabili vijana wengi. Kazi wanazozipata hazidumu. Wanaathirika katika mabadiliko yanayotokea katika mashirika mbalimbali. Kwa hiyo, baadhi ya vijana hawa (kama Richard) wanaamua kuokoka, kama njia ya kuyakabili maisha magumu wanayokumbana nayo. Richard anaokoka wakati akisikiliza mahubiri katika eneo la *Uhuru Park.*

> 125. Richard Ngunze **alikata kauli**. **Alifikia uamuzi** kwa kutotaka kufikwa na yaliyomfika huyo tajiri aliyezungumziwa na mhubiri. **Aliamua** kumkubali Bwana na kuinua mkono wake wa kulia kama walivyotakiwa … Kila mtu alikuwa ameinua mkono wake kwa hivyo **aliamua** kujiunga na wenzake. **(**Wamitila, 1999, Ukur. 154**)**

Katika dondoo la 125, virai '**alikata kauli** na '**alifikia uamuzi'** vinafuatana kiusambamba**.** Virai hivyo viwili ni visawe vinavyomaanisha 'aliamua', neno analolitumia mwandishi katika sentensi ya mwisho kwenye dondoo hilo. Kusudi la kurudia wazo lile lile kwa maneno tofauti lakini ambayo kimsingi ni visawe ni kusisitiza uamuzi wa Richard. Miundo ya kisintaksia imetumiwa kuambatana na kitendo cha mhusika cha kufanya uamuzi muhimu katika maisha yake. Mfuatano wa virai hivyo kiusambamba pia unaashiria mchakato wa kufikia uamuzi. Richard hakuamua kumkubali Bwana moja kwa moja tu, bali aliwazia uamuzi huo. Labda huo ndio msingi wa imani yake katika nguvu ya sala isiyotikisika.

Mwishoni mwa dondoo hili la 122, msimulizi anatoa maelezo ya ziada ambayo yanatilia shaka msingi wa uamuzi wa Richard. Mwandishi anaashiria kwamba Richard aliinua mkono wake kwa vile kila mtu alikuwa amefanya hivyo, "kwa hivyo aliamua kujiunga na wenzake." Hii inaonyesha kwamba Richard hakujua vizuri alichokuwa akifanya wakati huo. Alifuata tu mkondo. Kwa jumla hii ni njia mojawapo ya kumuumba mhusika Richard (mwanamume), kama mhusika dhaifu. Katika riwaya nzima, maamuzi ya Richard yamedhoofishwa. Uamuzi wake wa kuokoka ambao umeonyeshwa kama ni kufuata tu mkondo, unadhoofisha ufaafu wa imani yake katika nguvu ya sala. Hii ni njia ya kuuchimuza uwezo wa mwanamke (binti yake Susan) ambaye anaidengua imani hiyo katika nguvu ya sala.

Kama ambavyo Richard (katika *Nguvu ya Sala*) anafikia uamuzi wa kuokoka kwa sababu ya kushindwa kukabiliana na ugumu wa maisha unaosababishwa na tatizo la ukosefu wa ajira, nao Dude, Bushiri na vijana wengine (katika *Asali Chungu*) wanaohangaika kwa sababu ya kukosa ajira wanachukua uamuzi wa kuipokea kazi yoyote itakayowajia kwa sababu ya kukata tamaa. Katika hali yao ngumu ya kukatisha tamaa, Bushiri na Dude wanaikubali bila kusita kazi wanayopewa na Bi Amina ya kumridhisha kimapenzi. Wanatumiwa kama kifaa tu na mwenye pesa na uwezo, yaani Bi. Amina.

Kupitia mbinu ya usambamba wa kiusawe, mwandishi wa riwaya ya *Nguvu ya Sala* amegusia suala la msamaha. Hili tunaliona kwa kuzingatia mhusika Richard, ambaye, ingawa anajaribu kuonyesha kwamba yeye ni Mkristo kielelezo, inamwia vigumu sana kumsamehe mke wake Mary Kasiva, wakati anapogundua kwamba mtoto ambaye Mary amemzaa si wake (yaani yeye Richard).

126. [Richard] **alishindwa kumsamehe** mke wake. Mtumishi wa Mungu aliyesisitiza faida na thamani za

> huruma katika maisha na aushi za binadamu **aliwiwa vigumu**. **Alishindwa na kuemewa**.
> **(**Wamitila, 1999, Ukur. 183**)**

Katika dondoo la 126, mwandishi anatumia virai vitatu ambavyo kimsingi ni visawe kuonyesha unafiki wa baadhi ya Wakristo. Wakati ambapo Richard anasisitiza maisha ya Kikristo, hayuko tayari kutekeleza nguzo mojawapo ya dini ya Kikristo, yaani msamaha. Huu ni unafiki. Kirai cha kwanza kinachoonyesha Richard kutotaka kumsamehe mkewe kimejitenga na virai vingine vinavyohusiana nacho kiusawe, yaani vile ambavyo vimeonyeshwa mwishoni mwa dondoo. Hii ni kwa sababu, baada ya kutoa kirai cha kwanza kinachotaja kushindwa kwa Richard kusamehe, mwandishi anaona kwamba ni muhimu kumwonyesha msomaji kinaya kilichopo kwamba aliyeshindwa kusamehe ni "mtumishi wa Mungu aliyesisitiza faida na thamani za huruma." Kwa hiyo, kuna usambamba wa kiusawe kati ya kirai '**alishindwa kumsamehe**' katika sentensi ya kwanza na kirai '**aliwiwa vigumu**' mwishoni mwa sentensi ya pili, ambacho kinarudiwa mwanzoni mwa sentensi ya tatu. Yaani mwanzoni mwa sentensi ya tatu, tunapata kirai '**alishindwa na kuemewa**' kinachojitokeza mwishoni mwa dondoo. Kirai hiki kinashikamana na kirai katika tungo ya kwanza katika dondoo la 126 kwa sababu neno 'alishindwa' limekwisha tumiwa katika tungo hiyo ya kwanza.

Kitendo cha mwandishi cha kutenganisha kirai cha kwanza '**alishindwa kumsamehe**' na virai vingine viwili vinavyohusiana na kirai hicho kiusawe, yaani' '**aliwiwa vigumu**' kwa maelezo ya ziada kinaonyesha jinsi ambavyo mwandishi anaamua kumwonyesha msomaji kinaya kilichopo kwamba mtu anayedai kuwa msitari wa mbele katika kuishi maisha ya kikristo anashindwa kusamehe. Vinginevyo, mwandishi angefuatanisha virai vinavyohusiana kiusawe kabla ya kutoa maelezo zaidi kuhusu kitendo cha Richard cha kushindwa kusamehe. Hamu ya mwandishi ya kuonyesha kinaya kilichopo katika

kitendo cha Richard inabainika wazi. Ni kama kwamba mwandishi anamhukumu Richard kwa tabia yake ya kutaka kujionyesha kama 'Mkristo aliyekamilika.'

Katika riwaya ya *Asali Chungu* tunaona jinsi mnyonge anavyotumiwa na wenye mamlaka kwa manufaa yao. Mnyonge hatambui kwamba anatumiwa tu na wenye nacho. Badala yake anajivunia kufanikisha uchu wa wenye nacho. Wakati mwingine anatumiwa kuwanyanyasa wanyonge wenzake. Hili linadhihirika tunapoangalia jinsi Biti Daudi anavyotumiwa na Zuberi kumletea wasichana wadogo afanye mapenzi nao.

> 127. Ata! Kwani mimi nilishindwa? Umesahau Bwana wangu! **Nimeiangusha miamba kweli,** itakuwa kitoto kile? **Nimewatoa watu majumbani kwao**; **nimefungua milango ya chuma** na kupanda ghorofa ngapi, nikateremka na mabibiye kemkem, nikakuletea wewe, ije iwe mwehu yule? Anishinde nini?
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 25)

Tunaona jinsi ambavyo Biti Dauti anajitapa kwa uwezo wake wa kufanikiwa kumletea Zuberi mabibi. Maneno yake yametolewa kiusambamba. Vishazi ambavyo tumeviwekea wino uliokoza katika dondoo la 127 vina ulinganifu wa kisemantiki. Vyote vinataja uwezo ambao Biti Daudi anasema anao. Vishazi hivi vyote vinarejelea uwezo na majivuno. Biti Daudi haoni aibu yoyote kujaribu kumtoa mhanga Semeni, mfanyakazi mnyonge mwenzake, tena msichana tu ambaye angekuwa anamtetea dhidi ya wanaume kama Zuberi. Matumizi ya tungo hizo za nafsi ya kwanza yanalenga kusisitiza uwezo ambao anasema anao ulioonyeshwa katika vitenzi 'angusha', 'toa' na 'fungua.'

Mwenye mamlaka anatumia uwezo wake wa pesa na mali kujipatia chochote anachokitaka, mkiwemo kufanya mapenzi na wasichana wadogo ambao ni wanyonge. Mnyonge akikubali kutekeleza matakwa ya mwenye mamlaka, anaahidiwa manufaa kadhaa. Dude anashawishiwa na Bushiri kuhusu manufaa haya, pindi tu akikubali

kumstarehesha Bi Amina kimapenzi. Bushiri anatumia mbinu ya usambamba ili kumshawishi Dude akubali pendekezo la kumfanyia 'kazi' Bi Amina.

> 128. Sio kulipwa tu… **Utaendeshewa** maisha yako. **Utakuwa** bwana wa bibi wa nyumba kubwa. **Utatoka** katika umaskini. **Utavuliwa** guo la unyonge. **Utakuwa** mtu. **Utaona** raha. **Utajua** nini maisha… Wacha ujinga wako…. Ukitaka langu, ishike fursa hii barabara.
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 88)

Vishazi vilivyofuatana kiusambamba katika dondoo vinataja manufaa ambayo Dude atayapata mara tu akikubali pendekezo la kumfurahisha tajiri – Bi Amina. Vishazi vyote vinahusisha vitenzi katika nafsi ya pili. Hii inaashiria kwamba manufaa yote atayapata yeye Dude. Vishazi vyote vilivyo kwenye mpangilio wa usambamba vinahusisha udondoshaji wa nomino kiima au kiwakilishi chake. Kwa hiyo, ridhimu inayotokana na udondoshaji wa kiima inasaidia katika kusisitiza manufaa yaliyotajwa, na kumshawishi mnyonge anayelengwa akubali kufanya analoambiwa. Dude anaahidiwa kuvuliwa 'guo la unyonge' (yaani unyonge mkubwa ambao ameshindwa 'kujivua') na kwamba akikubali, atakuwa mtu kwa maana kwamba naye ataheshimiwa baada ya kutolewa katika umaskini. Sasa ndio atajua maisha ni nini. Hii inamaanisha kuwa kwa sasa, maisha anayoyaishi ni kama si maisha hasa, bali ni uhai tu.

Mtu mwenye mamlaka makubwa wakati mwingine huwa anataka watu wengine wayahisi mamlaka aliyo nayo. Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad,* tunaona jinsi ambavyo Fuad anataka mamlaka yake yatambuliwe zaidi na wakulima pamoja na wafanyakazi wake. Ili kufanikiwa katika lengo lake hili, anaamua kujinunulia gari linaloakisi hadhi yake kama bwana shamba na ambalo litamwezesha kujitenga na kutoingiliana na watwana wake.

> 129. **Aliwaza** kwamba yeye awe anaranda mji mzima huku akiendesha mwenyewe gari zuri… **Aliona** si kiasi chake,

> kijana mwenye pesa nyingi kama yeye kupanda gari la kubeba mizigo, yeye pamoja na watwana wake. **Alijihisi** amechoka kupanda teksi na kuendeshewa gari na dereva asiyeweza kumwamuru kama anavyotaka yeye.
>
> (Shafi, 1978, Ukur. 24)

Katika dondoo la 129, usambamba unaohusisha vitenzi vya kitambuzi umetumika kuwasilisha mawazo ya Fuad, ambayo yanapelekea vitendo vyake. Usambamba huo unahusisha matumizi ya vishazi ambavyo vinaanza na vitenzi vya kitambuzi: '**kuwaza**', '**kuona**' na '**kuhisi**'. Vitenzi hivyo vya kitambuzi vinafuatwa na mawazo ya Fuad kuhusu mamlaka zaidi yatakayotokana na umiliki wa gari: kuendesha gari hilo yeye mwenyewe, kutopanda gari la mizigo pamoja na watwana, na kutoendeshwa na mtu ambaye hangeweza kumwamuru.

Maudhui ya mabadiliko yameangaziwa pia katika riwaya teule kupitia kwa mbinu ya usambamba wa kiusawe. Baada ya serikali ya kisultani kupinduliwa, mabwana shamba wanayapoteza mashamba yao, pamoja na mamlaka yao yaliyotokana na umiliki wa mashamba hayo na wafanyakazi wengi. Mambo yamebadilika kiasi kwamba mabwana shamba sasa ndio wanyonge. Unyonge huu unabainika katika tabia na lugha ya Fuad, wakati akitangamana na wanamapinduzi ambao sasa wanakuja kwake kumjulisha matakwa mbalimbali ya serikali ya kimapinduzi.

> 130. "Fikira nzuri!" Fuad aliruka na kusema. "Mimi **nakubaliana moja kwa moja** na fikira hizo. **Najua vizuri** kwamba hilo ni jambo zuri na **naliunga mkono** kwa moyo wangu wote. **Niko tayari kabisa** kuishi kijamaa."
>
> (Shafi, 1978, Ukur. 58)

Katika dondoo hili, tunaona jinsi ambavyo Fuad yuko tayari kufuata masharti ya wanamapinduzi. Kauli zake zinazofuatana kiusambamba zinamfanya msomaji awe makini kujaribu kugundua kinachoashiriwa na uchimuzi huu unaofanywa kwa njia hii ya usambamba wa kiusawe. Vishazi vyote vinavyojenga usambamba wa kiusawe katika

dondoo hilo vinaanza na vitenzi vilivyo katika nafsi ya kwanza umoja, ingawa awali, kiwakilishi ‘mimi’ kinatumika. Vitenzi vyote vinavyotangulia kwenye kauli za Fuad vinaonyesha kujidunisha au kujitweza kwake mbele ya wanamapinduzi: ‘**nakubaliana**’, ‘**najua**’ ‘**naliunga mkono.**’ Pia, katika kila kishazi, vielezi au tungo zinazofanya kazi kama vielezi zimetumika kutoa taarifa zaidi kuhusu kitenzi. ‘Moja kwa moja,’ ‘vizuri’ na ‘kwa moyo wangu wote’ ni vielezi vinavyoelezea namna ambavyo Fuad yuko tayari kutekeleza kila atakachoambiwa. ‘Kabisa’ ni kielezi cha kiasi ambacho kinaelezea kiasi cha unyenyekevu wake katika hali mpya anamojikuta.

Kwa hivyo, kupitia usambamba wa kiusawe, msomaji anaweza akapata taswira ya bwana shamba huyu ambaye awali alikuwa mkali na mwenye matusi kwa wafanyakazi wake, na ambaye sasa hana mamlaka tena. Ni mnyenyekevu kupita kiasi kwa sababu ya hulka yake kama mtu mwenye hofu na pia mtu ambaye anatambua kwamba wakati umebadilika, na kuna uhalisi mpya.

Mapinduzi ya serikali yanahusisha hatua ya mabwana shamba kupoteza mashamba yao. Fuad naye hasalimiki. Anapoteza ardhi kubwa na badala yake anakatiwa sehemu ndogo tu kwenye shamba lake ya “kuendeshea maisha yake.” Mtu aliyekuwa mmiliki wa shamba kubwa, akilitumia kujipatia utajiri, sasa ndiye anayegawiwa tu sehemu kwenye shamba hilo. Badala ya kuwa mtendaji, yeye sasa ndiye mtendwa.

> 131. Maana yake ni kwamba shamba lako pia itabidi ligawiwe na wewe mwenyewe **utapewa sehemu yako** ili nawe uwe na kitu cha kukuendeshea maisha yako. **Utapatiwa ardhi inayokutosha**, lakini itakubidi uilime wewe mwenyewe…
> (Shafi, 1978, Ukur. 56)

Vishazi vilivyopangwa kiusambamba na ambavyo vinarejelea Fuad kugawiwa ardhi (badala ya yeye kuwa ndiye anayegawa ardhi) vinalingana kiusawe, yaani “**utapewa sehemu yako** [ya ardhi]…” na “**utapatiwa ardhi inayokutosha**.**”** Wanamapinduzi ndio watakaompatia sehemu tu kwenye shamba lake. Tena, wao ndio watakaompimia

ukubwa wa sehemu watakayompatia. Haya ni mabadiliko makubwa kwa vile kwa mabwana shamba, kunyang'anywa ardhi ni kunyang'anywa mamlaka waliyo nayo kwa wakulima.

Mwenye mamlaka anatambua kwamba hana mamlaka tena kwa mtu ambaye awali alikuwa anamchukulia kama mtumwa katika shamba lake. Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* tunamwona bwana shamba Fuad akilalamika tu kuhusu kuondoka kwa mfanyakazi wake Mkongwe.

> 132. Tena kitu kimoja… usichanganyike naye [Mkongwe]. Usichanganyike naye hata kidogo kwani yeye **amekwisha tutoka** na karibu namwona **atatukimbia** hapa nyumbani. Siku hizi **amezidi**, hafanyi kazi, **amekuwa mvivu**… **amekuwa mjeuri**.
>
> (Shafi, 1978, Ukur. 68)

Maonyo haya kuhusu Kijakazi nayo yametolewa kiusambamba: '**amekwisha tutoka… atatukimbia… amezidi… amekuwa mvivu… amekuwa mjeuri**.' Tena Fuad hana la kufanya kuhusu tabia ya Mkongwe. Fuad anayatoa maonyo yake kwa Kijakazi ambaye bado ni mtiifu sana kwake.

5.1.7 Mgeuko wa polepole (Gradation)

Kwa mujibu wa Galperin (1977), mgeuko wa polepole ni upangaji wa sentensi (au sehemu za jinsi moja za sentensi) ambao unaleta kukua kwa umuhimu au mhemko katika tamko. Anasema kwamba katika mgeuko wa polepole kila kipashio kinachofuata kinakuwa na nguvu zaidi kuliko kilichotangulia. Msomaji anaweza kuhisi kukua kwa umuhimu wa kila kipashio katika mfuatano. Galperin anaeleza kuwa mgeuko wa polepole kama mbinu ya kimtindo ni njia ambayo mwandishi anatumia kuonyesha mwonoulimwengu wake na tathmini yake isiyo na upendeleo kuhusu fenomena. Galperin anasisitiza kuwa uamilifu wa mbinu hii ni kuonyesha kiasi cha umuhimu wa vitu, kama anavyoona mwandishi au kumwonyesha msomaji umuhimu

wa vitu vinavyoelezwa kwa kutumia ulinganishaji au kuonyesha fenomena kwa njia inayodhihirisha kubadilika kwa fenomena hizo.

Katika *Nguvu ya Sala* tunaona usambamba wa aina ya mgeuko polepole ukitumika kuzungumzia suala la ushirikina.

> 133. Wakati Nzisa **aliyatega masikio yake** imara na mara hii hayakurudi muflisi ila yalifanikiwa. Ilikuwa sauti ya bundi… Nzisa **alianza kushikwa na hofu kubwa. Moyo wake ulianza kututatuta kwa kasi ya ajabu. Kichomi cha ghafla kilimkata maini**. Aliifahamu fika imani ya jamii yake kumhusu ndege huyo. Watu walisema kuwa kila aliapo ndege huyo karibu na makazi ya watu pangetokea dhara kubwa hasa kama alikuwepo mgonjwa katika mji uliohusika.
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 53)

Hisia za Nzisa zimepangwa kwa njia ya kuongezeka kwa hofu aliyokuwa nayo, wakati aliposikia sauti ya bundi, ndege anayeaminiwa na jamii mbalimbali kwamba anaweza kuleta mkosi. Vishazi vinavyoonyesha hofu ya Nzisa vimepangwa kwa njia ya usambamba wa mgeuko wa polepole. Kwanza kabisa '**aliyatega masikio yake.**' Kisha '**alianza kushikwa na hofu kubwa**', '**moyo wake ulianza kumtuta kwa kasi ya ajabu**' na hatimaye '**kichomni cha ghafla kilimkata maini.**' Kinachomfanya Nzisa awe na hofu kubwa ni imani ya jamii yake. Vishazi vimepangwa kwa njia ambayo vinaonyesha kuongezeka kwa mhemko wa Nzisa.

Bundi ni ndege kama ndege yeyote yule ambaye anatafuta chakula usiku, kwa vile ana uwezo wa kuona usiku. Katika tamaduni mbalimbali Kiafrika hasa, ndege huyu huhusishwa na kisirani au madhara kama vile ugonjwa au kifo. Hii ni kwa sababu usiku (ambapo ndege huyu hutoka kutafuta chakula) huhusishwa na mambo mabaya. Nzisa anapoisikia sauti ya bundi karibu na nyumba ambapo mume wake ni mgonjwa mahututi

anamhofia sana. Labda kisadfa, mgonjwa mwenyewe anafariki asubuhi inayofuatia, muda sio mrefu baada ya bundi kulia – kitu ambacho labda kilithibitisha hofu ya Nzisa.

Wamitila ametumia mbinu mbalimbali kumwinua mhusika wa kike na kwa njia hiyo vilevile kumdunisha mhusika wa kiume. Suala la jinsia ni suala kuu katika riwaya ya *Nguvu ya Sala*. Kupitia kwa ujenzi wa wahusika, Wamitila anaonyesha kwamba anaunga mkono harakati za wanawake kupata usawa wa kijinsia. Jambo hili tunaliona katika mahusiano kati ya Richard na binti yake Susan. Tunamwona baba akionyesha dalili za kumwogopa binti yake, ambaye anadhihirisha ujasiri mkubwa katika kumkabili baba yake:

> 134. Inaelekea [baba] **alihisi kuwa nilikuwa nikimwangalia**. **Macho yetu yalikutana**. **Aliyarudisha macho yake alipokuwa**; aliliinua parange. Alianza kuyapogoa matanzu ya ule mshomoro.
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 109)

Inaonekana kwamba, ingawa Richard ni mkali, ukali wake unatoweka anapokabiliana na ujasiri wa Susan. Mwandishi ametumia usambamba wa mgeuko wa polepole kutuonyesha jinsi ambavyo baba anahisi wasiwasi macho yake yanapokutana na ya binti yake. Usambamba wa mgeuko wa polepole unadhihirika kwamba Richard anahisi binti yake anamwangalia; macho yao yanakutana; Richard anayarudisha macho yake alipokuwa; anaendelea na kazi yake ya kuyapogoa matanzu ya mshomoro.

Richard anashindwa kudumisha mkodoo wa macho kati yake na binti yake (‘mkodoo’ ni neno analolitumia Wamitila katika riwaya hii). Richard kushindwa kufanya hivi ni ishara ya udhaifu mbele ya mwanamke ambaye bado ni msichana, tena binti yake. Ingawa Richard anaonyesha kwamba ana mamlaka katika familia yake, tukio hili, na matukio mengine katika riwaya yanaonyesha kwamba mamlaka yake katika familia yanaweza kudhoofishwa.

Udunishaji wa mhusika wa kiume kwa kuyadhoofisha mamlaka yake unabainika katika maelezo kuhusu Richard na hofu yake ya nyoka. Wakati ambapo Richard anamwogopa nyoka kwa vile anaweza kumdhuru kimwili, binti yake anasema kwamba yeye hamwogopi nyoka kwa ajili ya madhara ya kimwili, ila kwa ajili ya hadithi ya Biblia aliyowasimulia baba yao.

> 135. Aliinua shoka tena. Alikuwa hajaliachilia **alipomwona nyoka mkubwa** akitambaa na kunyinyirika kuelekea alipokuwa amesimama. **Alilitupa lile shoka** kisha **akatimua mbio** kuelekea nyumbani. Aliamua kuuacha mkuyu huo.
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 8)

> 136. Lakini **ghafla alishikwa na mchecheto** fulani. **Hofu ilimtambaa** mwili mzima. **Moyo wake ulipiga kwa kishindo sasa**. **Aligeuka kushoto**. **Macho yake yalitia nanga juu ya joka kubwa** lililonyenyereka kuelekea alipokuwa. **Alipiga usiahi**… Alizinduka ndotoni.
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 27)

Mambo mawili yanabainika katika madondoo ya 135 na 136. Madondoo yote mawili yanaelezea visa ambapo Richard anakabiliana na nyoka. Mara ya kwanza ni pale ambapo anataka kuukata mti wa mkuyu ambao ni madhababu kwa jamii yake. Mkuyu huo una umuhimu mkubwa kwa wanajamii – kiutamaduni. Lakini Richard anauchukulia utamaduni kama mambo ya giza au ujinga tu. Haya byanadhihirika katika mazungumzo yake na mzee mmoja anayejaribu kumkataza kuukata mti huo. Richard anataka kumwonyesha mzee huyo kwamba yeye hana cha kuhofia kwa vile ni Mkristo aliyeachana na mambo ya utamaduni. Anataka kudhihirisha ujasiri wake kwa kuukata mti huo bila madhara yoyote kumfika. Anapojaribu kuukata mti huo anaona joka likimjia. Badala ya kulikabili joka hilo kama mwanamume shupavu, Richard anatimua mbio. Anaonyesha woga na hofu kubwa.

Usambamba wa mgeuko wa polepole unadhihirika pia tunapoona kuongezeka kwa hofu ya Richard, kwanzia pale anapomwona nyoka mpaka anapotimua mbio. Mwandishi

anaonyesha kwamba si vizuri kuupuza utamaduni wa jamii yako kwa sababu ya dini za kigeni. Tena anaonyesha jinsi ambavyo mtu ambaye ni mkali na anayewanyanyasa wanafamilia wake si mtu jasiri. Hili linamdunisha kama mhusika mwanamume.

Katika dondoo la 136, tunamwona Richard Ngunze akikabiliana na nyoka tena, ila mara hii katika ndoto. Hata hivyo, katika hali hii pia tunapata vishazi vilivyopangwa kwa usambamba wa mgeuko wa polepole. Kwa vile hii ni mara ya pili Richard kuonyesha hofu kubwa anapokabiliana na nyoka, tunaweza kuhitimisha kwamba huyu ni mtu anayeogopa sana nyoka. Si mwanamume shupavu. Tabia ya Richard ni tofauti na matarajio ya jamii nyingi ambapo mwanamume anatarajiwa kuonyesha ushupavu kuliko mwanamke. Ufuatao ndio mfuatano wa vishazi vinavyoonyesha kuongezeka kwa hofu yake mpaka anapopiga usiahi na kuzinduka ndotoni: [Richard] **alishikwa na mchecheto** fulani. **Hofu ilimtambaa… Moyo wake ulipiga kwa kishindo sasa**. **Aligeuka kushoto**. **Macho yake yalitia nanga juu ya joka kubwa… Alipiga usiahi**…"

Ili kudhihirisha kwamba Richard si mwanamume jasiri, msimulizi anamlinganua na binti yake Susan. Susan anasema kwamba yeye hamwogopi nyoka kwa kuwa nyoka ana uwezo wa kuua bali anamwogopa kutokana na maelezo ya baba yake aliyewaambia kwamba nyoka ndiye aliyekuwa chanzo cha uasi katika bustani ya Eden (Dondoo 117). Wakati ambapo baba mzima anamwogopa nyoka, binti yake – msichana tu – hamwogopi mnyama huyo. Kusudi la mwandishi ni kuonyesha udhaifu wa imani ya Richard na pia kumdunisha kama mhusika wa kiume ambaye anadhihirisha kinaya katika hulka yake. Ni mkali na mwenye kuonyesha mamlaka makubwa nyumbani lakini mwenye hofu hata kuliko mabinti zake au kuliko mwanamke. Hapa usambamba umetumiwa kudengua mamlaka ya jinsia ya kiume na dini ya Kikristo.

5.1.8 Udondoshaji

Mbinu hii ya kisintaksia inahusisha udondoshaji wa neno au maneno. Kusudi huwa ni kutomchosha msomaji na taarifa anayoijua tayari. Pia, unatumika kumfanya msomaji afikirie faridi ambayo imedondoshwa. Ni njia ya kuchimuza kile ambacho hakikutajwa. Udondoshaji huleta kasi katika usomaji wa kazi ya kifasihi. Unajenga ridhimu fulani katika lugha na hivyo kuvuta nadhari ya msomaji.

Wamitila anatumia mbinu ya udondoshaji katika riwaya yake ya *Nguvu ya Sala* kutudhihirishia ugumu wa maisha jijini Nairobi. Kuna ushindani mkubwa, kila mtu akijaribu kujitafutia riziki. Ushindani huu umevuka mipaka na kuenea hadi hata kwa viumbe wengine wasiokuwa binadamu.

> 137. Richard aliyatupa macho yake juu ya lile karai. Palikuwepo na nzi sugu waliokuwa wakijitahidi kufaidi uhondo wa maji ya nazi. Walikuwepo pia nyuki ambao walikuwa katika harakati zao za kuhemea. **Nzi**. **Nyuki**. **Binadamu**. Wote walikuwa katika kinyang'anyiro cha kujitafutia. Ole wake yule ambaye angemuudhi mwenzake. **(**Wamitila, 1999, Ukur. 100**)**

Katika dondoo hili tunawaona viumbe wakiwa katika 'kinyang'anyiro cha kujitafutia.' Kwa vile waandishi hutunga kazi zao ili kutoa maudhui fulani kuhusu maisha ya binadamu, viumbe wengine katika kazi za kifasihi wanatumiwa kwa njia ya kiulinganishi au kiulinganuzi. Kwa hiyo, katika dondoo la 137, mwandishi anapozungumzia wadudu (nzi na nyuki) msomaji anajitahidi kufasiri uhusiano uliopo kati ya maelezo kuhusu wadudu hawa na maisha ya binadamu, ambaye pia ametajwa kama faridi ya tatu.

Mwandishi ametumia muundo wa sentensi usio wa kawaida ambapo kila nomino inayotaja kiumbe inajisimamia kama sentensi kigrafolojia. Kila tungo inaanza kwa herufi kubwa na kuishia kwa kituo. Katika matumizi ya kawaida ya lugha, muundo wa

sentensi ni ule unaohusisha kiima na kiarifu. Mwishoni mwa nomino hizo ambazo zingetenganishwa kwa alama ya mkato, tunapata kituo badala ya alama ya kistari kirefu; yaani sentensi yenyewe ingekuwa "Nzi, nyuki na binadamu – wote walikuwa katika kinyang'anyiro cha kujitafutia." Sehemu inayofuata nomino hizo, ambayo ingefanya kazi kama kiarifu imedondoshwa. Nayo imefanywa kuwa kama sentensi kamili yenye kiwakilishi 'wote' (nzi, nyuki na binadamu). Huu ni mtindo katika kazi za kifasihi ambapo nomino au tungo isiyokuwa sentensi (mintarafu ya muundo wa kiima na kiarifu) inafanywa kuwa sentensi kwa kuwekewa kituo.

Hata hivyo, muundo wa nomino kusimama kama sentensi ni njia ya kulichimuza jambo fulani. Vilevile, tunaona kwamba nomino 'binadamu' nayo imewekwa katika ngazi sawa na nomino zinazotaja viumbe visivyo binadamu. Hii inadhihirisha kiasi cha unyonge wa kiuchumi wa mtu anayejitahidi kuishi katika jiji la Nairobi. Ni hali ya kusikitisha. Mwandishi analenga kumfanya msomaji ahisi kuwa hali kama hiyo imevuka mipaka ya kibinadamu.

Mwandishi wa *Paradiso* anatumia mbinu ya udondoshaji kumulika tabia potovu za wahubiri. Amefanya hivi kupitia kwa mhusika Musa ambaye sasa amerukwa na akili. Ingawa Musa ni mwendawazimu, anawatambua Joshua na mkewe Lona (ambao alikuwa akihudumu nao katika kanisa la New Jerusalem) wakiwa wanapita katika sehemu fulani jijini Nairobi. Musa anatolea maneno yafuatayo:

138. Nyinyi ni shetani. Ati wahubiri? Wahubiri gani nyinyi? Nyinyi ni laghai. **Mwaiba**. **Mwalazimisha**. **Mwaongopa**. **Mwaua**. Huku **mwataja Yesu**. Shetani wakubwa nyinyi. Msitaje jina la Bwana bure.
(Habwe, 2005, Ukur. 75)

Mhusika Musa anataja mambo ambayo hata Joshua anaona kwamba ni mazito, ingawa mkewe Lona anajifanya kutoyatambua kama mazito. Katika kifungu hiki tunaona kwamba kila kitendo ambacho Musa anakirejelea kimesimama kama sentensi kwa

kuwekewa kituo, badala ya alama ya mkato. Katika kila kishazi, kiima kimedondoshwa. Udondoshaji wa kiima unaeleweka kwa vile kiima ni kile kile (Joshua na mkewe). Lakini, baada ya kiima kudondoshwa, vishazi hivyo vingetenganishwa kwa alama ya mkato, sio kwa alama ya kituo. Mkakati wa kukifanya kila kishazi kisimame kama sentensi ni njia anayoitumia mwandishi kuchimuza ujumbe unaobebwa katika kila kishazi.

Kuna ridhimu fulani inayotokana na vishazi vya tungo tenzi kusimama mfululizo kama sentensi bila kuambatanishwa na kiima au maneno mengine. Kiima 'nyinyi' yaani (Joshua na mkewe) katika kila kishazi kimeashiriwa tu kwa matumizi ya kipatanishi '**mw-**' kwenye kitenzi**.** Ridhimu inayojengeka inasaidia kuufanya ujumbe uliomo katika kila kishazi ukumbukike kwa msomaji. Tena, msomajii anaweza kutambua kinaya kilichopo anapoona jinsi ambavyo wahubiri wanafanya mambo ambayo ni kinyume na mafundisho ya Kikristo.

Kuwatumia wahusika walevi au wendawazimu ili kufichua ukweli fulani kuhusu mambo mazito au kuhusu wahusika wengine ni mbinu inayojulikana katika utunzi wa kazi za kifasihi. Hii ni kwa sababu inaaminika kwamba wakati mwingi walevi au wendawazimu husema wazi kwa vile huwa hawahofii chochote.

5.1.8.1 Udondoshaji katika uanzaji kati (In medias res)

Mbinu hii ni ya kawaida sana katika mwanzo wa riwaya. Waandishi huweza kuanza riwaya kwa kutaja wahusika au mahali fulani mwanzoni mwa riwaya bila kumpa msomaji usuli wowote au muktadha kuhusu mhusika au mandhari yanayozungumziwa. Mbinu ya uanzaji kati inalifanya tukio linaloelezwa liwe la kidrama zaidi. Uanzaji kati unatumika katika riwaya mbalimbali, lakini katika riwaya ya *Asali Chungu*, umechimuzwa zaidi. Katika riwaya hiyo mwandishi anamweka msomaji ghafla

(kitaswira) katika mandhari ya ofisi ya DC, ambaye jina lake halifichuliwi mpaka ukurasa wa tatu. Sura ya kwanza inaanza ifuatayo:

139. Chumbani kwa Bwana DC. (Mohamed, 1977, Ukur. 1)

Msomaji, bila ya taarifa yoyote ya awali ambayo anaweza kuirejelea, anajaribu kuelewa kwa upesi hali ambayo imemtokezea ghafla. Anajiweka katika mtazamo wa msimuliaji ili kujaribu kuelewa kinachoendelea katika mandhari yaliyotajwa. Ni kama kwamba msomaji anatarajiwa kuwa tayari anajua mahali (chumba chenyewe) na mtu (Bwana DC) anayezungumziwa. Tungo hiyo katika dondoo la 139 imewekewa kituo mwishoni kana kwamba ni sentensi, lakini katika sarufi, tungo hiyo imekiuka kanuni ya ujenzi wa sentensi, kwa vile haina muundo wa kiima na kiarifu. Inajitokeza kama kirai elezi cha mahali tu ambacho kingeweza kujitokeza mwanzoni mwa sentensi, yaani kwa muundo kama: "chumbani kwa Bwana DC kuna…" au "… chumbani kwa DC." Mwandishi ametumia "Chumbani kwa DC" ili kuichimuza tungo hiyo na kumfanya msomaji awe tayari kuona kitakachofuata chumbani humo.

Tungo "Chumbani kwa DC" ni kama maelekezo ya jukwaa katika drama ambapo mwandishi anamwelekeza msomaji kuhusu mandhari yaliyotajwa. Ni kama kwamba mwandishi anamwambia msomaji kuwa matukio yatakayofuata yanatokea kwenye chumba cha DC. Msomaji anatumia ubunifu wake kujaribu kufikiria namna chumba hicho kilivyo. Mwandishi anatarajia kwamba msomaji ana taarifa ya awali kuhusu mazingira kama hayo. Hivyo, msomaji ameshirikishwa tayari na mwandishi kuhusu tukio litakalotokea katika mahali palipotajwa.

Mwanzo huu wa masimulizi alioutumia mwandishi unajenga toni inayoiathiri hadithi nzima, kwa vile msomaji anaposoma hadithi nzima atagundua kwamba hadithi nzima

inamhusu mhusika mkuu Zuberi na matendo yake kama mfano wa makabaila wenzake na mienendo yao.

Kwa hivyo, mwenye mamlaka makubwa hapa ni DC. Ni lazima msomaji awe na ujuzi wa awali kwamba DC ni kifupisho cha *District Commissioner*, ngazi mojawapo katika utawala wa nyakati za wakoloni Wazungu barani Afrika na kwenye serikali zilizoandama uhuru. Yanayotokea chumbani mwa DC yanamfanya msomaji ajue mhusika mkuu – Bwana DC (Zuberi) ni mtu wa aina gani. Motifu ya mamlaka na nguvu dhidi ya unyonge inatambulishwa mapema kwenye hadithi.

5.1.9 Uorodheshaji

Kulingana na Galperin (1977), uorodheshaji ni mbinu ya kimtindo ambapo vitu, fenomena au sifa hutajwa kwa mfuatano ili kuzalisha mfululizo wa vitu vya aina moja kisemantiki, hata kama uhusiano kati ya faridi zilizo katika mfululizo ni wa mbali. Anaeleza kwamba uorodheshaji unaashiria uhusiano kati ya faridi zilizotajwa katika mfufulizo.

Waandishi wa riwaya teule wametumia mbinu ya uorodheshaji katika kubainisha pengo lililopo kati ya matajiri wenye mamlaka na watu maskini wanyonge. Katika riwaya ya *Paradiso* tunaona jinsi ambavyo wachungaji na wake zao wanaweza kuzimudu gharama za maisha, tofauti na watu wa kawaida. Katika riwaya za *Nguvu ya Sala* na *Asali Chungu* tunaona kwamba watu wengi wa kawaida ni mafukara; hawawezi kuhimili gharama za mahitaji ya kawaida ya maisha.

140. Rose alipata alichotaka; **pesa**, **mavazi**, **vyakula**, na wanawe walisoma katika skuli za hela kama Hilcrest na Braeburn.
(Habwe, 2005, Ukur. 65)

141. "Mfumo tulio nao ndio unaowafanya watu wawe hivi," alieleza June. Hebu angalia maisha ya hapa chuoni. **Karo**, **chakula**, **mavazi**: **pesa**. Kila kitu pesa." (Wamitila, 1999, Ukur. 159)

142. Mimi ndiye niliyeufahamu ubaya na uzuri wa kazi yangu; na ikiwa ni utu, utu hautaweza kubadilisha chochote kuhusu **unyonge** wangu. Hauwezi **kunipa starehe**, **kutumia**, **kuvaa**, au **kuishi**. Utu wangu utanipa wapi hayo?
(Mohamed, 1977, Ukur. 92)

Katika madondoo ya 140 – 142, waandishi wametumia mbinu ya uorodheshaji kiusambamba kuonyesha hali ambapo watu wasio nacho wanashindwa kumudu gharama ya mahitaji ya kimsingi kwa binadamu, kinyume na hali ambapo wenye nacho wanavipata bila wasiwasi wowote. Tunaona jinsi ambavyo Rose, mkewe Mchungaji Musa ana uwezo wa kupata chochote anachokihitaji. Hata hivyo, mzee mmoja katika kanisa la New Jerusalem analalamika kwamba, ingawa viongozi wa kanisa wanasisitiza utoaji wa zaka, "watu wengine hawana pa kutoa hiyo zaka. Hata kula hawawezi kula." Pia anataja kwamba pesa za zaka "wanazila wao," yaani wachungaji (Habwe, 2005, Ukur. 54). Hii inaonyesha jinsi ambavyo hali ya kiuchumi ya viongozi wa dini ilivyo bora kuliko ya watu wa kawaida. Kinyume na hali ya Rose katika *Paradiso*, mhusika June katika *Nguvu ya Sala* anatupa picha ambapo wanafunzi walio wengi katika chuo kikuu wanashindwa kuzimudu gharama za vitu kama karo, chakula, mavazi na ndiyo maana baadhi ya wanafunzi wanatenda vitendo visivyo vya kimaadili kama vile uavyaji mimba. Anaeleza kwamba mfumo wa maisha ndio chanzo cha vitendo kama hivi.

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, mhusika Bushiri anatuelezea hali ya unyonge walio nao vijana wengi kwa sababu ya ukosefu wa ajira. Anasema kwamba vijana kama yeye inabidi wafanye kazi yoyote wanayoweza kupata bila kujali mambo ya utu. Yeye anatafuta tu pesa za **starehe**, **kutumia**, **kuvaa**, au **kuishi**. Msimamo huu wa Bushiri unaambatana na maelezo ya mhusika June katika *Nguvu ya Sala* kwamba mambo kama haya yanasababishwa na mfumo wa maisha, yaani watu wanyonge kushindwa kuzimudu gharama za maisha. Sio kwamba vijana kama Bushiri wanapendelea

kumilikiwa na tajiri kama Amina, lakini wanajikuta hawana hiari. Hivyo, msomaji anashawishika kutowalaumu vijana kama Bushiri na Dude wanaonunuliwa kama mali na mwenye mamlaka (Bi Amina) ili wamstareheshe.

Kupitia kwa njia ya uorodheshaji, mwandishi wa *Paradiso* anasawiri maudhui ya vitendo visivyo vya kimaadili vinavyoikumba jamii. Anafanya hivi kupitia kwa mahubiri ya Mchungaji Michael:

> 143. **Mauaji**, **ubakaji**, **wizi, ufisadi**, **kashfa** ni miongoni mwa hatari tulizo nazo.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 56)

Mwandishi ametumia njia ya uorodheshaji wa nomino zinazotaja vitendo visivyo vya kimaadili ili kusisitiza hatari inayoikumba jamii kutokana na kuwepo kwa vitendo vya namna hii. Dhamira ya mwandishi ni kufichua tabia hizi mbaya ili kuihamasisha jamii juu ya uwepo wa vitendo hivi. Jamii inahimizwa kupambana na tabia hizi na kuziondoa. Baadhi ya vitendo hivi visivyo vya kimaadili vinatajwa pia kwa mbinu ya udondoshaji tuliyoiagalia katika sehemu 5.1.2.8 ambapo mhusika Musa anawaambia waziwazi Askofu Joshua na mkewe Lona kwamba wao **wanaiba, wanalazimisha**, **wanaongopa**, **wanaua**, na wanafanya hayo yote huku **wakitaja Yesu** (Habwe, 2005, Ukur. 75).

Isitoshe, baada ya Musa kuwapasulia ukweli kuhusu vitendo vyao, anaorodhesha vitendo visivyo vya kimaadili ambavyo Musa, aliyekuwa mchungaji mwenzao lakini ambaye sasa amerukwa na akili alikuwa akivifanya:

> 144. "Achana na yule **mbakaji** na **mwasherati**," alisema Lona.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 75)

Huku kutupiana maneno kati ya Lona na Musa (ingawa Lona hamtupii Musa maneno moja kwa moja) kunamsaidia msomaji kujua kiundani mambo yanayoendelea makanisani. Mwandishi anatumia wahusika ambao mara nyingi kisaikolojia

wanaaminika kusema ukweli: mhusika mwenye hasira (Lona) pamoja na yule aliyerukwa na akili (Musa) kutoa ukweli fulani kuhusu tabia za wahusika. Kwa hivyo, tunaweza kuhitimisha kwamba vitendo visivyo vya kimaadili, ambavyo Musa na Lona wanavitaja, vipo makanisani. Vitendo hivi vinalifanya kanisa likose msingi wa kuongoza waumini kimaadili.

Tena, tumeona jinsi ambavyo mwandishi wa riwaya ya *Paradiso* ametumia mbinu ya anafora kutaja vitendo visivyo vya kimaadili vinavyoendelea katika jamii. Katika dondoo la 96, tunaona jinsi ambavyo Lona anajitetea kwa kujihusisha na vitendo visivyo vya kimaadili yaani rushwa, kuua na udanganyifu (Habwe, 2005, Ukur. 130).

Kwa hivyo, akitumia mbinu tofauti za kiusambamba yaani anafora, udondoshaji na, uorodheshaji, Habwe anavimulika vile vitendo ambavyo anaona kwamba vinaidhuru jamii. Analenga kuonyesha unafiki na kinaya kilichopo ambapo viongozi wa dini ambao ndio wangekuwa kwenye msitari wa mbele kuvikemea vitendo visivyo vya kimaadili, ndio wanaohusika katika kuvifanya. Mwandishi anatumia njia ya kutunga kazi ya kifasihi ili kuvipiga vita vitendo hivyo.

Vitendo anavyovimulika Habwe bado vipo katika jamii zetu siku hizi na ni changamoto kukabiliana navyo. Mchungaji Michael anailinganisha hali katika jamii yake na ile katika miji ya Sodoma na Gomora inayozungumziwa katika Biblia. Anasema kwamba ulimwengu wa leo umeshinda kile kiwango cha Sodoma (Habwe, 2005, Ukur. 56). Hii ni hukumu kwa jamii.

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, mwandishi amesawiri maudhui ya Mungu kuwa ndiye mwenye mamlaka kushinda viumbe wote. Hili linadhihirika tukimwangalia mhusika Zuberi. Zuberi anapozeeka na afya yake kuzoroteka anaanza kutambua kwamba hana mamlaka kweli. Mwenye mamlaka ni Mungu. Anaanza kufanya vitendo vizuri

ambavyo angefanya akiwa bado na mamlaka. Anayaangalia maisha yake ya nyuma na kuona kwamba yote aliyoyatenda sasa hayana maana yoyote.

> 145. Hapo ilimlazimu **aabudu, atubie, astaghafiru** na **aombe** kwa Mola wake asimghadhibikie. Labda kwa unyenyekevu huo Mwenyezi Mungu Mwepesi wa kusamehe, ndimo alimotegemea kufutiwa yale maovu aliyoyatenda… akaishi kwa namna aliyoishi; akasahau mipaka yake, kuwa kwa hali yoyote ile yeye ni makhuluku...
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 98)

Mambo ambayo anafikiria kufanya Zuberi katika hali yake ya unyonge ambayo yametajwa kwa mbinu ya uorodheshaji (yaani kuabudu, kutubu, kustaghafiru, na kuomba) yanalenga kumshawishi Mungu amsamehe maovu yake ya nyuma. Anagundua kwamba yeye ni binadamu tu asiye na mamlaka kuhusu mustakabali wake. Msimulizi anasema [Zuberi] '**akasahau mipaka yake.**' Hii ina maana kwamba Zuberi hakutambua kwamba mamlaka yake yalikuwa na mipaka. "…akajiona hivi hivi anakufa wala **hana la kufanya**" (Mohamed, 1977, Ukur. 98). Hatimaye uwezo wote aliokuwa nao akaona umemponyoka. Pesa na cheo haviwezi kumwauni tena.

5.2 Matumizi ya Kauli ya Kutendwa

Katika riwaya ya *Paradiso*, mwandishi ametumia kauli ya kutendwa kuonyesha utashi wa mali miongoni mwa wachungaji. Katika kanisa la New Jerusalem, Joshua ni Askofu Mkuu. Ana askofu wasaidizi na shemazi. Naye mkewe pia ni kasisi katika kanisa hilo. Katika riwaya hii hatuambiwi jinsi wachungaji wanavyovipata vyeo hivi:

> 146. Nyumba yake Joshua ni ya kisasa si kama kibanda alichokaa hapo kibera. Kibanda hicho …hakikumstahili hasa **alipopandishwa na kuwa Askofu Mkuu**. Alistahili nyumba ya kisawasawa ili akitembelewa na wenzake waone Mungu tunayemwomba si wa umaskini Mungu ni Mungu wa baraka.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 43)

147. **Lona alipopewa cheo hicho cha ukasisi** Joshua aliona kakamilika.
(Habwe, 2005, Ukur. 80)

Katika dondoo la 146, tunaambiwa kwamba Joshua **alipandishwa** akawa Askofu Mkuu. Kishazi kitegemezi kilichosisitizwa kiko katika kauli ya kutendwa. Kirai 'alipopandishwa cheo' kinaashiria mtendaji, yaani kiima. Lakini katika kishazi hicho hakuna kiima chochote ambacho kimeashiriwa au ambacho kimeakisiwa, yaani mtu au watu waliompandisha cheo. Hata neno 'cheo' limedondoshwa. Huu ni uchimuzi unaolenga kumfanya msomaji azingatie upandishwaji cheo huo kwa makini. Hata katika dondoo la 147, tunapata kishazi kitegemezi '**alipopewa cheo hicho cha ukasisi'** lakini haionyeshwi ni nani aliyempa Lona cheo cha ukasisi, yaani hakuna kiima cha kimantiki.

Ili msomaji aweze kutambua ni nani anayewapandisha wachungaji cheo, inabidi atumie muktadha wa makanisa mengine ya kiprotestanti na pia hulka za wahusika wachungaji. Kwa vile uongozi na udhibiti wa makanisa haya huwa mikononi mwa wachungaji binafsi na wenye mamlaka makubwa, uamuzi wa kumpandisha mchungaji kwa njia isiyo ya moja kwa moja unafanywa na wachungaji wenyewe, yaani wao wenyewe ndio wanaojipandisha vyeo, kwa vile wana ushawishi au wanaweza kudhibiti mchakato na uamuzi wa kupandishwa cheo. Mume anapandishwa cheo, na mke vilevile. Msomaji anaweza akahisi kwamba Askofu Joshua na mke wake ndio ama wanajipandisha cheo au wana ushawishi katika mchakato wa upandishwaji cheo. Hulka ya Lona kama mtu anayetaka kudhibiti kila kitu hapo kanisani pia inaweza kumfanya msomaji afasiri kwamba mhusika huyo amehusika katika upandishwaji wake cheo. Katika dondoo la 55, tunaambiwa kwamba "Lona sasa ndiye aliyedhibiti mamlaka ya New Jerusalem" (Habwe, 2005, Ukur. 120). Pia tunaambiwa kwamba Lona alimdhibiti mumewe (Askofu Joshua). Hii inaashiria kuwa Lona ana nafasi ya muhimu katika maamuzi ya

kanisa la New Jerusalem, na huenda aliathiri uamuzi wa upandishwaji wake cheo, au amemshinikiza mume wake Askofu Joshua kumpandisha yeye (Lona) cheo.

Tena katika riwaya hii ya *Paradiso* tunaona kauli ya kutendwa ikitumiwa kiuchimuzi pia kuwasilisha maudhui ya ukwasi mkubwa wa wachungaji dhidi ya umaskini na unyonge wa waumini walio wengi. Ukwasi huu wa wachungaji unadhihirika katika vitu kadhaa, mkiwemo kuwanunulia watoto wao mali katika hata nchi za ng'ambo.

> 148. Kila mtoto katika hawa **amefunguliwa akaunti** katika benki ya Baroda. Licha ya akaunti, Boribori anawafungulia bima za maisha na za masomo katika shirika la Bima la British Assurance.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 213)

> 149. Alikuwa na mtoto mvulana mmoja, Jim. Jim **ashanunuliwa** nyumba mbili Marekani katika mji wa New York.
>
> (Habwe, 2005, Ukur.213)

Kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutendwa, mwandishi analenga kusisitiza upande wa yambwa tendewa ya kimantiki, yaani wahusika watendewa, kama tunavyoona katika kifungu na '**ashanunuliwa nyumba**' badala ya "Boribori amemfungulia kila mtoto akaunti…" au 'Alimnunulia mtoto wake Jim nyumba.' Mwandishi angeweza kutumia sentensi moja kwa kusema: "alikuwa na mtoto mvulana mmoja Jim, ambaye ashamnunulia nyumba mbili marekani…" Badala yake, mwandishi anatenganisha habari kuhusu Boribori kuwa na mtoto, na mtoto huyo kununuliwa nyumba. Habari kuhusu mtoto wa mchungaji kumiliki mali huko Marekani imechimuzwa na mwandishi pale mwandishi anapomdokezea msomaji tu kuhusu nani aliyemnunulia Jim nyumba.. Baada ya kifungu "ameshanunuliwa nyumba mbili," tungetarajia mwandishi kusema "na baba yake" ili sentensi iwe na mshikamano. Lakini mwandishi anachimuza uwezo wa mchungaji Boribori wa kununua mali hata katika nchi kama Marekani kwa

kudondosha kiima cha kimantiki (mtendaji), yaani baba yake na kusisitiza yambwa ya kimantiki (Jim, mtoto wake Boribori). Upangaji huu wa vipashio kwa kusisitiza watoto wa wachungaji umekusudiwa na mwandishi kumwonyesha msomaji maisha ya kitajiri ya watoto wa wachungaji. Kiasi hiki cha utajiri hakiambatani na maisha ya Kikristo ambayo yanafaa kutokuwa ya tamaa ya mali na pesa. Mwandishi anatuonyesha ukweli kinzani huu wa maisha na matarajio kuhusu wachungaji. Mchungaji Michael anadhihirisha jinsi maisha ya Mkristo wa kweli yanavyofaa kuwa. Yanafaa kuwa kama ya Yesu ambaye hakuwa na nyumba, gari, wala mke (Habwe, 2005, Ukur. 44).

5.3 Muhtasari wa Sura

Sura hii imechanganua mbinu za kisintaksia zilizotumiwa katika riwaya teule kusawiri maudhui ya dini na mamlaka. Mbinu ya kisintaksia iliyotumika hasa ni usambamba wa kiusawe. Hii inaashiria ufaafu wa mbinu hii katika kuwasilishia maudhui ya dini na mamlaka. Imebainika kuwa, mbinu za kisintaksia zinaingiliana, kwa mfano matumizi ya usambamba wa kiusawe na mbinu ya matumizi ya kauli ya kutendwa zinaingiliana kiuchimuzi. Udondoshaji pia unatokea katika urudiaji wa tungo. Katika riwaya za *Asali Chungu* na *Kasri ya Mwinyi Fuad*, urudiaji hadi mara saba au zaidi unatumika kwa ajili ya kushawishi. Mbinu za mgeuko wa polepole, pamoja na muundogeu hazikutumika sana katika riwaya zote teule. Huenda hii inatokana na hali ya kutotumika kwake hata katika matumizi ya kawaida ya lugha. Sura inayofuata inaangazia matumizi ya nduni za tamathali za usemi katika kuibua masuala ya dini na mamlaka katika riwaya teule za Kiswahili.

SURA YA SITA

MATUMIZI YA TAMATHALI ZA USEMI KAMA MBINU ZA KIMTINDO KATIKA UCHIMUZI WA MASUALA YA DINI NA MAMLAKA KATIKA RIWAYA TEULE

6.0 Utangulizi

Sura ya tano ilichunguza nduni za kisintaksia zilizotumiwa kimtindo na waandishi wa riwaya teule kusawiri maudhui ya dini na mamlaka. Sura hii inatimiza lengo la tatu. Inachunguza nduni za kimtindo katika tamathali za usemi ambazo zimetumika katika riwaya teule kuchimuza maudhui. Tunaangazia tamathali za aina mbalimbali zinazodhihirika katika riwaya teule, kama vile sitiari, tashbihi, tashihisi, chuku, kinaya, na nyinginezo.

Mbatiah (2001) anaeleza kuwa tamathali za usemi ni ukiushi wa kimaksudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana na mpangilio wa maneno ili kuleta maana mpya au msisitizo. Kwa upande wake, Wales (2014) anadai kuwa, asili ya tamathali za usemi ni balagha ya kirasimi ambapo zilitumiwa kama mbinu za kupangia na kufafanulia hoja, na kuathiri hisia za hadhira. Kwa hivyo, ivyo, tamathali za usemi zimekuwa zikihusishwa na sanaa ya utunzi wa kifasihi.

Ni dhahiri kuwa tamathali hutumiwa na waandishi kuimarisha maelezo yao kwa vile nyingi zinatoa taswira dhahiri kuhusu suala linalozungumziwa, kupitia kwa njia ya ulinganishaji. Zinatumiwa kama njia ya kuchimuzia ujumbe wa mwandishi. Ujumi unaotokana na matumizi ya tamathali humvuta msomaji na kumfanya azingatie na kutia maanani kinachowasilishwa katika tungo yenye tamathali husika.

Tamathali zinamwezesha mwandishi kusema machache kwa kutumia maneno machache na kwa uwazi kabisa. Badala ya kutumia maelezo marefu kuhusu hali fulani, mwandishi anaweza akatumia tamathali fulani ambayo itafupisha maelezo hayo marefu kwa maneno machache tu.

6.1 Tamathali za Usemi Zilizotumika katika Riwaya Teule

Kuna tamathali anuwai ambazo zimetumiwa na waandishi wa riwaya teule ili kuibua maudhui tofauti tofauti Miongoni mwa tamathali hizo ni pamoja na sitiari.

6.1.1 Sitiari

Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013), sitiari ni "tamathali ya usemi yenye maana ya kuhusisha kitu kimoja na kingine vyenye sifa zinazofanana." Naye Mbatiah (2001) anaeleza kuwa sitiari ni tamathali inayotumia ulinganishi, ambapo vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia na kimaumbile vinahusianishwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Pia, anasema kwamba sitiari huleta udhahiri na msisitizo katika maelezo. Hii ni mbinu ya kiulinganishi kama tashbihi ila ulinganishi huo haujitokezi waziwazi, yaani sitiari zinafanana na tashbihi ila katika sitiari vitu viwili vinalinganishwa bila matumizi ya maneno kama vile 'kama,' 'mithili ya,' 'mfano wa,' na kadhalika. Hapana matumizi ya viungio kama 'mithili' ya, 'mfano' wa, 'kama', na kadhalika. Sitiari, kama zilivyo tamathali nyingi, imejengeka kwenye uhamishaji wa maana. Chapman (1973, kama anavyorejelewa na Kitsao, 1975) anaeleza kwamba sitiari hulinganisha vitu kwa kuvifananisha kupitia njia ya kufupisha tashbihi ila misingi yake ya mshabaha haielezwi kwa maneno.

Kama ilivyo kwa tashbihi, sitiari zinalenga kumpatia msomaji taswira ya kile kinachozungumziwa. Taswira ni zana muhimu inayomsaidia msomaji kuelewa kwa vile kitambuzi, picha hazisahauliki kwa upesi na zinadhihirisha jambo kwa njia bora zaidi.

Akitumia sitiari, mwandishi wa riwaya ya *Paradiso*, ameibua maudhui ya rushwa ndani ya makanisa. Mwandishi anazungumzia jinsi wahudumu wa kidini wanavyohusika katika vitendo vya rushwa au ufisadi. Hili linadhihirika tukimwangalia mhusika Boribori, ambaye anachukua nafasi ya askofu wa kanisa la New Jerusalem, baada ya kifo cha Askofu Joshua. Askofu Boribori anakabiliwa na kesi ya ulanguzi wa madawa. Ili kujaribu kujinasua kutokana na kesi hiyo, Boribori anaamua kumhonga Moriasi, jaji mkuu wa kesi inayomkabili.

> 150. Moriasi na Boribori walirudi kutoka sehemu ya chemba. Boribori **alidondoka** shilingi milioni moja. Aliitoa kama **chai** kwa jaji Moriasi.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 212)

Mwandishi hataji rushwa moja kwa moja. Anatumia sitiari kutuonyesha kitendo kisicho cha kimaadili kilichotendeka. Mwandishi anatumia maneno 'sehemu ya chemba.' Hii ina maana kuwa tendo lilitendeka faraghani ambapo waliohusika hawakutaka watu wengine wapate taarifa kuhusu mkutano huo. Boribori anakutana na Moriasi wakati wa usiku. Mwandishi anasema, "Hakuna mtu hata mmoja aliyewashuhudia wakati wa usiku huo." Majira ya usiku yanazidisha ufaragha wa tendo hilo. Pia, kwa vile wakati mwingine usiku huhusishwa na vitendo viovu, Boribori kukutana na Moriasi usiku inaashiria kitendo ambacho si kizuri.

Tena, Boribori "**alidondoka**" shilingi milioni moja. Hii ni sitiari inayomaanisha kuwa Boribori alitoa hongo ya kiasi hicho cha pesa. Sitiari hiyo imejengwa kwa matumizi ya neno 'alidondoka,' badala ya neno 'alitoa.' Neno 'alitoa' lisingemvuta msomaji. Habwe anatumia neno 'alidondoka,' badala ya 'alitoa,' kumfanya msomaji azingatie kitendo hicho kisicho cha kimaadili cha hongo. Kwa kawaida kitu kinadondoka, au mtu anadondosha kitu, sio mtu kudondoka kitu. Hivyo, mtu kudondoka kitu fulani si matumizi ya kawaida ya lugha. Huu ni uchimuzi anaoutumia mwandishi kumfanya

msomaji azingatie lugha isiyo ya kawaida iliyotumika na ajaribu kufasiri umuhimu wa matumizi ya lugha hiyo. Katika muktadha huu, mwandishi analenga kwamba msomaji azingatie kitendo cha rushwa kinachofanywa na mtumishi wa Bwana, pamoja na ukwasi wa mchungaji huyu, kwa vile milioni moja ni kiasi kikubwa sana cha pesa kwa watu wengi.

Katika sentensi ya mwisho ya dondoo la 150, mwandishi anatupatia ufafanuzi zaidi wa kitendo kilichotendeka. Anasema kwamba Boribori aliitoa milioni moja "kama **chai** kwa jaji Moriasi." 'Chai' katika muktadha huu pia ni sitiari. Inamaanisha rushwa. Vilevile, sitiari hii ya 'chai' inajenga tasfida ambayo maana yake imezoeleka na watumiaji wa lugha katika jamii mbalimbali. Kama tasfida, 'chai' ni njia ya kuepuka ukali wa kusema 'rushwa.' Mwandishi asingesema: "aliitoa [milioni moja] kama rushwa kwa jaji Moriasi." Waandishi wa kazi za kifasihi hutumia lugha fiche ili kuwavuta wasomaji na kuwafanya wajaribu kufasiri ujumbe uliokusudiwa. Hivyo hakuna shaka kwamba Boribori alikuwa akimhonga Moriasi.

Katika riwaya hii ya *Paradiso* mwandishi anatumia sitiari nyingine kuibua maudhui ya rushwa. Akizungumzia ishara za siku za mwisho, mwandishi anataja vita, njaa na maradhi. Ishara nyingine ya siku za mwisho anayoitaja ni mlungula.

151. **Mlungula ulikuwa madhehebu** ya waja katika dunia.
(Habwe, 2005, Ukur. 123)

Kwa kusema kwamba "mlungula ulikuwa madhehebu" mwandishi anamaanisha kwamba mlungula sasa ulikuwa ni njia ya kawaida ya watu ya kuendelezea maisha. Mlungula unatokana na tamaa ya pesa ambayo mwandishi anaikemea sana anaposema, 'watu walijipenda na kupenda pesa' (Habwe, 2005, Ukur. 123). Kupenda pesa kupita kiasi kunasababisha hali ambapo mtu hajali jinsi anavyozipata; mradi tu amezipata.

Hata wachungaji katika kiwango cha uaskofu, kama Joshua na Boribori wanajihusisha na mlungula ili kupata pesa.

Naye Said Ahmed Mohamed ametumia sitiari kusawiri maudhui ya rushwa katika riwaya yake ya *Asali Chungu*. Kuna ukosefu wa kazi, hasa kwa vijana kama Dude. Tunaona kwamba ili kupata kazi katika Ofisi ya Leba, inabidi wanaotafuta kazi wamhonge ofisa wa Kihindi anayeshughulikia kuwatia watu kazi.

> 152. Mara nyingi aliwatia kazini jamaa zake wa Kihindi au yeyote aliyeweza **kumpa tonge**." Kazi njema zikawa za mabwana na matajiri; kina Dude mara nyingi wakiangukia utopasi. Na hata hizo za utopasi, huweza kupita mwaka mzima mtu anakwenda akirudi bila kupata lolote, ila kuwaona wale waliokuja mwisho wanatoka ofisini na furaha, wamekwisha pata kazi.
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 66)

"**Kumpa tonge**" ni sitiari inayomaanisha 'kumhonga'. Kazi ni chache na duni na rushwa pia inahitajika ili kuzipata. Wanyonge akina Dude wanaachwa wakizurura kutokana na kutokuwa na hata pesa za kuwahonga maofisa wa serikali kama huyo Baniani kwa sababu hasa vijana wanatafuta kazi ili kupata pesa.

Akitumia sitiari pia, mwandishi wa riwaya ya *Paradiso* anasawiri maudhui ya utashi wa pesa katika makanisa. Kwa sababu ya utashi wa pesa na mali, kanisa la New Jerusalem linapokea na kuwaombea wanasiasa. Tena kanisa hilo linashiriki moja kwa moja katika siasa za nchi kwa kukiunga mkono chama kimojawapo kinachogombea uchaguzi – chama cha FORD Kenya. Wanasiasa nao wanaleta pesa katika kanisa hilo.

> 153. Askofu Joshua na kasisi Lona Bosire walipokea misaada yote wakaiweka katika akaunti zao kwa niaba ya kanisa la New Jerusalem.
> Mapato yaliyotoka katika miradi ya kanisa…pia **yalimiminika** katika **fuko** lao.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 130)

154. **Kapu zima** la zaka, sadaka, fungu la kumi na matoleo mengine **alilivuna** Joshua.
(Habwe, 2005, Ukur. 48)

155. Akaunti zao **zilifura** kwa darahima.
(Habwe, 2005, Ukur. 134)

Katika madondoo ya 153 – 155 mwandishi ametumia sitiari mbalimbali. Kuna vitenzi anbavyo vimetumiwa kisitiari. Vitenzi hivi ni '**yalimiminika**', '**alilivuna**' na '**zilifura**'. Uamilifu wa kisitiari wa kitenzi '**yalimiminika**'katika muktadha huu unatokana na hali kwamba mapato (pesa) hayamiminiki, bali vitu vioevu ndivyo ambavyo humiminika. Tena, tunaambiwa kwamba kapu **zima** la sadaka, fungu la kumi, na matoleo mengine '**alilivuna**' Joshua. Kwa kawaida kinachovunwa ni mazao, sio pesa. Kwa hivyo, mwandishi kulitumia neno hilo katika muktadha huu ni kulihamishia maana na matumizi mengine, yaani pesa sasa zinavunwa mithili ya mazao. Halafu mwandishi anaeleza kwamba akaunti za Joshua na mkewe Lona **'zilifura**' kwa darahima, yaani 'kwa pesa'. Vilevile hapa tunaona matumizi ya kisitiari ya kitenzi 'zilifura' kwa vile mwili ndio hufura, sio akaunti. Mwandishi anatumia tungo sitiari '**zilifura** kwa darahima' badala ya neno 'zilijaa kwa pesa' kwa vile matumizi ya kauli 'zilijaa kwa pesa' yasingekuwa na athari ya kumvuta msomaji. Maana ya sitiari '**zilifura** kwa darahima' ni kwamba kiasi cha pesa kwenye akaunti zao kiliongezeka sana.

Matumizi ya vitenzi '**yalimiminika**,' '**alilivuna,**' na '**zilifura**' ni njia ya uchimuzi wa suala la utashi wa pesa katika makanisa ya kiprotestanti kwa njia ya sitiari. Maneno hayo yanavuta nadhari ya msomaji kwa vile yametumika katika mkutadha usio wa kawaida. Msomaji hawezi kukosa kushtushwa na matumizi ya lugha isiyo ya kawaida kama hiyo, na atajaribu kufasiri kusudi la matumizi yake na maana iliyomo katika tungo husika. Tukizingatia kwamba viongozi wa dini hawatarajiwi kukimbilia vitu vya

dunia, tabia yao ya kujaza akaunti zao zinazotokana na matoleo ya waumini ni kitu kinachokinzana na mafundisho ya Kikristo. Viongozi hawa hawaonyeshi mfano mwema kwa wanajamii wengine.

Mwandishi amemsawiri mhusika Joshua kama mtu mwenye kupenda mali:

> 156. Japo kila siku kanisani alidai Mungu alimwongoza na kumfichulia mambo lakini mara nyingi kama si hadaa yalikuwa ni mawazo yaliyokwenda na **utashi wake wa mali**.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 138)

Maelezo katika dondoo hili yanaziweka sitiari zilizotumika katika madondoo ya 153 – 155 katika muktadha. Mwandishi anatueleza moja kwa moja kwamba mchungaji huyu ni mtu mwenye utashi wa mali. Kwa hivyo, Askofu Joshua, anatumiwa kama mfano wa wachungaji wenye tamaa ya pesa na mali.

Kwa sababu ya utashi wa mali na pesa, wachungaji wanatumia mbinu fulani ili kupata pesa kutoka kwa waumini. Zaka na matoleo mengine kanisani yanasisitizwa na wachungaji pamoja na wasaidizi wao.

> 157. **Nyimbo zilinyunyizwa** na zikasaidia kuinua imani za watu na kuwaweka tayari kuabudu Maulana. Kwa hakika waumini walionekama wenye furaha na walioridhika na shughuli iliyokuwa ikipita
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 53)

Wachungaji wanatumia mbinu ya nyimbo “kuinua imani za watu na kuwaweka tayari kuabudu Maulana.” Mwandishi anatumia kauli “**nyimbo zilinyunyizwa**” badala ya “nyimbo ziliimbwa” ili kuchimuza mbinu hiyo ya makanisa kutumia nyimbo kama njia ya kulainisha nyoyo za waumini waweze kutoa zaka. Mwandishi anatumia kauli ‘nyimbo zilinyunyizwa’ badala ya ‘nyimbo ziliimbwa’ kwa vile kauli ‘nyimbo ziliimbwa’ ingesikika kama ya kawaida, na isingeivuta nadhari ya msomaji. Kwa

kawaida kitu kioevu ndicho kinachonyunyizwa. Kwa hiyo ‘kunyunyiza’ nyimbo kanisani ni kama kuwanyunyizia waumini kwa ajili ya kuwalainisha na kuwafanya wawe tayari kusikiliza na kutekeleza yatakayosemwa. Ndiyo maana “waumini walionekana wenye furaha na walioridhika na shughuli iliyokuwa ikipita.”

Maudhui ya tamaa ya pesa miongoni mwa wachungaji katika riwaya ya *Paradiso* yanasawiriwa pia kupitia kwa mhusika Zuhra, mhusika Mwislamu ambaye anaangalia mambo yanayotendeka makanisani kama mtu aliye kando:

> 158. Wanagombea washirika na zaka. Pesa zimekuwa **uti wa mgongo** wa injili hapa Mombasa.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 45)

Sitiari iliyosisitizwa inamaanisha kwamba pesa sasa zinaangaliwa kama kitu cha msingi katika shughuli za makanisa. Ni kama kusema bila pesa hakuna injili. Ni kinaya kwamba injili imefanywa kuwa kama bidhaa katika makanisa. Makanisa hayafai kuweka pesa kipaumbele, ingawa zinahitajika katika shughuli mbalimbali za kanisa. Hivyo, mwandishi anakemea tabia hii ya wachungaji kuweka pesa kipaumbele cha mahubiri yao. Badala ya kugombea usambazaji wa injili wanagombea washirika na zaka. Lona anajitahidi kuhakikisha kwamba kanisa linajaa kwa kuleta “mikakati mbalimbali ya injili mle kanisani” (Habwe, 2005, Ukur. 120). Lakini zaka yenyewe haitumiwi kufanya kazi ya kuendelezea injili bali inatumika kuwatajirisha wachungaji. Waumini wanalalamika kwamba pesa za zaka ‘wanazila wao,’ yaani wachungaji.

Mbali na sababu zinazoelezwa na mwandishi za waumini kwenda kanisani, mwandishi anazungumzia sababu za wachungaji kuanzisha makanisa. Kuna makanisa kadhaa katika sehemu moja wakati ambapo kijuujuu, lengo lao ni lile lile – kumwabudu Mungu.

159. Kanisa jingine… **lilimea** Kibera. Mtaa wa Kibera ulikuwa nyumbani mwa makanisa ya sampuli zote.

Makanisa hayo yalivunjika kila siku. Mapya yalijengwa na watu wawili, hata watatu. Yote lengo lake likawa kwenda Paradiso.

(Habwe, 2005, Ukur. 160)

Sitiari '**lilimea**' inamaanisha kwamba kanisa jingine lilianzishwa katika eneo hilo hilo la Kibera. Tayari kuna makanisa mengine kadhaa katika sehemu hiyo. Makanisa 'yanamea' kama mimea. Sitiari hii inaonyesha mtazamo wa mwandishi kuhusu kuanzishwa kwa makanisa haya. Anaona kwamba makanisa yamekuwa mengi mno isivyohitajika, na hata mengine 'yalizua taharuki' tu, yaani hayakuwa katika msingi wa kumwabudu Mungu (Habwe, 2005, Ukur. 160). Msingi wa kuanzisha makanisa haya, siyo injili au kwenda paradiso ya baadaye, ila ni **kujitafutia riziki** (Habwe, 2005, Ukur. 220). Kwa sababu ya kujitafutia riziki, makanisa hata hayadumu. Viongozi wa makanisa wanashindania uongozi wa makanisa ili waweze kudhibiti zaka na matoleo mengine kadhaa.

Mwandishi pia anaangazia suala la injili ya utajiri au ya maendeleo ambayo ndiyo inayopewa kipaumbele makanisani. Jambo hili bado lipo katika makanisa ya kiprotestanti leo. Badala ya injili kusisitiza lengo la kwenda paradiso ya baadaye, injili ya wachungaji inasisitiza kujenga paradiso ya hapa duniani. Aina hizi mbili za paradiso zimerejelewa sana na mwandishi, tukizingatia wahubiri kama vile Joshua na Boribori wanaojenga maisha ya utajiri na starehe hapa duniani kama kwamba ni paradiso yao ya hapa duniani.

160. Sasa **injili iliyovuma** New Jerusalem ilikuwa ya maendeleo ya kiuchumi.

> Askofu Joshua alikashifu mtu yeyote aliyeendelea kuja kanisani na Mungu Baba hajampa gari au kumzawadisha kana kwamba injili na utajiri ni mambo yaliyofungamana.
>
> **Matunda ya mahubiri** haya ungeyaona Jumapili yoyote. Ibada zilifanywa kwa zamu na kila zamu maegesho ya magari yalijaa kwa magari mapya…
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 120)

161. Yeyote aliyetaka utajiri wa haraka **alikimbilia injili**.

(Habwe, 2005, Ukur. 220)

Mwandishi anatumia neno '**iliyovuma**' kisitiari, badala ya kusema '**iliyohubiriwa**' ili kuchimuza jambo analolizungumzia kwa lengo la kumwathiri msomaji. Msomaji anaweza kulinganisha jinsi injili sasa inavyohubiriwa na picha aliyo nayo akilini ya jinsi upepo unavyovuma. Mfuatano wa maneno 'sasa,' na 'iliyovuma,' na jinsi yanavyohusishwa na injili ya maendeleo ya kiuchumi unaonyesha kwamba mwandishi hakubaliani na injili ya aina hii. Hii ni bayana katika kauli yake, "kana kwamba injili na utajiri ni mambo yaliyofungamana." Mtazamo wa mwandishi ni kwamba utajiri na injili ni mambo yasiyofungamana. Kwa njia fulani anasema kwamba injili ya namna hii ambayo sasa inasisitiza utajiri siyo injili ya kweli ambayo itampeleka mtu ahera au paradiso ya baadaye. Kauli hii inapatana na jinsi ambavyo mwandishi amesisitiza kwamba binadamu, badala ya kufanya vitendo vitakavyoweza kumpeleka paradiso ya baadaye, anafikiria paradiso ya hapa duniani, ambayo haina msingi wa dini.

Lakini injili ya aina hii inaleta manufaa kwa wachungaji. Mwandishi ametumia sitiari '**matunda ya mahubiri**' kurejelea manufaa haya. Injili ya utajiri inawavuta waumini wengi wanaoikimbilia (Dondoo 161). 'Alikimbilia injili' ni sitiari nyingine iliyotumiwa na mwandishi kusisitiza hoja yake. Matumizi ya sitiari hii yanatuonyesha mtazamo hasi wa mwandishi kuhusu injili ya utajiri. Watu kukimbilia injili inaonyesha kukurupuka tu bila kufikiria misingi ya Ukristo. Wanalenga utajiri au faida ya kiuchumi tu. Maegesho ya kanisa yanajaa kwa magari ya waumini wanaotoka 'pembe mbalimbali za

ulimwengu.’ Hawa wote wanaleta pesa kanisani. Kwa hivyo, ibada ‘zilifanywa kwa zamu’ kwa ajili ya kuhudumia idadi hii ya waumini na kuingiza pesa zaidi kanisani. Katika dondoo la 58 tunaona jinsi mwandishi anavyotumia urudiaji kurejelea ibada kadhaa zinazopangwa na kanisa la New Jerusalem, kutokana na ongezeko la waumini. Wachungaji wanatajirika kutokana na ibada kadhaa na waumini wengi wanaoleta pesa kanisani. Baada ya kutajirika, wachungaji wanahamia maeneo ya kifahari jijini Nairobi na tena wananunua magari ya kifahari kama *Land Cruiser*, *Prado* na *Mercedes benz* (madondoo 272 – 275)

Riwaya teule zote tulizozichunguza katika utafiti huu zinasawiri maudhui ya unyonge sambamba na uwezo au mamlaka. Akitumia sitiari, mwandishi wa riwaya ya *Paradiso* anaonyesha pengo lililopo kati ya maskini na tajiri.

> 162. Nyumba yake [Boribori] nayo ni **masimulizi**. Imetamba kwenye nusu ekari. Ina matagaa sita. Walijenga waashi kutoka Israel. Vyuma kutoka Ujerumani… Maegesho – magari sita.
> (Habwe, 2005, Ukur. 222)

Katika dondoo la 162 mwandishi anatuonyesha maisha ya kitajiri ya mchungaji Boribori. Huyu ni mmojawapo wa wachungaji tajiri. Wengine ni wachungaji kama Askofu Joshua na mkewe Lona, Mchungaji Musa, na Mchungaji Michael. Sitiari imetumika kusawiri maisha ya kitajiri ya mchungaji Boribori. Nyumba yake inaelezwa kuwa ni ‘**masimulizi**’. Hii ni sitiari inayomaanisha kwamba hii si nyumba ya kawaida tu, ila ni nyumba ambayo kila anayeiangalia anaweza kumsimulia mwenzake kuhusu ufahari wake. Kuna maelezo mengi yanayofuata sitiari hiyo ambayo yanaelezea zaidi ufahari wa nyumba hii ili kudhihirisha kiasi cha utajiri wa mwenye nyumba hii – waashi kutoka Israel, vyuma kutoka Ujerumani, na vigae kutoka Ufaransa. Nyumba hii ya Mchungaji Boribori inalinganuliwa na nyumba za wakazi wa Kibera, ambao ndio wanaohudumiwa na wachungaji kama Boribori, lakini ambao ni maskini. Huko Kibera,

watu wanaishi katika vibanda. Wachungaji wanapotajirika, wanahama kutoka sehemu hiyo ya Kibera na kuenda kuishi kwenye mitaa ya kitajiri pamoja na kujijengea nyumba nzuri. Askofu Joshua anahama kutoka Kibera kwenda mtaa wa kifahari wa Woodley. Hata Mchungaji Michael naye anahama kutoka kibanda chake cha Kibera na kwenda Fort Jesus Estate.

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, maelezo kuhusu pengo kati ya matajiri na maskini yametolewa kupitia kwa mbinu ya sitiari. Hii inadhihirika tunapoangalia nyumba za wakazi wa eneo la Ng'ambo.

> 163. Wakapita Ng'ambo ambako majumba, kama kawaida, yalikuwa yamekaliana ovyo, **matonge kwa matone**… 'kila ndege huruka kwa mbawa zake.' Bali kwa dhahiri, **mbawa za watu wengi huku Ng'ambo zilikuwa dhaifu**.
>
> **(**Mohamed, 1977, Ukur. 89**)**

Nyumba za watu maskini wa sehemu ya Ng'ambo zenye mapaa ya madebe na makuti zilikaliana ovyo. Sitiari '**matonge kwa matone**' imetumika kumpa msomaji taswira kuhusu majumba haya. Msomaji anaweza akapata taswira ya nyumba zilizojazana katika sehemu hiyo. Tena, sitiari '**mbawa za watu wengi huku Ng'ambo zilikuwa dhaifu**' inatumiwa kudhihirisha unyonge wa wakazi maskini wa eneo la Ng'ambo. Wakazi hao wameelezwa kama kwamba ni ndege ambao mbawa zao ni dhaifu na hawawezi kuruka masafa ya juu sana. Kisitiari mbawa ni uwezo wa kiuchumi. Makazi ya watu wa Ng'ambo yanalinganuliwa na makazi ya kitajiri ya Zuberi ambayo ni jumba kubwa lenye ukuta uliolizunguka bustani nzuri.

Maudhui ya pengo kati ya maskini na tajiri yameendelezwa pia katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* ambapo tunamwona kabaila Fuad ambaye ana mali nyingi ambazo zinampa maisha anayoyataka, tofauti na maisha duni ya wafanyakazi wake pamoja na wakulima. Fuad ana shamba kubwa la karafuu pamoja na wafanyakazi kadhaa

wanaofanya kazi katika shamba hilo. Anapata pesa nyingi kutokana na zao la karafuu. Pesa hizo anazitumia anavyotaka.

> 164. ...siku kama hiyo, siku ambayo Fuad huja mjini kuuza karafuu… **huzama katika starehe** za mjini na anaporejea nyumbani huwa yu chopi hajali kitu chochote.
> (Shafi, 1978, Ukur. 21)

> 165. Muda ulivyopita ndivyo meza ya Fuad ilivyojaa watu na ilipofika saa tisa juu ya meza yake palikuwa na **msitu wa chupa** zilizojaa aina tofauti za ulevi.
> (Shafi, 1978, Ukur. 22)

Fuad hafanyi kazi yoyote. Wafanyakazi wanachuma karafuu na kuzisafirisha hadi mjini. Baada ya karafuu hizo kuuzwa, pesa zinaingia mfukoni mwa Fuad ambaye anapenda starehe. Mwandishi ametumia sitiari '**huzama katika starehe**' kuonyesha jinsi ambavyo Fuad anaanza kustarehe, bila kuhofia kuishiwa na pesa kwa vile anazo za kutosha, baada ya kuziuza karafuu. Ishara mojawapo ya starehe ya Fuad ni '**msitu wa chupa**' za pombe kwenye meza yake na marafiki zake. '**Msitu wa chupa**' ni sitiari inayorejelea chupa nyingi zilizokuwa kwenye meza ya Fuad. Fuad anatumia pesa zinazotokana na jasho la wafanyakazi wanyonge kuzama katika starehe kwa njia ya kunywa pombe kupita kiasi. Huu ni unyonyaji.

Maudhui ya unyonge katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* yamesisitizwa kwa sitiari nyingine. Wakati ambapo Fuad anaishi maisha ya starehe kwa kununua magari na kunywa pombe mjini, wakulima wengi na wafanyakazi ni maskini kabisa. Mwandishi anawataja majirani wakulima ambao Fuad anasema atashirikiana nao katika kulima, baada ya shamba lake kugawiwa wakulima kwa nguvu.

> 166. Jambo lililomshangaza [Kijakazi] lilikuwa kule kumsikia Fuad akiwataja watu kama Pandu, Haji na Makame kama majirani zake; watu ambao, hapo zamani, hakuwa na mahusiano nao yoyote. Watu hao walikuwa wakiishi hapo Koani lakini walikuwa ni katika **mafukara wa kutupwa**.
> (Shafi, 1978, Ukur. 56)

> 167. Hayo ndiyo yalikuwa maisha ya ulimwengu huu… kwa watu wa chini kama Dude.… Kuna maisha kwa wale waliotononoka kiasi cha kuwashibisha na kuwanenepesha mbwa wao… Kuna wengine, kama Dude, walioletwa dunuani **kwa kuteremkia migongo ya ufukara**…
> **(**Mohamed, 1977, Ukur. 67**)**

Mwandishi anatumia sitiari ya '**mafukara wa kutupwa**' kumaanisha kwamba wakulima hao majirani wa Fuad (Pandu, Haji na Makame) walikuwa maskini kabisa. Kitu cha kutupwa ni kitu kisicho na thamani yoyote. Mwandishi anawalinganisha wakulima hao na kitu cha kutupwa, kama kwamba ni takataka. Awali Fuad hataki kuchanganyika na watu kama hao kwa vile anawaona kama watu wa tabaka la chini. Hivyo, sitiari hii inachimuza hali anamojikuta Fuad. Hadhi yake imeshuka kiasi kwamba yuko tayari kushirikiana na wale ambao awali alikuwa anawaona kama watu wasio na umuhimu wowote.

Katika dondoo la 167, Said Mohamed ametumia sitiari '**kuteremkia migongo ya ufukara**' ili kusawiri maudhui ya unyonge dhidi ya uwezo mkubwa. Sitiari hii inaonyesha kwamba kuna wale ambao wamerithi ufukara kutoka kwa wazazi wao. Hivyo, wanazaliwa katika mazingira ya unyonge. Watu kama hawa wanajiona kama wanyonge sana kiasi cha kutoona kwa nini wanaishi. Ni kama kwamba hawana nafasi katika ulimwengu. Nafasi ya kuishi ni ya 'wale waliotononoka kiasi cha kuwashibisha na kuwanenepesha mbwa wao…' Kwa njia fulani binadamu wanyonge wanalinganishwa na mbwa, na hali ya mbwa hata ni afadhali zaidi kuliko ya binadamu. Hiki ni kinaya.

Dude anajiona kama mtu ambaye 'ameteremkia mgongo wa ufukara' kwa vile mama yake Semeni alikuwa maskini kabisa, aliyetegemea biashara ya kujiuza baada ya kubakwa na tajiri Zuberi. Baada ya kifo cha mama yake, inabidi Dude aache shule,

halafu aelekee mjini kutafuta riziki. Kuna kinaya katika hali hii ambapo Zuberi (baba yake Dude) ni tajiri. Hivyo kwa kweli, Dude ni mtoto wa mtu tajiri. Hakuteremkia katika mgongo wa ufukara kwa upande wa baba, kwa vile baba yake ni tajiri. Hata hivyo, hili halimsaidii kwa sababu wakati huu Dude na Zuberi hawafahamiani kama baba na mtoto.

Ugumu wa maisha ya vijana kama Dude unaelezwa na mwandishi moja kwa moja. Katika ufafanuzi huo wa moja kwa moja unaodhihirisha mwandishi kupenyeza masimulizi, sitiari kadha zimetumika.

> 168. Katika mushkeli tunamwona Amina na ule utashi wake na ashiki anavyosibu kumpata Dude hatimaye. Kwa kweli si Dude tu, bali anatumia **utajiri wake kuwa ni mtego** wa kumnasia nobe yeyote ampe lile alilolihamu yeye. Dude ambaye toka hapo kalemazwa, kapotoshwa tuseme, na juu yake yaje yale **maisha yake magumu yaliyomvaa** toka kuzaliwa kwake, ilikuwa rahisi kumnasa. Hivi zikaonekana **ncha** mbili tofauti zikikaribiana. Moja ni ile **ya ukarimu na uwezo wa kutoa** ambayo ilidhibitiwa na Amina, na nyengine ni **ya ule ulofa na haja iliyombana Dude**.
>
> **(**Mohamed, 1977, Ukur. 104**)**

Katika dondoo la 168 utajiri wa Bi. Amina anaoutumia kuwavutia vijana maskini ili wamstareheshe kimapenzi umeelezwa kwa sitiari ya '**mtego**.' Pia kuna sitiari kwamba maisha magumu '**yalimvaa** Dude toka kuzaliwa kwake.' Sitiari hii inalingana na ile inayosema kwamba Dude '**aliteremkia mgongo wa ufukara**' (Dondoo la 167) pamoja na ile ambayo Bushiri anaitumia kumshawishi Dude aikubali kazi ya Bi Amina. Bushiri anamsihi Dude aikubali kazi hiyo ili avuliwe '**guo la unyonge**' (Mohamed, 1977, Ukur. 88).

Pia nguvu zinazomnasa Dude (na vijana kama yeye) zimelinganishwa na ncha ambazo zina uwezo wa kuvuta kama ule wa sumaku. Dude yuko kati ya ncha hizi mbili zinazovutana. Tunaelezwa kwamba kuna **ncha ya ukarimu na uwezo** ya Amina na ile ya ulofa wake na haja. Dude anavutwa na ile ncha inayodhibitiwa na Amina yenye

uwezo na ukarimu. Juu ya 'yale maisha magumu yaliyomvaa [Dude] tangu kuzaliwa kwake, ilikuwa rahisi kumnasa.' Hapa tunaona mamlaka makubwa aliyo nayo mtu mwenye uwezo wa kifedha. Anayatumia mamlaka hayo kujipatia anachotaka, mkiwemo kuwanasia watu wanyonge. Kuna kinaya kwamba hata kama Amina ni tajiri mwenye uwezo mkubwa, kuna kitu anachokihitaji kutoka kwa mnyonge kama Dude.

Kwa vile anavyomilikiwa na kudhibitiwa na tajiri, mnyonge analinganishwa na mali. Amina anammiliki Dude kama mali.

169. 'We poa bibiye, usitaharuki. Niachie mie; mambo yote yatakuwa waa, waa kabisa. Nitafuzu kama nilivyofuzu kwa yule kijana msalihina, **nikamteka** akawa **mali yako**.'
(Mohamed, 1977, Ukur. **62**)

170. 'Basi… Nataka wewe uwe **mali yangu** pasi na mtu kuweza kuniingilia; umesikia hivyo?'

'Nimesikia,' Dude alijibu kwa utiifu. 'Hilo usiogope.'

Yeye mwenyewe alistaajabu kiasi gani alichomwogopa Bi Amina sasa… **Kweli papa limemmeza.**

(Mohamed, 1977, Ukur. 120)

Said Mohamed amesisitiza sana maudhui ya unyonge dhidi ya uwezo kwa njia ya sitiari, kama inavyodhihirika pia katika madondoo 169 na 170. Vijana ambao Amina anawanasa kupitia kwa mtego wa utajiri wake wanamilikiwa kama mali yake, kuamriwa anavyotaka yeye. Binadamu (Dude) analinganishwa na mali. Hata Dude mwenyewe anatambua kwamba hana njia ya kujinasua kutoka katika mtego huu wa Amina kwa vile yeye (Dude) ni mnyonge kabisa. Hivyo, anakubali kwamba '**papa limemmeza**'. Hii ni sitiari inayomaanisha kwamba Dude sasa anakubali kuwa anamilikiwa kikamilifu na hana uwezo wa kujinasua kiuchumi. Anadhibitiwa na nguvu za kiuchumi asizoweza kupigana nazo kiuchumi. Dude na vijana wengine wanyonge wanaamua kuifanya kazi yoyote ile inayowajia ili angalau wapate riziki, mkiwemo kumilikiwa kama watumwa wa ngono.

Katika riwaya ya *Paradiso* tunaona jinsi ambavyo umaskini unawafanya watu 'wamwagike' makanisani kwa wingi ili kuepuka umaskini kupitia kwa njia ya kuombewa na wachungaji.

171. Muasya aliamini watu **waliomwagika** kanisani ilikuwa kwa sababu ya dhiki.

(Habwe, 2005, Ukur.)

172. Maadui nao walikuwa wale waliofika na **milima ya shida na vikapu vya matarajio** wakatoka maskini bila kuambulia chochote.

(Habwe, 2005, Ukur.82)

Kupitia kwa mhusika Muasya, tunapata kujua kwamba watu '**wanamwagika**' kanisani kwa sababu ya dhiki. Sitiari 'walimwagika' inamaanisha kwamba watu wanakwenda kanisani kwa wingi. Kwa vile watu 'wanamwagika' kanisani kutafuta suluhisho la umaskini wao, hii inaonyesha kwamba tatizo la umaskini ni kubwa sana. Neno 'walimwagika' limetumika kuonyesha mtazamo hasi kuhusu sababu zinazowapeleka kanisani. Kwa kawaida vitu ndivyo vinavyomwagika, sio binadamu. Kwa hiyo, matumizi ya sitiari hiyo yanachimuza kiasi cha shida iliyopo miongoni mwa wakazi maskini. Inaonyesha hali ya watu wengi kukata tamaa, na hivyo kujaribu kuona kama kanisa linaweza likasaidia kuwakwamua kutoka katika umaskini.

Mwandishi ametumia sitiari mbili katika dondoo la 172. Sitiari ya '**milima ya shida**' inaashiria shida nyingi ambazo wingi wake unatia hofu, ambazo mtu anaona hawezi kukabiliana nazo. Nayo sitiari '**vikapu vya matarajio**' inaonyesha kwamba watu wanaichukulia injili kama wenzo wa kusuluhishia matatizo yao, sio kama njia ya kwenda paradiso. Hii ni kinyume na matarajio kwamba waumini wangekuwa wanamtafuta zaidi Mungu, sio kutafuta tu masuluhisho ya matatizo yao. Lakini mwandishi anaonyesha kwamba baadhi ya watu wenye nia mbaya wanaokwenda

makanisani au kwenye mikutano ya injili kwa azma ya kutatuliwa matatizo yao tu wanaambulia patupu.

Sitiari pia zimetumika kusisitizia hali ya mfarakano ndani ya makanisa na pia baina ya makanisa yanayoanzishwa kila kukicha. Mfarakano unatokana na chuki iliyopo ndani ya makanisa, ambayo pia chanzo chake ni ushindani mkali. Ushindani huu ni kwa ajili ya zaka.

173. Kanisa hili [la New Jerusalem] **liliporuka kileleni** kila aina ya shtuma zilitolewa na makanisa menza.
(Habwe, 2005, Ukur. 53)

174. Michael alipozidi kuvuma katika midomo ya watu alikuwa **akitia kitumbua chake mchanga** na viongozi wengine.
(Habwe, 2005, Ukur. 67)

175. [Michael] alielewa tosha **wambea ndio kensa** iliyovamia makanisa na kuyaangusha.
(Habwe, 2005, Ukur. 49)

Sitiari zimetumika kuonyesha hali ya kutoaminiana na chuki ndani ya makanisa. Kuna umbea na shtuma kati ya makanisa. Kanisa la New Jerusalem '**liliporuka kileleni**' ni sitiari inayomaanisha kanisa hilo lilipoanza kupata umaarufu au lilipoanza kuwa na waumini wengi pamoja na kufanikiwa kiuchumi. Pia, Michael anapopata umaarufu kutokana na ufanisi wake katika kuhubiri injili, viongozi wengine wanaanza kumwonea wivu na chuki. Hii ndiyo maana ya sitiari '**akitia kitumbua chake mchanga**,' yaani aliuharibu uhusiano kati yake na wachungaji wenzake. Mwandishi anasema, "Kila [Michael] aliposifika kwa miujiza iliyomkuza, Askofu Joshua aliudhiwa, moyo ukamwelea" (Habwe, 2005, Ukur. 67). Hapa tunaona askofu mzima akimwonea wivu mhubiri chipukizi badala ya kumhimiza na pia kushangilia kazi ya Bwana. Hiki ni kinaya, kwa vile Ukristo unahimiza upendo, sio chuki. Hali inayomkabili Michael ni ya hatari kwa vile riwaya hii inazungumzia baadhi ya wachungaji kutiliana sumu. Wivu

wa wachungaji kwa wenzao unatokana na utashi wa pesa na mali na pia cheo na nafasi katika jamii. Mwenye pesa na cheo anakuwa na mamlaka makubwa katika jamii.

Riwaya za *Paradiso*, *Nguvu ya Sala* na *Kasri ya Mwinyi Fuad* zinaangazia suala la wakati na mabadiliko, mintarafu dini na mamlaka. Hili limefanywa na waandishi kupitia sitiari mbalimbali. Hali zinabadilika na wahusika vilevile. Wamitila, katika riwaya yake ya *Nguvu ya Sala* anazungumzia suala la mabadiliko moja kwa moja, ambapo anayalinganisha na maji ya kasi:

> 176. … nilishaanza kuyadadisidadisi mambo fulani fulani kuihusu dini. …nilishaanza kuwa na wasiwasi mkubwa tarafu ya msimamo wa dini kumhusu mwanamke. …*Labda **mabadiliko ni maji ya kasi** na husemwa yajapo lazima uyape nafasi.*
> (Wamitila, 1999, Ukur. 161)

Susan anapitia mabadiliko. Hapo awali ana imani katika '**nguvu ya sala**' kama alivyohimizwa na wazazi wake. Lakini baadaye anaanza kuwa mtu mdadisi kuhusu suala la dini na kutambua kwamba mkabala wa 'nguvu ya sala' unashindwa kukabiliana na hali nyingi za kiuhalisia, hasa nafasi ya mwanamke katika jamii. Anatumia sitiari '***mabadiliko ni maji ya kasi***' na kwamba '**yajapo lazima yapishwe**,' kuashiria jinsi mabadiliko yanavyofaa kupishwa kwa vile ni ya lazima. Mabadiliko yanakuwa na mamlaka fulani dhidi ya nguvu za binadamu. Susan anaona kwamba wazazi wake bado wamekwamia katika imani na utamaduni na lazima wagundue ukweli, wazinduke, waanze kuwa na mkabala mpya kuhusu masuala ya maisha. Anamwambia baba yake: 'hata siku hizi watu hawana imani kubwa na hiyo dini' (*Nguvu ya Sala,* Ukur. 198).

Habwe, katika riwaya yake ya *Paradiso* anasawiri maudhui ya mabadiliko ambapo mwema hubadilika akawa mui. Hili linadhihirika tukimwangalia mhusika Michael. Sitiari mbalimbali zinatumika kuelezea mabadiliko anayoyapitia mchungaji huyu. Michael ameanza vizuri katika kazi yake ya kueneza injili na anaazimia kuwa kama

Yesu. Yeye ni mchungaji kielelezo, na anapata umaarufu sana. Lakini baadaye anabadilika kabisa na kuwa mtu ambaye hajali kabisa analolifanya. Katika mawazo yake mwenyewe anateleza na kuingia katika 'bwawa' la kishetani. Wakati huu, wema wake unatoweka.

177. Ni nini kilichomharibikia **akatia guu katika bwawa** kama hili? Bwawa la tope, bwawa la maangamizi na bwawa la kishetani.
(Habwe, 2005, Ukur. 153)

178. Kwa hakika **Michael aligeuka na kuwa nyambizi** huko chini ya bahari.
(Habwe, 2005, Ukur. 160)

179. Baadhi ya waliookoka **waliteleza** kwenye **sakafu telezi ya dunia.**
(Habwe, 2005, Ukur.123)

Mabadiliko anayoyapitia Michael yanaelezwa kisitiari. Katika dondoo la 177 tunaona kwamba kubadilika kwake na kuwa mchungaji mui kunaelezwa kama ni '**kutia guu katika bwawa.'** Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013) bwawa ni "mkusanyiko mkubwa wa maji mengi …" Badala ya maji, mwandishi anaonyesha kisitiari yaliyomo kwenye bwawa hili ambamo Michael ametia guu: tope, maangamizi, shetani. Faridi hizi zote zinazotaja vitu vilivyomo kwenye bwawa ambamo Michael anatia guu ni hasi. Kwa hiyo, tabia yake vilevile inageuka na kuwa hasi. '**Bwawa la tope**' inaashiria kwamba sasa Michael amejichafua kwa dhambi. 'Bwawa la maangamizi' ina maana kuwa kusudi la Michael la kuingia paradiso limetoweka. Nalo 'bwawa la kishetani' ina maana kuwa Michael hayuko tena katika njia ya Bwana ila yuko kwenye njia ya shetani – kitu ambacho kila Mkristo anajaribu kuepuka.

Katika dondoo la 178 tunaambiwa kwamba Michael '**aligeuka na kuwa nyambizi**' huko chini ya maji. Hapa mwandishi anatumia sitiari hiyo (aligeuka na kuwa nyambizi) kumlinganisha Michael na nyambizi, ambayo husafiri chini majini bila kuonekana. Hii

ina maana kuwa kwa juu Michael anaonyesha kwamba bado ni mcha Mungu, lakini kwa ndani vitendo vyake ni dhambi yenyewe. Anageuka na kuwa mnafiki kabisa kwa vile anaendelea kuhubiri neno la Bwana wakati ambapo pia anaendelea na uzinzi kwa kufanya mapenzi nje ya ndoa.

Mabadiliko ya kuiacha njia adilifu na kuingia ile isiyo adilifu yanawahusisha pia waumini wengine, sio wachungaji peke yao. Katika dondoo la 179, mwandishi anasema kwamba "baadhi ya waliookoka waliteleza katika sakafu telezi ya dunia." Kutoka kwenye njia ya wokovu na kufanya dhambi kumefananishwa na kuteleza. Mara nyingi anayeteleza huwa ana hakika kwamba yuko imara. Anajikuta ameteleza ghafla na wakati mwingine kuanguka. Dunia imelinganishwa na sakafu telezi. Hii ni kwa sababu ya hadaa zake. Waliookoka inabidi wawe waangalifu sana wasije wakateleza wakaingia kwenye dhambi. Mchungaji Michael anajikuta ameteleza na kuingia katika dhambi kwa kufanya mapenzi nje ya ndoa na Patricia. Kusudi la mwandishi katika madondoo ya 177 – 179 ni kuonyesha kwamba dunia ina vishawishi vingi ambavyo hata vinawavuta wachungaji na watu waliookoka. Ni kama kwamba wakati mwingine binadamu hana uwezo wa kujidhibiti. Mwema anaweza akabadilika akawa mui.

Vilevile katika riwaya ya *Paradiso* mwandishi anaibua maudhui ya mabadiliko ya "mui kuwa mwema." Mabadilko kama haya yanahusisha wahusika Musa na Michael. Awali, Musa hataki kusikia lolote kuhusu mambo ya dini, na anamkataza mkewe Rose kushiriki katika shughuli za kanisa. Hata hivyo, Rose anamshawishi mumewe Musa polepole mpaka 'akasalimu amri.'

180. [Rose] alimsukuma [Musa] pole pole kwa **mwendo wa kinyonga** hadi mwenyewe **akasalimu amri**….. Bandu bandu huisha gogo. Rose **alimbandua Musa pole pole.**
(Habwe, 2005, Ukur. 32)

181. Rose hakuamini **nyuki aliyekuwa zumbukuku** ndiye anayemzomea **yeye nyigu** aliyezembea **kazi ya kutengeneza asali**.
(Habwe, 2005, Ukur. 33)

Katika madondoo ya 180 na 181, sitiari kadha zimetumika kusawiri mabadiliko ya mui kuwa mwema. Rose anatumia '**mwendo wa kinyonga**' yaani mwendo wa kiutaratibu, katika kumbadilisha Musa. Pia, Rose '**anambandua**' Musa polepole mpaka Musa '**anaposalimu amri**' yaani mpaka Musa anapokubali kuokoka. Anakuwa mchungaji. Kabla hajabadilika, Musa analinganishwa na '**nyuki zumbukuku.**' Anapobadilika, Musa anaanza kumzomea mke wake Rose, ambaye analinganishwa na '**nyigu**' ambaye kimaumbile hatengenezi asali. Mabadiliko ya Musa yanakuwa kamili, yaani anabadilika kabisa na kuwa muumini, kiasi cha kumzomea mkewe Rose kwa 'kuzembea kazi ya kutengeneza asali,' yaani kuzembea kazi ya kanisa ya kujitayarishia paradiso ya baadaye. Lakini, baadaye Musa anabadilika tena na kuwa mhusika mui kwa kushiriki katika uzinzi. Anafumaniwa akifanya mapenzi na mke wa mtu. Ni kama kwamba Musa naye 'anatia guu katika bwawa'. Hivyo, Musa anabadilika na kuwa mwema, kisha anabadilika tena na kuwa mui.

Mwandishi wa riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* anasawiri maudhui ya mnyonge kujitambua. Awali **Kijakazi** hajui kwamba mabadiliko ya serikali yametokea na kwamba sasa mambo yameanza kubadilika kwenye shamba la Fuad. Hata hivyo, kidogo kidogo, anaanza kuelewa kwamba bwana shamba (Fuad) hana mamlaka tena.

182. Baada ya Kijakazi kujiuliza maswali yote yale, kidogo kidogo alianza **kuona mwanga**.
(Shafi, 1978, Ukur. 89)

Polepole Kijakazi anaanza kung'amua kwamba Fuad hana nguvu tena; nguvu sasa wanazo 'wale watu' wanaokuja kuzungumza na Fuad, yaani wanamapinduzi. '**Kuona**

mwanga’ ni sitiari inayomaanisha kung’amua jambo fulani. Kuona mwanga kwa Kijakazi kuna athari ya kuipunguza hofu yake kwa Fuad na tena kupunguza utiifu wake kwa bwana huyo. Baadaye anazikataa amri za Fuad na tena hata anakataa kumwita ‘bwana’ tena. Hatimaye, mnyonge Kijakazi naye anang’amua kwamba yeye ndiye amejikwamiza katika unyonge aliomo. Anabadilika kama walivyobadilika wafanyakazi wengine na kuasi mamlaka ya Fuad. Huo unakuwa mwisho kabisa wa mamlaka ya Fuad.

Mwandishi wa *Paradiso* anasawiri maudhui ya ukandamizaji katika kanisa. Katika baadhi ya makanisa ya kiprotestanti wachungaji wanakuwa na mamlaka makubwa kiasi kwamba waumini wanakandamizwa kwa njia fulani. Kuna hali ya wasiwasi na hofu. Kila muumini anaamua kunyamaza, asije akaathirika. Hali hii tunaiona katika kanisa la Bethany. Michael, Mchungaji wa kanisa hilo, amebadilika kabisa na kuanza kufanya vitendo visivyo vya kimaadili. Anahusika katika kashfa ya mapenzi nje ya ndoa na Patricia. Ingawa kashfa hii inajulikana wazi katika kanisa, Michael hajali. Waumini nao wanaogopa kukemea wazi kitendo cha Michael kwa vile kufanya hivyo kunaweza kupelekea madhara kwa yule anayethubutu kuzungumzia kashfa hiyo.

> 183. Ilibidi ufanye uteuzi kama ulitaka kukaa pale Bethany **uushone mdomo wako** na kuacha upekuzi wa mienendo ya mchungaji.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 160)

Hapa mwandishi ametumia sitiari “**uushone mdomo wako**” kumaanisha “unyamaze kabisa.” Sitiari yenyewe inaashiria kwamba kuna madhara fulani ukizungumzia mienendo ya Mchungaji. Athari kubwa ni kulazimika kuliondoka kanisa lako. Hii ni kwa sababu ya mamlaka makubwa aliyo nayo Michael sasa, kutokana na umaarufu wake na utajiri uliotokana na umaarufu huo.

Vitendo na tabia za wachungaji vinapelekea kanisa kuvunjika, badala ya kuwepo kanisa la Kristo la pamoja. Mchungaji Michael anapobadilika na kuwa mui anaiacha hata azma ya kuunda kanisa la Kristo lenye umoja, kama Yesu alivyohimiza.

> 184. **Kimbunga** hiki **kilipiga kanisa dafrao** hadi likavunjika vipande viwili.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 153**)**

Katika muktadha wa dondoo la 184, 'kimbunga' ni sitiari inayorejelea kashfa ya mchungaji Michael ya kushiriki katika uzinzi. Kimbunga hicho kinasababisha misukosuko katika kanisa la Bethany, yaani nguvu zilizolikumba kanisa la Bethany. Na 'kulipiga kanisa dafrau' ni sitiari pia inayomaanisha kuliathiri vibaya sana. Hata hivyo, Michael hajali kuhusu athari hizi kwa kanisa lake. Kuna kundi la wanaomuunga mkono mchungaji Michael na pia kundi la wanaompinga. Kusudi la mwandishi ni kusisitiza kinaya ambapo mchungaji kielelezo ndiye anayehusika katika uzinzi. Yule ambaye anakemea uzinzi ndiye anayehusika katika kuufanya. Mwandishi anaonyesha hali ambapo makanisa hayajakuwa mfano mwema kwa jamii.

Lakini, mwandishi anaonyesha kwamba katika maisha, mui anaweza akabadilika akawa mwema, baada ya kutambua makosa yake. Hii inadhihirishwa na mhusika Michael ambaye anaamua kubadilisha mwenendo wake, baada ya 'kutia guu katika bwawa.' Anaamua kuwa mfano mwema tena kwa Wakristo wengine na jamii kwa kulenga paradiso ya baadaye. Swali analojiuliza Michael yaani, "Ni nini kilichomharibikia **akatia guu katika bwawa** kama hili?" (dondoo la 177) linaonyesha kwamba Michael anajutia kitendo chake cha uzinzi na yuko tayari kurekebisha mwenendo wake.

Akitumia sitiari, mwandishi wa riwaya ya *Asali Chungu* anasawiri maudhui ya mnyonge kumnyanyasa mnyonge mwenzake. Mnyonge anatumiwa na mwenye mamlaka kumkandamiza mnyonge wenzake.

185. ‘Bi Mkubwa nimetumwa nikuite’
Mastura alisita pale alipomtokezea Biti Daudi.
‘Nani?’ Biti Daudi aliuliza kwa hamasa, kama vile lile jina la Biti Daudi lilikuwa si lake…
‘Wewe Bi-mkubwa,’ Mastura alijibu kwa unyonge na hadhari ili lile **bomu la asubuhi** lisije likampasukia.
(Mohamed, 1977, Ukur. **22**)

186. Lawama na malalamiko juu ya matendo ya Bwana Zuberi yakaendelea; na mara zogo likakua na kuhanikiza… Ndipo Kabore, yule tarishi, alipoitwa ndani kwa Bwana. Alipotoka ndani akawa **ameunoa ulimi wake**.
‘Zogo likiendelea, tamaa ya kuonana na Bwana itakuwa hakuna. Fanyeni zogo na ufidhuli wenu, maana mnajitia kujua nyie.’
Kwa kujisalimisha, wote wakakubali **kufyata mikia yao**.
(Mohamed, 1977, Ukur. 4)

Katika dondoo la 185 tunaona jinsi ambavyo Biti Daudi anawanyanyasa wafanyakazi anaowasimamia. Anawatukana ovyo kwa vile anataka kuonyesha mamlaka yake kwao katika kiwango chake, ingawa naye ni mfanyakazi tu kama wao. Tofauti ni kwamba amepewa wajibu wa kuwasimamia wenzake. Anajipendekeza kwa waajiri wake (Bi Amina na Bwana Zuberi) kwa kuwakandamiza wenzake ili yeye aonekane kama mtu mwenye bidii. Kusudi lake ni kupata upendeleo kwa njia ya kusaidiwa kifedha. ‘**Bomu la asubuhi**’ ni sitiari inayoashiria tusi ambalo mfanyakazi Mastura angetusiwa, kama asingekuwa mwangalifu. Biti Daudi anafurahia mamlaka aliyo nayo kwa wafanyakazi walio chini yake. Anawahangaisha ili kuthibitisha madaraka aliyo nayo.

Naye Kabore, tarishi wa Zuberi (Bwana DC) anatumiwa na Zuberi kuwadhibiti watu wanaokuja kumwona kwa sababu rasmi. Anaposhindwa kulidhibiti zogo linalofanywa na wanawake wanaolalamika kati yao kuhusu tabia ya Zuberi, anaitwa ndani na ofisa huyo, na anapotoka ndani ofisini mwa DC ‘akawa **ameunoa ulimi wake.**’ Hii ni sitiari inayomaanisha ‘akawa anaongea kwa ukali.’ Tishio la kutoweza kumwona Bwana DC linafanya kazi yake: wanawake wote wakakubali ‘kambayo ni sitiari’ inayomaanisha

kwamba wanawake hao ‘wakanyamaza kabisa kwa hofu.’ ‘Wanafyata mikia yao’ kwa sababu hata wao kufika hapo imekuwa shida. Wengine ndio wanarudi tu hapo mara nyingine, baada ya kushindwa kumwona Bwana DC mara kadhaa. Kabore hatambui kwamba yeye pia ni mnyonge anayetumiwa tu na wenye mamlaka. Wanawake wanamchukulia Kabore kama mtumwa, kwa vile wanaposhuhudia mavazi yake wanaona ishara tupu za utumwa – ‘mkanzu’ wake, ‘… kofia ya tarbushi iliyopoteza mkia’ na ‘nguo zilizompwaya…’ Kwa hivyo, ni kama kwamba wanawake hawa wanamhurumia tu huyu bwana ambaye wanatambua kwamba ni mnyonge tu kama wao, lakini wanaona kwamba yeye hajitambui; anafikiri kwamba naye ni mmojawapo wa wale wenye mamlaka.

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, mwandishi pia anasawiri maudhui kwamba mamlaka yana kikomo. Zuberi anawanyanyasa wafanyakazi wake na wanawake wakulima kwenye ardhi yake. Anambaka Semeni, msichana mtumishi wa nyumbani kwake. Lakini mwishowe naye anazeeka na kuugua na kutambua kwamba yote aliyoyafanya alipokuwa na mamlaka ni ya bure. Anajuta sana na kung’amua kwamba kuna ‘malipo’ kwa kuwatesa wanyonge, hasa Semeni. Mamlaka yana kipindi na mipaka yake.

187. Asubuhi ile, Zuberi alipokwisha kukoga na kunywa chai, alikaa ukumbini akiwaza **mchezo wake wa jana**…
(Mohamed, 1977, Kur. 17 - 18)

188. Lile jina la Semeni lilikuwa na maana kubwa kwa Zuberi. Lilitosha kumpa mseto wa mawazo na fikira za yale yaliyopita ambazo alitoka nazo pale hospitali, zikamchukua kumwonyesha **televisheni ya siku zake za nyuma**, siku za matendo. Aliviona vitakuro vyake siku ile, siku ya siku, vya mchana kuliwa usiku – **siku aliyoiramba asali**. Na Semeni akatoweka.
(Mohamed, 1977, Ukur. 174)

Siku inayofuatia kumbaka Semeni inakuwa ya furaha kwa Zuberi lakini sasa, badala ya ‘kuiramba asali’ anauramba uchungu wa matokeo ya kitendo chake. Kiangaza nyuma

chake kinalinganishwa na kuangalia televisheni – kisitiari. Zuberi sasa hafurahishwi na yale anayoyaangalia kwenye televisheni hiyo. Yanaleta uchungu mtupu kwake. Asali sasa imekuwa chungu. Inaonekana kwamba maneno ya Bi Pili kwa Zuberi, baada ya bwana huyo kukataa kutekeleza wajibu wake kwa Semeni, yanatimia. Bi Pili anamwambia Zuberi: "Bwana wewe, mtukufu wa jina na tajiri mwenye uwezo… nakwambia umekula wa mwenzako, miguu itakuelekea. Mungu si Asumani." Bi Pili anatambua unyonge wake. Anajua kwamba hawezi kumfanya Zuberi chochote kwa vile bwana huyo ana mamlaka makubwa. Hivyo, anamwonya Zuberi na tena kumsihi Mungu mwenye mamlaka yote ayaone matendo ya tajiri huyu mwenye uwezo mkubwa.

Mwandishi anairejelea sitiari ambayo ndiyo anwani ya riwaya yake ya *Asali Chungu*. Anatupatia taswira ya mhusika Zuberi, kabaila aliyekuwa na mamlaka makubwa lakini ambaye sasa amezeeka na kuugua, na kila kitu kumbadilikia.

> 189. Midomo yake ilimtetemeka, akainua mkono wake wa kuonyesha kidole pale alipokiona kivuli cha Semeni; halafu akameza mate. Yalikuwa **mate mazito machungu**. Huo ndio ulikuwa mwisho wa ladha yake. Kweli **utamu umegeuka uchungu**, lakini hakuwa na budi kuumeza. Kama aliwahi kunywa asali, ndipo leo kajua kuwa **asali chungu.**
> (Mohamed, 1977, Ukur. 186)

Maelezo katika kifungu hiki yanaifafanua anwani ya riwaya kinagaubaga. Pamoja na sitiari ya asali kuwa chungu, kuna sitiari zingine ambazo mwandishi amezitumia kufafanua maudhui kwamba majuto ni mjukuu, hata kwa wenye mamlaka. Mwandishi anasema kwamba Zuberi "akameza mate…**mazito machungu**" baada ya kukiona kivuli cha Semeni kimemsimamia. **Utamu umegeuka uchungu.** Katika vitendo vyote vibaya alivyowatendea watu wanyonge, kitendo cha kumbaka Semeni (kuiramba asali) ndicho hasa kinamgeukia na kuwa majuto mazito. '**…ndipo leo kajua kuwa asali chungu**.' Wakati moto uliowashwa na wanamapinduzi ukirindima na kuteketeza jumba

pamoja na mwili wa Zuberi, fikira ya mwisho ya Dude ni kwamba '**Dunia ina malipo yake**' (Mohamed, 1977, Ukur. 187). Zuberi kalipwa kwa vitendo vyake vya kikatili.

Yanayomfika mhusika Zuberi katika *Asali Chungu* ni kama kwamba yanakinzana na hoja ya mwandishi wa riwaya ya *Nguvu ya Sala* kwamba Mungu anauona udhalimu unaofanywa na wenye uwezo kwa wanyonge lakini hawaadhibu. Katika riwaya ya *Nguvu ya Sala*, Wamitila anatumia sitiari ya jua kama jicho la Mungu. Jua linalimulika eneo ambapo kuna mwili wa kijana aliyeuawa na watu jijini Nairobi kwa sababu ya kunyakua kibogosho cha mwanamke fulani. Watu wa jijini Nairobi wametovukwa na huruma kabisa kwa sababu ya hali ngumu ya maisha. Wanapambana na maisha.

> 190. Mm…labda ndivyo yalivyokuwa maisha. **Pambano** dhidi ya nguvu wasizoziweza watu. Je, **Mungu aliyaona haya**? [Richard] aliinua macho yake juu na kuyaelekeza mbinguni lakini yakapofushwa kwa muda na jua… **Limelimulika lile eneo sasa**; gimba nene la duara lililozungukwa na viwingu …Labda vile vilikuwa vinyusi vya jicho hilo; vikope vya kulilinda lisifikwe na uchafu. Uchafu wa kulisumbua jicho hilo… **jicho la Mungu.**
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 117)

Mwandishi anajiuliza ikiwa Mungu anaingilia katika masuala ya binadamu. Kuna vitendo vingi vya kikatili vinavyotendeka mjini na kwa mujibu wa mwandishi, inaonekana kwamba Mungu haingilii kati ingawa anaviona. Ndio maana mwandishi anatumia sitiari ya jua kama jicho. Jua linalimulika vizuri lile eneo ambapo kijana ameuawa kwa ukatili – jicho la Mungu. Swali la jumla kuhusu ugumu wa maisha na ukatili wa watu mjini linatangulia maelezo kuhusu jicho la Mungu. Je, **Mungu aliyaona haya**? Swali hili liko katika Sura ya 17 (Habwe, 2005, Ukur. 117) lakini jibu lake lilishatolewa katika Sura ya 13 (Habwe, 2005, Ukur. 84). Katika sura ya 13, mwandishi anadokeza kuwa tukio la mauaji ya kijana na matukio mengine kama hayo Mungu anayaona lakini haingilii kati kuyazuia. Hii inatilia mkazo motifu ya mwandishi

kwamba ‘**nguvu ya sala**’ inashindwa kukabiliana na masuala ya kawaida ya kila siku ya mwanadamu, yaani mapambano yao na maisha.

Kwa hivyo, wakati ambapo mwandishi wa riwaya ya *Nguvu ya Sala* anaonyesha kwamba Mungu anauona uonevu lakini hawaadhibu wanaowaonea wenzao, mwandishi wa riwaya ya *Asali Chungu* kwa upande wake anaonyesha kwamba Mungu hatimaye anawaadhibu wale wenye mamlaka wanaowaonea wenzao, kama anavyomwadhibu Zuberi, mwenye kuwanyanyasa wanyonge.

Katika dondoo la 190 kuna sitiari ya maisha kama pambano. Mwandishi anazungumzia ugumu wa maisha ya jijini Nairobi. Watu wengi jijini Nairobi, mkiwemo vijana kama Richard, wanashindwa kuzimudu gharama za maisha. Sitiari ya maisha kama pambano imetumika kusawiri ugumu wa maisha jijini Nairobi: “…labda ndivyo yalivyokuwa **maisha**. **Pambano** dhidi ya nguvu wasizoziweza watu.” Katika sitiari hii, mwandishi hamtajii msomaji moja kwa moja kwamba ‘maisha ni pambano’ ila anauchimuza mlingano kati ya maisha na pambano kwa kutumia tungo mbili zilizotenganishwa na alama ya kikomo, badala ya alama ya kistari kirefu, yaani tungo yenyewe ingekuwa: “**labda ndivyo yalivyokuwa maisha – pambano dhidi ya nguvu wasizoziweza watu**.”

Hali ya kiuchumi ina mamlaka fulani juu ya maisha ya watu. Wanajikuta wakivutwa huku na huku na nguvu wasizoweza kukabiliana nazo kwa ufanisi. Katika pambano hili dhidi ya hali ya kiuchumi, mvutano kati ya wakazi wa Nairobi hauwezi kuepukika kwa sababu ya hali ya kushindania riziki.

Maudhui ya nafasi ya utamaduni katika jamii sambamba na dini mpya, hasa Ukristo yamegusiwa pia kisitiari katika riwaya ya *Nguvu ya Sala*. Kwa sababu ya ujio wa dini

ya Kikristo, watu kama Richard wanaamini kwamba tamaduni zao ni kitu kilichopitwa na wakati; hazina uamilifu tena katika jamii.

> 191. Imani hizo hazina nafasi katika ulimwengu wa leo. Mzee hizo ni fikira za zamani ambazo zimepitwa na wakati.
> Umelogwa wewe? Zimepitwa na wakati gani? Imani zetu?
> …
> Mm. [Wazungu] wametukomboa kutokana na **giza la utamaduni**."
> Hakika ni ukombozi huo!
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 6)

Richard anaulinganisha utamaduni wa jamii yake na giza. Tena anaulinganisha Ukristo na ukweli. Kwa kutumia sitiari ya utamaduni kama giza, kama anavyodai Richard, mwandishi analenga kuonyesha kinaya kilichopo ambapo Richard anaiangalia imani mpya kama mwanga, na utamaduni wake kama 'giza.' Mwandishi anataka kuonyesha kwamba mtu kudharau utamaduni wake ni upuuzi.

Wamtila ametumia sitiari nyingine kuonyesha jinsi ambavyo Richard ameathiriwa na dini mpya ya Ukristo ambayo imemfanya achukulie mkabala wa '**nguvu ya sala**' ndio mkabala pekee unaoweza kutumika kukabiliana na kila changamoto ya maisha, kitu ambacho hata binti yake anaona kwamba sio sahihi.

> 192. Kwake [baba] kilichokuwa muhimu ni kuyafuata mafundisho ya dini na kuithamini nguvu ya sala. Kwa kiasi kikubwa imani hiyo **ilishampofua** na kumfanya ashindwe kuuangalia uhalisi.
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 71)

Mwandishi anatumia sitiari kwamba imani '**ilishampofua**' Richard. Maana ya sitiari hii ni kwamba Richard anazingatia mno mkabala wa nguvu ya sala; hazingatii mikabala mingine, kitu ambacho kinaonyesha mtu kutokuwa na uelewa wa maisha. Binti yake Susan anasema kwamba imani ilimfanya baba yake ashindwe kuona uhalisi. Uhalisi wenyewe ni kwamba maisha ni changamani, na mtu kufikiria kwamba kuna mkabala mmoja tu wa kuyakabili ni upuuzi. Susan anauchukulia upuuzi huu kama ni upofu. Hivyo, kinaya ni kwamba, ingawa Richard anamwambia mzee kuwa utamaduni wa

jamii yao ni giza, hata yeye mwenyewe anachukuliwa na binti yake kama ni kipofu ambaye hana mtazamo mpana wa masuala ya dunia.

Suala la jinsia limegusiwa pia kisitiari katika riwaya teule. Jamii imempa mwanamume mamlaka makubwa kuliko mwanamke. Hili linadhihirika tukimwangalia mhusika Musa, ambaye anamdhibiti mke wake Rose.

> 193. Aaa. Nisikupate unakwenda kanisani. Wala sitaki kuelezwa mambo ya kike mimi. Nikisema hapa hapana wa kunieleza jingine. **Kama wataka kuwa jogoo** hapa basi sema tuagane. Musa alikuwa mkali. Mkewe aliona vyema kumtii bila kuzua kivumbi…
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 65)

Musa anamzuia kabisa mke wake Rose kwenda kanisani. Sitiari ya '**kuwa jogoo**' inaamaanisha 'kuwa kama mwanamume,' kwa vile jogoo ni kuku dume. Mwanamume analinganishwa na jogoo ambaye huwatawala kuku wa kike. Dondoo la 193 linaonyesha jinsi mwanamume anavyomdhibiti mwanamke, ambaye (mwanamke) anaona hana la kufanya ila kutii tu amri ya mwanamume. Mwanamke asipofanya hivyo, ndoa inavunjika, na ikivunjika, yeye ndiye anayeathirika zaidi kwa vile atalazimika kuondoka.

Katika kujaribu kumwimarisha mhusika wa kike, Wamitila anatumia sitiari mbalimbali. Njia mojawapo aliyoitumia mwandishi ni kumsawiri mhusika wa kike akiwa na uwezo mkubwa kimasomo. Mwandishi amefanya hivi kupitia kwa mhusika mkuu Susan na baadhi ya marafiki wenzake wa kike anaosoma nao katika chuo kikuu.

> 194. Matokeo ya mtihani wa mwigo yalishatoka sasa. Nilikuwa mwanafunzi wa pili katika orodha ya wanafunzi kumi bora. Wa kwanza alikuwa Catherine Ouko, msichana **mfupi sana**; labda ndiye aliyekuwa **mfupi** kuliko wote shule nzima. Alikuwa na **akili shupavu…**
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 119)

Katika dondoo la 194 mwandishi ametumia sitiari ya mwanafunzi Catherine Ouko kuwa ni mfupi sana kimaumbile lakini ambaye kiakili ni shupavu kabisa. Hapa mwandishi anaulinganua ufupi wa kimaumbile na 'ufupi wa kiakili' ambapo anaonyesha kwamba ufupi wa kimaumbile hauwi sawa na 'ufupi wa kiakili.' Mwandishi anauchimuza uwezo wa Catherine kimasomo kwa kuzididimiza sifa zake za kimaumbile. Baada ya kutueleza kwamba Catherine ni mfupi, mwandishi anaongezea kwamba 'labda ndiye aliyekuwa mfupi kuliko wote shule nzima.' Mwandishi amefanya hivi ili mlinganuo kati ya ufupi wa msichana huyu na uwezo wake wa kimasomo ujitokeze na udhihirike zaidi.

Katika riwaya ya *Paradiso*, maudhui ya msamaha yameibuliwa pia kwa njia ya sitiari. Tunaona jinsi ambavyo Askofu Joshua anakurupuka kujaribu kumwua Boribori, baada ya mkewe (wa Joshua) Lona kudokeza kwamba Boribori amemnyanyasa kingono.

> 195. [Joshua] alikwenda katika chumba cha kulala akashika bastola yake. Boribori angepatikana mle ndani **angepewa risasi lake** palepale. Joshua hakutaka kumwachia Mungu wa Adhama afanye uamuzi na kumwadhibu Boribori.
> Aliona ni vizuri kama atamwadhibu mwenyewe.
> (Habwe, 2005, Ukur. 139)

Askofu Joshua, kwa kuhofia usalama wake anamiliki bastola. Hii ni kwa sababu ya cheo na utajiri wake. Haigi mfano wa Yesu, ambaye hakuhitaji walinzi. Katika dondoo la 195, sitiari '**angepewa risasi lake**' imetumiwa kumaanisha kwamba Boribori angeuawa moja kwa moja. Kama mwandishi mwenyewe anavyofafanua, Joshua hamwachii Mungu wajibu wa kumwadhibu Boribori, bali yeye anaamua kufanya hivyo mwenyewe. Anashindwa kumsamehe Boribori. Hiki ni kinaya, kwa vile Joshua hafuati mafunzo ya Kristo aliyehimiza msamaha, wakati ambapo msamaha ni nguzo ya Ukristo, na Joshua anadai kwamba yeye ni Mkristo.

Suala hili la Wakristo waliookoka kushindwa kutekeleza nguzo ya Kikristo ya msamaha imeangaziwa pia katika sehemu ya 4.2.6 ambapo Habwe anatumia mbinu ya urudiaji kudhihirisha jinsi ambavyo inamwia vigumu mhusika Lydia, mke wa Mchungaji Michael kumsamehe rafiki yake Patricia. Patricia ameingilia ndoa yake (Lydia) na Michael. Sasa katika sehemu hii, Habwe vilevile anatumia mbinu ya sitiari kuonyesha jinsi ambavyo mhusika Askofu Joshua naye anashindwa kusamehe. Tena katika riwaya ya *Nguvu ya Sala*, tunaona hali hiyo hiyo ya Mkristo kushindwa kusamehe. Akitumia mbinu ya usambamba wa kiusawe (Sehemu 5.1.2), Wamitila anaonyesha namna ambavyo Richard, mtu ambaye anajiona kama Mkristo aliyekamilika anashindwa kumsamehe mke wake Mary Kasiva, ambaye amejifungua mtoto wa nje ya ndoa yake na Richard.

6.1.2 Tashbihi

Wamitila (2003) anaeleza kuwa tashbihi ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia waziwazi. Anasema kuwa tashbihi hutambulishwa na matumizi ya viungio: 'kama', 'mfano wa', 'mithili ya', 'ja' 'kama vile', n.k. Kwa mujibu wa Wamitila, hii ni tamathali inayotumiwa sana katika kazi za kifasihi. Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013) inatoa maelezo yanayolingana na yale ya Wamitila kwa kueleza kwamba tashbihi ni usemi wa ufananisho au mlinganisho wa vitu viwili au zaidi kwa kutumia maneno kama vile 'kama.'

Waandishi wa riwaya za *Asali Chungu* na *Paradiso* wametumia tashbihi kusawiri maudhui ya pengo kati ya matajiri na maskini. Katika *Asali Chungu* tunaona kwamba mapebari kama Zuberi ndio wenye nacho, na katika *Paradiso*, matajiri ni wachungaji kama Askofu Joshua, Boribori na Michael.

196. Nyumba ilikuwa imeamka. Matayarisho mbalimbali yameshafikia kileleni. **Nyumba hii ilikuwa mfano wa hoteli**;

> hamkani na shughuli huanza kabla ya jua halijapasua, na kumalizikia pale bwana na bibi mwenye nyumba wanapoingia chumbani mwao kulala.
> (Mohamed, 1977, Ukur. 11)

Katika dondoo la 196, Said Ahmed Mohamed anailinganisha nyumba ya Zuberi na hoteli kwa sababu nyumba hiyo ina wafanyakazi wengi kwa mujibu wa shughuli zake nyingi. Kama ilivyo katika hoteli, shughuli katika nyumba hii zinaanza macheo hadi machweo. Hii inaonyesha uwezo mkubwa wa kiuchumi wa Zuberi kama mmiliki wa nyumba hii na wafanyakazi hawa wote, ingawa yeye hawalipi vizuri. Nyumba yake kulinganishwa na hoteli inaonyesha hadhi yake katika maeneo anakoishi ambako kuna ufukara mwingi.

Katika riwaya ya *Paradiso*, tunaona kwamba hata wachungaji ni wakwasi sana kama walivyo matajiri wa kilimwengu. Kutokana na kukusanya zaka, fungu la kumi, na matoleo mengine mbalimbali, wachungaji wanatajirika sana. Hata mchungaji Michael, ambaye awali anataka kuwa kama Yesu, kwa vile Yesu takriban karibu hakuwa na chochote, anabadilika na kuanza kuishi maisha ya anasa.

> 197. Sasa nitafanya nini?” Mchugaji alijiuliza akiwa kwenye ofisi yake **yenye kupambwa utadhani balozi**.
> (Habwe, 2005, Ukur. 170).

Ofisi za wachungaji zinaonyesha ukwasi mkubwa. Ofisi ya Michael ni “**yenye kupambwa utadhani balozi.”** Mwandishi ametumia tashbihi hiyo ili kuuchimuza ukwasi wa wachungaji. Ofisi ya Mchungaji Michael inalinganuliwa na hali ya kiuchumi ya wakazi wa Kibera. Raia wengi, mkiwemo waumini wanaohudhuria ibada za wachungaji ni maskini, lakini kinaya ni kwamba waumini hao maskini ndio wanaotoa zaka ambayo inawatajirisha wachungaji. Toni ya mwandishi inaonyesha kwamba hakubaliani na aina hii ya ubadhirifu. Mtazamo wake huu unatokana na uamuzi wake wa kutumia neno “**utadhani,**” ambalo linashiria hisia hasi kuhusu ofisi hiyo ya mchungaji. Balozi ni mtu anayeiwakilisha nchi yake, na yeye hutendewa tofauti na raia

wengine. Kumiliki ofisi kama ya balozi ni kujikweza. Ni kama kwamba hata naye mchungaji amejitenga na waumini wengine, wakati ambapo anatarajiwa kuishi maisha ya wastani. Kwa hivyo, Habwe anatuonyesha kwamba wachungaji nao wana imani sana katika vitu vya kidunia (paradiso ya hapa duniani) kama ile waliyo nayo watu wengine wowote wa ulimwengu.

Ukwasi wa Mchungaji Michael unadhihirika hata katika maisha ya nyumbani kwake ambako tunaona kwamba gharama za maisha sasa anazimudu. Kuteleza kwake na kuingia katika dhambi kunadhihirika pia katika mabadiliko ya kimwili anayoyapitia mfanyakazi wake wa nyumbani:

> 198. Nyaleso …alikuwa mwembamba. Lakini sasa amekunywa katika kisima cha pale **akajaa kama tembo**. Ukimwangalia ni **kama jitu**.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 196)

Mwandishi anatumia tashbihi mbili mfululizo. Anasema kwamba Nyaleso, mfanyakazi msichana wa Michael '**akajaa kama tembo.**' Maana yake ni kwamba msichana huyo alinenepa sana. Tena mwandishi anasisistiza mabadiliko haya kwa kusema kuwa msichana huyo sasa alikuwa '**kama jitu,**' yaani sasa alikuwa mkubwa sana kimaumbile. Kwa kumlinganisha na vitu viwili ambavyo ni vikubwa kiumbo, mwandishi anasisitiza ujumbe wake kuhusu mabadiliko yanayotokea katika nyumba ya Mchungaji Michael, yaani kunenepa kwa Nyaleso kunaashiria kubadilika na kutajirika kwa Michael – kisitiari. Umbile la Nyaleso linabadilika kwa sababu ya utajiri uliopo katika nyumba ya Mchungaji Michael. Hii inatokana na ubora wa maisha katika nyumba hiyo kwa vile Michael sasa ana pesa nyingi ambazo zinamwezesha kuishi maisha bora.

Habwe pia anamulika tatizo la ufisadi. Maofisa serikalini wanajitajirisha na kutumia mali ya jamii kwa maslahi yao wenyewe. Ukwasi wa Amuko unatokana na wizi wa

rasilimali za serikali. Ana gari la *Range Rover* ambalo hawezi kuhimili gharama ya mafuta yake. Lakini anatumia ofisi yake kupata mafuta hayo kwa njia zisizo halali:

> 199. [Amuko] alikuwa na gari la *Range Rover* **lililomeza mafuta kama zimwi**. Mafuta haya aliyapata kutokana na kashfa mle ofisini.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 47)

Katika dondoo hili, tashbihi iliyosisitizwa inamaanisha kwamba gari la Amuko lilitumia mafuta mengi kupita kiasi. Ili kuweza kuhimili gharama ya mafuta hayo Amuko anatumia ufisadi. Mwandishi anasema, 'Mafuta haya aliyapata kutokana na kashfa mle ofisini.' Kashfa hiyo ni ufisadi. Katika jamii, watu kama Amuko hujaribu kuishi maisha ambayo ni ya kiwango cha juu kuliko kipato chao kwa sababu ya tamaa ya maisha ya starehe. Kwa vile kipato chao hakiwezi kutosheleza tamaa yao ya maisha ya starehe, wanaingia katika ufisadi huku watu wa kawaida wanateseka kwa sababu ya ufukara. Maisha haya ni yale ya pesa nyingi, magari ya kifahari na wanawake. Amuko angeweza kununua gari lisilo la kifahari ambalo angeweza kuhimili gharama zake, lakini kwa sababu ya tamaa ya pesa na kupenda kuishi maisha ya starehe, anatumia ufisadi ili kuishi maisha anayoyatamani au kutosheleza mahitaji yake ya kibinafsi.

Katika riwaya ya *Asali Chungu* mwandishi ametumia tashbihi kusawiri maudhui ya unyonge unaowakabili raia wengi. Semeni, kwa mfano ni mfano wa vijana waathirika kwa sababu ya unyonge. Anampoteza mama yake mzazi akiwa bado mdogo sana. Kutokana na kukosa mtu wa kumtunza, Semeni anapepesuliwa na nguvu za maisha ambazo anashindwa kukabiliana nazo katika umri wake mdogo.

> 200. Kuunguako ndiko kuteketeako. Hana mtu wa kumwendesha sasa ameshavunja ungo; akawa anatangatanga na ulimwengu – leo kwa huyu, kesho kwa yule. **Akarushwa kama mpira**, naye akafuata. Hakuwa na hila ya kujiokoa; mtoto mdogo mwanamwali akaelekea mjini.
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 46)

Semeni anatangatanga tu. 'Kurushwa kama mpira' haina maana kwamba watu hao wanamchezea tu ila hakuna aliye tayari kuchukua jukumu la kumtunza msichana huyu. Lakini mpira ni kitu cha kuchezea; kwa hivyo, Semeni kurushwa kama mpira ni kuchukuliwa kama kitu kisicho cha muhimu, ingawa wanaorushiana 'mpira' huo hawafanyi hivyo kimaksudi. Semeni anazaliwa katika unyonge. Naye pia anamkabidhi mtoto wake Dude unyonge huo. Kwa njia hiyo, ni kama kwamba mama mnyonge anamrithisha mtoto wake unyonge.

Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* tunamwona mhusika Kijakazi, msichana ambaye amezaliwa katika unyonge wa utumwa. Anafanyishwa kazi nyingi wakati akiwatumikia mabwana shamba. Baada ya kifo cha Malik Kijakazi ana hiari ya kufanya kazi kwa kujipimia. Lakini kwa vile amezaliwa katika utumwa, anaamini kwamba hayo ndiyo majaliwa yake, yaani kuwatumikia mabwana shamba. Anaamua kwamba furaha yake itatokana na kuwafurahisha mabwana zake – kwanzia kwa bwana Malik na baadaye mtoto wao Fuad. Mwandishi anaonyesha kutokubaliana na jinsi Kijakazi anavyofanya kazi kitumwa.

> 201. Kwa Kijakazi, mwendo wa kufanya kazi kwa Fuad ulikuwa ni ule ule. Alifanya kazi kama wakati wa uhai wa marehemu Bwana Malik… **akifanya kazi kama mashine.** Akili yake yote ilikuwa iko katika kufikiria kazi… **Alifanya kazi kama punda** na hapana binadamu aliyeweza **kufanya kazi mfano wa mwanamke huyo.**
>
> (Shafi, 1978, Ukur. 9)

Katika aya ile ile, mwandishi ametumia tashbihi zenye maana ya kiusawe ambazo zinaonyesha jinsi Kijakazi anavyofanya kazi kupita kiasi. Katika tashbihi ya kwanza mwandishi anamlinganisha Kijakazi na mashine; katika tashbihi inayofuata Kijakazi analinganishwa na punda. Sifa inayohusika katika ulinganishaji huu ni ile ya kufanya kazi nyingi bila kuchoka. Katika tashbihi ya tatu mwandishi anasema kuwa hakuna binadamu wa kumlinganisha naye Kijakazi katika kufanya kazi. Ni sawa na kusema

kuwa alifanya kazi kama mnyama. Kijakazi kufanya kazi namna hiyo inatokana na yeye kutojua kwamba naye ana mamlaka fulani kuhusu maisha yake; sio mnyonge sana kiasi ambacho anajidunisha. Mfumo wa utumwa umeisha.

Ili kuonyesha kwamba Kijakazi ndiye anayejiweka katika hali ya kunyonywa na mabwana shamba, tunamlinganisha na watumishi wengine ambao wanakataa kunyonywa, bila mabwana shamba kuwafanya chochote. Mkongwe na Mariam ni watumishi kwenye kasri ya Fuad ambao wameamua kufanya kazi kwa kujipimia, sio kama Kijakazi. Kwa mfano, tofauti na Kijakazi, Mariam hafanyi kazi kupita kiasi.

> 202. Si kama Mariam alikuwa mkaidi hapo kazini. Alikuwa anajitahidi kufanya kazi zake kama anavyoweza lakini alikuwa hakubali **kutumwa kama punda.** (Shafi, 1978, Ukur. 12)

> 203. “Hapana kosa lolote kufanya kazi yako vizuri. Sidhani kama kuna mtu atakayekufukuza hapa na pia sioni sababu kwa nini **ufanye kazi yako kama mnyama,**” Mkongwe alimwambia Kijakazi.
> Siku nyingi Mkongwe alifanya kazi pamoja na Kijakazi na hakuacha kusema naye ili **afanye kazi kibinadamu…** (Shafi, 1978, Ukur. 18)

Ingawa watumishi wengine kama Mariam na Mkongwe wanatambua mapema kwamba Fuad ni mnyonyaji tu, inachukua muda Kijakazi kutambua ukweli huu. Mariam na Mkongwe wanaona kwamba kuna hiari ya kutotumikishwa kama wanyama. Wanamshauri Kijakazi lakini hawasilikizi, kwa vile ukweli bado haujamdhihirikia.

Katika riwaya ya *Asali Chungu* mwandishi ametumia tashbihi kuchora maudhui ya unyonyaji vilevile. Tajiri Amina anatumia uwezo wake wa kifedha kuwaajiri vijana na kuwatumia kujistarehesha. Wanaposhindwa kufuata masharti yake anawafukuza moja kwa moja. Baada ya kufukuzwa, vijana hao wanapoteza manufaa yote waliyokuwa

wameyapata kutoka kwa Amina. Dude anaposhindwa kufuata maagizo aliyopewa na Amina ya kutomwonyesha mwanamke mwingine mapenzi, Amina anamwacha mara moja.

> 204. Alimwepuka [Dude] makusudi; hakupenda kumwangalia. Dude sasa ni kiraha; kinyaa… Moyo wake ulikuwa umeshaamua, kama ulivyowahi kuamua mara nyingi katika maisha yake… **Atamtema Dude kama mate**; na katu hatorudi kumramba. Na yeye Dude hajui kiasi gani alichojivunjia.
>
> (Mohamed, 1977, Kur. 128 – 129)

Tashbihi '**atamtema kama mate**' inaashiria uamuzi wa Amina usiobadilika. Mate yakishatemwa hayarudishwi kinywani. Dude analinganishwa na mate sasa baada ya kutemwa. Amina ana pesa zake na ni rahisi sana kumnasa kijana mwingine wa kumtoshelezea mahitaji yake. Sasa ni zamu ya Dude kuachwa. Kauli kwamba: 'Na yeye Dude hajui kiasi gani alichojivunjia' inamaanisha kuwa Dude sasa amepoteza manufaa yote aliyokuwa akipata katika uhusiano wake na Amina, yaani pesa, nyumba, gari, mavazi, na kadhalika. Inabidi aurudie udude wake.

Suala la unyonge limeangaziwa pia katika riwaya ya *Nguvu ya Sala*. Katika Sura ya ishirini na nane (sura ya mwisho ya riwaya) Susan anatafakari tena mwito wa baba yake wa **nguvu ya sala**. Anajiuliza maswali kadha kuhusu ufaafu wa mwito huo.

> 205. Nilimwangalia baba tena na kuuwazia mwito wake wa ***nguvu ya sala*** ambao aliukazania kwa muda mrefu. *Je, ulikuwa wa kufaa au ulikuwa tasa? Je, matatizo mangapi ambayo yangesuluhishwa kwa mwito huo?* ***Umaskini uliowavaa watu nchini kama lubega****, tofauti zilizokuwapo kati ya matajiri na maskini, udhalilishaji wa wanawake katika jamii yetu.*
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 199)

Tashbihi '**umaskini uliowavaa watu nchini kama lubega**' inaashiria umaskini uliozidi sana. Inaonekana kwamba kuna mwambatano kati ya umaskini na watu, ambao sio rahisi kuuvunja. Hili ni suala mojawapo analojaribu kuliangazia Wamitila katika

riwaya yake. Ni dhahiri kwamba Susan anaona kwamba mwito wa **nguvu ya sala** umepungukiwa sana na haufai katika kukabiliana na matatizo kama yale ambayo yametajwa katika dondoo 206, yaani umaskini, tofauti kati ya watu maskini na matajiri, udhalilishaji wa wanawake, na mengineyo. Swali lake la mwisho: '**Nguvu ya Sala**?' linaashiria kutoridhika kwake na mkabala huo wa kidini ambao baba yake anashikilia.

Akitumia tashbihi, Wamitila pia anagusia suala la athari za malezi mabaya kwa watoto. Kwa sababu ya misingi yake mikali ya kidini, Richard ni mkali kupita kiasi kwa wanafamilia wake. Anawapiga watoto kwa sababu ndogo ndogo tu kwa vile anaona kwamba wamevunja kanuni za kikristo, na wanamharibia jina kama Mkristo kielelezo katika jamii. Hata hivyo, ukali wake ni wa bure kwa vile binti yake Joselyn anashika mimba akiwa bado anasoma. Mkabala huo wa ukali inaonekana haufanikiwi kumwogofya Roselyn kutoshika mimba.

> 206. Roselyn alilia kwa sauti kutokana na maumivu ya bakora ya babake ambayo **aliachilia kama mtu anayemcharaza punda kihongwe**.
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 193)

Richard kumpiga binti yake Roselyn 'kama mtu anayemcharaza punda kihongwe' ni tashbihi inayodhihirisha jinsi baba huyu anavyokosa huruma kabisa kwa binti yake. Kwa kutumia tashbihi hiyo, mwandishi anaonyesha kwamba hakubaliani na kipigo cha kiasi hicho kwa kosa la binti huyo kushika mimba. Kuna kinaya katika tabia ya Richard kwa vile ukali wake ndio umechangia kisa hiki cha binti yake kushika mimba. Kwa hiyo, Richard anampiga bintiye kwa kosa ambalo yeye mwenyewe amechangia kufanyika kwake. Anafaa kujilaumu kwanza kwa kusisitiza mno mafundisho ya kidini badala ya kumfundisha binti yake hali halisi ya dunia ili aiepuke hali kama hiyo.

Mwandishi wa riwaya ya *Nguvu ya Sala* anaonyesha jinsi ambavyo ujasiri wa mwanamke unavyoweza kuzaa matunda katika mahusiano yake na mwanamume. Mwanamke anahimizwa kuwa shupavu.

> 207. Baba alinitazama kisha akashusha pumzi ndefu. Alirudi na kuketi kwenye kochi alilokalia mwanzo na **akanywea kizembe kochini kama kifaurongo** kilichoguswa.
> (Wamitila, 1999, Ukur. 198)

Mwandishi ametumia tashbihi '**akanywea kizembe kama kifaurongo**' kudhihirisha kwamba baba huyo alipoa kabisa. Susan anajikakamua na kupambana na baba yake kuhusu suala la malezi. Anamlaumu baba yake kumfukuza Roselyn nyumbani baada ya binti huyo kushika mimba akiwa bado masomoni. Ingawa baba yake anafoka na kurindima, Susan anabaki imara akitoa hoja zake. Mwishowe, baba yake anapoa na inaonekana kwamba anatambua ukweli ambao binti yake anampasulia. Anatambua kwamba mara hii hasira yake haitafua dafu. Hata Susan anaitambua hasira ya baba yake kama ni udhaifu, sio ushupavu. Matumizi ya maneno '**akanywea kizembe**' ni hasi. Kwa mujibu wa Kamusi Kiswahili ya Sanifu (2014), 'kunywea' ni kujikunyata kwa hofu au wasiwasi. Tena baba sasa analinganishwa na kifaurongo. Maana yake ni kwamba hasira na kufoka kwake ni bure tu; kama kwamba ni bandia. Huu ni mfano mwingine wa dhamira ya mwandishi wa riwaya hii ya kumdunisha mhusika mwanamume ili kumwimarisha mhusika wa kike. Tashbihi hii inamdhihaki Richard kama mhusika mwanamume, ambaye amewatia hofu mabinti zake na mama yake kwa kipindi kirefu.

Ingawa mwandishi wa riwaya ya *Nguvu ya Sala* amemwimarisha mhusika Susan kuwakilisha wanawake wenye mwamko, kuna wahusika wengine wa kike ambao wametumiwa kwa njia ya kuwalinganua na mhusika huyu (Susan). Ni wahusika ambao hawana mwamko, ambao wanaendeleza imani kwamba nafasi ya mwanamke iko katika

ndoa. Wahusika wa aina hii ni Bathsheba na Rose Mafali. Hawa wanaolewa mara tu baada ya kidato cha nne wakiamini kwamba mwanamke hana haja ya kusoma ikiwa angeishia kuwa mtunzaji wa nyumba tu. Msimamo wa Susan ni tofauti na wa wasichana wenzake.

> 208. Bethsheba alikuwa nambari ishirini na mbili. Yeye hakujali sana. Hakuona sababu ya kuyaendeleza [masomo]; miaka hiyo ilimtosha. Alidai kuwa waliotakiwa kusoma ni wanaume wala sio wanawake ambao wangeishia kuwa watunzaji wa nyumba tu. Mimi sikuamini hivyo asilani. Hayo yalikuwa mawazo yaliyopitwa na wakati na kwa kiasi kikubwa niliamini kuwa huko kutosoma kwa wanawake ndiko kulikochangia katika kuwafanya wabakie palepale; **kuzungukia palapale kama pia**.
>
> (Wamitila, 1999, Kur. 119 - 120)

Susan anaona kwamba wanawake kama Bathsheba wanajitweza na kutosoma kwao kunachangia hali ya kuwafanya wadharauliwe au wasithaminiwe na '**kuzungukia palepale kama pia.**' Wanawake kama hawa hawana mamlaka yoyote. Lakini wanafaa kuchangia ukombozi wao kwa kujiendeleza kimasomo.

Mawazo ya wanafunzi wa kike kama Bathsheba, rafikiye Susan katika *Nguvu ya Sala*, yanalingana na mawazo ya Lydia na Patricia katika riwaya ya *Paradiso*, ambao nao wanaonyesha kukubali hali kwamba mwanamke ni kiumbe duni ukimlinganisha na mwanamume, wakidai kwamba hata Mungu alipanga hivyo (dondoo 62).

Maudhui ya wivu, chuki, migogoro na ufarakano ndani na kati ya makanisa ya kiprotestanti yameibuliwa katika riwaya ya *Paradiso* kwa njia ya tashbihi pia. Wahubiri wanaoneana wivu na kwa hiyo wanashindwa kushirikiana. Kama tulivyoona katika Dondoo la 92 kwa mfano, kuna utengano kati ya Askofu Joshua na Mchungaji Michael kwa sababu Joshua anamwonea wivu Michael. Anaona kwamba Michael amepata waumini wengi wanaomwamini.

209. Jambo hili wakati mwingine lilimletea Joshua wivu mpaka **akavimba shingoni kama pili** anayemeza mbuzi.
(Habwe, 2005, Ukur. 55)

210. Kila uchao uhusiano baina ya Michael na Joshua uliendelea kutumbukia nyongo. Ni **kama majogoo mawili yaliyokaa katika kizimba kimoja**. Kila mmoja katika majogoo hao alitaka utawala.
(Habwe, 2005, Ukur.76)

Katika dondoo la 209, mwandishi ametumia tashbihi **"akavimba shingoni kama pili"** kuonyesha kiasi cha wivu aliokuwa nao Askofu Joshua. Taswira ya pili anayemeza mbuzi inaonyesha vizuri kiasi cha wivu alio nao Joshua. Wivu ni hisia ambayo Mkristo hafai kuwa nayo. Mtu ambaye ni kiongozi wa kidini kama alivyo Askofu Joshua hatarajiwi kuonyesha wivu wa kiwango hiki. Mfano huu wa Askofu Joshua kuwa mwivu unatumiwa na mwandishi kuonyesha jinsi ambavyo viongozi wa kidini wameshindwa kuwa mfano kwa waumini wengine na tena kwa jamii kwa jumla. Lakini, kinyume na Joshua, Mchungaji Michael hana wivu kwa Joshua. Michael ametumiwa na mwandishi ambaye anamlinganua na Askofu Joshua ili kuichimuza tabia ya askofu huyo isiyo ya kikristo.

Ili kusisitiza jinsi hali ilivyo kati ya wachungaji walioshindania uongozi, mwandishi anawalinganishwa Michael na Joshua na **majogoo** wawili ambao hawawezi kukaa kizimba kimoja, kwa vile kila mmoja anataka kuwa ndiye kiongozi au mwenye mamlaka katika kanisa la New Jerusalem (dondoo la 210). Tunajua kwamba chanzo cha ushindani huu ni pesa zinazotokana na zaka inayotolewa kanisani. Taswira ya majogoo inahusisha dhana ya uongozi, ambapo Askofu Joshua anataka kuwa ndiye kiongozi anayedhibiti masuala yote katika kanisa la New Jerusalem.

Mwandishi wa riwaya ya *Paradiso* anasawiri maudhui ya mui kuwa mwema tena. Michael anapobadilika na kurudi kwenye njia ya wokovu, anakuwa ni kielelezo cha mchungaji mwema.

> 211. Yeye Michael alijaribu **kusimama wima kama mti uliomea karibu na mto**.
>
> Michael naye amesimama kidete sasa **kama mbuyu**. Amekataa kupepesuliwa na upepo wa raha za dunia.
> (Habwe, 2005, Ukur. 225)

Tamathali zilizotumika katika dondoo la 211 zinamwonyesha mhusika Michael ambaye sasa, baada ya kuingia katika dhambi ya mapenzi nje ya ndoa na Patricia, amebadilika tena na kuwa mhusika mwema. Mwandishi anaonyesha kuwa mtu anaweza akabadili mwenendo wake, hata baada ya kuingia katika dhambi. Michael anabadilika na kuwa kielelezo bora zaidi hata kuliko awali, yaani kabla hajaingia katika dhambi.

Mchungaji bora anafaa kusimama wima katika imani. Katika sifa hii, Michael amelinganishwa na mti uliomea karibu na mto, ambao inaonekana unakuwa wima kwa sababu ya kupata maji ya kutosha. Michael pia amelinganishwa na mti wa mbuyu. Hii ni sifa ya uimara. Mbuyu ni mti wenye shina kubwa sana, na kwa hiyo haupepesuliwi na upepo. Hivyo, mchungaji ambaye atakuwa kielelezo anafaa kusimama imara ili asiyumbishwe na dhambi au raha za dunia.

Zaidi ya Michael kuchorwa kama mchungaji kielelezo, kanisa lake la Bethany pia limechorwa kama kanisa kielelezo. Hii ni kutokana na juhudi za Michael mwenyewe. Amejitahidi kuhakikisha kwamba kanisa lake ni tofauti sana na makanisa mengine kama vile New Jerusalem. Kwa mfano, hajihusishi na kashfa kama vile ulanguzi wa madawa ambao unafanywa na akina Askofu Joshua na mchungaji Boribori.

> 212. Bethany ilikuwa **kama nyota** iliyong’ara katika usiku wa giza totoro pale Kibera.

(Habwe, 2005, Ukur. 112)

213. Bethany lakini kilikuwa **mfano wa kilima cha Zayuni** ambapo mtu angeweza kutafuta toba na suluhu ya kweli kwa Bwana.

(Habwe, 2005, Ukur.113)

Mwandishi anatumia tashbihi kulielezea kanisa la Bethany kama kielelezo bora kwa makanisa mengine. Bethany imelinganishwa na nyota na pia kilima cha Zayuni. Picha hii ni tofauti sana na ile ya kanisa la New Jerusalem. Mwandishi anaposema kwamba Bethany ilikuwa nyota iliyong'ara katika usiku wa giza totoro pale Kibera anamaanisha kwamba hakukuwa na kanisa jingine lenye sifa kama za kanisa la Bethany. Makanisa hayo yamefanywa kuonekana kama ni sehemu ya giza; hayatoi mwanga kwa waumini. Tena tunaona ushirikiano mkubwa sana kati ya waumini wa kanisa la Bethany. Hii ndiyo maana hasa ya kanisa, kwani kanisa si majengo tu, bali ni waumini wake. Kila sifa inayotolewa kulielezea kanisa la Bethany inaashiria picha kinyume katika makanisa mengine. Kwa hiyo tunaona kwamba, kwa mfano, tofauti na picha ilivyokuwa katika kanisa la Bethany, hakuna hali ya waumini kuingiliana kama ndugu katika makanisa mengine.

6.1.3 Tashihisi

Wamitila anaielezea tashhisi kama tamathali ya usemi ambapo vitu visivyokuwa hai au na uhai huwasilishwa au kusawiriwa kwa namna ilivyo sawa na binadamu ya kuweza kufikiri na kuhisi. Aghalabu pia hurejelea sifa ya kuwapa wanyama sifa za kibinadamu. Naye Mbatiah (2001) anasema kuwa mbali na kuvihusisha vitu vya kimaumbile kama miti, milima, mito, n.k. tamathali tashihisi pia inatumiwa kuvipa uthabiti vitu dhahania kwa kuvipa sifa za kibinadamu. Anatoa mfano ambapo kifo kinaelezwa kama "mwizi wa uhai." Anafafanua kwamba kitu kinapopewa uthabiti kwa njia hii huwa kinaeleweka vizuri zaidi.

Mwandishi wa riwaya ya *Asali Chungu* anatumia tashihisi kusawiria maudhui ya udhalimu wa mwenye utajiri na mamlaka dhidi ya mnyonge. Wakati Zuberi akinyata kuelekea kwenye chumba cha Semeni, tunaona jinsi ambavyo mwandishi anatumia uhuishaji kuelezea mazingira ya ukumbi wa jumba lake:

214. Alikunja pazia la mlango, akapapasa ukuta wake na kuwasha swichi. **Taa zake za therea… zilimwitikia** pamoja, zikamwaya anga la kupendeza…

Madirisha yake yenye virukia vya vioo **yalikuwa yanatazamana huku na huku**. Mapazia ya kitambaa… **yalikuwa yakichezacheza kwa furaha** … Kutani baina ya madirisha, palikuwa pamepachikwa vichwa vya nyemela… Vimekabiliana… **vikamshuhudia** Zuberi aliyekuwa akikata ukumbi wake kwelekea bewani.

(Mohamed, 1977, Ukur. 7)

215. Ngazi aliiteremka salama pasi na vishindo. **Hapana aliyemsikia wala kumwona, ila milango** ambayo sasa alikuwa akiifungua na kuifunga.

(Mohamed, 1977, Ukur.9)

Tashihisi ya taa kumwitikia Zuberi inaakisi uwezo wake wa kiuchumi. Huyu ni mtu tajiri sana na kwa hivyo baada ya kuwasha swichi, taa haziwaki tu bali zinamwitikia kama kwamba zinaitikia amri yake. Ni kama kwamba hata taa zinamtii. Madirisha yanapewa hisia ya kutazama. Yanatazamana kana kwamba kuna kitu ambacho yanaambiana kuhusu mhusika anayepita ambaye tunamwona akielekea kufanya tendo la ukatili. Vichwa vya nyemela vinamshuhudia Zuberi akikata ukumbi wake. Kinachoashiriwa hapa ni kwamba, ingawa anatoka chumbani na kupita ukumbini kisirisiri, vichwa vya nyemela vimemshuhudia akielekea kutenda kitendo cha kikatili. Ni kama kwamba Zuberi amejificha lakini hajafanikiwa kabisa kwani ameshuhudiwa. Mwandishi anataka msomaji mwenyewe amshuhudie mhusika huyo – kitaswira – na tendo analodhamiria kufanya. Vichwa vya nyemela vina macho ingawa hayaoni. Hata hivyo, msomaji anapata taswira akilini kuhusu Zuberi kushuhudiwa. Mwandishi analenga kumfanya msomaji awe makini kushuhudia vitendo vya Zuberi.

Nayo milango anayoifungua na kuifunga Zuberi inamsikia na kumwona. Vitu hivi kumshuhudia na kumsikia inampa msomaji kuhisi kwamba mhusika huyu anaelekea kufanya kitu kisichokubalika, ingawa hakuna anayemwona. Vitenzi vya mwishoni mwa dondoo la 215 ni vya hisia za kuona na kusikia, ikimaanisha kuwa ni kama kwamba kuna mtu ambaye amemwona na kumsikia Zuberi.

Pengo la kiuchumi kati ya matajiri na maskini linabainika tunapochunguza makazi ya Zuberi na makazi ya raia wa kawaida kama vile wakazi wa sehemu ya Ng'ambo. Zuberi ana jumba la kifahari lililozungukwa na kuta ndefu. Kama tajiri na pia mfanykazi wa serikali wa ngazi ya juu, ni lazima ajihami kiusalama kwa kulizungushia jumba lake kuta ndefu.

> 216. Jumba hili lilikuwa lile lile. Kuta zake zilizokwenda juu ghorofa moja zilikuwa daima **zikiwakejeli** makafiri na wachochole. Waomba pesa wapitapo, husimama na kuinua nyuso zao kuangalia juu;
>
> (Mohamed, 1977, Ukur.120)

Kwa kusema kwamba kuta za jengo hili zilikuwa zikiwakejeli makafiri na wachochole, mwandishi anaonyesha uwezo mkubwa wa mwenye jumba hili. Makafiri na wachochole wanahisi hofu wanapoziangalia kuta hizo. Ni kama kwamba zinawajulisha kuwa hawawezi kufanya chochote dhidi ya yule anayelindwa ndani ya kuta hizo. Ni kama kwamba zinaucheka unyonge wao. Kuta hizo pia ni ishara ya mpaka kati ya walio ndani ya kuta hizo ambao ni wenye uwezo na mamlaka, na wale walio nje, ambao ni wanyonge wasio na mamlaka. Zimevitenga kisitiari vikundi hivyo vya watu.

Kinyume na jumba la Zuberi, makazi ya watu wa maeneo mbalimbali ya nchi kama vile sehemu ya Ng'ambo ni duni sana. Tunaelezwa kuwa majumba ya watu wa Ng'ambo "yalikuwa yamekaliana ovyo, matonge kwa matone" (dondoo la 163). Tena taswira tunayoipata akilini kuhusu makazi ya watu wa Ng'ambo ni tofauti na picha kuhusu jumba la Zuberi linalozungukwa na ukuta mrefu pamoja na bustani kubwa.

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, mwandishi anaitumia tashihisi nyingine kudhihirisha maudhui ya ufukara uliomo nchini. Tashihisi hii ni ile ya bidhaa kuwacheka watu wanyonge wasio na uwezo wa kuvinunua. Unyonge huu unadhihirika kwa mujibu wa yale anayoyashuhudia Dude, wakati akipita kwenye sehemu za mafukara akielekea kwa matajiri Zuberi na Amina:

> 217. Mbali zile mboga na matunda ya viungo vya mchuzi; vyote vilikuwa **vikichekelea furaha na kuwaita wanunuzi** kujinunulia walichopenda. Kulikuwa na kila kitu sokoni kwa mwenye pesa zake, lakini kwa Dude palikuwa patupu.
> (Mohamed, 1977, Ukur. 78)

Mwandishi anasawiri hali ya unyonge wa kifedha ambapo bidhaa zipo lakini uwezo wa watu kuzinunua haupo. Kwa hivyo, mwandishi anasawiri kinaya hicho. Ndiyo maana mwandishi anatoa maelezo marefu ya orodha ya vitu vilivyomo kwenye marikiti, lakini kwa watu wanyonge kiuchumi kama Dude, sokoni ni patupu. Tashihisi iliyotumika ya bidhaa kuwacheka wanyonge wasio na pesa inajenga tashititi ambapo inaonekana kwamba mwandishi anaicheka hali hii. Tashititi iliyotumiwa na mwandishi inadhihirisha na kusisitiza hali ya unyonge wa kifedha waliyo nayo watu wengi, ukiilinganisha na hali ya watu wenye uwezo mkubwa wa kifedha kama Amina na Zuberi.

Uwezo wa kiuchumi wa matajiri kama Amina umeelezwa kitashihisi. Amina anamiliki gari la kifahari aina ya *Vauxhall*, sawa na la mume wake Zuberi. Sawa na mume wake, Amina ana ardhi na nyumba yake mwenyewe. Ana uwezo wa kiuchumi wa kujipatia kila anachokitaka, mkiwemo kujinunulia vijana kama Bushiri na Dude kuja kwake kumstarehesha kingono. Maelezo yametolewa kuusisitiza ufahari wa gari la Amina.

> 218. Nguzo za umeme na simu zilikumbwa nyuma pale *Vauxhall* ya kijani **ilipokuwa ikitafuna masafa** yaliyobaki kabla ya kufika Maungani… Ikakata upepo huku **upepo ukinguruma** kwenye vioo vyake.
> (Mohamed, 1977, Ukur. 89)

Katika maelezo ya dondoo 218, gari limepewa sifa ya kiumbe hai ya kuweza kutafuna kitu. Msomaji anaweza akapata taswira ya gari hili wakati likielekea kwa Zuberi. Picha yenyewe inasisitizwa na maelezo kwamba nguzo za umeme na simu zilikuwa 'zikikumbwa nyuma.' Pia, upepo unanguruma kama kwamba ni kiumbe hai. Gari ndilo limepewa kipaumbele hapa. Uwezo wa gari umesisitizwa na aina ya gari pia kutajwa ili kumpa msomaji picha ya wenye nacho ambao ndio wamiliki wa gari hili. Pia msisitizo wa mwendo wa gari unakusudiwa kuleta taharuki fulani kwa msomaji ambaye atataka kuona gari likifika na yapi yanayomsubiri Dude kwa matajiri.

Mbali na gari, mwandishi anaelezea ardhi wanayoimiliki Amina na mume wake Zuberi, ambayo ukubwa wake unaonyesha ukwasi wa makabaila hawa.

> 219. 'Hili shamba lote ni la Bwana Zuberi. Huku halina mwisho, na huku mpaka bondeni. Halafu linapanda kilima; halafu linateremka, ndio linapakana na Bi Amina. Na **hilo lake linamwambia la Bwana Zuberi sogea huko**,' Bushiri alisema akiashiria.
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 92)

Bwana Zuberi na mke wake ni watu 'wenye chao.' Mbali na kila mmojawao kumiliki gari la *Vauxhall*, bibi na bwana pia wana mashamba makubwa – mke lake na mume lake. Bushiri analielezea shamba la Zuberi: 'Huku halina mwisho, na huku mpaka bondeni… linapanda kilima … linashuka ndio **linapakana na Bi Amina**.**'** Mwandishi hasemi kwamba shamba la Zuberi 'linapakana na *la* Bi Amina,' bali anasema: 'linapakana na Bi Amina.' Huu ni uchimuzi unaomsisitiza mmiliki wa shamba lile jingine, yaani Bi. Amina. Pia, kwenye uhuishaji huu wa shamba mwandishi anaeleza: Na '**hilo lake [la Amina] linamwambia la Bwana Zuberi sogea huko.**' Tunapata uhuishaji mara mbili. Kwanza kabisa, mashamba haya yanahuishwa kwa kupewa uwezo wa kuzungumza pamoja. Tena badala ya mwandishi kusema: 'Na **hilo lake lina*li*ambia la Bwana Zuberi sogea huko**,' anatumia kiambishi *mw-* ambacho pia

kinaonyesha uhuishaji wa shamba kikamilifu ikawa sasa shamba linazungumza na binadamu. Maelezo haya yote ambapo mashamba ya bwana na bibi yamehuishwa yanalenga kuonyesha tofauti iliyopo kati ya wenye ardhi kubwa hawa na wanyonge wasio na ardhi. Mabwana shamba wana mashamba 'yasiyo na mwisho' wakati ambapo raia wengi hawana hata pa kuchomeka ubeu wa muhogo (Mohamed, 1977, Ukur. 20). Inambidi msomaji ajaribu kuhisi na kutambua maana ya uhuishaji uliotumika kwa kukifikiria kile ambacho kimechimuzwa, yaani makabaila kumiliki ardhi kubwa, huku wanyonge hawana ardhi.

Sawa na mashamba ya Amina na Zuberi, nyumba ya Amina nayo imeelezwa kwa njia ya uhuishaji. Amina ni mtu ambaye tunaona anaishi maisha kivyake. Ana gari, shamba, na nyumba yake mwenyewe kwa ajili ya starehe zake.

> 220. Nyumba ya Bi Amina imejengwa karibu na ufukwe nyuma ya kisiwa cha Weba; **imejitenga kutafuta faragha**, mbali na vijumba vya kijiji chenyewe… Kwa pale kisiwani, hiyo ilikuwa nyumba pekee iliyovutia. Kwa ukubwa labda inashindana na ule msikiti; lakini kwa uzuri hapana nyengine iliyoweza **kuivua kilemba.**
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 116)

Ingawa Amina anaishi na mume wake Zuberi, ana uhuru wa kumiliki mali yake mwenyewe. Hatuambiwi ikiwa mali hii aliipata kutoka kwa mumewe Zuberi au kama alijinunulia mwenyewe. Pia hatuambiwi kwa nini ana shamba lake mwenyewe. Lakini, tunaelezwa pia kuwa Amina alikuwa ni 'mtoto wa watu' yaani naye pia anatoka katika familia tajiri. Nyumba ya Bi Amina iko katika kijiji cha Weba ambapo yeye huenda mara kwa mara kupunga hewa. Nyumba yenyewe '**imejitenga kutafuta faragha**' mbali na vijumba vya kijiji. Tashihisi ya nyumba ya Amina kujitenga kutafuta faragha inaashiria hadhi ya Amina kujitenga kisitiari na hadhi ya wakazi wa sehemu hiyo. Mwandishi amezidunisha nyumba za wakazi wa sehemu hiyo kwa kuziita 'vijumba'

kutokana na jinsi nyumba za watu hawa maskini zinavyolinganuliwa na nyumba ya kifahari ya Bi. Amina.

Nyumba yake Amina ni ya kipekee na ya kifahari kiasi kwamba kwa ukubwa inashindana na msikiti peke yake. Mwandishi anailinganisha nyumba ya Amina – mtu binafsi – na nyumba ya Mungu (msikiti). Ulinganishaji huu unalenga kumshawishi msomaji azingatie hali hiyo ya nyumba ya mtu binafsi kushindana na msikiti wa umma. Pia msomaji anaweza akazingatia mmiliki wa nyumba hiyo mwenyewe kama mtu anayejikweza kuliko Mungu. Utukufu wa nyumba hii umeelezwa kwa njia ya uhuishaji: "kwa uzuri hapana nyengine iliyoweza **kuivua kilemba**." Nyumba ya Amina inapendeza sana kiasi cha kulinganishwa na mtu aliyevaa kilemba, yaani nyumba imepewa uwezo wa kuvaa kilemba kama binadamu.

Katika riwaya ya *Nguvu ya Sala*, mwandishi anatumia tashihisi kusawiri maudhui ya uhalifu unaotokana na ugumu wa maisha jijini Nairobi, kama tunavyoona katika dondoo lifuatalo.

> 221. [Richard] alishangaa. *Mbona binadamu wametovukwa na huruma kiasi hiki?…* Labda **maisha ya mjini yaliwanyang'anya binadamu chembe za huruma** zilizobakia, wameshapokwa hisia zote za kibinadamu…
> (Wamitila, 1999, Ukur. 117)

Tashihisi iliyotumiwa na mwandishi katika dondoo la 221 ni kwamba '**maisha ya mjini yaliwanyang'anya binadamu chembe za huruma**'. Hii ni tashihisi kwa sababu kitendo cha kunyang'anya kinatarajiwa kutendwa na binadamuu au kiumbe hai. Neno '**yaliwanyang'anya'** linaashiria kwamba kuna nguvu fulani ya kimaisha ambayo inapelekea watu hawa kukosa utu, kwa vile wananyang'anywa; hawapotezi tu. Hii inawafanya kuwa 'watendwa' wala sio 'watendaji.'

6.1.4 Kinaya

Kulingana na Mbatiah (2001), kinaya ni usemi wenye maana iliyo kinyume na kile unachosema. Aghalabu kinaya hutumiwa kutilia mkazo ujumbe fulani. Kinaya pia pia huangazia utata wa maisha kwa kubainisha mwanya uliopo baina ya jinsi mambo yanavyoonekana na jinsi yalivyo hasa. Wamitila (2003) anatumia istilahi 'kejeli', ingawa anaonyesha pia kwamba mbinu hii inaweza kuitwa 'kinaya.' Anaeleza kwamba tunaweza kuitambua kejeli katika hali ambapo kuna kinyume fulani katika usemi, hali au tukio.

Wamitila (2003) anaeleza aina mbalimbali za kejeli, mkiwemo kejeli ya hali, kejeli ya kibalagha, kejeli ya kidrama, kejeli ya kijaala, na kejeli ya kiusemi. Katika sehemu hii tunahusika na kejeli ya kiusemi. Kulingana na Wamitila, kejeli ya kiusemi hujitokeza pale ambapo msemaji fulani atasema maneno fulani akiwa na dhamira nyingine.

Wamitila (2003) anaelezea dhana nyingine husika ya **dhihaka**. Anasema kwamba dhihaka ni aina ya kejeli ambayo inadhamiriwa kuigusa hisia ya mtu kwa njia ya waziwazi na aghalabu kwa nia ya kufichua ubaya fulani au udhaifu alio nao mhusika fulani. Anasisitiza kuwa kimsingi, katika dhihaka maneno yanayotamkwa hukusudiwa kuchochea hisia za ndani za anayeambiwa na hupaniwa, labda hata kumkasirisha.

Katika riwaya teule za Kiswahili zilizotumika katika utafiti huu, mbinu za kinaya na kejeli zimetumika kwa ajili ya kuibua maudhui mbalimbali kuhusu dini na mamlaka:

Maudhui ya tamaa ya pesa na chakula miongoni mwa Wakristo yameibuliwa na mwandishi wa riwaya ya *Paradiso*. Tamaa ya pesa na kula vimeingia katika makanisa kiasi kwamba hata wafiwa wanatakiwa kutoa pesa. Apondi, mama yake Mchungaji Michael, (na mkewe Mango) anapofariki, watu wa kanisa la Budalangi wanadai pesa za kushughulikia matanga pamoja na ng'ombe wa kuwachinjia watumishi wa Bwana.

Mango, babake Mchungaji Michael, anaona kwamba sababu ya watu kuja kwenye matanga ni kula:

> 222. Mali ilikuwa imepotea pia katika kulisha jamaa na **watumishi wa Bwana.**
> (Habwe, 2005, Ukur. 95)

Waombolezaji wanafanya mambo kinyume ambapo badala ya kuwafariji wafiwa, wao wanaomba pesa na chakula kutoka kwa wafiwa. Naye Michael anaona kwamba watu wa Budalangi wanatumia kisababu cha kujipatia pesa" (Habwe, 2005, Ukur. 95). Mango anawaita Wakristo hao wanaodai pesa na chakula "**watumishi wa Bwana."** Kuna kinaya katika maneno ya Mango kwa vile kitendo cha Wakristo hawa waombolezaji kuomba pesa na chakula ni kinyume na mafundisho ya Kikristo yanayosisitiza huruma kwa mtu aliye katika shida kama ile ya kufiwa. Tamaa ya pesa na chakula ni kinyume cha maadili ya kikristo yanayosisitiza kiasi au wastani.

Katika riwaya ya *Nguvu ya Sala*, ugumu wa maisha jijini Nairobi na matatizo ya uhalifu yanayotokana na ugumu huo yamesawiriwa kwa kutumia mbinu ya kinaya vilevile. Kwa mfano, mwandishi anawaita watu wanaompiga kijana ambaye amenyakua kibogosho tu cha mwanamke fulani 'wastaarabu.'

> 223. Walifyoa na kurereja matusi. Walivurumiza magongo. Yule kijana alikuwa bado analia; alipiga usiahi sasa. Alimsihi Mungu wake amnusuru na hujuma za **wastaarabu** hawa waliokuwa wanatishia kumwua…
> (Wamitila, 1999, Ukur. 115)

Mwandishi anapowaita watu hao wanaompiga kijana 'wastaarabu,' tunapata kinyume cha mambo ambapo watu wanatenda kwa namna isiyo ya kistaarabu, yaani neno na kitendo haviambatani. Msomaji anaweza akatambua mlinganuo uliopo kwamba watu hawa kwa kweli ni makatili, sio wastaarabu, bila kuambiwa moja kwa moja na mwandishi. Hata hivyo, kuna kinaya kwamba wanaompiga mtoto huyu nao pia ni

wanyonge kiuchumi kama mwenzao wanaompiga. Kwa mujibu wa mhusika Susan, mfumo wa maisha ndio unaosababisha matukio ya kikatili kama haya. Watu hawa wote wanapambana dhidi ya nguvu zinazowazidi. Wanauana. Hoja ya mwandishi ni kwamba nguvu ya sala haiwezi kusaidia kuzuia vitendo kama hivi.

Wakati umati ukimpiga kijana, mwanamke ambaye amenyakuliwa kibogosho chake hajaribu kuwazuia ila anasubiri kuona hatima ya kitendo hicho. Mwandishi anatuambia kwamba mwanamke huyo anasubiri "hadi aliporidhika **haki imetendeka"**:

> 224. Hakuwa na haraka ya kutoka pale hadi aliporidhika **haki imetendeka**.
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 115)

Kwa kusema 'haki imetendeka,' mwandishi anatumia kauli ambayo ni kinyume cha hali tunayoiona ambapo kisa cha kumuua kijana aliyenyakua kibogosho ambacho 'hata hakikuwa na chochote ndani isipokuwa karatasi za shashi na vitaulo vya *stayfree'* haiwezi ikawa haki. Maisha ya mtu yamelinganuliwa na kibogosho tu, ambacho ndani yake hata hamna kitu chochote cha thamani. Maelezo kwamba ndani mwa kibogosho hicho mlikuwa na "karatasi za shashi zilizokuwa na kamasi na vitaulo vya *stayfree,*" yanatumiwa na mwandishi kumwonyesha msomaji kwamba kitendo kinachotendeka sicho cha haki. Tena, haki inayotendeka kupitia kwa watu kuchukulia sheria mikononi, siyo haki kweli.

Kinaya kimetumiwa pia katika riwaya ya *Asali Chungu* kuwasilisha maudhui ya uwezo na mamlaka dhidi ya unyonge. Mwandishi anatumia neno 'waungwana' kuwarejelea watu ambao ama sio waungwana, au ambao hawatendi kiungwana. Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013), neno '**muungwana**' linamaanisha "mwenye adabu na tabia zinazokubalika katika jamii." Maana nyingine ni "mtu asiye mtumwa."

> 225. Jikoni mfereji ulikuwa ukimwaya maji. Maji kila pahali – chooni, ambako **waungwana** wakikoga …
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 12)

226. Hata kwa siku moja, mikononi tungemtia tu… Nilijua hutoshindwa… Heheeee, nacheka tena. Nawacheka wale wanaojipa uke mbele ya **waungwana**.
(Mohamed, 1977, Ukur. 26)

Katika dondoo la 225 tunaona makabaila Zuberi na mkewe Amina wakiitwa **waungwana**. Ingawa msomaji angeshawishika kwamba maana inayokusudiwa na msemaji ni ile inayowarejelea Zuberi na mkewe kama 'watu wasio watumwa,' muktadha wa riwaya nzima kuhusu vitendo vya 'waungwana' hawa unaashiria kinyume cha maana kwamba muungwana ni "mtu mwenye adabu na tabia zinazokubalika katika jamii." Isitoshe, wakati huu ambapo mwandishi anaandika riwaya yake, mfumo wa utumwa ulikuwa hauko tena.

Katika dondoo la 226 tunaona kwamba maneno ya Biti Daudi anapomrejelea Zuberi kama 'muungwana' si ya moyo safi. Ingawa anamrejelea Zuberi kama muungwana, tunaona kwamba hamheshimu; anamdharau kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Hata Biti Daudi anamwambia Zuberi maneno yanayombeza mkewe Amina lakini Zuberi hata hatambui hilo. Mwandishi anaeleza: "Zuberi kasahau ya kutukaniwa mkewe… Mwenyewe kaona anasifiwa" (Mohamed, 1977, Ukur. 26). Jambo hili linathibitisha kwamba Biti Daudi anamwita Bwana Zuberi '**muungwana**' kwa njia ya kinaya. Hapa tunaona hali ambapo mnyonge anajua kwamba ni mnyonge lakini anamchukulia mwenye mamlaka kama mtu asiye na akili, na analitumia neno 'waungwana' kwa njia ya kinaya, siyo kwa njia ya heshima.

Biti Daudi, ambaye ni mnyonge pia anatumiwa na matajiri Bwana Zuberi na mkewe Amina kwa ajili ya maslahi yao tu. Inaonekana kwamba yeye anaitambua hali yake ya unyonge lakini naye anajali tu maslahi yake. Hivyo, yuko tayari kuwasaidia matajiri kuwanyanyasa wanyonge wenzake. Yuko tayari kumsaidia Zuberi kufanya mapenzi na Semeni, msichana mdogo mhudumu ambaye ni fukara kabisa. Baada ya Zuberi

kumwambia jinsi ambavyo amefanikiwa kumbaka Semeni, bibi huyo hashtushwi na habari hiyo, ila anamwonyesha Zuberi kwamba anafurahia 'mafanikio' hayo. Anasema anawacheka wale wanaojipa uke mbele ya **waungwana**. Lakini, kitendo ambacho Zuberi amefanya cha kumbaka Semeni si cha kiungwana. Inaonekana kwamba Biti Daudi anamwambia maneno hayo Zuberi ili kumfurahisha tu. Ni njia yake ya kujipendezesha kwa tajiri huyo (Zuberi) ili apate manufaa fulani, kwa vile tunaona kwamba mwishoni mwa mazungumzo yao anamwomba Zuberi pesa.

Said Mohamed, katika riwaya yake ya *Asali Chungu* anatumia neno '**waungwana**' tena kuwarejelea watu ambao kusema kweli sio waungwana. Amina ni bibi tajiri ambaye anautumia uwezo wake wa pesa na mali kuwanasa vijana wanyonge kwa ajili ya kuwatumia kumstarehesha kimapenzi. Mmojawapo wa vijana hawa ni Dude. Baada ya kupata pesa na mali kutoka kwa Bi Amina, Dude naye sasa anarejelewa kama muungwana.

> 227. Wote waliteremka. Mwenyeji wao, Mzee Mbaruku, mwangalizi wa nyumba ya Bi Amina, alifika hima kuwalaki; akawa anatoa mizigo waliyokuja nayo **waungwana**. Dude akafunga vioo vya gari na kutia milango yote kufuli.
> (Mohamed, 1977, Ukur. 112)
>
> 228. Dau la kiasi lililetwa… Mzee Mbaruku akaanza kupakia mizigo kwenye hilo dau, na alipomaliza akawataka **waungwana** waingie. Bi Amina alivua viatu na buibui lake… Kwisha hivyo… alipandisha kanzu yake na kuyawacha huria mapaja yake kulimbukwa kuonekana na wale…
> **(**Mohamed, 1977, Ukur. 114)

Dude pia kuitwa muungwana ni kinaya. Huyu ni kijana aliyezaliwa katika ufukara mwingi. Ni mtoto anayetokana na kisa cha Zuberi kumbaka Semeni. Ingawa baba yake ni tajiri, jambo hili linabaki siri mpaka mwishoni mwa riwaya. Anakulia katika ufukara kwa vile mama yake ni fukara kabisa. Dude, kama lilivyo jina lake ni 'dude' tu.

'Uungwana' wake ni wa muda tu unaotokana na uhusiano wake wa kimapenzi na Amina. Dude amefadhiliwa mavazi, gari na hadhi tu na Amina. Ndiyo maana tunaona kwamba ugomvi unapotokea kati yao, Amina anamnyang'anya Dude kila kitu na Dude anarudi kwenye udude wake – si 'muungwana' tena.

Uhusiano wa Amina na Dude pia si wa kiungwana. Ni uhusiano wa kiuzinzi. Amina ana mume wake Zuberi ambaye anatambulika rasmi. Lakini, anatumia uwezo wake wa pesa na mali kumteka Dude ili kijana huyo amfanyie kazi, kazi ambayo ni ya kumridhisha kingono tu. Uhusiano wao si halali. Kwa msingi wa kutotenda kiungwana, ni kinaya kuwarejelea Dude na Amina kama '**waungwana**.'

Kitendo cha Amina kulivua buibui lake na kisha kupandisha kanzu yake mpaka mapaja yake yakaonekana kwa kijana wa kiume pamoja na Mbaruku (mwanamume pia) si cha kiungwana. Lakini Amina anatenda hivi kwa vile ana uwezo wa pesa na mali, na anaona hakuna yeyote ambaye anaweza kumkaripia. Utajiri wake unamfanya apuuze maadili ya dini yake ya Kiislamu.

Kinaya katika riwaya ya *Asali Chungui*, kinadhihirika tena katika mawazo ya Zuberi wakati akinyatia chumba cha Semeni kumbaka. Zuberi anamshukuru Mungu kwa kumpa hila ya kufunga matambara miguuni ili asisikike. Tena, baada ya kumbaka Semeni na 'kupoza raghba yake.' Zuberi anamrejelea Mungu katika mawazo yake.

229. Baadaye akawa tayari kukikabili chumba cha Semeni. Akaanza kunyatia. Alinyemelea kwa ustadi mkubwa. **Mungu bariki** alikuwa amefunga matambara miguuni.
(Mohamed, 1977, Ukur. 114)

230. Aliporejea chumbani kwake usiku wa jana, Zuberi alipoa na kuburudika. Hamu yake imezimwa; raghba yake imepozwa… Yaliyobaki yalikuwa ya kesho, na **kesho ina Mungu**.
(Mohamed, 1977, Ukur. 21)

Ni kinaya Zuberi kumrejelea Mungu, akiashiria kwamba Mungu amemsaidia kufanikisha mpango wake wa kikatili. Ni kama kwamba anaona kuwa Mungu yuko naye. Anawaza kwamba Mungu atamsaidia kuikabili kesho. Lakini, Mungu hawezi kuhusishwa au kumsaidia mtu katika kutekeleza mipango ya kikatili. Badala yake, baadaye Zuberi anajutia na kulipia kitendo chake hiki cha ukatili cha kumbaka msichana mnyonge.

Katika riwaya ya *Asali Chungu* maudhui ya unyonyaji wa wanyonge yameendelezwa pia kupitia kwa kinaya ambapo tunamwona mnyonge akimhusudu mnyonge mwenzake. Hata hivyo, anaona kwamba angalau mnyonge mwenzake yuko afadhali. Watu kama Zuberi na mkewe Amina, pamoja na makabaila wengine ni matajiri, ilhali raia wa kawaida ni maskini wanyonge kabisa. Vijana kama Dude hawana ajira. Wanazurura tu. Ndio maana Dude hata anawahusudu wanyonge kama yeye lakini ambao angalau wana kazi, ingawa kazi hiyo pia haiwaingizii wanyonge hao kipato cha maana.

231. Hawa, aliona Dude walikuwa wapagazi. Naye alikuwa **anawahusudu wapagazi** kila siku – vifua vyao vipana…walikuwa wanaume kweli kweli, mtu hawezi kuwachezea.

(Mohamed, 1977, Ukur. 50)

232. Hapa lilimpita rikwama limepakia madondo; nyuma jengine limepakia nazi au mbata… Hilo pia litakuwa katika heka heka ya kupelekwa kwenye ghala ya tajiri mmoja. **Dude aliwahusudu wale wapagazi** waliokuwa wakitimka na yale marikwama… Migongo yao…; vifua vyao vizima… Hawakuvaa chochote zaidi ya vindeketera…

(Mohamed, 1977, Ukur. 75)

Dude anawahusudu wapagazi na wasukuma rukwama – watu ambao ni mafukara pia kama yeye lakini ambao wanaonyesha kuridhika na shughuli zao, wakati ambapo yeye anatafuta kazi. Dude kuwahusudu watu ambao karibu ni maskini hohehahe ni kinaya. Vilevile, ni kinaya watu hao mafukara kuonyesha furaha, ingawa wanafanya kazi ya

sulubu ambayo inaingiza kipato kidogo tu. Wanaofaidika na nguvu na jasho la watu hawa wanyonge ni matajiri.

Mfano mwingine ambapo kinaya kimetumika kusawiri maudhui ya unyonge katika *Asali Chungu* ni kuhusu Mzee Kheri Karibu. Dude anajihisi mnyonge sana kiasi cha kumhusudu Mzee Kheri Karibu. Huyu ni mzee ambaye hana chochote. Haoni, hasikii, na tena ni mlemavu wa miguu. Maisha ya mzee huyo sasa ni kukaa mbele ya msikiti na kuombaomba tu vijipesa kutoka kwa wapita njia.

> 233. *Labda Kheri Kharibu ndio akacheka namna ile, kwa sababu ulimwengu alikuwa hauoni, hausikii, wala haufuati kuviona viroja na vituko vyake.* ***Watu kama hawa wana nafuu****.*
>
> Dude naye alitamani apate afueni ile.
> (Mohamed, 1977, Ukur.77)

Ni kinaya mtu mnyonge kabisa kama Mzee Kheri Karibu kucheka kila mara wakati ambapo hali yake inahuzunisha. Angetarajiwa kuonyesha huzuni kubwa kwa wapita njia. Hata hivyo, kicheko chake si kicheko cha kawaida cha furaha. Kwa vile mzee huyu amekuwa katika hali hiyo kwa muda mrefu, ameizoea na kuikubali hali yake ingawa haifurahii. Dude kumhusudu mnyonge kama Mzee Kheri Karibu, wakati ambapo yeye (Dude) angalau ana afya na anaweza kujitafutia kazi, ni kinaya. Lakini kwa sababu ya hali yake ya kukata tamaa, Dude anaona kwamba hata ile hali ya Mzee Kheri Karibu kutoona chochote ni afadhali, kuliko yeye (Dude) ambaye anauona ulimwengu wenye shida kubwa. Hivyo, kwa njia ya kinaya, Dude anasema kwamba watu kama Mzee Kheri Karibu wana nafuu. Kutotambua kinachoendelea duniani pia ni kuwa na nafuu.

Hali nyingine inayotuonyesha kinaya katika riwaya ya *Asali Chungu*, mintarafu maudhui ya unyonge ni pale ambapo Bushiri anarejelea jela kama mahali ambapo pangeweza kumnusuru. Baada ya kufungwa mara kadhaa, Bushiri anapata kazi kwa

Amina. Awali anaona ni afadhali kukaa jelani akapata chakula kuliko kukaa nje akawa hana chochote cha kujikimu.

> 234. …niliona bora utumwa wa kuwa mfungwa kuliko kuwa na uhuru katika ulimwengu ambao hauwezi hata kunipa chakula… Nje kuna maonevu, unyonge na utumwa… Yakinijia mawazo hayo, huona nijitie katika hatia ili **nirudi jela ninusurike**. Hustahabu taabu ya kutumwa jela nikapata chochote, mradi silali na njaa, kuliko kutamba na ulimwengu mchana kutwa, au mara nyingi kumeza mate.
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 83)

Ni kinaya Bushiri kusema kwamba bora kurudi jela ili '**anusurike**' kwa vile kufungwa jelani si kunusurika, bali ni kufungwa tu na kunyimwa uhuru. Hata hivyo, katika hali ya unyonge aliyomo, kwa mtazamo wake, kufungwa jelani ni kama kunusurika kwa vile angalau jelani halali njaa, kinyume na maisha nje ya jela ambako analala njaa.

Said Ahmed Mohamed pia anaonyesha kinaya mintarafu jinsi mafukara wanavyofaidika katika siku za maulidi.

> 235. Kwa mafukara, hizo huwa ni **siku ambazo Mwenyezi Mungu humwaya neema zake kwa mlango wa nyuma** ili kuwaneemesha maskini wasiojiweza, japo kwa mwaka mara moja; na hiyo huwa **ni kama kuwarejeshea akali ya matone yao ya damu iliyonyonywa**… hutapikwa.
>
> (Mohamed, 1977, Ukur. 29)

Kuna kinaya katika maneno haya kwamba utajiri huu walio nao mabepari na makabaila wameupata kutokana na jasho la watu maskini. Sasa matajiri hao ndio wanawagawia maskini wali na nyama, kama njia ya kuwakirimu wanyonge ili kutekeleza nguzo ya kutoa zaka katika Uislamu. Lakini mwandishi anasema kwamba huku ni kuwarudishia maskini sehemu ndogo tu ya damu yao ambayo matajiri hao wenyewe wameinyonya. Kwa njia hiyo, sio kwamba matajiri hao wamewapa maskini chakula kwa kweli, ila ni kama kuwarudishia tu wanyonge hao kilicho chao.

Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, mwandishi anatuelezea utofauti wa kimamlaka kati ya tajiri bwana shamba (Fuad) na maskini, Mzee Serwani.

> 236. Mzee huyu hakujua nia halisi ya matembezi ya Fuad na hata kama angejua **angeona ni fahari kubwa kwake kwa kuwa na binti anayefaa bwana shamba mkubwa yule**.
> (Shafi, 1978, Ukur. 14)

Mwandishi anatueleza kiasi cha unyonge wa watu kama Mzee Serwani. Kinaya ni kwamba badala ya tajiri kuona kwamba amepata bahati kumpenda binti huyo, tunaambiwa kwamba babu ya binti huyo ndiye angekuwa na bahati kuona kuwa mjukuu wake anapendwa na tajiri. Bahati ya mnyonge inatokana na msingi kuwa tajiri ana uwezo mkubwa wa mali na pesa, na hivyo anaweza kumpenda binti ya mtu yeyote anayemtaka. Hivyo, maskini mnyonge ndiye angefaidika kwa binti yake kuchaguliwa na tajiri. Watu kama Fuad wako katika nafasi hii ya uwezo na mamlaka kwa sababu ya mali waliyo nayo. Hata hivyo, utajiri huu unatokana na mabwana shamba kuwakandamiza wanyonge, ambacho pia ni kinaya.

Mali na fedha vinampa kabaila Fuad uwezo wa kujijengea hata msikiti wake mwenyewe. Mara nyingi msikiti huwa ni wa umma. Hivyo, mtu kujijengea msikiti wake mwenyewe si jambo la kawaida. Hapa pia mwandishi anauchimuza uwezo mkubwa wa kifedha wa Fuad kumiliki mali. Mali inampa Fuad mamlaka hata ya kujijengea msikiti.

> 237. Fuad alijenga msikiti mdogo, mzuri, karibu na nyumba yake na **ndani ya msikiti huo walisali wale waliokuwa na madhehebu ya kiibadhi tu kama yeye mwenyewe.**
> (Shafi, 1978, Ukur. 16)

Hapa tunamwona mtu ambaye mwenendo wake wa maisha ni mbovu kabisa lakini anajenga msikiti. Anawatesa wafanyakazi na anajaribu kuwanajisi watumishi wake wa kike. Ingawa yeye ni Mwislamu lakini anakunywa pombe, kitu ambacho ni haramu katika Uislamu. Tunaona mlinganuo wa mwenendo wake na imani yake. Ni kama

kwamba anafikiri kuwa uwezo wa mali na pesa unampa mamlaka ya kufanya chochote hata labda kupendelewa na Mungu. Msikiti anaoujenga Fuad "wanasali wale waliokuwa na madhehebu ya kiibadhi tu kama yeye mwenyewe." Hii ni tofauti na mwenendo wa kiislamu ambapo msikiti huwa ni kwa wote, bila ubaguzi. Hiki pia ni kinaya. Mtu ambaye anajenga msikiti kuonyesha vile alivyo Mwislamu wa kweli anafanya kitu ambacho ni kinyume na Uislamu, yaani kubagua waumini.

Kinaya kinachoitawala riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* ni jinsi Kijakazi anavyodumisha unyonge wake kwa kujitolea kuwafanyia kazi mabwana shamba wasiomjali, bila kuchoka. Ingawa haitarajiwi kwa mtu anayeteswa kuwa na furaha, lakini yeye Kijakazi anajawa na furaha kwa kumfanyia bwana shamba kazi bila kupumzika.

238. …. shamba la Bwana Malik lilikuwa daima zuri… Mabondeni, mpunga ulistawi kwa wingi… **yote haya yalimletea Kijakazi furaha maalum ijapokuwa yeye hakupata kitu chochote katika mazao yanayopatikana shambani humo**.
(Shafi, 1978, Ukur. 2)

239. Kusema kweli **kazi zilikuwa zimeshamchosha Kijakazi ijapokuwa kila alilofanya alilifanya kwa furaha**… furaha iliyochanganyika na machovu.
(Shafi, 1978, Ukur. 3)

Katika dondoo la 238 tunaona kinaya ambapo vitu kwenye shamba la Bwana Malik ambavyo Kijakazi hafaidiki navyo ndivyo vinavyomletea '**furaha maalum.**' Mwandishi amechimuza kinaya hiki pia kwa kutumia kivumishi ili kuelezea zaidi furaha aliyokuwa nayo Kijakazi ambayo inalinganuliwa na hali yake ya utumwa. Katika dondoo la 239 tunaona kwamba, ingawa kazi zinamchosha Kijakazi, anazifanya kwa furaha. Furaha yenyewe imechanganyika na machovu. Kinaya kinatokana na hali

kwamba Kijakazi halazimishwi kuzifanya kazi hizi, kwa vile mfumo wa utumwa haupo tena, ila anazifanya yeye mwenyewe kwa hiari.

Akitumia kinaya, mwandishi wa riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* anaibua maudhui ya ubinafsi na unafiki. Mapinduzi yanayofanywa na watu wa kawaida yanaleta mabadiliko ambapo mwenye mamlaka (bwana shamba) anayapoteza mamlaka yake na kuwa mnyonge, na aliyekuwa mnyonge (mfanyakazi na mkulima) sasa ndiye mwenye mamlaka. Baada ya kunyang'anywa ardhi, mabwana shamba wanakuwa wanyonge kabisa. Wanakutana kwa Fuad kuzungumzia hali yao.

> 240. "Hata mimi walipokuja kwangu walinambia maneno hayo hayo! Hawa watu wana wazimu? **Hawajui kama ni dhambi kubwa kumnyang'anya mtu mali yake**," Swelum naye aliingia kati.
>
> (Shafi, 1978, Ukur. 57)

Mabwana shamba wanalalamikia hatua ya serikali ya kimapinduzi kuchukua ardhi yao ilhali wamewatesa sana wakulima kwa kuwafukuza wakulima hao mashambani mwao, kuwang'olea mimea na kuwachomea makonde. Sasa mabwana shamba hao ndio wanaona kwamba kunyang'anywa shamba, na wakulima wakapata angalau ardhi kidogo ni dhambi kubwa, ilhali dhambi kubwa ni mabwana shamba kuwanyang'anya ardhi raia walio wengi ambao hawana ardhi. Mabwana shamba wanaiona hatua ya kuwasaidia wakulima wasio na ardhi kama ni dhambi, ingawa ardhi hiyo mabwana shamba hawakuipata kwa njia halali; yaani kiuhalisi, ardhi hiyo sio mali yao kama wanavyodai. Kinaya ni kwamba aliyekuwa anamnyang'anya mkulima ardhi na anaona ni sawa, sasa yeye ndiye anaona kwamba sio haki yeye kunyang'anywa ardhi. Huu ni ubinafsi na unafiki. Fuad anamwomba Mungu awashinde wanamapinduzi, ila sio dhahiri kama Mungu 'atawashinda' wanaofanya mambo ya haki. Makabaila wameipata ardhi kubwa kwa kushirikiana na serikali ya kikoloni.

Mwandishi wa riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* anasawiri maudhui ya ubinafsi wa mnyonge. Hili linadhihirika tukimwangalia mhusika Kijakazi. Hali ya wafanyakazi ni ya kusikitisha. Wananyanyaswa na kukandamizwa na mabepari na makabaila. Hata hivyo, wanapambana na kuipindua serikali ili wao wenyewe waweze kuboresha maisha yao. Hata hivyo, baadhi ya wanyonge kama Kijakazi hawachangii juhudi hizi. Kijakazi anaona kwamba harakati za kujikomboa hazimhusu yeye.

> 241. "Umaskini ulikuwa umejaa nchini na unyonge umewazonga wananchi. Hata hivyo, …wafanyakazi hawakwisha kufanya migomo, maandamano na mikutano… ya kupinga mabepari na makabaila na kudai uhuru kutoka kwa wakoloni…
>
> Yeye [Kijakazi] alifurahi kuona yote yaliyotokea [nchini] **hayakumhusu**. Kila mara alikuwa **akishukuru Mungu kwa kumpa uwezo wa kufanya kazi yake vizuri**.
> (Shafi, 1978, Ukur. 11)
>
> 242. Mambo ya ujamaa hakuyaelewa hata kidogo. Aliona **yote yale hayakumhusu yeye**.
> (Shafi, 1978, Ukur. 56)

Katika madondoo ya 241 na 242, Kijakazi anadhihirisha ubinafsi. Badala ya kujiunga na wanyonge wenzake katika juhudi za kujiokoa, anajifikiria yeye binafsi. Haoni kwamba harakati zinazofanywa na wanyonge wenzake zitamfaidi hata yeye. Yeye anaziangalia juhudi hizi kama mtu aliye kando. Mtu kutoitambua hali yake mbaya na kufikiri kuwa yale wanayoyafanya wafanyakazi wenzake kujaribu kujikomboa '**hayakumhusu yeye**' ni kinaya. Badala ya kumwomba Mungu kumpa uwezo wa kujikomboa, yeye anamshukuru Mungu kwa kumpa uwezo wa kumtumikia bwana shamba, wakati ambapo wafanyakazi wenzake wanajitahidi kupigana dhidi ya mabwana shamba kama Fuad anayemdhulumu.

Mwandishi wa riwaya ya *Nguvu ya Sala* anadhihirisha udhaifu wa misingi mikali ya dini kama ile ya mhusika Richard. Richard ni mkali kupita kiasi kwa vile anataka familia yake iwe kielelezo kwa familia zingine katika misingi ya thamani za Kikristo.

Richard ni pasta ingawa ni mkali kuliko rafiki yake Nichodemus, ambaye si pasta lakini ni mpole. Kinaya ni kwamba Richard ambaye ni pasta ndiye angetarajiwa kuwa mpole.

> 243. Babake Bathsheba alikuwa Mkristo. Hakuwa pasta kama babangu ila alikuwa mzee wa kanisa na wala sidhani kama alikuwa mkali kama alivyokuwa baba. **Labda siku moja angekuwa mkali; siku ambayo angekuwa pasta.**
> (Wamitila, 1999, Ukur. 16)

Msomaji anatarajia kwamba pasta ndiye angekuwa mpole na siyo mkali. Susan anaposema: '**Labda siku moja angekuwa mkali; siku ambayo angekuwa pasta**,' anamdhihaki baba yake. Anatubainishia kinyume hicho cha hali, ambacho ndicho kinaya chenyewe. Kinaya kinajitokeza kwa kumhamishia Richard sifa ambayo ingekuwa siyo hulka yake, yaani pasta kuhamishiwa sifa ya ukali, wakati ambapo muumini wa kawaida ndiye anayepewa sifa ya upole.

6.1.5 Kejeli

Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013), kejeli ni maneno ya dharau. Wamitila (2003) anatumia istilahi dhihaka na anaichukulia kama aina ya kejeli. Anasema kwamba dhihaka inadhamiriwa kuigusa hisia ya mtu kwa njia ya waziwazi na aghalabu kwa nia ya kufichua ubaya fulani au udhaifu alio nao mhusika fulani. Pia, anasema kwamba dhihaka hukusudiwa kumtweza au kumuumiza mtu, na kwamba inakuwa na dhamira mbaya. Mbatiah (2001) naye anatoa maelezo yanayolingana na ya Wamitila anaposema kwamba kejeli ni maelezo yanayoitweza na kuidunisha hali fulani. Kwa mujibu wa Mbatiah, matamshi yenye kejeli huwa ni ya kuchoma, kukata na kutia uchungu. Vilevile, anaeleza kwamba kejeli ni aina ya kinaya yenye ukali wa kipekee.

Mbali na matumizi ya sitiari, maudhui ya mgongano kati ya utamaduni na dini ya Kikristo yamedhihirishwa katika *Nguvu ya Sala* kwa njia ya kejeli pia. Kama tulivyoona katika dondoo 190, Richard anachukulia kwamba utamaduni wa jamii yake ni giza

(sitiari ya utamaduni kama giza), na kwamba Mzungu amemkomboa Mwafrika kwa kuleta mwanga wa Ukristo.

> 244. "Imani hizo hazina nafasi katika ulimwengu wa leo. Mzee hizo ni fikira za zamani ambazo zimepitwa na wakati…
> …[Wazungu] wametukomboa kutokana na giza la utamaduni."
> "**Hakika ni ukombozi huo!"**
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 6)

Kama inavyobainishwa katika dondoo la 244, Richard anasisitiza kwamba imani za jadi zimepitwa na wakati na kwamba Wazungu wamewakomboa wanajamii kutokana na "giza la utamaduni." Mzee, ambaye anashangazwa sana na mtazamo wa Richard kuhusu imani za jamii yake, anamjibu Richard kwa kejeli, "**Hakika ni ukombozi huo**." Maneno ya mzee yanaashiria kwamba Richard hajui anachokisema; ni kama mjinga. Toni ya maneno ya mzee ni hasi, kwa mujibu wa muktadha wa mazungumzo haya na tena matumizi ya alama ya mshangao. Ingawa kauli ya mzee iko katika hali yakinishi, kinyume ndicho kimeashiriwa katika kauli hiyo, yaani "Huo si ukombozi." Kinyume hiki ndicho kinachounda kinaya ambacho kinalenga kumkejeli Richard, kwa vile mzee amekwisha pinga msimamo wa Richard kuhusu utamaduni wa jamii yake.

Akitumia kejeli, mwandishi wa riwaya ya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* anasawiri maudhui ya mwenye mamlaka kutoyathamini maisha ya mnyonge. Fuad anajaribu kumshawishi Kijakazi asimwache, kwa vile wafanyakazi wote wanaelekea kumwacha. Lakini maneno ambayo Fuad anamwambia Kijakazi yamejaa kejeli:

> 245. Kijakazi sharti ufahamu kwamba wewe ni kama mzee wangu kwani wewe ndiye uliyenilea. Nakuahidi kwamba **utakapofariki nitakufanyia mazishi makubwa yasiyowahi kufanywa hapa Koani.**
>
> (Shafi, 1978, Ukur. 67)

Fuad anamkejeli Kijakazi kwa kumwambia atamshukuru kwa mazishi makubwa. Hapa tunaona maneno ya mtu mwenye mamlaka akimkejeli mnyonge ambaye ni mtumwa

wake. Fuad hamheshimu Kijakazi. Badala ya kumwahidi zawadi ya vitu kama mavazi au mali, Fuad anamwahidi mazishi mazuri, yaani kumshukuru baada ya yeye Kijakazi kuaga dunia. Kwa mfu, hakuna mazishi mazuri kwa sababu hatambui chochote anachofanyiwa.

Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi*, mwandishi amesawiri maudhui ya unyonyaji. Hili linabainika tunapochunguza maneno ambayo Fuad anamwambia Kijakazi. Maneno anayomwambia yanaonyesha kwamba anachofaidika nacho Fuad ni kazi ya Kijakazi tu, kwa vile anaona kwamba Kijakazi yuko tayari kuendelea kufanya kazi kitumwa. Anajua kwamba Kijakazi hajatambua kwamba makabaila wamepoteza mamlaka.

> 246. "Usichanganyike naye [Mkongwe] hata kidogo kwani yeye amekwishatutoka… lakini mwache aondoke. **Atakapoondoka itakubidi wewe Kijakazi ufanye kazi zaidi."**
>
> (Shafi, 1978, Ukur. 68)

Ni dhahiri katika dondoo la 246 kwamba Fuad anamchukulia Kijakazi kama mjinga anayefurahia kufanya kazi zaidi, anamwambia kwamba mtumishi mwenzake atakapoondoka, itambidi yeye Kijakazi afanye kazi zaidi. Ni kama kwamba anamwambia Kijakazi kuwa atakuwa na fursa zaidi ya kufanya kile anachokifurahia, yaani kufanya kazi nyingi. Fuad anamtarajia Kijakazi kufurahia habari hiyo. Hapa tunaona jinsi ambavyo mnyonge hajitambui na yeye mwenyewe anachangia hali yake ya utumwa. Mwandishi anaidhihaki hali hii, kupitia kejeli ya Fuad.

Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, mwandishi anatumia kebehi kuibua maudhui ya mnyonge kutoitambua hali yake ya kuonewa na kunyonywa na kwa hivyo kutochangia juhudi za kumwokoa au kujiokoa. Hili linabainika katika tabia ya Kijakazi. Mwandishi anamkebehi Kijakazi pia kuhusu jinsi anavyoazimia kumfurahisha bwana shamba wakati ambapo bwana shamba hamjali Kijakazi, ila anaijali tu kazi ambayo

Kijakazi anamfanyia. Hii ni hali ya kushangaza ambapo mnyonge anajitahidi kumfurahisha na kumjali bwana huyo mwenye mamlaka, ilhali mwenye mamlaka hamjali mnyonge.

247. Ole wake Kijakazi kwa msiba mkubwa aliokuwa nao kwa kufiwa na **Bwana wake**, alikuwa mnyonge kuwashinda wote na kila wakati …. huomboleza mpaka macho yakavimba. Kifo cha Bwana Malik kilikuwa ni msiba mkubwa kwa Kijakazi.
(Shafi, 1978, Kur. 8 - 9)

248. Kiasi cha saa tatu za usiku teksi ilifika pale nyumbani kumleta Fuad.
"Oh! Haijambo **bwana** amerudi salama!" Kijakazi alisema akishusha pumzi na kupumua**…**
Alimkunjulia chandarua…. alisimama kwa unyonge pembeni ya kitanda na kumtazama **bwana wake mpenzi** ….
(Shafi, 1978, Kur. 22 - 23)

249. Kijakazi alikuwa akimvua viatu Fuad na wakati huo ilimjia huruma kubwa kumhurumia **Bwana wake, Fuad mpenzi**…
(Shafi, 1978, Ukur. 76)

Katika madondoo ya 247 - 249, mwandishi anamdhihaki Kijakazi kwa kuwajali watu wasiomjali, ila wanaojali kazi anayowafanyia tu. Mwandishi anadhihirisha kejeli kwa kurudiarudia kirai '**bwana wake**' na wakati mwingine kuongezea neno 'mpenzi' mara kadhaa ili kuichimuza tabia ya kushangaza ya Kijakazi. Kauli inaporudiwarudiwa sana inaanza kuashiria maana au umuhimu fulani. Kwa hivyo, kirai 'bwana wake' kinaporudiwarudiwa mara nyingi msomaji anaanza kujiuliza kuhusu umuhimu wa matumizi ya kirai hicho. Msomaji anaweza akalinganisha hali ya utumwa ya Kijakazi na heshima na utiifu wake kwa mabwana shamba kwa upande mmoja na jinsi anavyotendewa na mabwana shamba hao. Mlinganuo uliopo kati ya tabia ya Kijakazi na tabia ya mabwana shamba ndio unaozalisha kejeli.

Mwandishi pia anamdhihaki Kijakazi kwa kutumia kirai '**bwana wake mpenzi**.' Kijakazi anamchukulia Fuad kama bwana wake mpenzi, lakini Fuad hamjali.

Mwandishi anamdhihaki mnyonge kwa kutotambua kwamba mtu anayemjali, yaani kabaila, hamjali yeye. Kama njia ya kumkejeli zaidi Kijakazi, mwandishi anabadilisha kauli kidogo katika dondoo la 248 na dondoo 249. Katika dondoo la 248, mwandishi anasema '**bwana wake mpenzi**' na katika dondoo 249 anatumia kauli '**Bwana wake, Fuad mpenzi**.**'** Huu ni msisitizo wa aina fulani ambao msomaji atajaribu kuufasiri. Msomaji ataona kwamba si kawaida mtumwa kumpenda namna hiyo bwana anayemtesa.

Mtazamio wa mwandishi unabainika tukiangalia maelezo mengine anayoyatoa. Maelezo haya ni hasi na yanachangia uwasilishaji wa kejeli anayoijenga mwandishi. Katika dondoo la 247 msimulizi anasema kwamba kifo cha Bwana Malik kilikuwa ni **msiba mkubwa** kwa Kijakazi na kwamba yeye ndiye aliyekuwa **mnyonge kuwashinda wote**. Hizi ni kauli ambazo zinalinganuliwa na hali ya maisha ya Kijakazi. Mabwana shamba hawampi Kijakazi chochote, na kwa hiyo kifo cha Bwana Malik hakiwezi kuwa ni msiba mkubwa kwa Kijakazi. Vilevile, Kijakazi asingekuwa 'mnyonge kuwashinda wote,' mkiwemo hata mkewe marehemu Malik. Maelezo haya yanamfanya msomaji ajiulize huyu ni mtumishi wa aina gani? Badala ya kumsikitikia Kijakazi, msomaji anaweza kumwona kama mtu ambaye ana hitilafu akilini.

Shafi Adam Shafi pia anasawiri maudhui ya unyanyasaji wa wasichana katika riwaya yake ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, ambapo wafanyakazi wasichana wananyanyaswa na mabwana shamba. Mabwana shamba karibu wanaweza kufanya lolote katika mashamba yao bila kuhofia adhabu yoyote. Hata hivyo, mwandishi anayadhoofisha mamlaka ya tajiri kwa kumkejeli bwana shamba Fuad pale ambapo bwana shamba huyo anajaribu kumkamata mtumishi wake Mariam kwa nguvu lakini anashindwa.

250. “Mwachilie, sasa nitamwita huku ndani na akifika atashika adabu yake: nitamwita mmoja katika wale mbwa wenzake **aje anisaidie kumkamata**.”

Fuad alikuwa mwingi wa mwili lakini kwa ajili ya kukaa bure maisha yake yote, unene aliokuwa nao ulikuwa ni wa maji matupu. Hakumweza Mariam kwa vibiru na ilimbidi ampate mtumishi wake mwingine kumsaidia.
(Shafi, 1978, Ukur. 13)

Fuad anajaribu kumbaka mfanyakazi wake Mariam kwa vile (Fuad) ana mamlaka yasiyo na kikomo. Hata hivyo, mwandishi anaonyesha kwamba katika mamlaka hayo kuna udhaifu vilevile. Mwandishi anaukejeli udhaifu huo, kwani Fuad anashindwa kwa urahisi kumkamata Mariam. Ni dhahiri kwamba mwandishi anamkejeli Fuad kwa kumpunguzia sifa zake kama mwanamume. Anaonyesha kwamba ingawa Fuad ni bwana shamba mwenye mamlaka makubwa, yeye kama mwanamume ni bure kabisa. Unene wa mwili ni wa bure; hajiwezi kama mwanamume. Ili kuifanya kejeli hii ieleweke kwa msomaji mwandishi anatoa maelezo ya ziada kwa kusema: “Hakumweza Mariam kwa vibiru na ilimbidi amtafute mtumishi wake mwingine kumsaidia.” Kwa mwanamume ye yote, hii ni hitilafu kubwa. Kisa hiki cha Fuad kujaribu kumkamata msichana mtumishi wake na kushindwa, pamoja na mpango wake wa kupata usaidizi kutoka kwa mfanyakazi mwingine kumkamata Mariam, vinamfanya msomaji alinganue mamlaka aliyo nayo Fuad na udhaifu wake (Fuad) wa kimwili.

Katika dhamira yake ya kumkuza mhusika mwanamke kwa kumdunisha mhusika wa kiume, mwandishi anamshushia sifa Richard katika riwaya ya *Nguvu ya Sala*. Hii ni kwa sababu ni dhahiri kwamba mwandishi hakubaliani na ukali na mamlaka anayoyatumia Richard dhidi ya mabinti zake. Ukali huu unatokana na imani yake kali.

251. “Mbona mlikuwa mnaongea Kizungu?” aliuliza baba.
“Kuna ubaya gani kuongea Kiingereza naye baba?” niliuliza.
Hakunijibu wala mama naye hakunijibu lakini wote wawili walinikodolea macho.

> “Hiyo iwe mara ya mwisho,” alifoka baba.
> **Sikumwelewa**. **Sikujua kama alikusudia iwe mara ya mwisho kuongea Kiingereza na James au kuandamana naye**.
> (Wamitila, 1999, Ukur. 107)

Katika dondoo la 251 tunaona jinsi ambavyo mwandishi anamdhihaki Richard kupitia kwa mhusika Susan. Susan anamdhihaki baba yake kwa kutumia neno ‘Kizungu’ badala ya neno ‘Kiingereza.’ Hivyo, ni kama kwamba Susan anamkosoa baba yake bila ya kumwambia, kwamba neno sahihi ni ‘Kiingereza,’ siyo ‘Kizungu.’ Hii ni njia ya kuonyesha tofauti iliyopo kati yake na baba yake kimasomo. Mwandishi analinganua msimamo mkali na mamlaka aliyo nayo Richard kwa upande mmoja na udhaifu wake wa kimasomo. Inakumbukwa kwamba wakati ambapo Richard haendelei na masomo yake mpaka chuo kikuu, binti yake anafanikiwa kufanya hivyo. Kwa hivyo, dhihaka hii ni njia ya kumdunisha kama mhusika mwanamume anayeonyesha udume nyumbani kwa kuonyesha kwamba uelewa wake wa baadhi ya mambo ni wa chini kuliko wa binti yake.

Richard anapomwambia Susan kwamba “hiyo iwe mara ya mwisho,” Susan anamkejeli baba yake kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa kusema kwamba hakuelewa kama baba yake alikusudia kusema iwe mara ya mwisho kuongea Kiingereza au iwe mara ya mwisho kuandamana na James. Huku pia ni kumdhihaki baba yake kama mtu ambaye anasema mambo ambayo hayaeleweki bayana. Anaudhihaki ukali wa baba yake na kudunisha mamlaka aliyo nayo baba katika familia.

Katika *Nguvu ya Sala*, mwandishi anagusia suala la jinsia kwa kuonyesha jinsi ambavyo tabia ya mtoto wa kike inadhibitiwa zaidi kuliko ya mtoto wa kiume. Kuna matarajio mengi kumhusu mtoto wa kike kuliko mtoto wa kiume. Ingawa mtoto wa kiume hazungumziwi moja kwa moja katika riwaya hii, tunaona kwamba Richard anasisitiza

kwamba baadhi ya tabia hazifai kwa mtoto wa kike. Baadhi ya tabia hizi ni pamoja na kuangua kicheko, kucheza dansi, kuwa mdadisi, na kutumia mapambo. Susan anaikejeli misimamo ya baba yake kwa vile baba huyo anazikemea tabia ambazo ni za kawaida tu kwa binadamu.

> 252. Baba aliichukia sana tabia hii ya kuangua kicheko. Alisema kuwa haikuwa tabia nzuri kwa mtoto wa kike. Nakumbuka jinsi alivyonicharaza siku moja baada ya kunisikia nikicheka kwa sauti ya juu. Niliamini kuwa tabia hiyo ilikuwa mbaya na haikosi **hata Mungu aliichukia**.
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 31)

> 253. Roselyn alikuwa karibu na dirisa lililoelekea upande wa chini, akinenguanengua kiuno… Alichelea kukutwa seli na babake; **ingekuwa kiama** kama angetekwa bakunja akiuchezesha mwili wake. **Kufuru si kufuru ile** kuuachia mwili wake hivyo. Baba yake angeghadhibika. **Yaelekea angefanya kitendo kikubwa kuliko alivyofanya Masiha baada ya kuwakuta walanguzi na wachuuza-njiwa katika hekalu la Bwana.**
>
> (Wamitila, 1999, Ukur. 111)

Katika madondoo ya 252 na 253, Richard ameonyeshwa kama mtu ambaye anakasirika na kuwaadhibu watoto kwa mambo yasiyo ya maana. Susan anayaeleza mambo haya kwa toni ya kejeli kwa kutumia msamiati na kauli zinazomfanya msomaji kumwona Richard kama mtu ambaye hana akili, kwa vile hazingatii mantiki yoyote. Susan anatumia chuku kuonyesha jinsi ambavyo baadhi ya maagizo ya Richard hayana maana. Richard anawazuia watoto wake wa kike kucheka akisema kwamba '**haikuwa tabia nzuri kwa mtoto wa kike.**' Susan anaudhihaki msimamo huu kwa kusema kwamba '…**haikosi *hata Mungu aliichukia*.**' Hata mwandishi amesisitiza kejeli hii kigrafolojia kwa kutumia herufi mlazo. Kuna kinaya katika mlinganuo wa tabia ya kucheka na uamuzi wa Mungu, kwani Mungu hawezi kuichukia tabia ya kucheka ambayo ni sifa ya maumbile ya binadamu. Imani ya Kikristo ni kwamba Mungu ndiye alimuumba binadamu.

Kuhusu kitendo cha mdogo wake Roselyn kucheza dansi, na jinsi ambavyo baba yake angekichukulia, Susan anaeleza kuwa '**ingekuwa kiama**' kama baba yao angemkuta Roselyn akifanya hivyo. **A**nasema kuwa baba yao angekiona kitendo hicho cha kucheza dansi kama kufuru ('**kufuru si kufuru ile…**'). Eti baba yao angeghadhibika na labda **angefanya kitendo kikubwa kuliko alivyofanya Masiha baada ya kuwakuta walanguzi na wachuuza-njiwa katika hekalu la Bwana.** Hapa chuku imetumika kuzalisha kejeli. Maelezo ya Susan yanaonyesha kejeli kwa sababu ya kutokuwepo kwa ulinganifu kati ya kitendo cha kucheza dansi kwa upande mmoja, na ghadhabu pamoja na adhabu ambayo inaaminika Richard angeitoa kwa yule ambaye angempata akicheza dansi. Kile ambacho Richard angefanya kimezidi mno ukali kuliko ile tabia inayodhihirishwa (kucheza dansi). Hakuna misingi ya Kikristo inayochukulia kucheza dansi kama kufuru kubwa. Kitendo hicho cha kucheza dansi hakiwezi kulinganishwa na watu kufanyia biashara katika hekalu la Bwana. Kwa kutumia mlinganuo huo, mwandishi anaonyesha kwamba Masiha asingefanya kile ambacho Richard angekifanya, na Richard ni binadamu tu. Ni kama kusema kwamba binadamu angetoa adhabu kali zaidi kuliko hata ile ambayo ingetolewa na Mungu, kitu ambacho kinaonyesha kuzidi mipaka kwa vitendo vya Richard, na kwamba vitendo vyake haviambatani na Ukristo anaouhubiri. Hiki ni kinaya.

6.1.6 Chuku

Kwa mujibu wa Mbatiah (2001), chuku (pia udamisi) ni tamathali ya usemi inayotumia lugha ya kutilia chumvi, aghalabu kwa madhumuni ya kusisitiza. Naye Wamitila (2003) anaeleza kwamba chuku ni mbinu inayotumiwa kuelezea hali ya kuikuza sifa ya kitu fulani kuliko kawaida. Anasema kuwa chuku huchangia katika kuyachimuza masuala fulani katika kazi inayohusika.

Habwe ametumia mbinu ya chuku pia kuendeleza maudhui ya masengenyo, chuki na wivu ndani ya makanisa katika riwaya yake ya *Paradiso*. Katika dondoo la 174 tunaona jinsi ambavyo mwandishi ametumia sitiari kuonyesha chuki hii. Katika dondoo hilo, tunaambiwa kwamba, kwa kuendelea kufanikiwa katika mahubiri yake, Mchungaji Michael alikuwa 'akitia kitumbua chake mchanga,' yaani akijitia hatarini. Hivyo, mwandishi amesisitiza maudhui hayo ya chuki ndani ya makanisa pia kwa kutumia mbinu ya chuku.

> 254. Baadhi ya viongozi walimsengenya. "Huyu amekuja tu ameona ndiye **atakayeokoa ulimwengu mzima wa Nairobi,"** alisema Monayo.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 39)

Katika dondoo hili, maneno yanayotumiwa na mmojawapo wa viongozi wa kanisa la New Jerusalem yanaonyesha chuku, na yanaibua maudhui ya wivu ndani ya kanisa. Kuna chuku katika maneno "**atakayeokoa ulimwengu mzima wa Nairobi,**" kwa vile Nairobi sio ulimwengu mzima. Monayo anatumia maneno hayo yenye chuku kwa sababu ya chuki dhidi ya Mchungaji Michael. Kwa mujibu wa maneno ya mwandishi, "Haikuwa rahisi Michael kushindwa katika sala." Viongozi wengine wanamtakia kushindwa. Wanamwona kama mtu ambaye amejikweza na kujitakia makubwa, na walitarajia kushindwa kwake wakati wowote, kama Askofu Joshua anavyotabiri: "Tumpe miaka miwili. Atashindwa tu kwani anafikiri sisi tumeanza lini?" (Habwe, 2005, Ukur. 39). Lakini, chuki ni tabia ambayo haiambatani na mafundisho ya Kikristo ambayo yanasisitiza umoja na upendo kati ya Wakristo wote.

Pamoja na mbinu ya anafora ambayo tumeiangalia katika sehemu ya 5.1.1 (dondoo la 92), Habwe pia ametumia chuku kuendeleza maudhui ya ufisadi na kujilimbikizia mali. Chuku iliyotumika inamhusu mhusika Amuko. Amuko ni mhusika ambaye amepata mali nyingi kutokana na ufisadi.

255. Ataacha vipi ufisadi wake wa ofisini ambao ndio umemletea magari kochokocho aliyo nayo na **nyumba ambazo hazihesabiki**.

(Habwe, 2005, Ukur. 41)

Tunaambiwa kwamba Amuko sasa ana '**nyumba ambazo hazihesabiki.**' Hii ni chuku inayolenga kudhihirisha kiasi cha mali ya Amuko aliyoipata kutokana na ufisadi anaouendeleza ofisini. Maana ya '**nyumba ambazo hazihesabiki**' ni 'nyumba nyingi sana.' Mwandishi hatumii kauli 'nyumba nyingi sana' kwa sababu maneno hayo yasingemwathiri msomaji. Chuku inatokana na hali kwamba si sahihi kusema kuwa nyumba hazihesabiki. Nyumba ni faridi kubwa ambazo zinaweza kuhesabiwa. Lakini matumizi ya '**nyumba ambazo hazihesabiki**' yanalenga kuchimuza taswira ya nyumba nyingi sana. Msomaji anaweza akalinganua kiasi hiki cha ukwasi wa Amuko na umaskini wa raia wengi nchini ambao pesa zao ndizo zimetumika kuwatajirisha watu kama Amuko. Msomaji ataweza kuhisi hali hii isiyo ya haki. Amuko ametumiwa kama mfano tu wa viongozi serikalini wanaojilimbikizia mali kwa ufisadi. Ina maana kwamba ufisadi ni tatizo kubwa na ambalo mwandishi anajaribu kulipiga vita kupitia kwa kazi yake. Wanaojilimbikizia mali kupitia kwa ufisadi wanapata uwezo mkubwa wa kifedha, kama ule alio nao Amuko. Uwezo wake unadhihirika katika dharau yake kwa Mchungaji Michael. Anamwona mchungaji kama mtu asiye na chochote. Ni rahisi Amuko kutoa zawadi ya gari kwa Mchungaji Michael, gari ambalo ni dhahiri linatokana na ufisadi wake. Tabia ya kutafuta mali kama msingi wa mamlaka inapatikana miongoni mwa wachungaji na watu ambao sio viongozi wa kidini. Katika dondoo la 4 tunaona jinsi viongozi wa kidini wanavyohodhi mali katika kujaribu kujenga paradiso yao ya hapa duniani..

Kupitia kwa mhusika Michael, mwandishi anaonyesha kukinaishwa na vitendo visivyo vya kimaadili ambavyo vinaendelea katika jamii kama vile mauaji, ubakaji, wizi,

ufisadi, na kashfa. Anaonyesha kwamba vitendo hivi ni miongoni mwa hatari zilizomo katika jamii na vimezidi mno.

> 256. Huwezi kutazama televisheni huku ukila chakula **kwani utatapika**.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 56)

Chuku anayoitumia Michael ni kwamba ukiangalia televisheni wakati ukila chakula unaweza hata ukatapika. Chuku imejengwa katika kulinganisha vitu viwili: vitendo vinavyozungumziwa, yaani wizi, ubakaji au ufisadi kwa upande mmoja na kitendo cha kutapika. Kifiziolojia hivi sio vitendo ambavyo vinaweza kusababisha kitendo cha kutapika, ingawa vinaweza kusababisha hisia nyingine kama vile karaha au huzuni, lakini sio kiasi cha mtu kutapika. Hata hivyo, kwa vile chuku huwa inalenga maana fiche, tunaona kwamba Mchungaji Michael anaashiria hali ambapo watu wamekinaishwa kabisa na hali ya maovu yaliyokithiri katika jamii. Michael analinganisha kiwango cha vitendo visivyo vya kimaadili na kile cha Sodoma (dondoo la 263). Kanisa lina mamlaka fulani ya kuvipiga vita vitendo visivyo vya kimaadili kwa vile injili ina nguvu fulani ya kuweza kumbadilisha muumini kitabia.

6.1.7 Maswali ya Balagha

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013) inaeleza kwamba swali la balagha ni swali linaloulizwa kwa lengo la kusisitiza jambo fulani na ambalo halihitaji jibu. Michira (2018) anafafanua kwamba maswali ya balagha kwa kawaida hutumiwa katika tungo za kifasihi. Anaongezea kwamba badala ya kuhitaji majibu, masuali haya yanaulizwa ili kuonyesha mshtuko, kutosadiki, mshangao na wakati huo huo kuchochea fikira na mawazo. Huwa kuna maana ya ndani ya swali la balagha kuliko inavyoonekana kijuujuu.

Swali la balagha huvuta umakini wa msomaji na kumfanya afikirie juu ya umuhimu wa kitu fulani muhimu kinachosemwa. Msomaji anajiona kama kwamba ndiye anayeulizwa swali husika, na hivyo inabidi ajaribu kufikiria kwa undani jibu la swali ambalo anaulizwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Maswali ya balagha yanatumiwa na waandishi kuleta athari ya kidrama kwa vile ni kama kwamba yanachochea mawasiliano kati ya mwandishi na msomaji, pale ambapo msomaji anajaribu kulijibu swali lililooulizwa na mwandishi.

Katika riwaya ya *Paradiso*, kuna maswali ya balagha ambayo yameelekezwa kwenye suala la kashfa inayowahusisha wachungaji. Kashfa imeangaziwa sana katika riwaya hii ya *Paradiso*. Kuna kashfa ya Mchungaji Musa kufumaniwa akifanya mapenzi na Salome. Naye Askofu Boribori anapatikana katika kashfa ya ulanguzi wa madawa ya kulevya ambao ulianza katika uongozi wa Askofu Joshua. Michael naye anahusika katika kashfa ya mapenzi na Patricia.

257. **Ni nani asiyejua kashfa ya Michael pale iliyomhusisha Patricia?**
(Habwe, 2005, Ukur. 204)

258. **Lakini ni lipi ambalo James Boribori hajaungama?** Katika mambo aliyoungama Boribori ni kuwa ulanguzi huu ulianza na Joshua. Mkewe Joshua, marehemu Lona, ndiye aliyekuwa mharakati wa shughuli hii.
(Habwe, 2005, Ukur. 207)

Kuna kinaya ambacho kinadhihirika katika maswali ya balagha yanayoulizwa kuhusu kashfa makanisani. Makanisa ni mahali ambapo vitendo vya kashfa kama vile mapenzi nje ya ndoa, rushwa na ulanguzi wa madawa unakemewa. Lakini tunaona kwamba kashfa zimejaa kanisani. Kashfa inamhusisha hata Mchungaji Michael, ambaye katika riwaya ya *Paradiso*, amesawiriwa kama mchungaji kielelezo. Mwandishi anaonyesha kwamba kuna uozo katika asasi ya kanisa na dini. Vitendo visivyo vya kimaadili

vimezidi katika asasi hiyo. Akitumia swali la balagha kuhusu kashfa ya Michael na Patricia, mwandishi anaonyesha kuwa kashfa zinazowahusisha wachungaji zinajulikana wazi. Hata hivyo, wachungaji wana mamlaka makubwa kiasi kwamba juhudi za waumini za kuzungumzia au kukemea vitendo vya wachungaji zinakatizwa. Muumini akizungumzia mienendo ya mchungaji huenda akalazimika kuliondoka kanisa lake.

Tamaa ya pesa na mali inapelekea hata kashfa ya ulanguzi wa madawa katika kanisa. Mchungaji Boribori anahusika katika ulanguzi wa madawa ili kujiingizia pesa zaidi. Boribori anaendeleza ulanguzi ambao tunaambiwa ulianzishwa wakati wa uongozi wa binamu yake, Askofu Joshua. Katika swali "*Ni lipi ambapo Boribori hajaungama?*" mwandishi anaashiria kwamba Boribori tayari amefanya vitendo vingine visivyo vya kimaadili. Kitendo cha ulanguzi wa madawa ni mojawapo tu ya vitendo alivyovitenda. Mwandishi anaonyesha kwamba kanisa halijawa mfano mzuri wa mienendo mizuri kwa jamii.

Akitumia mbinu ya balagha, Habwe pia anaangazia suala la maana ya Ukristo. Mtazamo wa Mchungaji Michael ni kwamba maana ya kuwa Mkristo ni kuwa kama Yesu. Yeye anaazimia kuwa kama Yesu ambaye hakuoa wala hakuwa na familia.

259. **Au ina maana gani kuwa Mkristo? Si kuwa kama Yesu?**
(Habwe, 2005, Ukur. 44)

Michael anaona kwamba Yesu hakuwa na kwake, hakuwa na gari, nyumba, wala mke. Pia, Michael anatoa mfano wa Paulo ambaye alijitoa mhanga, na alifanya hayo yote kwa sababu hakuwa na familia iliyomshughulisha. Kwa hiyo, yeye anaona kwamba maana ya kuwa Mkristo ni kule kuiga mfano wa Yesu mwenyewe, kwa vile Yesu "Hakuwa na kwake. Hakuwa na gari. Hakuwa na mke. Hakuwa na nyumba" (Habwe,

2005, Ukur. 44). Michael hataki pia kujali vitu hivyo. Yesu hakuangalia umiliki wa mali kama msingi wa mamlaka. Katika kutumia maswali ya balagha tunayoyaona katika dondoo la 259, mwandishi analenga kukemea tamaa ya pesa na mali au vitu vya dunia. Tamaa ya vitu hivi ndiyo inayosababisha vitendo vingi visivyo vya kimaadili kama vile rushwa na ulanguzi wa madawa ambavyo mwandishi ameviangazia katika riwaya hii.

Mbinu ya balagha pia imetumiwa katika riwaya ya *Paradiso* kuangazia suala la unafiki ndani ya makanisa. Wokovu si wa kweli. Kuna watu ambao wanadai kwamba wameokoka lakini vitendo vyao haviakisi madai yao.

260. Siku hizi kila mtu anasema ameokoka. Lakini **ni wangapi waliookoka kweli?**
(Habwe, 2005, Ukur. 56)

261. **Kyalo alishangaa kama huwezi kumwamini mhubiri utamwamini nani?**
(Habwe, 2005, Ukur. 59)

Mwandishi anaashiria kwamba katika jamii, waliookoka kikamilifu ni wachache sana. Baada ya swali hilo mwandishi anaongezea maelezo haya: "Ulimwengu umejaa imani. Lakini huu ni unafiki mtupu!" (Habwe, 2005, Ukur. 56). Kwa mujibu wa mwandishi, inashangaza kwamba wahubiri, ambao wangekuwa mfano kwa waumini na kwa jamii kwa jumla, nao pia ni wanafiki tu. Wanawaambia watu wengine kuokoka ilhali wao wenyewe hawaokoki kikweli. Swali la Kyalo linaashiria kwamba hakuna ukweli tena katika jamii. Unafiki umekithiri katika jamii. Ni kinaya kwamba kuna wengi katika jamii wanaodai kuwa wameokoka ilhali ukweli umeadimika miongoni wa watu.

6.1.8 Haipofora

Hii ni aina ya tamathali ambapo mwandishi huuliza swali halafu akalijibu yeye mwenyewe moja kwa moja. Haipofora hutumiwa kumvuta msomaji kuzingatia kile

ambacho mwandishi anataka msomaji azingatie. Ni njia ya mwandishi kujibu maswali ambayo msomaji angejiuliza.

Haipofora imetumika katika riwaya ya *Paradiso* kuibua maudhui kwamba miujiza katika makanisa ya kiprotestanti kweli ipo. Inawezekana kwamba dhamira mojawapo ya mwandishi wa riwaya ya *Paradiso* ni kuonyesha kwamba baadhi ya miujiza katika makanisa ya kiprotestanti ni ya kweli; sio uongo.

> 262. Kuja kwa watu katika kanisa hili haikuwa bure. **Ni watu wangapi waliopata miujiza na baraka?**
>
> Musa pia alikuwa na sifa kubwa. **Ni watu wangapi waliopona mahali pale kupitia sala zake zilizotolewa kila siku ya Jumapili na Jumanne?**
>
> **Ni wanawake wangapi walioshika mimba baada ya huo mkutano? Ni wengi ajabu**!
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 30)

Inaonekana kwamba mwandishi anamshawishi msomaji kuamini kwamba miujiza katika makanisa ya kiprotestanti kweli ipo. Kwa kutumia mbinu ya haipofora katika dondoo 262, mwandishi anajaribu kupinga shutuma ambazo zimetolewa kwa makanisa ya kiprotestanti kwamba miujiza inayosemekana kufanyika katika makanisa hayo ni ya uongo. Miujiza na baraka ndizo baadhi ya sababu zinazowaleta watu kanisani na katika mikutano ya kidini. Kupitia kwa mbinu ya haipofora, mwandishi anathibitisha kufanyika kwa miujiza katika makanisa ya kiprotestanti. Hii inaashiria kwamba kuna watu wanaopinga kuwepo kwa miujiza hii, kama anavyosema, "tomaso ambao hawakuamini walishuhudia kwa kuona viwete wakitembea bila taabu." (Habwe, 2005, Ukur. 30).

6.1.9 Dokezo

Michira (2018) anaeleza kwamba dokezo ni mbinu ambapo kazi ya kifasihi hurejelea mahali, mtu au kitu ambacho kinajulikana katika matini za dini au za kidini, sayansi, siasa, historia, michezo au kitanzu kingine cha fasihi kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Kulingana na Wamitila (2003), dokezo ni mbinu ya urejelezi au ya kutaja kitu, hali, mhusika au tukio fulani kwa njia isiyo waziwazi.

Habwe anatumia mbinu hii katika riwaya yake ya *Paradiso* ili kuonyesha kwamba mambo mengi katika jamii yameenda kombo, na asasi ambayo ingesaidia kuyarekebisha, yaani kanisa – nayo imejaa vitendo visivyo vya kimaadili. Mwandishi anatumia dokezo kwa kuurejelea mji wa Sodoma, mji unaojulikana katika Biblia kama mji wenye dhambi kubwa ambao Mungu aliamua kuuteketeza kwa sababu ya dhambi hizo zilizozidi kiwango.

263. Ulimwengu wa leo umeshinda kile kiwango cha **Sodoma**.
(Habwe, 2005, Ukur. 56)

Sodoma (pamoja na Gomora) ni mji unaorejelewa katika Biblia ambao inasemekana Mungu aliuangamiza kwa sababu ya dhambi. Lakini kiulinganishi, mwandishi anasema kwamba ulimwengu wa leo unashinda Sodoma, mintarafu ya dhambi. Hii inaashiria kiasi cha kuzorota kwa maadili katika dunia ya leo. Mungu aliiteketeza Sodoma kwa sababu dhambi ilikuwa imezidi katika mji huo. Kwa hivyo, ikiwa katika ulimwengu wa leo hali ya maadili ni mbaya zaidi kuliko ya Sodoma, hiki ni kiasi kisichostahimilika. Labda ndio maana Michael anasema kwamba “huwezi kutazama televisheni huku ukila chakula kwani utatapika” (Habwe, 2005, Ukur. 56).

Uteketezaji wa miji ya Sodoma na Gomora ni ishara kwamba Mungu haiachi dhambi kuendelea bila kuwaadhibu wafanya dhambi. Hii inadokezwa katika mawazo ya mhusika Michael.

> 264. Michael aliona kifo cha Joshua na mkewe kama kile **kisa cha Sodoma na Gomora.**
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 134)

Michael anawalinganisha Askofu Joshua na mkewe Lona na miji ya Sodoma na Gomora. Analinganisha kuangamia kwa wachungaji hawa wawili na kuangamia kwa miji hiyo. Askofu Joshua na mkewe, Kasisi Lona wanafariki katika ajali ya gari. Michael anaona kwamba kuangamia kwa wachungaji ni adhabu kutoka kwa Mungu. Anaona kwamba Mungu amewaangamiza kwa sababu ya dhambi zao kuzidi mipaka. Ikiwa sababu ya kuangamia kwa miji ya Sodoma na Gomora ilikuwa ni dhambi kubwa isiyostahimilika kwa Mungu, hivyo hivyo Mungu hakuweza kustahimili dhambi za wahubiri hawa wawili (Joshua na Lona). Suala la ubinafsi katika *Paradiso* pia linajitokeza kupitia kwa mbinu ya dokezo. Wachungaji hawawajali kondoo (waumini), bali wanajijali wao wenyewe. Hii ni kweli kinzani kwa vile wachungaji wanatarajiwa kuwachunga kondoo wao.

> 265. [Michael] aliamini kasisi alipaswa kuwa mfano mwema kwa wale anaowaongoza. La sivyo atakuwa **kama kiongozi aliyezungumziwa katika Ezekieli 34** anayejiendeleza bila kuwazia kondoo wake.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 67)

Ni kama kwamba mwandishi anamdokezea msomaji kusoma sura hiyo yote. Katika sura hiyo, Mungu anasema kwamba wachungaji wamewatelekeza kondoo. Wachungaji wanakula vizuri na kuvaa vizuri lakini hawawajali kondoo. Hali hii tunaiona miongoni mwa wachungaji katika riwaya ya *Paradiso* ambapo wachungaji wamejitajirisha: wanavaa vitu vya bei, wanaendesha magari ya kifahari na kuishi katika nyumba nzuri,

wakati ambapo waumini ambao ndio wanaotoa zaka na matoleo mbalimbali kanisani wanahangaika na maisha kwa sababu ya ufukara.

Akitumia dokezo, mwandishi wa *Paradiso* pia anaibua maudhui ya unafiki. Wachungaji wanatenda kinyume na maneno au ushauri wao kwa waumini:

> 266. Musa alikuwa mkubwa wake [Michael] na ndiye ayemwonya dhidi ya **wanawake kama Delila**.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 49)

Katika Biblia, Delila ni mwanamke kahaba anayemsaliti Samson kwa kumshawishi atoe siri ya nguvu zake. Kisha Delila anawafunulia maadui zake Samson waliomtuma siri hiyo, ambao sasa wanamwangamiza Samson. Kinaya ni kwamba hata Musa, ambaye anamwonya Michael dhidi ya wanawake kama Delila, anahusika katika kashfa anapofumaniwa akifanya mapenzi na mke wa mtu. Musa ni mchungaji mashuhuri lakini anatenda tofauti kabisa na anavyowashauri wengine kutenda.

6.1.10 Matumizi ya Majina kama Ishara

Kulingana na Wamitila (2003) 'ishara' hutumiwa kuelezea kitu fulani katika kazi ya kifasihi ambacho huwakilisha kingine. Kuwakilisha huku kunaweza kutokana na uhusiano uliopo kati ya vitu hivyo viwili au uwezo wake wa kuibua fikira fulani katika akili ya msomaji. Naye Mbatiah (2001) anasema kwamba tunazifasiri ishara katika shairi, riwaya au tamthilia kwa kurejelea muktadha wake.

6.1.10.1 Mbinu ya Majazi

Michira (2018) anaeleza kwamba waandishi wakati mwingine huwapa wahusika majina yenye maana ya kiishara au hata yenye kinaya. Majina hayo huweza kuakisi au kukinzana na sifa, imani, au tabia za wahusika katika hadithi. Wamitila (2003) anaelezea majazi kama mbinu ya kuwapa wahusika majina ambayo yanaakisi au

yanatuelekeza kwenye wasifu wa tabia zao. Jina la mhusika linakuwa kielelezi cha tabia zake. Anasema kwamba majazi huhusisha pia majina ya mahali. Mwandishi anaweza kuitumia mbinu hii kuchimuza mtazamo na mwono wake kuwahusu wahusika fulani na hata mwelekeo wa hadithi nzima. Kwa hiyo, tunaona kwamba ni muhimu sana kuchunguza matumizi ya mbinu hii ya majazi, kwa vile majina ya wahusika yanatumika katika kuwasilisha maudhui katika kazi ya kifasihi.

6.1.10.1.1 Matumizi ya Aptronimu

Aptronimu ni majina yanayohusianisha wahusika na hulka zao. Yanaonyesha mawazo yao, vitendo wanavyovitenda na mielekeo yao.

6.1.10.1.1.1 Aptronimu katika Riwaya ya *Paradiso*

Lona: Lona ni mke wa Askofu Joshua. Naye pia ni kasisi katika kanisa la New Jerusalem. Maana ya jina Lona ni "simba mdogo wa kike." Tukichunguza mienendo yake katika riwaya tunaona kwamba jina hili ni stahiki kwa mhusika huyu. Linaambatana na maudhui anayoyawasilisha mwandishi kuhusu dini na mamlaka. Lona ni mjeuri sana na hamwogopi mtu yeyote. Katika riwaya ya *Paradiso*, mhusika huyu ametumiwa kusawiria maudhui ya tamaa ya pesa na mali, pamoja na mamlaka. Anapenda mali kama vile magari ya bei na kuishi katika maeneo ya kifahari. Aidha, Lona anajihusisha na siasa za nchi ili kupata upendeleo wa kisiasa. Hata hivyo, mwandishi anamtumia vilevile kutolea maudhui ya kijinsia kwamba, tofauti na wahusika kama Lydia na Patricia ambao wanakubali kwamba mwanamke ni kiumbe dhaifu akilinganishwa na mwanamume, Lona ni mwanamke ambaye anashindania nafasi yake na cheo katika jamii. Yeye pia ni kasisi katika kanisa la New Jerusalem na ana ushawishi mkubwa ndani ya kanisa hilo. Hata anamdhibiti mume wake Askofu Joshua. Mwandishi amempa sifa ambazo kwa kawaida huhusishwa zaidi na wanaume,

kama vile kuendesha gari kwa kasi na kutukana na madereva wengine. Huyu ni mwanamke mwenye mamlaka makubwa; si mtu wa kuchezewa na yeyote.

Joshua: Huyu ni Askofu wa kanisa lake mwenyewe – kanisa la New Jerusalem. Hili ni kanisa maarufu sana katika eneo la Kibera. Maana ya jina lake ni "Mungu ndiye wokovu." Analinganishwa na Joshua wa Biblia aliyefanikiwa kuwapeleka Waisraeli Kanaani. Lakini, mwandishi amempa jina hili Joshua wa riwaya ya *Paradiso* kimaksudi ili kumlinganua na Joshua kimaadili Biblia. Kinyume na Joshua wa Biblia, Joshua wa New Jerusalem amepungukiwa kisifa. Mwandishi amemtumia pia kuwasilishia maudhui ya utashi wa pesa na mali. Anamiliki magari ya kifahari na anasisitiza injili ya kwenda paradiso. Anahubiri injili ya utajiri ambayo haitawapeleka waumini katika paradiso. Hivyo, tofauti na Joshua wa Biblia, Joshua wa *Paradiso* ni mhusika ambaye hatawapeleka waumini kwenye paradiso ya Bwana, bali atawapeleka kwenye paradiso ya hapa duniani iliyojaa anasa.

Musa: Musa ni mchungaji wa ngazi ya juu katika kanisa la New Jerusalem. Yeye pia analinganishwa na Musa wa Biblia aliyewaongoza Waisraeli kutoka Misri kuelekea Kanaan, lakini ambaye hakufanikiwa kuwaingiza huko. Maana ya jina Musa ni "mtoto aliyeokolewa kutoka kwenye maji." Lakini, kama alivyo mchungaji mwenzake, Askofu Joshua, Musa pia ni kinyume cha Musa wa Biblia – kitabia. Anafumaniwa katika kitendo cha mapenzi na mke wa mtu. Baada ya tukio hilo, anaacha uchungaji na kuwa mfanyabiashara, hadi anapoishia kufilisika na kurukwa na akili. Kwa hivyo, mwandishi amemtumia kuwasilisha maudhui ya kashfa za ngono zinazowahusisha wachungaji. Wachungaji wenza kama vile Michael na Askofu Joshua nao wanahusika katika kashfa za ngono.

Michael: Maana ya jina hili ni "zawadi kutoka kwa Mungu." Kama jina lake linavyoashiria, Michael ni kama zawadi kutoka kwa Mungu kwa vile kwa jumla, yeye ni mchungaji kielelezo, ingawa kuna wakati ambapo anateleza akaingia kwenye dhambi ya uzinzi na pia akaanza kuvutiwa na kishawishi cha pesa na mali. Lakini, baadaye ananyanyuka tena kwa kufuata njia nyoofu ya Kikristo. Kwa kumtofautisha na wachungaji wengine akina Askofu Joshua na mkewe Lona, Musa Bosire na Boribori, mwandishi anaonyesha sifa za mchungaji kielelezo. Mwandishi amemtumia mhusika huyu kuibua maudhui ya mwema kuwa mui, ambapo Michael anabadilika na kuwa mtu mwenye tamaa ya pesa na mali na tena anashiriki katika mapenzi nje ya ndoa yake. Hata hivyo, mwandishi anamtumia vile vile kuwasilisha maudhui ya mui kuwa mwema kwa vile Michael anajirudi na kuanza kutenda mema tena. Kubadilika huku kunatoa ujumbe kwamba mtu yeyote anaweza akateleza na kuingia katika dhambi, lakini baadaye akarekebisha mienendo yake.

6.1.10.1.1.2 Aptronimu katika Riwaya ya *Nguvu ya Sala*

Riwaya ya *Nguvu ya Sala* ina wahusika wakuu wawili ambao ndio wanaoendeleza maudhui makuu ya riwaya hiyo. Wahusika hawa ni Richard Ngunze na binti yake Susan.

Richard Ngunze: Kuna mambo mawili kuhusu matumizi ya jina hili katika riwaya ya *Nguvu ya Sala.* Jina "Richard" linamaanisha "mtawala mwenye nguvu na ambaye ni shupavu." Richard ni mkali kwa vile anajaribu kujenga familia ambayo ni kielelezo cha familia ya Kikristo kwa majirani wote. Anaonekana kama mtu shupavu kweli. Hata hivyo, sifa hii inalinganuliwa na sifa yake nyingine ya udhaifu. Binti yake anaudhihaki ukali wake kwa kusema kwamba ukali huo kwa kweli ni udhaifu. Kuna maudhui ya kijinsia yanayosawiriwa kupitia kwa mhusika huyu ambapo tunaona jinsi

anavyoonyesha udume wake kwa kuwanyanyasa mke wake na mabinti zake, lakini tunaona pia jinsi ambavyo binti yake (au mwanamke) anamshinda kiakili katika hoja kuhusu maisha, mintarafu dhima ya nguvu ya sala katika kukabiliana na changamoto za maisha, hasa za kiuchumi. Kwa hivyo, Richard amesawiriwa kama mhusika mwenye mamlaka makubwa kwa upande mmoja katika familia lakini mwandishi amemtumia mhusika huyu pia kudengua mamlaka hayo kwa kumwonyesha kama mhusika dhaifu.

Susan Ngunze: Jina hili linamaanisha "ua la bondeni la aina ya yungiyungi." Kwa kupewa jina lenye maana hii, Susan ameonyeshwa kama ua ambalo linaweza likadhuriwa na ukali wa baba yake. Ua la yungiyungi linapendwa na watu wengi. Huyu ni mhusika ambaye mwandishi amemtumia kusawiria maudhui ya ushupavu na ujasiri wa mwanamke. Kinyume na mama yake, Susan anayakabili mamlaka ya baba yake (Richard) kwa ushupavu na ujasiri. Susan ni mhusika ambaye ametumiwa kuudengua msimamo wa baba yake kwamba nguvu ya sala ndiyo nguzo muhimu katika kukabiliana na changamoto za maisha.

6.1.10.1.1.3 Aptronimu katika Riwaya ya *Asali Chungu*

Zuberi: Ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Asali Chungu*. Mwanzoni mwa riwaya, mhusika huyu anatambulishwa kwa cheo chake tu cha 'Bwana DC' (Pia kama 'bwana'au 'Bwana Mkubwa'). Jina lake 'Zuberi' linatajwa katika ukurasa wa tatu wa riwaya hiyo. Maana ya jina 'Zuberi' ni "mwenye nguvu." Jina hili limeteuliwa na mwandishi kimaksudi. Kabla ya maisha yake kukumbwa na matatizo ya kiafya na uzee, Zuberi ni mhusika ambaye anaonyesha mamlaka makubwa. Ana mali, cheo, watumishi, na kila kitu ambacho anakitamani maishani. Mwandishi amemtumia kusawiria maudhui ya utajiri na uwezo wa watu kama Zuberi dhidi ya unyonge wa watu kama Semeni, Dude na Mzee Omari. Lakini mwandishi, kupitia kwa mhusika huyu, anaonyesha

kwamba mamlaka na unyanyasaji unaofanywa na makabaila kama Zuberi utakoma na watajutia vitendo vyao; yaani asali waliyoonja itageuka iwe chungu kwao.

Dude: Maana ya jina hili ni dhahiri kabisa. Dude ni 'mtoto haramu' wa Zuberi na Semeni ambaye anazaliwa kutokana na kisa cha Zuberi kumbaka Semeni. Sifa za udude wake zinatokana na mazingira ya kuzaliwa kwake na kukua kwake. Anakulia katika mazingira ya kimaskini kwa sababu mama yake ni fukara kabisa. Dude ni 'dude' tu, hana hata jina la pili. Mwandishi amemtumia mhusika huyu kuwasilishia maudhui ya unyonge kupelekea unyonge zaidi. Mama yake ni mnyonge au maskini; hivyo, Dude naye anaishi maisha ya unyonge baada ya kukosa rasilimali za kumwendeleza kimasomo. Pia, mwandishi amemtumia Dude kusawiri maudhui ya changamoto za kiuchumi zinazowakumba vijana wasio na ajira.

Bi Amina: Maana ya jina hili ni 'mtu msema kweli; mwaminifu'. Mwandishi ametumia mhusika mwenye sifa kinyume na maana ya kisemantiki ya jina lake. Kwa vyovyote vile, Amina si mwaminifu hata kidogo kwa mume wake Zuberi. Anafanya mapenzi nje ya ndoa. Mwandishi ametumia jina hili Amina kusawiri maudhui ya mlinganuo katika maisha ambapo vitu tunavyoamini kuwa ndio ukweli, sio ukweli kabisa. Amina siye mtu wa kuaminika. Lakini mwandishi amemsawiri kama mwanamke mwenye mamlaka au uwezo mkubwa. Ana gari la kifahari (*Vauxhall*) ambalo linafanana na la mume wake. Tena, ana ardhi kubwa kama ya mume wake pamoja na nyumba yake mwenyewe. Anafanya mapenzi nje ya ndoa, kama anavyofanya mume wake. Kwa vyovyote vile, huyu ni mhusika mwenye mamlaka makubwa. Hata hivyo, mamlaka aliyo nayo kama mwanamke yana kikomo pale ambapo yanakabiliana na utamaduni. Anashindwa kuizuia ndoa kati ya binti yake na Dude, kwa sababu kiutamaduni mwanamume ndiye

anayefanya uamuzi wa mwisho kuhusu jambo kama hilo. Uamuzi wa Zuberi kwamba Shemsa aolewe na Dude ndio unaoshinda.

Semeni: Huyu ni msichana ambaye anakulia katika mazingira duni kabisa. Anaajiriwa katika jumba la Zuberi kama mtumishi. Maana ya jina Semeni si dhahiri. Inawezekana ni kutokana na kitenzi 'sema' ambapo mwandishi anawaomba wasomaji waseme kitu kuhusu yaliyomfika msichana huyu. Au wanaotaka kusema na waseme, yeye hajali. Lakini kiundani, mwandishi huenda anarejelea kitendo cha unajisi alichofanyiwa na Zuberi pamoja na maisha ya kimalaya anayoyaishi. Mwandishi amemtumia mhusika huyu kuwasilisha maudhui ya umaskini na unyonge dhidi ya utajiri na uwezo wa watu kama Zuberi.

Biti Daudi: Maana ya jina Daudi ni "Mpendwa." Lakini, sehemu "biti" ina maana ya "binti yake Daudi." Huyu ni mwanamke wa makamo ambaye ni msimamizi wa wafanyakazi katika jumba la Bwana Zuberi. Anawanyanyasa watumishi wa kike wote. Ni mpendwa kwa Bi Amina na Zuberi – mume wake Amina vilevile, lakini siye mpedwa kwa wafanyakazi katika jumba la Zuberi kwa vile anawanyanyasa. Yeye ni mnyonge pia, lakini anasaidia katika unyanyasaji wa wafanyakazi wanyonge kama yeye. Ni mtu anayejipendekeza kwa matajiri.

6.1.10.1.1.4 Aptronimu katika Riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*

Fuad: Maana ya jina Fuad ni "dhamira." Linaashiria mtu mwenye huruma kwa wenzake. Lakini mwenendo wa Fuad katika riwaya hii ni kinyume kabisa na sifa hii ya ukarimu, yaani hana huruma yoyote kwa wafanyakazi wake na wakulima wanaolima kwenye shamba lake. Ni kabaila tajiri anayewanyonya tu wafanyakazi wake, siye mtu mwenye huruma.

Kijakazi: Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2003) ‘kijakazi’ ni mtumwa mwanamke. Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, Kijakazi anatenda kitumwa kama 'kijakazi’ kweli. Anazaliwa katika mazingira ya kitumwa na anaamini kwamba hayo ndiyo majaliwa yake. Anakubali kunyonywa na makabaila ambao hawamjali hata kidogo. Anaamini kwamba yeye hana mamlaka yoyote na kwamba kazi yake ni kuwatumikia makabaila. Lakini mwishoni, Kijakazi anang’amua kwamba yeye mwenyewe ndiye amejifungia katika utumwa. Anagundua kwamba ana uwezo wa kufanya maamuzi muhimu katika maisha yake.

6.1.10.2 Matumizi ya Toponimu

Toponimu ni majina ya mahali. Waandishi wametumia toponimu katika riwaya teule ya mahali kusawiria maudhui ya dini na mamlaka. Majina ya mahali yanafungamana na maelezo ya mwandishi kuhusu dini na mamlaka.

Katika riwaya ya *Paradiso* tunaonyeshwa wachungaji ambao, baada ya kutajirika wanahamia maeneo ya matajiri yenye usalama, tofauti na sehemu ya ovyo ya Kibera ambapo wachungaji hao wameanzisha makanisa na ambapo ndipo chanzo cha utajiri wao. Hiki ni kinaya. Ni kinaya mchungaji kujitenga na kondoo (waumini) anaowachunga. Wachungaji wamejitenga kimahali na kihadhi vilevile.

267. Katika kundi hili [la watu waliohudumu chini ya Joshua na Musa] ni **Michael pekee aliyekaa Kibera bado.**
(Habwe, 2005, Ukur.43)

268. Kutoka **Woodley** [Lona] alishuka barabara ya Joseph Kang’ethe na akaingia **Kibera Drive**. Hatimaye aliingia **Fort Jesus Estate** ambapo Michael alisogea baada ya kutoka **Kibera Matopeni**.
(Habwe, 2005, Ukur.68)

269. Musa naye alikaa **Buruburu**. **Pia** yeye **aliona** Mungu alikuwa amejibu maombi yake kwa kumpa nyumba. Musa alisema

> kuwa ilikuwa vizuri kukaa mahali pa usalama. **Kibera kulikuwa na fujo**.
>
> (Habwe, 2005, Ukur. 43)

Askofu Joshua na mkewe Lona wanaishi **Woodley** - sehemu ya kifahari ambapo matajiri huishi. Mchungaji Musa anaishi **Buruburu**. Naye Mchungaji Michael anaishi "**Fort Jesus Estate** ambapo alisogea baada ya kutoka Kibera Matopeni." Wachungaji hawa wote wanaihepa sehemu ya Kibera ambapo wameanzisha makanisa. Wanaliona eneo la Kibera kama eneo lisilo salama kwa vile sasa wao ni matajiri na wanahofia mali yao. Hata Michael, mchungaji kielelezo katika riwaya ya *Paradiso*, ambaye anasema kwamba anataka kuwa kama Yesu kwa kutomiliki mali, anahama kutoka **Kibera Matopeni** na 'kusogea' **Fort Jesus Estate**. Mwandishi ametumia majina ya mahali pa kifahari kimaksudi. Jina **Kibera Matopeni** linaleta taswira ya mandhari yasipofaa, kwa vile matope huhusishwa na uchafu. Ni eneo ambako mafukara wanaishi. Tofauti na Kibera Matopeni, jina Fort Jesus Estate linaleta taswira ya makazi yanayofaa, kwa vile Fort Jesus ni mtaa, sio sehemu ya ovyo kama Kibera.

Katika dondoo la 268 tunamwona Lona (mke wa Askofu Joshua) akishuka kisitiari kutoka huko mtaa wa kitajiri wa Woodley, akipitia Kibera Drive, na baadaye anaingia Fort Jesus Estate kwa Michael. Hii inaonyesha kwamba mtaa wa Woodley, ambako wachungaji Lona na mumewe Joshua wanakaa umejitenga sana kiuolezi na tena kisitiari na eneo la Kibera. Sababu anayoitoa Askofu Joshua (na mkewe Lona) ya kuhamia Woodley ni kwamba "Mungu alikuwa kambariki na gari la *Toyota* **aliona** ahamie mahali pa salama pa kuliweka hilo gari" (Habwe, 2005, Ukur. 43). Hapa tunaona kwamba anachokijali zaidi mchungaji huyu ni mali yake, siyo waumini anaowahudumia ambao wanakaa katika sehemu hiyo isiyo na usalama ya Kibera.

Mwandishi ametumia maneno yanayoonyesha kutoridhika kwake na hali hii ya wachungaji kujitenga na kondoo wao kwa ajili ya usalama. Mwandishi anasema: "Musa

naye alikaa Buruburu." "***Pia yeye aliona*** Mungu alikuwa amejibu maombi yake kwa kumpa nyumba." Kwa kusema: "Musa ***naye,***" mwandishi anamaanisha "kama alivyodai Musa." Halafu anasema '*pia yeye,*' yaani tena kama Joshua. Huu ni uchimuzi kwa njia ya msisitizo unaomfanya msomaji afikirie sababu zinazotolewa na wachungaji kujitenga na Wakristo wanaowahudumia. Kwa kutumia uchimuzi huo wa kiisimu, mwandishi anaonyesha kwamba sababu zinazotolewa na wachungaji hawa si halisi; ni visingizio tu. Pia, matumizi ya maneno: "Musa alisema kuwa" yanalenga kumwelekeza msomaji kwenye madai ya mchungaji huyo. Yanamfanya msomaji kuchukua mtazamo wa msimuliaji katika riwaya.

Habwe pia anatumia majina ya maeneo katika nchi za Ulaya na Marekani ili kuchimuza ukwasi wa wachungaji.

270. Licha ya akaunti, Boribori anawafungulia bima za maisha na za masomo katika shirika la Bima la **British Assurance**.
(Habwe, 2005, Ukur. 213)

271. Alikuwa na mtoto mvulana mmoja, Jim. Jim ashanunuliwa nyumba mbili **Marekani** katika mji wa **New York**.
(Habwe, 2005, Ukur. 213)

Katika dondoo la 270 tunaona kwamba Mchungaji Boribori anaweza kuwafungulia watoto wake wote bima za masomo katika shirika la bima la kifahari la **British Assurance**, sio shirika la kienyeji tu la ndani nchini (Kenya). Tena, amekwisha mnunulia mtoto wake wa kiume nyumba; sio moja tu, bali nyumba mbili **Marekani**. Hata sio Marekani tu, ila pia ni katika jiji kubwa kuliko yote Marekani – jiji la **New York**. Majina haya yote yametumiwa na mwandishi kimaksudi kwa ajili ya kuchimuza ukwasi wa wachungaji na kuulinganua na umaskini wa waumini wao.

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, unyonge wa watu maskini unalinganishwa na uwezo wa matajiri kupitia kwa mbinu ya toponimu. Mwandishi anatoa maelezo kuhusu makazi

ya watu maskini wa Ng'ambo. Majumba yao yamekaliana ovyo (Dondoo 163), kinyume na majumba ya makabaila kama Zuberi. Jina Ng'ambo limetumiwa kisitiari kudhihirisha kwamba kuna utengano mkubwa wa kiuchumi kati ya matajiri na maskini. Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013), maana ya neno ng'ambo ni upande wa pili wa mto au barabara. Pia, neno hilo lina maana ya 'nje ya mipaka ya nchi, hasa baada ya kuvuka bahari.' Hivyo, kwa kuwarejelea watu wa sehemu ya Ng'ambo, mwandishi anadhihirisha tofauti ya kiuchumi iliyopo kati ya raia wenye nacho kwa upande mmoja na raia wasio nacho kwa upande mwingine.

6.1.10.3 Majina ya Magari

Magari ni mojawapo ya vitu ambavyo vinadhihirisha ukwasi wa wachungaji na matajiri wengine. Kwa hivyo, katika riwaya teule, majina ya magari ya bei yametumiwa na waandishi kuakisi ukwasi wa kikundi kimoja cha raia tajiri na kukilinganua na kikundi kingine cha raia maskini hohehahe.

Katika riwaya ya *Paradiso*, mwandishi ametumia majina ya magari ya bei ili kuonyesha jinsi wachungaji wanavyoishi maisha ya starehe ya hapa duniani (paradiso ya hapa duniani), wakati ambapo wanahubiri kuhusu njia ya kwenda paradiso ya baadaye. Tena, wachungaji kama Askofu Joshua, katika injili yao ya maendeleo au utajiri, wanasisitiza umiliki wa magari kama ishara kwamba Mungu amezijibu sala zao kwa kuwabariki na magari. Umiliki wa magari ya bei umeakisiwa katika matumizi ya majina ya magari ya kifahari ambayo yanajulikana duniani kote:

272. Gari lake [Musa] sasa lilikuwa ***Range Rover***. Aliendeshwa na Bwana mmoja Rotino ambaye zamani alikuwa katika jeshi.
(Habwe, 2005, Ukur. 66)

273. Lona alishuka na gari lao la ***Toyota Land Cruiser***.
(Habwe, 2005, Ukur. 68)

.

274. Boribori na mwendakati wake pamoja na Judy walifurahi huku wakirudi nyumbani katika gari lao la ***Mercedes***.
(Habwe, 2005, Ukur. Habwe, 2005, Ukur.)

275. Gari lake alilolipenda [Joshua] ni ***Prado***. Madirisha yake yamepambwa kwa pazia maalum. Yeye alikaa kushoto dereva aliyestaafu kutoka jeshi akimwendesha.
(Habwe, 2005, Ukur. 221**)**

Katika madondoo 272 - 275 tunaonyeshwa majina ya magari ya kifahari wanayoyamiliki (magari) wachungaji. Mchungaji Musa anamiliki gari aina ya ***Landrover***. Askofu Joshua na mkewe Lona Bosire wana magari ya kifahari aina ya ***Prado*** na ***Toyota Land Cruiser***. Naye Boribori anamiliki gari la ***Mercedes****.* Hata naye Michael, ambaye si tajiri sana, anamiliki gari la *Toyota.* Magari haya yote ni ya bei ya juu. Wachungaji wamezingatia zaidi umiliki wa mali za dunia na kutochukulia kwenda paradiso kama kipaumbele. Wachungaji wanatumia mbinu kadha za kupata pesa ili kuweza kujinunulia magari haya ya kifahari. Wanasisitiza aina kadhaa za matoleo kanisani: zaka, sadaka, fungu la kumi, na matoleo mengine ili kuwafanya waumini watoe pesa. Katika dondoo la 73, tunaona lugha inayotumiwa kuwalazimisha waumini kimbinu kutoa pesa kanisani. Wakati ambapo wachungaji 'wanabarikiwa' na Mungu kwa magari ya bei, waumini wanaohubiriwa injili ya utajiri wanabaki maskini. Kinaya ni kwamba zaka na matoleo hayo mengine yanatoka kwa watu maskini wa Kibera.

Mtazamo wa Habwe kuhusu maisha ya utashi wa magari wa wachungaji unadhihirika katika maelezo yake kuhusu tamaa ya wachungaji ya magari. Katika dondoo la 275 mwandishi anasema: "**gari lake alilolipenda**," ikiashiria kwamba Askofu Joshua anamiliki magari mengine ya bei ambayo hayahitaji. Zaidi ya gari hilo la *Prado* kuwa ni la bei, madirisha yake "**yamepambwa kwa pazia maalum,**" yaani sio pazia la kawaida. Na akiwa katika gari hilo, yeye "**akikaa kushoto [huku] dereva aliyestaafu kutoka jeshi akimwendesha**." Hapa Askofu Joshua analinganishwa na viongozi wa

ngazi za juu serikalini, kama vile marais na mabalozi wanaokaa kushoto huku ‘wakiendeshwa.” Askofu Joshua haendeshwi na dereva wa kawaida tu, bali anaendeshwa na dereva aliyestaafu kutoka jeshi. Msisitizo umewekwa kwenye hadhi ya mtu anayeendeshwa, siyo gari. Mwandishi angesema: “dereva… **akiliendesha gari**.” Baada ya kutoa maelezo kuhusu ufahari wa gari la Askofu Joshua, mwandishi sasa analenga waliomo garini: mmiliki wa gari na dereva wake. Maelezo haya yote yanaonyesha uwezo mkubwa wa Askofu Joshua na utashi wake wa cheo na mamlaka.

Tunaona umiliki wa magari kama ishara ya uwezo wa mtu vilevile katika riwaya za *Kasri ya Mwinyi Fuad* na *Asali Chungu* ambapo mabwana shamba na watawala wanamiliki magari ya kifahari. Hivyo, katika kusisitiza umiliki wa magari, viongozi wa kidini kama tunavyoona katika riwaya ya *Paradiso*, wanatenda kama wanavyotenda matajiri wengine wa kilimwengu.

276. “Ala! Kwani kesho wanakuja?” Bibi Maimuna alijidai kustaajabu kama kwamba hakujua kuwa kila Jumapili Bwana Zein na mkewe huja kwa **gari lao jipya** la aina ya **May flower** kuwatembelea

(Shafi, 1978, Ukur. 6)

277. Siku chache baadaye, Fuad alinunua **gari kubwa** la aina ya ***Rambler*** lenye rangi ya bahari.

(Shafi, 1978, Kur. 24 -25)

278. Nguzo za umeme na simu zilikumbwa nyuma pale ***Vauxhall* ya kijani** ilipokuwa ikitafuna masafa yaliyobaki kabla ya kufika Maungani.

(Mohamed, 1977, Ukur. 89)

279. Nyuma ***Vauxhall* nyengine ya maziwa** ilikuwa imeshafika, na dereva wake Hassani…

(Mohamed, 1977, Ukur. 95)

Mbali na mashamba makubwa, makabaila wana magari. Katika dondoo la 276 kutoka katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* tunaona kwamba Bwana shamba Zein na mkewe wana gari jipya la ***May Flower***. Fuad ana gari kubwa aina ya ***Rambler***. Naye

Zuberi na mkewe Amina – kila mmojawao ana gari aina ya ***Vauxhaul***. Wamiliki hawa wote wa magari si watu wa kawaida, bali ni watu wenye nacho. Watu wengi wa kawaida huwa hawawezi kuhimili gharama za kununua na kutunza magari kama haya. Ufahari wa magari haya umechimuzwa kwa kutolewa maelezo ya ziada. Gari la Bwana Zein na mke wake ni '**jipya**' '**aina ya May Flower.**' Nalo gari la Fuad ni '**kubwa**' la 'aina ya ***Rambler***,*'* 'lenye rangi ya bahari.' Katika riwaya ya *Asali Chungu*, Bwana Zuberi anamiliki ***Vauxhaul*** '**ya kijani**', wakati ambapo mkewe anamiliki ***Vauxhaul*** '**ya maziwa.**' Umiliki wa magari unaambatana na uwezo wa kifedha walio nao mabwana shamba.

6.2 Muhtasari wa Sura

Sura hii imejadili nduni za kitamathali za kimtindo zilizotumika katika kusawiri maudhui mbalimbali kuhusu dini na mamlaka katika riwaya teule za Kiswahili. Maudhui makuu yaliyosawiriwa kwa mbinu za kitamathali katika riwaya zote teule ni yale ya unyonge na uwezo. Riwaya ya *Asali Chungu* ndiyo ambayo imeangazia maudhui haya zaidi. Mohamed na Habwe wametumia sitiari hasa kusawiri maudhui haya, tofauti na Wamitila na Shafi, ambao wametumia kejeli zaidi. Tamathali za balagha, dokezo na haipofora hazikutumika sana katika riwaya teule, mintarafu ya masuala ya dini na mamlaka. Waama, mbinu hizi zimetumika katika riwaya ya *Paradiso* peke yake. Kwa jumla, kati ya waandishi wa riwaya teule, Habwe ndiye mwandishi ambaye ametumia karibu tamathali zote za usemi, isipokuwa tamathali za tashihisi na kejeli. Kwa hiyo, inabainika kwamba Habwe ndiye anafanikiwa zaidi katika kuwasilisha ujumbe wake kwa msomaji kwa kutumia lugha ya kitamathali. Sura inayofuata inabainisha muhtasari, mahitimisho ya utafiti huu, pamoja na mapendekezo kwa tafiti za baadaye.

SURA YA SABA

MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

7.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchanganua kimtindo masuala ya dini na mamlaka katika riwaya teule za Kiswahili kwa kuzingatia viwango vya kiisimu vya kileksika, kisintaksia na kisemantiki. Riwaya hizo teule ni *Paradiso* ya John Hamu Habwe, *Nguvu ya Sala* ya Kyallo Wadi Wamitila, *Asali Chungu* ya Said Ahmed Mohamed na *Kasri ya Mwinyi Fuad* ya Shafi Adam Shafi. Tumechunguza jinsi waandishi wanavyotawala lugha kiisimu ili kuibua maudhui mintarafu viwango vya kiisimu vilivyobainishwa. Viwango hivyo ndivyo vinavyojenga msingi wa malengo ya utafiti huu.

Nadharia ya Uchimuzi ndiyo iliyoongoza ukusanyaji na uchanganuzi wa data ya utafiti huu, tukizingatia mihimili yake ya ukiushi na usambamba, yaani madondoo yaliyochaguliwa kutoka riwaya teule ni yale ambayo yalikuwa na tungo zilizodhihirisha ukiushi au usambamba. Data ilikusanywa na kuchanganuliwa mintarafu ya malengo ya utafiti huu, yaani kwa kuzingatia nduni za kileksika, za kisarufi na za kitamathali. Uchambuzi wa data ulibainisha kwamba mbinu za urudiaji kama njia ya kusisitizia ujumbe pamoja na sitiari zilitumiwa sana na waandishi wa riwaya teule katika kusawiri maudhui. Motifu ya unyonge dhidi ya uwezo wa kiuchumi pamoja na masuala ya kijinsia yalijitokeza katika riwaya zote teule.

7.2 Mahitimisho ya Utafiti

Katika utafiti huu tulichunguza jinsi waandishi wa riwaya teule za Kiswahili wanavyotawala mbinu za lugha ili kuibua maudhui tofauti tofauti. Katika kutekeleza azma hiyo, utafiti huu uliongozwa na malengo matatu mahsusi: kuchanganua uteuzi wa kileksika kama nduni ya kimtindo katika kusawiri maudhui katika riwaya teule;

kuchanganua nduni za mtindo za kisintaksia zilizotumika katika kusawiri maudhui katika riwaya teule; kujadili nduni za kimtindo katika tamathali za usemi zilizotumiwa kusawiri maudhui katika riwaya teule.

Katika sehemu inayofuata tunajadili mahitimisho ya utafiti mintarafu kila lengo. Ingawa tumezitenganisha mbinu hizi kulingana na jinsi zinavyojitokeza, kuna mwingiliano kati ya mbinu hizi kwa vile zote ni mbinu za lugha. Kwa mfano, usambamba wa kisintaksia wakati mwingine unahusisha pia urudiaji wa leksimu. Tena sitiari inaweza ikahusisha usambamba wa kisintaksia.

7.2.1 Uteuzi wa Kileksika kama Nduni ya Kimtindo katika Kuchimuza Maudhui katika Riwaya Teule

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza uteuzi wa kileksika kama nduni ya kimtindo katika kuchimuza maudhui katika riwaya teule za Kiswahili. Uchunguzi huu uligundua kwamba waandishi wametawala lugha kileksika kupitia mbinu mbalimbali ili kuibua maudhui tofauti. Mbinu hizo ni pamoja na visawe, uhamishaji wa nomino kutoka ngeli moja hadi nyingine, urudiaji, kinyume, matumizi ya vitenzi vya kitathmini, matumizi ya vitenzi vya kitambuzi, na uolezi. Mbinu hizi zote zimetumiwa kuuchimuza ujumbe wa waandishi.

Miongoni mwa waandishi ambao kazi zao tumezichunguza, Habwe (2005) ndiye anayetumia mbinu zote za kileksika zilizotajwa. Hii inaweza kuashiria kwamba Habwe anawasilisha ujumbe wake kwa msomaji kwa njia madhubuti zaidi tukilinganisha na waandishi wengine wa riwaya teule tulizozichunguza. Hata hivyo, mbinu ya kileksika ambayo Habwe ameitumia zaidi ni vitenzi vya kitathmini. Mbinu hii ameitumia hasa katika kusawiri maudhui ya tamaa ya pesa, pamoja na kuonyesha mitazamo ya kijinsia. Kwa vile mbinu hii ya vitenzi vya kitathmini imetumiwa kuibua maudhui haya,

tunaweza kuhitimisha kwamba mwandishi anayachukulia masuala hayo kuwa ni ya msingi.

Mbinu kuu ya kileksika ambayo imetumiwa na waandishi wa riwaya zote katika utafiti huu ni urudiaji. Urudiaji huu unatokea katika vifungu vya aya na wakati mwingine hata katika sehemu mbalimbali za riwaya. Katika riwaya ya *Paradiso*, Habwe ameitumia mbinu hii kudhihirisha maudhui ya umuhimu wa msamaha kwa waumini. Pia, ametumia urudiaji kusawiri maudhui ya utashi wa uongozi na mamlaka. Katika riwaya za *Asali Chungu* na *Kasri ya Mwinyi Fuad* waandishi wametumia urudiaji kusisitiza maudhui ya tatizo la ukosefu wa kazi pamoja na unyonyaji.

Kati ya riwaya nne tulizozichambua, usawe wa kileksika umetumika katika riwaya tatu za *Paradiso*, *Nguvu ya Sala* na *Asali Chungu* kusawiri maudhui ya dini na mamlaka. Hata hivyo, riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* haitumii mbinu hii. Usawe uliotumika unahusisha visawe katika kifungu mahsusi, aya, na tena katika kurasa au sura tofauti za riwaya. Upangaji wa visawe katika aya moja unaashiria msisitizo zaidi na jazba ya mwandishi kuhusu suala analolizungumzia kuliko upangaji ambapo visawe vinajitokeza katika kurasa tofauti za riwaya.

Waandishi wa riwaya za *Paradiso* na *Nguvu ya Sala* wametumia mbinu ya udunishaji wa nomino au matumizi ya nomino za ngeli ya 7/8 ambazo zinachukuliwa kama nomino zenye uduni fulani (ingawa uainishaji wa nomino kisemantiki hauzingatiwi siku hizi). Mbinu hii haikutumiwa na waandishi wa riwaya za *Asali Chungu* na *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* mbinu hii imetumika kuibulia maudhui ya ukatili na uonevu yanayotokana na ugumu wa maisha katika sehemu za mijini. Naye Habwe, ametumia mbinu hii kuonyesha kwamba kuna unafiki katika madhumuni ya watu wanaokimbilia injili makanisani.

Riwaya za *Asali Chungu* na *Paradiso* zimetumia mbinu ya kileksika ya uhamishaji wa nomino kutoka ngeli moja hadi nyingine ili kusawiri maudhui kuhusu tofauti za kiuchumi kati ya maskini wanyonge na matajiri wenye uwezo. Katika riwaya zote mbili, mbinu hii ya uhamishaji wa nomino inahusisha faridi 'pesa.' Pesa ndiyo faridi inayomtofautisha maskini na tajiri mintarafu kiwango cha maisha. Katika *Paradiso* kuna maudhui ya pesa kupewa kipaumbele na wachungaji, badala ya paradiso au neno la Bwana. Katika riwaya ya *Asali Chungu*, mhusika mmoja (Bi Mwanakweli) anataja kwamba "ukiwa na pesa una kila kitu." Mwandishi anaonyesha jinsi ambavyo matajiri wenye pesa wana karibu kila kitu.

Riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad,* tofauti na riwaya nyingine teule haikutumia sana mbinu za kileksika. Badala yake, Shafi ametumia zaidi mbinu ya uolezi ambayo anaitumia kusawiri maudhui ya mabadiliko yanayohusisha mwenye mamlaka kupoteza mamlaka yake, na mnyonge kupata mamlaka. Mwandishi anaonyesha kwamba hii inawezekana ikiwa mnyonge anaweza kuungana na kushirikiana na mnyonge mwenzake ili kuleta mabadiliko. Mamlaka wala unyonge sio hali za kudumu.

Mbinu ya matumizi ya msamiati wa kitathmini imetumiwa zaidi katika riwaya za *Paradiso* na *Nguvu ya Sala*. Katika riwaya hizi mbili msamiati wa kitathmini umetumiwa kuonyesha kategoria mbili za wanawake: mwanamke aliyeikubali nafasi ya kuwa mke tu wa nyumbani anayopewa na utamaduni pamoja na hoja za kidini kwa upande mmoja (Lydia na Patricia katika *Paradiso*, na Mary Kasiva katika *Nguvu ya Sala*) na mwanamke ambaye ameikataa nafasi hiyo na ameamua kushindania usawa wa kijinsia katika jamii (Lona katika *Paradiso*, na Susan katika *Nguvu ya Sala*).

7.2.2 Matumizi ya Nduni za Kisintaksia katika Kuchimuza Maudhui katika Riwaya Teule

Lengo la pili lilikuwa ni kuchanganua matumizi ya nduni za kisintaksia katika kuchimuza maudhui katika riwaya teule. Kuhusu lengo hili, tulizingatia mbinu ya usambamba hasa, kama mhimili wa Nadharia ya Uchimuzi uliotumika kuchimuzia maudhui katika riwaya teule. Mbinu mahsusi za kisintaksia zilizotumiwa na waandishi wa riwaya teule kusawiria maudhui katika riwaya teule ni pamoja na anafora, epifora, tanakuzi, mjalizo, usambamba kiusawe, mgeuko wa polepole, urudiaji, udondoshaji, matumizi ya kauli ya kutendwa kimtindo, na uorodheshaji.

Kati ya mbinu za kisintaksia zilizotajwa, mbinu iliyotumiwa na waandishi wote ni usambamba kiusawe. Usawe wa aina hii unatumia kauli zinazolingana kimatumizi, ingawa maana zake ni tofauti. Mbinu ya usambamba wa kiusawe inaleta msisitizo fulani wa suala linalozungumziwa na mwandishi wa kazi ya kifasihi kwa vile ni njia ya kuchimuzia ujumbe wa mwandishi. Msomaji anaweza akauzingatia usawe katika kufasiri uamilifu au maana ya matumizi ya tungo zenye usawe wa kiusambamba. Kwa hivyo, waandishi wa riwaya teule wanaweza kufikisha ujumbe wao kwa msomaji kwa ufanisi mkubwa kupitia mbinu hii ya kisintakia. Hii ni kwa sababu tunapata kauli zaidi ya moja zinazofafanua jambo lile lile. Hata hivyo, Mbali na mbinu ya usambamba wa kiusawe, mbinu ya anafora nayo imetumiwa sana na waandishi wa riwaya teule.

Wakati mwingine, tungo zile zile zinaonyesha uchimuzi kwa mbinu tofauti za kisintaksia. Kwa mfano, mbinu ya usambamba wa kiusawe inahusisha pia matumizi ya vitenzi vya kauli ya kutendwa, ambavyo vimechimuzwa katika muktadha fulani.Hii inaonyesha kwamba mbinu tofauti za kisintaksia zinaweza zikaingiliana katika kuyasawiri maudhui fulani.

Katika uchanganuzi wa data iliyokusanywa kutoka katika riwaya teule, imegundulika kwamba urudiaji wa vishazi kiusambamba unatokea mara mbili hadi mara saba, ingawa urudiaji unahusisha hasa mara kati ya mbili na tano. Urudiaji mara nyingi unalenga kusisitiza jambo linalozungumziwa. Msisitizo huu unaweza kuwa na lengo la kushawishi. Pia, urudiaji wa vipashio mara kadhaa unaonyesha jazba. Unaonyesha kwamba jambo linalozungumziwa linamwathiri sana mwandishi au mhusika kiasi kwamba anaamua kutumia miundo yenye urudiaji mara kadhaa.

Wamitila ametumia mbinu ya usambamba unaohusisha mpangilio wa kishairi katika riwaya yake ya *Nguvu ya Sala*. Lakini ameutumia mara moja tu. Hivyo, hatuwezi kusema kuwa hii ni sifa ya kimtindo ya riwaya hii. Mbinu hii haikutumika katika riwaya zingine teule. Wamitila ametumia mpangilio huu wa kishairi ili kutaja vitendo visivyo vya kimaadili na matatizo mbalimbali yanayoikumba jamii, kwa mfufulizo. Mfululizo huo unavifanya vitendo hivyo kusikika kwamba vimezidi. Hili ndilo kusudi la mwandishi. Mtindo huo wa kishairi unaketa ridhimu fulani inayomvuta msomaji na hivyo kumsaidia mwandishi kuwasilisha ujumbe wake kwa msomaji huyo. Vitendo hivyo vinavyotajwa kwa mtindo wa kishairi ni ukatili, uzinzi na ukahaba, ukosefu wa ajira na mimba zisizotakikana, vita na ukosefu wa amani duniani. Ingawa mambo hayo yangeweza kutajwa kwa kutumia sentensi mbalimbali au kwa kuyaorodhesha, mwandishi anaamua kutumia tungo zilizopangwa kishairi, lakini ambazo zinaonyesha usambamba fulani.

Tena, hata kwenye matumizi ya mbinu za kisintaksia, Habwe ndiye anayetumia mbinu nyingi zaidi za kisintaksia, kati ya zile zilizobainika katika riwaya teule isipokuwa mbinu ya mgeuko wa polepole na mbinu ya muundogeu. Hii inamaanisha kwamba mwandishi huyu amejitahidi vilivyo kuufikisha ujumbe wake kwa msomaji kupitia kwa

mbinu anuwai za kisintaksia. Riwaya ya *Paradiso* imetambulika kuwa na mtindo wa ukwasi wa mbinu za lugha kuliko riwaya zingine teule.

Ili unaotumia mbinu mbalimbali za kisintaksia usimchoshe msomaji, udondoshaji unatokea sana katika urudiaji wa kianafora na wa kitanakuzi. Hapa tunazungumzia udondoshaji wa vipashio ambavyo vingerudiwa, kama muundo wa kirai au kishazi cha awali ungedumishwa katika vipashio vinavyofuata. Vipashio vinavyodondoshwa ni vile ambavyo vishatumika, na kwa hivyo vinatabirika. Vifaa vya mshikamano vikizidi sana, msomaji atachoka na kukinaishwa. Hii inaweza ikamfanya aamue kutoendelea kuisoma kazi husika. Urudiaji wa kiubunifu unaweza kuivuta nadhari ya msomaji, lakini usipotumiwa vizuri, unaweza kuwa na matokeo ambayo ni kinyume cha kusudi la mwandishi. Msomaji ni kiungo cha msingi katika kuikamilisha kazi ya kifasihi. Asipoisoma, akaifasiri na kuelewa yaliyomo, kazi hiyo itakuwa haijakamilika.

Katika usambamba wa kianafora, kiepifora, kitanakuzi na kimjalizo, kishazi cha mwisho katika mpangilio wa kianafora kinaweza kuongezewa maelezo ambayo yanakifanya kiwe tofauti kimuundo na vishazi vinavyokitangulia. Katika riwaya ya *Paradiso* tunaona jinsi ambavyo Habwe anatoa maelezo ya ziada katika kishazi cha mwisho katika mpangilio wa kianafora na kitanakuzi katika baadhi ya tungo. Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* mwandishi anaongezea maelezo kwenye kishazi cha mwisho katika tungo mojawapo yenye mpangilio wa kiepifora. Maelezo haya yanaonyesha msisitizo ambao mwandishi anauweka kwenye taarifa iliyoko kwenye kishazi hicho cha mwisho chenye maelezo ya ziada. Kishazi hicho kinakuwa na uzito fulani kuliko vishazi vilivyokitangulia na kwa hivyo, ndicho kinachobeba wazo kuu la mwandishi wa riwaya kwa mujibu wa suala husika.

Katika riwaya zote teule, mbinu za kisintaksia za mgeuko wa polepole, muundogeu, pamoja na mjalizo hazikutumika sana. Mbinu ya mgeuko wa polepole imetumika mara nne tu katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* peke yake. Nayo mbinu ya mjalizo imetumiwa mara mbili tu katika riwaya ya *Paradiso*. Kutotumika sana kwa mbinu hizi huenda kunatokana na hali kwamba miundo hii ni nadra katika matumizi ya lugha kwa jumla, hasa muundogeu.

7.2.3 Matumizi ya tamathali za usemi kama mbinu za kimtindo katika kuchimuza maudhui katika riwaya teule

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza matumizi ya tamathali za usemi kama mbinu za kimtindo katika kuchimuza maudhui katika riwaya teule. Tamathali kadhaa za usemi zimetumika katika riwaya teule, mkiwemo uhuishaji, sitiari, tashbihi, tasfida, chuku, dokezo, kinaya na kejeli. Kuhusu lengo hili, utafiti huu umegundua yafuatayo:

Sitiari ndiyo tamathali ya usemi ambayo imetumiwa zaidi na waandishi wote wa riwaya teule kuibua maudhui ya dini na mamlaka hasa katika riwaya ya *Paradiso*. Kwa vile sitiari hujitokeza zaidi katika matumizi ya lugha kuliko tamathali nyingine, inaweza ikachukuliwa kwamba hii ndiyo mbinu inayofaa zaidi ya kuwasilishia ujumbe kwa msomaji.

Kejeli ni tamathali ambayo imejitokeza sana katika riwaya za *Nguvu ya Sala* na *Kasri ya Mwinyi Fuad*, ingawa imetumika zaidi katika *Nguvu ya Sala*, kwa mujibu wa motifu ya mwandishi ya kumkweza mhusika wa kike kwa/na kumtweza mhusika wa kiume. Katika *Nguvu ya Sala*, anayekejeliwa ni Richard ambaye anaonekana kuwa na mamlaka makubwa, kama mwanamume, lakini anayedhihakiwa na binti yake, kama njia ya kuweka wazi udhaifu wake kama mwanamume. Kejeli imetumika kuudhihaki

msimamo wa Richard kwamba ‘nguvu ya sala’ ndiyo iliyo na uwezo wa kukabiliana na matatizo ya ulimwenguni, msimamo ambao binti yake Susan anaudengua kwa hoja madhubuti. Mwandishi amekusudia kupiga vita taasubi ya kiume kwa kumwinua mwanamke. Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, kejeli imetumika kukejeli mamlaka ya kabaila Fuad na pia kukejeli hali yake ya kuyapoteza mamlaka kwa wanyonge.

Mbinu za chuku, balagha, dokezo na haipofora zimetumika katika riwaya ya *Paradiso* peke yake. Hata katika matumizi ya tamathali za usemi, Habwe ndiye anayetumia tamathali za usemi karibu zote. Hii inatokana na maudhui anuwai anayoyasawiri katika riwaya yake. Pia, inaonekana kwamba zile tamathali ambazo ni za kawaida sana hata katika lugha ya kawaida ndizo ambazo zimetumika zaidi katika riwaya teule, yaani sitiari na tashbihi.

Kupitia kwa tamathali za usemi, riwaya zote zimeangazia maudhui ya umaskini dhidi ya utajiri. Riwaya za *Asali Chungu* na *Kasri ya Mwinyi Fuad* ndizo hasa zimeangazia maudhui haya zaidi. Tamathali ambazo zimezingatiwa katika kutoa maudhui haya hasa ni sitiari, tashibihi, tashihisi, kinaya na kejeli. Ili kutoa maudhui haya, mwandishi wa *Asali Chungu* ametumia sitiari, tashihisi na kinaya hasa wakati ambapo mwandishi wa *Kasri ya Mwinyi Fuad* ametumia tashibihi, kinaya na kejeli hasa. Hii ina maana kwamba *Asali Chungu* kwa kiasi kikubwa inaelezea jinsi unyonge na utajiri ulivyo katika jamii. Nayo *Kasri ya Mwinyi Fuad* inaudhihaki utajiri na mamlaka, zaidi ya kueleza jinsi utajiri unavyojitokeza.

Imebainika kuwa katika riwaya zote teule (isipokuwa riwaya ya *Nguvu ya Sala*) majina ya magari yametumika kama ishara ya utajiri na uwezo. Katika riwaya ya *Paradiso*, tunaona jinsi ambavyo wachungaji wanamiliki magari ya bei ambayo wanayapata

kutokana na zaka inayotolewa na waumini maskini wa eneo la ovyo la Kibera. Nazo riwaya za *Asali Chungu* na *Kasri ya Mwinyi Fuad* zinatuonyesha jinsi ambavyo makabaila wanavyomiliki magari ya bei wakati ambapo raia wa kawaida – wafanyakazi wao na wakulima ni maskini kabisa. Majina ya magari ya bei kama vile *Rambler, Land Cruiser, Range Rover*,na *Mercedes Benz* ndiyo yametumika. Haya sio magari ya kawaida tu ila ni magari ya bei na ya ufahari, na hii ndiyo inayoweka bayana pengo la kiuchumi lililopo kati ya matajiri na maskini ambalo waandishi wameliangazia katika riwaya zao.

7.3 Mchango wa Utafiti Huu

Utafiti huu ulichunguza masuala ya msingi katika riwaya teule za Kiswahili kwa kutumia mkabala wa elimumitindo. Tulichunguza jinsi waandishi walivyotumia lugha ili kuibua maudhui mbalimbali kupitia mbinu tofauti. Kwa undani, waandishi wa riwaya tulizozichunguza wameangazia asili ya masuala tunayokumbana nayo katika jamii zetu hata siku hizi kama vile suala la unyanyasaji na usawa wa kijinsia, ufukara, ufisadi, na uhalifu hasa mijini. Utafiti huu umesaidia kusisitiza kwamba waandishi wa kazi za kifasihi, kwa mfano, riwaya zilizoteuliwa katika uchunguzi huu hawaandiki katika ombwe tupu, bali huangazia masuala ambayo ni ya muhimu kwa wanajamii au hadhira lengwa na wasomaji kwa jumla waonapo kwamba kuna masuala nyeti au ya muhimu yanayowagusa wao kama waandishi. Hii ni njia ya waandishi kujaribu kuhamasisha hadhira lengwa na wasomaji kwa jumla kuchochea mabadiliko katika fikira na labda pia mabadiliko katika mienendo ya watu katika jamii na watu binafsi. Kwa jumla, utafiti huu umejadili mwambatano kati ya masuala ibuka na maisha kwa jumla. Hili ni jambo muhimu ambalo halijaangaziwa sana na watafiti wengine.

Data ambayo imekusanywa katika utafiti huu inaweza kutumiwa kuchunguzia masuala haya kwa kulenga suala mahsusi ambalo limeangaziwa na waandishi wa riwaya teule. Kwa mfano, inabainika katika data tuliyoikusanya katika utafiti huu kwamba suala la jinsia, hasa nafasi ya mwanamke katika jamii limejitokeza sana. Suala hili la jinsia linaweza likachunguzwa kwa kutumia data tuliyoikusanya kwa mkabala huu huu wa kimtindo au kwa kutumia mkabala tofauti, kama vile uchanganuzi wa usemi.

Utafiti huu umesisitiza mkabala wa kimtindo wa maelezo ya kiisimu yakifuatwa na fasiri ya kifasihi ya ruwaza zinazobainishwa katika maelezo ya kiisimu. Huu ni mkabala ambao haujatumiwa sana na watafiti wengine kuchunguza kazi za kifasihi za Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti wetu ni mchango mkubwa kwa uchunguzi wa kimtindo katika Kiswahili.

Utafiti huu umefanikiwa kuhusisha Nadharia ya Uchimuzi na Orodha ya kategoria za kiisimu na kimtindo iliyobuniwa na Leech na Short (2007). Orodha hii inaweka bayana viwango vya kiisimu vinavyofaa kuzingatiwa katika uchunguzi wa kimtindo, yaani kiwango cha kileksika, kiwango cha kisintaksia, na kiwango cha kisemantiki. Orodha hiyo ilituongoza kiutaratibu kuchunguza nduni za kiisimu zilizochimuzwa. Huu ni mpango unaoweza kutumiwa katika kufanyia tafiti nyingine za kimtindo.

7.4 Hitimisho

Utafiti huu ulichunguza mbinu za kileksika, kisintaksia na tamathali za usemi ambazo (mbinu) waandishi wa riwaya teule walizitumia kiubunifu ili kuibua maudhui kuhusu masuala ya dini na mamlaka. Tuliambatanisha maelezo ya kiisimu na uhakiki wa kifasihi katika fasiri ya matumizi ya lugha katika riwaya teule. Mkabala huu ni tofauti na mkabala wa awali uliosisitiza maana ya ‘mtindo kama mtu,’ yaani kudhihirisha utambulishi wa mwandishi wa kazi husika mintarafu matumizi yake ya lugha. Ingawa

masuala ya dini na mamlaka ni mada kuu katika riwaya husika, riwaya hizi zimezungumzia masuala ibuka katika jamii zetu kama vile ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana, ufisadi, usawa wa kijinsia, unyanyasaji, tamaa ya pesa na mali inayodhihirika katika injili ya utajiri, na kadhalika. Maudhui haya yamejadiliwa katika utafiti huu kwa mujibu wa matumizi ya mbinu za lugha – kileksika, kisintaksia, na kisematiki (kwa kuzingatia tamathali za usemi).

7.5 Mapendekezo

Masuala ya dini na mamlaka yanaweza kuchunguzwa kwa kutumia mikabala mingine, hasa mkabala wa uchanganuzi wa usemi au matawi mengine ya elimumitindo kama vile elimumitindo ya kitambuzi, elimumitindo ya kijinsia, na nyinginezo.

Utafiti huu umezingatia utanzu wa riwaya, lakini kazi za tanzu nyingine za fasihi, kazi zisizo za kifasihi, pamoja na matini za kimaongezi zinaweza pia kuchunguzwa kwa mkabala wa kimtindo tulioutumia katika utafiti wetu.

Mbinu za kitakwimu, hasa za kikopasi au mbinu za mseto zinaweza kutumiwa kuzichanganua riwaya zinazopatikana kielektroniki.

Zaidi ya Nadharia ya Uchimuzi, nadharia nyingine zinaweza kutumika kufanyia utafiti wa kimtindo wa riwaya za Kiswahili.

Kwa sababu ya upeo na mipaka ya utafiti huu, kipengele cha uwasilishaji wa usemi na fikira hakikuchunguzwa katika utafiti huu. Watafiti wengine wanaweza kukichunguza kipengele hicho kimtindo.

Watafiti wengine wanaweza wakahusisha Akili Unde katika tafiti za kimtindo.

MAREJELEO

Abdulmughuni, S.A. (2019). Stylistics, literary criticism, linguistics and discourse analysis. *International Journal of English Linguistics;* Vol.9, No.2.

Abed, Z.A. (2019). "Stylistic analysis of selected short stories by Flannery O'Connor and William Sydney Porter." [Unpublished master's dissertation]. Middle East University.

Abrams, M.H. (1978). *A Glossary of Literary Terms.* Macmillan India Limited.

Adam, S.A. (1978). *Kasri ya Mwinyi Fuad.* Vide~Muwa Publishers Limited.

Adane, S. (2012). "A stylistic analysis of *The Beautiful Things that Heaven Bears"* [Unpublished master's dissertation]. Addis Ababa University.

Adele, B. (1992). "Parallelism." In D.N. Freedman (Ed.), *The Anchor Yale Bible Dictionary* Vol.5, pp. 154 – 162. New York: Doubleday, 1992

Ajtony, Z. (2013). Approaching literature with linguistic means: A few conclusions. *Acta Universitatis, Sapientiae, Philologica*, 5, 2 (2013) 255-263.

Alfadil, A.A. (2013). *An Introduction to English Stylistics.*

Al-meedi, R.T. & Mukhef, R.N. (2017). Aspects of political language and parallelism. *Journal of Education and Practice.* Vol.8. No.34.

Al-Mehraby, A.A.A. (2010). "Stylistics (Linguistic) in the novels of William Golding" [Unpublished doctoral dissertation]. University of Aligarh.

American Bible Society (1996). *Good News Bible*. Harper Collins.

Aston E.O. (1947). *Swahili Grammar.* Longman Group UK Ltd.

Awonuga, C., Chimuaya, L., & Meshioye, C. (2018). Deviation-type foregrounding and literary interpretation: the Example of James, Kirkup's "The Thunder and Lightning." *International Journal of Language and Literature.* Vol. 6, No.1, pp. 69 – 79.

Azvedo, M.M. (2009). Literary linguistics in the context of a literature department. Selected Proceedings of the 11th Hispanic Linguistics Symposium. University of California.

BAKITA (2004). *Tafsiri Sanifu*. Toleo Na.6. Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA).

Behnam, B. (1996). A stylistic study of cohesive features in English prose fiction with some pedagogical implications for non-native contexts [Unpublished doctoral dissertation]. University of Sheffield.

Bhosale, B.P. (2016). A stylistic analysis pf T.S. Eliot's *The Waste Land* [Unpublished doctoral dissertation]. Dr. Babasaheb Ambedkar Marathwada University

Boyne, M. (2009). Sentenced to destruction: a stylistic analysis of the syntax of two post-apocalyptic novels. *Working with English: Medieval and Modern Language, Literarture and Drama* 5.1 (2009): pp. 1-20.

Bradford, R. (1997). *Stylistics*. Routledge.

Braun, V. & Clarke, V. (2006) Using thematic analysis in psychology. *Qualitative Research in Psychology*, 3:2, 77-101.

Bujanova, K. (2013). A corpus-linguistic analysis of Mitchell's *Gone with the Wind* and Hemingway's *A Farewell to Arms* [Unpublished master's thesis]. University of Oslo.

Burke, M. (2014). *The Routledge Handbook of Stylistics.* Routledge.

Candria, M. (2019). Stylistics and linguistic analyses of literary works. *Journal of Cultural, Literary, and Linguistic Studies.* 3(1); 29-34.

Chaitra, S.R. (2006). The fiction of John Fowles – a stylistic analysis [Unpublished doctoral dissertation]. University of Mysore.

Chandio, M.T. na wenzake (2017). Stylistic analysis of Ahmed Ali's short story *Our Lane*. *Journal of Education and Educational Development.* Vol.4 No.2 (Dec.2017).

Chimerah, R. & Njogu, K. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.

Creswell, J.W. (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative and Mixed Methods Approaches.* 3rd Ed. Sage Publications.

Culpeper, J. (2014). *Language and Characterisation.* Routledge.

Diasamidze, I. (2014). Point of view in narrative discourse. *Procedia – Social and Behavioral Sciences*. 158 (2014) 160 – 165.

Enjdjala, V. (2020). Functional stylistic analysis – *You are Beautiful*. The Namibia University of Science and Technology.

Enkvist, N.E. (1973). *Linguistic Stylistics.* Mouton & Co. Publishers.

Enon, J.C. (1998). *Educational Research, Statistics and Measurement.* Makerere University.

Fabb, N. (1997). *Linguistics and Literature*. John Wiley and Sons Ltd.

Fairclough, N. (1996). *Language and Power.* Addison Wesley Longman Limited.

Fowler, R. (1977). *Linguistics and the Novel.* Methuen and Co. Ltd.

Galperin, I.R. (1977). *Stylistics*. 2nd Edition. Vishaya Shkola.

Gathenya, E.W. (2018). Mielekeo na mtindo wa Shafi Adam Shafi katika riwaya za *Kuli* na *Haini* [Unpublished master's thesis]. Kenyatta University.

Gonzalez, R.E. & Clivilles, S., B. (1988). Stylistic analysis and the novel metaphor. *Pragmalinguistica,* 5 – 6, 1997 – 1988, 373 – 389. DOI:http://dx.doi.org/10.25267/Pragmatistica.1997.15.16

Green, N, & Searle-Chatterjee, M. (2008). *Religion, Language and* Power. Routledge.

Gregoriou, C. (2014). The linguistic levels of foregrounding in stylistics. In Burke, M., Ed. *The Routledge Handbook of Stylistics.* Routledge.

Gregorou, C. (2009). *English Literary Stylistics.* Palgrave Macmillan.

Habwe, J. (2005). *Paradiso*. The Jomo Kenyatta Foundation.

Habwe J. & Karanja P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Phoenix Publishers Ltd.

Harris, A.A. (1975). Analysis of point of view in the novels of Kurt Vonnegut, Jr., as applied to oral interpretation. [Unpublished master's dissertation]. North Texas State University.

Hassan, G. (1987). Literary stylistics: pedagogical perspectives in an EFL context. [Unpublished doctoral dissertation]. University of Nottingham.

Huang, Y. (2018). The application of stylistic analysis in college English teaching. *Advances in Economics, Business and Management Research,* Vol.75.

Isti'anah, A. (2018). Speech and thought presentation in Jhumpa Lahiri's *Interpreter of Maladies*. Universitas Sanata Dhama.

Jeffries, J. (2010). *Critical Stylistics*. Palgrave Macmillan.

Jeffries, L. & McIntyre (2010). *Stylistics.* Cambridge University Press.

Kahigi, K.K. (2022). *Misingi ya Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili.* KAUTTU.

Kandagor M., Ogechi, O.N. & Vierke, C. (Eds). (2017). *Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja.* Eldoret: Moi University Press.

Kazungu, K. (1982). Deviation and foregrounding in chosen literary texts [Unpublished master's thesis]. University of Nairobi.

Khan, A.B., et al. (2015). Stylistic analysis of the short story *'The Last Word*' by Dr. A.R. Tabassum. *Austrtalia International Academic Centre.* Vol.6 No.3. Doi: 10.7575/aiac .alls.v.6n.3p.10.

Kihore et al (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (SAMAKISA). TUKI.

Kimgung S.K. (2021). Mitindo ya uhalisia mazingaombwe katika riwaya teule za Kiswahili kama nyenzo za mivurugo katika jamii [Unpublished doctoral dissertation]. Moi University.

Kipacha, A. & Jilala, H. (2021). *Nadharia za Elimumitindo ya Kiswahili.* Daud Publishing Company Ltd.

Kitsao, J. (1975). A stylistic approach adopted for the study of written Swahili prose texts [Unpublished master's dissertation]. University of Nairobi.

Kitsao, J. (1982). An investigation of themes in Swahili literature and an application of stylostatistics to chosen texts [Unpublished doctoral dissertation]. University of Nairobi.

Kobia, J.M. & Mwilaria, R. (2015). A stylistic analysis of the 'Epic of Job.' *The International Journal of Education and Research.* Vol.3 No.6 June 2015.

König, E. na Pfister, M. (2017). *Literary Analysis and Linguistics*. Berlin: Erich Shmidt Verlag GmbH & Co.

Kosasih, M.M. (2019). A stylistic analysis of Chinua Achebe's *Things Fall Apart*. *International Journal of English, Literature and Social Science (IJELS).* Vol.4, Issue 5, Sep – Oct 2019.

Laplante, B. (2006). The rise of cohabitation in Quebec: power of religion and power over religion. *The Canadian Journal of Sociology*. Vol. 31, No.1, pp. 1-24.

Lar P.D. (2018). Linguistic study of Helon Habila's *Waiting for an Angel* and *Measuring Time* [Unpublished doctoral dissertation]. Ahmadu Bello University.

Latif, F. (2020). A stylistic analysis of the novel *Forty Rules of Love* by Elif Shafak. [Unpublished master's dissertation]. University of Computer and Emerging Sciences.

Leech, G.N. & Short, M. (2007) *Style in Fiction*. 2nd Ed. Pearson Education Limited.

Leech, G.N. (2013). *Language in Literature: Style and Foregrounding.* Routledge.

Leech, G. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. Longman.

Levinson, S.C. (1983). *Pragmatics.* Cambridge University Press.

Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia na Misingi ya Uchambuzi*. Afroplus Industries Limited.

Maguire, M. & Delahunt, B. (2017). Doing a thematic analysis: A practical, step-by-step guide for learning and teaching scholars. *All Ireland Journal of Teaching and Learning in Higher Education*. Vol.3 (2017).

Makoti, V.S. (2004). Mshikamano wa kisarufi katika Kiswahili [Unpublished doctoral dissertation]. Moi University.

Manan, A.S. (2018). Point of view in Conrad's *Almayer's Folly*: a stylistic perspective. *Kemanusiaan.* Vol. 25, Supp. 1, (2018), 167–190. School of Humanities, Universiti Sains Malaysia.

Marijani, F.C. (2014). Analysis of literary devices in selected novels of Severine Ndunguru. [Unpublished master's dissertation]. The Open University of Tanzania.

Massamba D.P.B. et al (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu* (SAMIKISA). TUKI.

Massamba D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* TUKI.

Mathivannan, S.M. (2008). A stylistic study of Vikram Seth's novel *'An Equal Music.'* [Unpublished doctoral dissertation]. Bharathiar University.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha*. Serengeti Educational Publishers.

Mbatiah, M. (2016). *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na Maendeleo yake*. The Jomo Kenyatta Foundation.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Standard Textbooks, Graphics and Publishing.

McIntyre, D. (2012). *Linguistics and Literature: Stylistics as a Tool for the Literary Critic*. University of Huddersfield, UK

Memon, S.M. (2017). Stylistic analysis of Ahmed Ali's short story *Our Lane*. *Journal of Education and Educational Development.* Vol.4 No.2.

Meniailo, V. (2020). V.Arnold's Theory of Foregounding and its Application to Text Analysis. *Interliteraria*, 25/1:1 16 – 25.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu*. Longhorn Publishers.

Michira, J.N. (1993). Uchanganuzi wa kimtindo wa lugha ya wachuuzi na lugha ya matangazo ya biashara redioni [Unpublished master's dissertation]. University of Nairobi.

Michira, J.N. (2018). A stylistic analysis of John Habwe's *Pendo la Karaha*. *International Journal of Humanities and Social Sciences,* Vol.6. Issue 6.

Mishra, D. (2016). A stylistic analysis of select novels of William Golding [Unpublished doctoral dissertation]. The English and Foreign University.

Mocănaşu, D.R. (2020). Determining the sample size in qualitative research. *IFIASA*. https://doi/10.26520/mcdsare.2020.4.181-187.

Mogere, O.M. (2003). Uhakiki wa riwaya za Ahmed Mohamed katika misingi ya kifeministi [Unpublished master's dissertation]. University of Nairobi.

Mohamed, S.A. (1989) *Asali Chungu*. East African Educational Publishers.

Mooti, F.M.A. (1978). A stylistic study of Joseph Conrad's novels. [Unpublished doctoral dissertation]. University of Sheffield.

Motanya, M.M., Kisurulia, E. & Sawe, S. (2021). Ukiushi kama elementi ya kimtindo katika baadhi ya riwaya za Ken Walibora. *International Academic Journal of Social Sciences and Education. 2(2),* 340-353.

Mugenda, O. & Mugenda, A. (2003). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Acts Press.

Mugir, S.K., Khadum, B.A, & Khalaf, H.M. (2019). A stylistic analysis of *For Whom the Bell Tolls.* College of Basic Education, University of Diyala. Vol.35, No.19 (2019): 2337 – 2365.

Muhi, T.H. (2012). A pragmatic approach to literary interpretation of fiction with reference to *The Merchant of Venice*. The University of Mustansiriyah.

Mwamzandi, M.Y. (2014). Swahili word order choices: insights from information structure [Unpublished doctoral dissertation]. University of Texas.

Mwita, B.M. (2009). Uhakiki wa mtindo katika baadhi ya tamthilia za Penina Muhando (Mlama). *Mulika*, Na.28, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Mwita, L. et al. (2018). *Isimu na Fasihi ya Lugha za Kiafrika*. Moi University Press.

Nkwera, F.M.V. (1989). *Sarufi na Fasihi*. Tanzania Publishing House.

Nnadi, I.C. (2010). A Linguistic analysis of Chukwuemeka Ike's novels [Unpublished doctoral dissertation]. University of Jos.

Niazi N. (2013). A Stylistic analysis of D.H. Lawrence's *Sons and Lovers*. *International Journal of Applied Linguistics & English Literature*, Vol. 2 No. 4.

Nofal, K.H. (2013). Darkness in Conrad's *Heart of Darkness*: a linguistic and stylistic analysis. *The Buckingham Journal of Language and Linguistics*. Vol.6 pp 77-93.

Nørgaard, N., Montoro, R., Busse, B. (2010). *Key Terms in Stylistics*. Continuum International Publishing Group.

Nyandiwa, H. (2015). Uchanganuzi wa kimtindo wa *Zinguo la Mzuka* na *Mbaya Wetu* [Unpublished master's dissertation]. University of Nairobi.

Nzabonimpa, B.J. (2017). *Understanding Literature: A Didactic Compendium*. Nsaka University.

Obuchi, S.M. (1996). Isimu-matini: muumano katika riwaya mbili za Mohamed Suleiman Mohamed [Unpublished doctoral dissertation]. University of Nairobi.

Obuchi, S.M. (2019). Isimu-matini: muumano kimsamiati na kiurejelezi katika *Kiu* na *Nyota ya Rehema.* Katika *Koja la Taaluma za Insia.* Karl Jamer Publishers Ltd.

Obuchi, S.M. (2016). *Taaluma ya Maana: Semantiki na Pragmatiki.* The Jomo Kenyatta Foundation.

Okal, B.O. (2021). Uhakiki wa riwaya ya *Paradiso* kwa msingi wa Nadharia ya Uhalisia. *Swahili Forum* 28 (2021): 14-33 14

Onchangu, R.N. (2003). Mtindo katika riwaya na hadithi fupi za Clara Momanyi [Unpublished master's dissertation]. University of Nairobi.

Ongarora, S.O. (2017). Efficacy of syntactic and morphological deviation in Kiswahili short stories: a case study of *Arusi ya Buldoza na Hadithi nyingine. International Journal of Science Arts and Commerce.* Vol.2. No.1.

Onyinyechi, N.P. (2014). A stylistic analysis of Isidore Okpewho's *The Last Duty. An International Journal of Language, Literature and Gender Studies*. Vol.3 (1).

Opande, N.I. (2015). Uchanganuzi wa vijenzi unganishi vya mshikamano katika matini za Kikisii [Unpublished doctoral dissertation]. Moi University.

Oso, W.Y. (2016). *Social Research: Principles and Practices*. The Jomo Kenyatta Foundation.

Osoro, G. (2003). Uhakiki wa riwaya za Said Ahmed Mohamed. [Unpublished maste's Dissertation]. University of Nairobi.

Otieno, T.M. (2020). A linguistic stylistic analysis of Henrik Ibsen's *A Doll's House*. *International Journal of Language and Linguistics.* Vol.8. No.5, 2020, pp.205-215.

Palmer, F.R. (1981). *Introduction to Theoretical* Linguistics. Cambridge University Press.

Panjaitan, L. (2018). Speech and thought presentation in Jane Austen's *Emma*: The case of free indirect discourse. [Unpublished master's dissertation]. University of Sumatera Utara.

Philipo, Z.T. & Kuyenga, F.E. (2017). *Sintaksia ya Kiswahili*. Karijamer Publishers Limited.

Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu.* Central Tanganyika Press.

Raiser, K. (2013). *Religion, Power, Politics.* Geneva: World Council of Churches.

Rayya, T. (2002). Mombasa Swahili women's wedding songs: a stylistic analysis [Unpublished doctoral dissertation]. University of Nairobi.

Riffaterre, M. (2015). Criteria for Style Analysis, *WORD*, 15:1, 154-174, DOI: 10.1080/00437956.1959.11659690 T.

Rubanza, Y.I. (2003). *Sarufi: Mtazamo wa Kimuundo*. Chuo Huria cha Tanzania.

Sani, H.M. (2016). A linguistic stylistic analysis of gender variations in selected television news reportage [Unpublished doctoral dissertation]. Ahmadu Bello University.

Sathikulameen, A. (2013). A linguistic stylistic study of *Amitav Ghosh* and its pedagogical implications [Unpublished doctoral dissertation]. University of Madras.

Short, M. (2013). *Exploring the Language of Poems, Plays and Prose.* Routledge.

Silavwe, M.I. (2016). Mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* ya Edwin Semzaba [Unpublished master's thesis]. Open University of Tanzania.

Simpson, P. (1993). *Language, Ideology and Point of View*. Routledge.

Simpson, P. (2004). *Stylistics: A Resource Book for Students.* Routledge.

Song, S. (2009). A Stylistic Analysis of *Miss Brill* by Katherine Mansfield" in *Review of European Studies*. Vol.1, No.2

Stockwell, P. & Whiteley, S. (2014). *The Cambridge Handbook of Stylistics*. Cambridge University Press

Thomas, L. na wenzake (2004). *Language, Society and Power.* Routledge.

Thoms, G.S. (2008). Syntax in experimental literature: a literary linguistic investigation. [Unpublished doctoral dissertation]. University of Strathclyde.

Toolan, T. (2013). *Language in Literature*. Routledge.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la 3. TUKI.

TUKI (2006). *English – Swahili Dictionary.* TUKI.

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha.* TUKI.

Udeze, N., Udeze, C. & Orji D.M.A. (2017). A linguistic stylistic study of Wole Soyinka's *Night and Death*. *UJAH* Vol.18 No.3.

UKEssays. (November 2018). Study of the foregrounding theory English language essay. Retrieved from https://www.ukessays.com/essays/english-language/studu-of-the-foregrounding-theory-english-language-essay.php?vref=1

Uzoma, N.E. (2012). Stylistic study of Ngugi wa Thiong'o's *Wizard of the Crow* and Okri's *The Famished Road*. [Unpublished master's thesis]. University of Niger

Van Peer, W. & Hakemulder, J (2006). Foregrounding. *Encyclopedia of Language and Linguistics,* Vol. 4 pp. 546-550.

Varghese, L.M. (2012). Stylistic analysis of Emily Brontĕ's *Wuthering Heights*. *Journal of Humanities and Social Sciences*. Vo.2, Issue 5 (Sep. - Oct. 2012), pp 46 – 50.

Vitale, A.J. (1981) *Swahili Syntax.* Foris Publications.

Wafula, R.M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. The Jomo Kenyatta F

Wales, K. (2014). *A Dictionary of Stylistics*. Routledge.

Wamitila, K.W. (2003). *Nguvu ya Sala*. Longhorn Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Focus Publications Ltd.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi*. Focus Publications Ltd.

Wareing, S. et al. (2004). *Language, Society and Power.* Routledge.

Wasike, C.K. (2020). Mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika kazi za fasihi: kielelezo cha tanzu teule za fasihi andishi [Unpublished doctoral dissertation]. Moi University.

Wodak, R. (Ed.). (1989). *Language*, *Power and Ideology: Studies in Political Discourse.* Amsterdam: John Benjamins Publishing Company.

Yeibo, E. (2011). Group types as style markers in J.P. Clark Bederemo's Poetry. In Academy Publisher. *Theory and Practice in Language Studies,* Vol. 1, No.8, pp. 928 - 934.

Zeenathaman, M.A. (2018). Linguistic analysis of the select novels of Bapsi Sidhwa. *Language in India.* www.languageinindia.com. ISSN 1930-2940 18:1 January 2028.

VIAMBATISHO

Kiambatisho 1: Madondoo ya Data kutoka *Paradiso*

1. Lakini leo alitaka waelewe kanuni muhimu ya injili. Nayo ni kujitayarisha katika ulimwengu kwa **maisha ya ahera**.
(Habwe, 2005, Ukur. 56)

2. Michael **aliishi Paradiso** na baadaye angeishi katika **Paradiso nyingine**.
(Habwe, 2005, Ukur. 142)

3. Kuvaa kwao na kutembea kwao kulionyesha kuwa **wao waliishi ahera**.
(Habwe, 2005, Ukur. 130)

4. Ahera walikoishi **walihodhi mapesa**, **nyumba** za kukodisha na **magari** mtawalia. **Kula kwao** kulidhihirisha pia kuwa ni kwa juu.
(Habwe, 2005, Ukur. 130)

5. Akaunti zao zilifura kwa **darahima**. (Habwe, 2005, Ukur. 134)

6. Moja katika **miradi** ya pale kanisani ni kuwabwaga na kuwazoa kutoka shuleni **wana** wa mchungaji.
(Habwe, 2005, Ukur. 213)

9. Mary alikuwa **mama wa nyumbani.** **(**Habwe, 2005, Ukur. 5)

16. Moyo wake [Michael] lakini ulikumbuka maisha yana hatua tatu: **kuja**, **kuoa** na **kuondoka**.
(Habwe, 2005, Ukur.90)

17. Mungu ndiye anayefahamu **kuja**, **kuweko** na hata **kutoka**.
*(*Habwe, 2005, Ukur. 96)

18. Nyumba yake Joshua ni **ya kisasa** si kama **kibanda alichokaa hapo Kibera**. Kibanda hicho …hakikumstahili hasa alipopandishwa na kuwa Askofu Mkuu.
(Habwe, 2005, Ukur. 43)

19. Waliachana usiku ule. Amuko akaelekea **Mountain View** naye Michael akaenda katika **kibanda chake Kibera**.
(Habwe, 2005, Ukur. 42)

24. Siku hizi zilionekana kana za mwisho kweli maana maradhi, ufukara, mizozo na ukosefu wa kanisa ni baadhi ya **vijisababu** vilivyosukuma watu kanisani.
(Habwe, 2005, Ukur. 52)

31. Michael alishangaa ni kwa jinsi gani matanga yamekuwa **kisababu** cha kujipatia pesa.

(Habwe, 2005, Ukur. 95)

32. Mango aliona kuingia paradiso yatakuwa mapenzi ya Bwana Yesu. Michael alikuwa na **pasipoti** ya moja kwa moja.

(Habwe, 2005, Ukur. 141)

37. [Mwenyezi Mungu] **anaposamehe husamehe** kabisa. Hakumbuki hata moja **alilosamehe**. 'Ni wakati gani mtu anapaswa **kusamehe**?' aliwaza. Labda anapomwomba Maulana ampe nguvu ya **kusamehe** na uwezo wa kudumisha **msamaha huo**.

(Habwe, 2005, Ukur. 209)

38. "Lakini **ulisamehe**?" wazo la kwanza lilikuja juu. **Ulisamehe** kwa nini una fundo bado? … Alikubali ni vizuri **kumsamehe** mwenzako kwani nawe hujui utakosa nini. Nawe ukikosa utahitaji **msamaha** kwani katika dunia hapana asekosa.

(Habwe, 2005, Ukur. 210)

39. Bwana Mganga hakutaka tena kuoa mke mwingine. Aliwaona **wanawake** kama vinyonga. Walibadilika kulingana na mazingira. Alipofikiria kuwa mama yake ni **mwanamke** pia ilimsikitisha. Kwani alikosa imani nao wote! Pale alipofanya kazi alikuwa na shida ya kutengana na **wanawake**. Ni kama kila **mwanamke** aliyemwona alikuwa kama Lona. Bosi wake alikuwa **mwanamke**. Lakini alikuwa mpole na msikivu. Mganga hakutaka kumsikiliza sana.

(Habwe, 2005, Ukur. 71)

54**.** **Labda** ni kweli. **Labda** si kweli. Ni nani ajuaye? **Labda** mamake anajua. **Labda** ndiye aliyemweleza. **Labda** mtoto anaropokwa.

(Habwe, 2005, Ukur. 86)

55. Lona sasa ndiye **aliyedhibiti** mamlaka ya New Jerusalem.

(Habwe, 2005, Ukur. 120)

56. Hakuna tena kilichomtisha Lona. Tayari **amemdhibiti** mumewe. **Alidhibiti** uchumi. **Aliwadhibiti** waumini. Sasa **alidhibiti** siasa za nchi. Maana hata rais wa nchi alimfahamu. Si muhali kumwona akitumika siku za holidei akiomba au kama amekaa na wakubwa wa serikali huku kajipamba lile joho…. Hata kama Lona **alidhibiti** kila kitu, kuna kitu kimoja tu **hakukidhibiti** nacho ni wakati na ahadi yake kwa Bwana.

(Habwe, 2005, Ukur.131)

57. Fununu zilisambazwa na wadhabidhabina kuwa Boribori angefungua kanisa lake ili naye **akalidhibiti**, atoe wa kutoa na kuchomeka humo ndani wa kuchomeka.
(Habwe, 2005, Ukur. 137)

60. **Yeyote** aliyetaka utajiri wa haraka **alikimbilia** injili.
(Habwe, 2005, Ukur. 220)

61. **Askofu Joshua** na **kasisi Lona Bosire** walipokea **misaada yote** wakaiweka katika akaunti zao **kwa niaba ya kanisa** la New Jerusalem. Mapato yaliyotoka katika miradi ya kanisa…pia yalimiminika katika **fuko lao**.
(Habwe, 2005, Ukur. 130)

62. Salome **hakuzuiliwa** na Kyalo kwenda New Jerusalem.
(Habwe, 2005, Ukur. 70)

63. Hata vile vikao vya nyumbani vya sala ambavyo alisema **viliharibu wanawake** sasa **alimkubali mkewe kuvishiriki**.
(Habwe, 2005, Ukur. 71)

58. Usiwasumbue watu tutapika wenyewe. Sisi ni **wanawake ati**.
(Habwe, 2005, Ukur**.** 98)

65. Mbona Mungu **inasemekana** aliumba mwanamke kwa ubavu wa mwanamume?" Patricia **alidai**.

"Lakini **mahali kwingi** katika Biblia mwanamke **ameitwa** kiumbe dhaifu," Patricia aliuliza tena.

Biblia **imeeleza waziwazi** kuwa mwanamke ni kiumbe dhaifu," Lydia alisema.
(Habwe, 2005, Ukur. 101)

66. Michael aliangalia wale wanawake walivyofanya mle ndani akakinai kuwa kazi ya nyumbani walikuwa **washenga kwayo**.
(Habwe, 2005, Ukur. 99)

67. Nyinyi naona mu **mafundi wa kupika** sana," Michael alisema **akitabasamu**.
(Habwe, 2005, Ukur. 100)

68. Lydia na Patricia waliandaa meza. Michael aliacha kusoma **gazeti la Victory** akajongea mezani na kuanza kula.
(Habwe, 2005, Ukur. 100)

70. Mume wa awali wa Lona, Bw. Mganga, alipaondoka pale nyumbani bila chuki yoyote. **Alielewa** kila mwanamke ana haki ya kupenda aliyemtaka.
(Habwe, 2005, Ukur. 71)

72. **Kasisi** Michael **aliendelea kushuka kitambi**.
(Habwe, 2005, Ukur. 160)

73. Tangazo jingine ndugu zangu na dada zangu katika Yesu ni kwamba matoleo yenu yamepungua. Kitabu cha Malaki kinasema **matoleo ni lazima** kwa waumini. Matoleo **yapaswa** kuwa mazuri. Baadhi yenu mnaleta kanisani masazo ya supermarket, yaani change. **Si ruhusa** kuleta shilingi moja kanisani au hata shilingi kumi…
…**ni haramu** kucheza muziki katika vyombo hivyo **ikiwa hukuchangia**.
Kuanzia Jumapili ijayo, vifuko vya sadaka vitakuwa kule mbele na kila mmoja **atapaswa** kupeleka zaka yake kila mtu akimwona.
Mara minong'ono ikazuka kanisani…. Hajui kuna watu wengine hawana pa kutoa **hiyo zaka**. Hata kula hawawezi kula. Tena hizo pesa si **wanazila wao**,….
(Habwe, 2005, Ukur. 54)

75. Tonje alifungua kanisa **lake** mwenyewe. Yeye na babake hawaonani uso kwa uso. Kila mmoja yuko na mambo **yake**," Zuhra alieleza.
(Habwe, 2005, Ukur. 45)

89. [Joshua] alikwenda katika chumba cha kulala akashika bastola yake. … **Aliona** ni vizuri kama atamwadhibu [Boribori] mwenyewe.
(Habwe, 2005, Ukur. 139)

90. Wanawe wawili wa kike walisomea Chuo Kikuu cha Daystar kwa hiyo **aliona** asiwadhiki sana kwa kukaa Kibera.
(Habwe, 2005, Ukur. 43)

91. Kitu kimoja **aliamini** ni kuwa atampigia ahsante yule kijana maskini, Michael. … **Aliamua** ampe moja katika magari yake.
Alifikiria ampe lile gari la Peugeot.
(Habwe, 2005, Kur. 47 - 48)

92. **Kundi la Michael** lilisisitiza kuna uhuru wa kukaa hali **kundi la Joshua** lilitaka liondoke. **Kundi la Joshua** lilidai kuwa ndilo lenye haki tu kuwepo katika jengo hili.
(Habwe, 2005, Ukur. 76)

93. Michael alikuwa na maono ya kanisa la Yesu. Kanisa hili si la kuvunjikavunjika kama amiba. **Ni kanisa la** umoja. **Kanisa la** msamaha. **Kanisa la** utekelezaji na kutumaini mwisho. ….. KANISA LA PARADISO.
(Habwe, 2005, Ukur. 225)

94. Kibera nzima Jumapili ilikuwa kama uwanja wa disko. **Kunao** waliofanya ya shari. Pia, **kunao** waliofanya ya shwari. **Kunao** ambao makanisa yalikuwa kama vyama vya ushirika kwamba mtu akifa aweze kufanyiwa mchango wa kusafirishwa nyumbani. **Kulikuwa na**

makanisa ambapo watu walikwenda kutupa wakati kwa sababu ya uvunjifu. **Mengine yalikuwa ni mahali pa kwenda kama mazoea** bila kuwepo na sababu maalum. Bethany lakini kilikuwa mfano wa kilima cha Zayuni ambapo mtu angeweza kutafuta toba na suluhu ya kweli kwa Bwana.

(Habwe, 2005, Ukur. 113)

95. **Ataacha vipi** ulevi? **Ataacha vipi** wapenzi wake wa kike? **Ataacha vipi** ufisadi wake wa ofisini ambao ndio umemletea magari kochokocho aliyo nayo na nyumba ambazo hazihesabiki.

(Habwe, 2005, Ukur. 41)

96**.** **Ni wangapi** walao rushwa? **Ni wangapi** wauao? **Ni wangapi** wadanganyao?"

(Habwe, 2005, Ukur. 130)

97. [Michael] alitaka kuwa kama Yesu… [Yesu] **Hakuwa na** kwake. **Hakuwa na** gari. **Hakuwa na** mke. **Hakuwa na** nyumba.

(Habwe, 2005, Ukur. 44)

98. …lakini hivyo ndivyo ilivyo kazi ya Mungu. **Ina** milima. **Ina** mabonde. **Ina** vilio. **Ina** vicheko.

(Habwe, 2005, Ukur. 68)

111. Kwa kweli vitendo vya mzazi huwa mfano mwema kwa wana. Yeye Joshua **hakuwa mwaminifu**. Wala Lona **hakuwa mwaminifu**.

(Habwe, 2005, Ukur. 129)

112. **Waumini wengine** walipofanya bidii katika sala **wengine** wakalangua madawa. **Waumini wengine** walipoufuata uso wa Bwana, wenzao **wengine** waliuza bangi katika mataifa ya nje ili kupata dola.

(Habwe, 2005, Ukur. 208)

113. Hivyo ndivyo madhabahu ya Mungu yalivyokuwa siku hizi. Kulikuwa na **wale waliomwabudu Mungu kwa haki na ukweli** lakini **wengine walitumia madhabahu kama nyenzo** ya kutafuta maisha.

(Habwe, 2005, Ukur. 208)

114. Nyumba hii Boribori ameihama sasa. **Hakuihama kwa hiari, amehama kwa lazima**. **Amehama kwa ajili ya hadaa**. Sasa Boribori analala mto uliochanika.

(Habwe, 2005, Ukur. 222)

115. Kila uchao **matendo yake yakawa** baidi na usemi wake. **Ubaya wake ukawa** fufufu na **wema ukawa** mchache.
(Habwe, 2005, Ukur. 131)

116. Uaskofu uligeuka na kuwa **sio huduma** tena kwa Bwana lakini **kazi**. Kazi ya mshahara wa mwisho wa mwezi.
(Habwe, 2005, Ukur. 67)

119. [Michael] ...yeye alijikaza ili asimame na kumfanyia Bwana kazi **bila ujanja**, **bila ghilba.**
(Habwe, 2005, Ukur. 66)

120. [Michael] aliona kanisa la Bwana likisambaratika **kila siku**, **kila mwezi**, **kila mwaka**.
(Habwe, 2005, Ukur. 77)

121. Kisa na maana ni nini?" Michael aliwaza. **Ushindani**, **ulafi** wa vitu vya dunia hii. **Tamaa** ambayo Bwana Yesu alisema tusiwe nayo.
(Habwe, 2005, Ukur. 77)

122. Kyalo hakuwa kama mkewe. **Hakupenda** masuala ya dini. Tangu alipozaliwa **hakuwa** amekwenda kanisani. **Hakuona** haja yoyote ya kujidhiki na sala ndefu ambazo zilichosha. **Hakupenda** hasa sala za kelele. Aliona kuwa mke wake alikuwa mjinga kwa kujishughulisha na hadaa za wahubiri**.**
(Habwe, 2005, Ukur. 49)

123. **Vitendo vya dini vilimuudhi**. **Kelele na vurumai vilishtadi kanisani**. Huko walitafuta pepo lakini huko ndiko walikokugeuza na kukufanya Jehanamu kwa **vitendo**, **tamaa** na **utashi wa dunia**.
(Habwe, 2005, Ukur. 97)

138. Nyinyi ni shetani. Ati wahubiri? Wahubiri gani nyinyi? Nyinyi ni laghai. **Mwaiba**. **Mwalazimisha**. **Mwaongopa**. **Mwaua**. Huku **mwataja Yesu**. Shetani wakubwa nyinyi. Msitaje jina la Bwana bure.
(Habwe, 2005, Ukur. 75)

140. Rose alipata alichotaka; **pesa**, **mavazi**, **vyakula**, na wanawe walisoma katika skuli za hela kama Hilcrest na Braeburn.
(Habwe, 2005, Ukur. 65)

143. **Mauaji**, **ubakaji**, **wizi, ufisadi**, **kashfa** ni miongoni mwa hatari tulizo nazo.
(Habwe, 2005, Ukur. 56)

144. "Achana na yule **mbakaji** na **mwasherati**," alisema Lona.
(Habwe, 2005, Ukur. 75)

146. Nyumba yake Joshua ni ya kisasa si kama kibanda alichokaa hapo kibera. Kibanda hicho …hakikumstahili hasa **alipopandishwa na kuwa Askofu Mkuu**. Alistahili nyumba ya kisawasawa ili akitembelewa na wenzake waone Mungu tunayemwomba si wa umaskini. Mungu ni Mungu wa baraka.

(Habwe, 2005, Ukur. 43)

147. **Lona alipopewa cheo hicho cha ukasisi** Joshua aliona kakamilika.

(Habwe, 2005, Ukur. 80)

148. Kila mtoto katika hawa **amefunguliwa akaunti** katika benki ya Baroda. Licha ya akaunti, Boribori anawafungulia bima za maisha na za masomo katika shirika la Bima la British Assurance.

(Habwe, 2005, Ukur. 213)

149. Alikuwa na mtoto mvulana mmoja, Jim. Jim **ashanunuliwa** nyumba mbili Marekani katika mji wa New York.

(Habwe, 2005, Ukur. 213)

150. Moriasi na Boribori walirudi kutoka sehemu ya chemba. Boribori **alidondoka** shilingi milioni moja. Aliitoa kama **chai** kwa jaji Moriasi.

(Habwe, 2005, Ukur. 212)

151. **Mlungula ulikuwa madhehebu** ya waja katika dunia.

(Habwe, 2005, Ukur.123)

153. Askofu Joshua na kasisi Lona Bosire walipokea misaada yote wakaiweka katika akaunti zao kwa niaba ya kanisa la New Jerusalem.

Mapato yaliyotoka katika miradi ya kanisa… pia **yalimiminika** katika **fuko** lao.

(Habwe, 2005, Ukur. 130)

154. **Kapu zima** la zaka, sadaka, fungu la kumi na matoleo mengine **alilivuna** Joshua.

(Habwe, 2005, Ukur.48)

155. Akaunti zao **zilifura** kwa darahima. (Habwe, 2005, Ukur. 134)

156. Japo kila siku kanisani alidai Mungu alimwongoza na kumfichulia mambo lakini mara nyingi kama si hadaa yalikuwa ni mawazo yaliyokwenda na **utashi wake wa mali**.

(Habwe, 2005, Ukur.138)

157**. Nyimbo zilinyunyizwa** na zikasaidia kuinua imani za watu na kuwaweka tayari kuabudu Maulana. Kwa hakika waumini

walionekana wenye furaha na walioridhika na shughuli iliyokuwa ikipita

(Habwe, 2005, Ukur. 53)

158. Wanagombea washirika na zaka. Pesa zimekuwa **uti wa mgongo** wa injili hapa Mombasa.

(Habwe, 2005, Ukur. 45)

159. Kanisa jingine…. **lilimea** Kibera. Mtaa wa Kibera ulikuwa nyumbani mwa makanisa ya sampuli zote.

Makanisa hayo yalivunjika kila siku. Mapya yalijengwa na watu wawili, hata watatu. Yote lengo lake likawa kwenda Paradiso.

(Habwe, 2005, Ukur.160)

160. Sasa **injili iliyovuma** New Jerusalem ilikuwa ya maendeleo ya kiuchumi.

Askofu Joshua alikashifu mtu yeyote aliyeendelea kuja kanisani na Mungu Baba hajampa gari au kumzawadisha kana kwamba injili na utajiri ni mambo yaliyofungamana.

Matunda ya mahubiri haya ungeyaona Jumapili yoyote. Ibada zilifanywa kwa zamu na kila zamu maegesho ya magari yalijaa kwa magari mapya….

(Habwe, 2005, Ukur. 120)

162. Nyumba yake [Boribori] nayo ni **masimulizi**. Imetamba kwenye nusu ekari. Ina matagaa sita. Walijenga waashi kutoka Israel. Vyuma kutoka Ujerumani…..Maegesho – magari sita.

(Habwe, 2005, Ukur. 222)

171. Muasya aliamini watu **waliomwagika** kanisani ilikuwa kwa sababu ya dhiki.

(Habwe, 2005, Ukur. 49)

172. Maadui nao walikuwa wale waliofika na **milima ya shida na vikapu vya matarajio** wakatoka maskini bila kuambulia chochote.

(Habwe, 2005, Ukur. 82)

173. Kanisa hili [la New Jerusalem] **liliporuka kileleni** kila aina ya shtuma zilitolewa na makanisa menza.

(Habwe, 2005, Ukur. 53)

174. Michael alipozidi kuvuma katika midomo ya watu alikuwa **akitia kitumbua chake mchanga** na viongozi wengine.

(Habwe, 2005, Ukur. 67)

175. [Michael] alielewa tosha **wambea ndio kensa** iliyovamia makanisa na kuyaangusha.

(Habwe, 2005, Ukur. 49)

177. Ni nini kilichomharibikia **akatia guu katika bwawa** kama hili? Bwawa la tope, bwawa la maangamizi na bwawa la kishetani.

(Habwe, 2005, Ukur. 153)

178. Kwa hakika **Michael aligeuka na kuwa nyambizi** huko chini ya bahari.

(Habwe, 2005, Ukur. 160)

179. Baadhi ya waliookoka **waliteleza** kwenye **sakafu telezi ya dunia.**

(Habwe, 2005, Ukur. 123)

180. [Rose] alimsukuma [Musa] polepole kwa **mwendo wa kinyonga** hadi mwenyewe **akasalimu amri**….. Bandu bandu huisha gogo. Rose **alimbandua Musa pole pole.**

(Habwe, 2005, Ukur. 32)

181. Rose hakuamini **nyuki aliyekuwa zumbukuku** ndiye anayemzomea **yeye nyigu** aliyezembea **kazi ya kutengeneza asali**.

(Habwe, 2005, Ukur. 33)

183. Ilibidi ufanye uteuzi kama ulitaka kukaa pale Bethany **uushone mdomo wako** na kuacha upekuzi wa mienendo ya mchungaji.

(Habwe, 2005, Ukur. 160)

184. **Kimbunga** hiki **kilipiga kanisa dafrao** hadi likavunjika vipande viwili.

(Habwe, 2005, Ukur. 153)

193. Aaa. Nisikupate unakwenda kanisani. Wala sitaki kuelezwa mambo ya kike mimi. Nikisema hapa hapana wa kunieleza jingine. **Kama wataka kuwa jogoo** hapa basi sema tuagane. Musa alikuwa mkali. Mkewe aliona vyema kumtii bila kuzua kivumbi…

(Habwe, 2005, Ukur. 65)

195. [Joshua] alikwenda katika chumba cha kulala akashika bastola yake. Boribori angepatikana mle ndani **angepewa risasi lake** palepale. Joshua hakutaka kumwachia Mungu wa Adhama afanye uamuzi na kumwadhibu Boribori. Aliona ni vizuri kama atamwadhibu mwenyewe.

(Habwe, 2005, Ukur. 139)

197. Sasa nitafanya nini?" Mchugaji alijiuliza akiwa kwenye ofisi yake **yenye kupambwa utadhani balozi**.
(Habwe, 2005, Ukur. 170).

198. Nyaleso …alikuwa mwembamba. Lakini sasa amekunywa katika kisima cha pale **akajaa kama tembo**. Ukimwangalia ni **kama jitu**.
(Habwe, 2005, Ukur. 196)

199. [Amuko] alikuwa na gari la Range Rover **lililomeza mafuta kama zimwi**. Mafuta haya aliyapata kutokana na kashfa mle ofisini.
(Habwe, 2005, Ukur. 47)

209. Jambo hili wakati mwingine lilimletea Joshua wivu mpaka **akavimba shingoni kama pili** anayemeza mbuzi.
(Habwe, 2005, Ukur. 55)

210. Kila uchao uhusiano baina ya Michael na Joshua uliendelea kutumbukia nyongo. Ni **kama majogoo mawili yaliyokaa katika kizimba kimoja**. Kila mmoja katika majogoo hao alitaka utawala.
(Habwe, 2005, Ukur. 76)

211. Yeye Michael alijaribu **kusimama wima kama mti uliomea karibu na mto**.
Michael naye amesimama kidete sasa **kama mbuyu**. Amekataa kupepesuliwa na upepo wa raha za dunia.
(Habwe, 2005, Ukur. 225)

212. Bethany ilikuwa **kama nyota** iliyong'ara katika usiku wa giza totoro pale Kibera.
(Habwe, 2005, Ukur. 112)

213. Bethany lakini kilikuwa **mfano wa kilima cha Zayuni** ambapo mtu angeweza kutafuta toba na suluhu ya kweli kwa Bwana.
(Habwe, 2005, Ukur. 113)

222. Mali ilikuwa imepotea pia katika kulisha jamaa na **watumishi wa Bwana.**
(Habwe, 2005, Ukur. 95)

254. Baadhi ya viongozi walimsengenya. "Huyu amekuja tu ameona ndiye **atakayeokoa ulimwengu mzima wa Nairobi,"** alisema Monayo.
(Habwe, 2005, Ukur. 39)

255. Ataacha vipi ufisadi wake wa ofisini ambao ndio umemletea magari kochokocho aliyo nayo na **nyumba ambazo hazihesabiki**.
(Habwe, 2005, Ukur. 41)

256. Huwezi kutazama televisheni huku ukila chakula **kwani utatapika**.
(Habwe, 2005, Ukur. 56)

257. **Ni nani asiyejua kashfa ya Michael pale iliyomhusisha Patricia?**
(Habwe, 2005, Ukur. 204)

258. **Lakini ni lipi ambalo James Boribori hajaungama?** Katika mambo aliyoungama Boribori ni kuwa ulanguzi huu ulianza na Joshua. Mkewe Joshua, marehemu Lona, ndiye aliyekuwa mharakati wa shughuli hii.
(Habwe, 2005, Ukur. 207)

259. **Au ina maana gani kuwa Mkristo? Si kuwa kama Yesu?**
(Habwe, 2005, Ukur. 44)

260. Siku hizi kila mtu anasema ameokoka. Lakini **ni wangapi waliookoka kweli?**
(Habwe, 2005, Ukur. 56)

261. **Kyalo alishangaa kama huwezi kumwamini mhubiri utamwamini nani?**
(Habwe, 2005, Ukur. 59)

262. Kuja kwa watu katika kanisa hili haikuwa bure. **Ni watu wangapi waliopata miujiza na baraka?**
Musa pia alikuwa na sifa kubwa. **Ni watu wangapi waliopona mahali pale kupitia sala zake zilizotolewa kila siku ya Jumapili na Jumanne?**

Ni wanawake wangapi walioshika mimba baada ya huo mkutano? Ni wengi ajabu!
(Habwe, 2005, Ukur. 30)

263. Ulimwengu wa leo umeshinda kile kiwango cha **Sodoma**.
(Habwe, 2005, Ukur. 56)

264. Michael aliona kifo cha Joshua na mkewe kama kile **kisa cha Sodoma na Gomora.**
(Habwe, 2005, Ukur. 134)

265. [Michael] aliamini kasisi alipaswa kuwa mfano mwema kwa wale anaowaongoza. La sivyo atakuwa **kama kiongozi aliyezungumziwa katika Ezekieli 34** anayejiendeleza bila kuwazia kondoo wake.
(Habwe, 2005, Ukur. 67)

266. Musa alikuwa mkubwa wake [Michael] na ndiye aliyemwonya dhidi ya **wanawake kama Delila**.
(Habwe, 2005, Ukur. 49)

267. Katika kundi hili [la watu waliohudumu chini ya Joshua na Musa] ni **Michael pekee aliyekaa Kibera bado.**
(Habwe, 2005, Ukur. 43)

268. Kutoka **Woodley** [Lona] alishuka barabara ya Joseph Kang'ethe na akaingia **Kibera Drive**. Hatimaye aliingia **Fort Jesus Estate** ambapo Michael alisogea baada ya kutoka **Kibera Matopeni**.
(Habwe, 2005, Ukur. 68)

269. Musa naye alikaa **Buruburu**. **Pia** yeye **aliona** Mungu alikuwa amejibu maombi yake kwa kumpa nyumba. Musa alisema kuwa ilikuwa vizuri kukaa mahali pa usalama. **Kibera kulikuwa na fujo**.
(Habwe, 2005, Ukur. 43)

270. Licha ya akaunti, Boribori anawafungulia bima za maisha na za masomo katika shirika la Bima la **British Assurance**.
(Habwe, 2005, Ukur. 213)

271. Alikuwa na mtoto mvulana mmoja, Jim. Jim ashanunuliwa nyumba mbili **Marekani** katika mji wa **New York**.
(Habwe, 2005, Ukur. 213)

272. Gari lake [Musa] sasa lilikuwa **Range Rover**. Aliendeshwa na Bwana mmoja Rotino ambaye zamani alikuwa katika jeshi.
(Habwe, 2005, Ukur. 66)

273. Lona alishuka na gari lao la **Toyota Land Cruiser**.
(Habwe, 2005, Ukur. 68)

274. Boribori na mwendakati wake pamoja na Judy walifurahi huku wakirudi nyumbani katika gari lao la **Mercedes**.

(Habwe, 2005, Ukur. 213)

275. Gari lake alololipenda [Joshua] ni **Prado**. Madirisha yake yamepambwa kwa pazia maalum. Yeye alikaa kushoto dereva aliyestaafu kutoka jeshi akimwendesha.
(Habwe, 2005, Ukur. 221)

Kiambatisho 2: Madondoo ya Data kutoka *Nguvu ya sala*

7. Labda maisha ya mjini **yaliwanyang'anya** binadamu chembe za huruma zilizobakia, **wameshapokwa** hisia zote za kibinadamu na kubakia **makatili** au **magombe** ambayo yalikuwa tayari kumkumta pembe yeyote aliyepita mbele yao bila ya kuwazia lolote.

*(*Wamitila, 1999, Ukur. 118**)**

8. Kwa kiasi kikubwa nilihisi kuwa baba **alishindwa** kulielewa hili kutokana na namna **alivyotopea** na **kubobea** katika imani yake. Kwake kilichokuwa muhimu ni kuyafuata mafundisho ya dini na kuithamini **nguvu ya sala**.

*(*Wamitila, 1999, Ukur. 71**)**

10. Mary Kasiva alikuwa **mke wa nyumbani** alishughulika na kazi za nyumbani wiki nzima, kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi. Siku ya Jumapili alijiunga na mumewe kwenda kanisani. Hiyo ilishakuwa ratiba yake sasa na wala hakuwa na hiari tena.

(Wamitila, 1999, Ukur. 178)

23. Yule **kijana**… Alimsihi Mungu wake amnusuru na hujuma za wastaarabu hawa waliokuwa wanatishia kumwua kwa sababu ya kunyakua **kibogosho** cha mwanamke mmoja mnene ambacho hakikuwa na chochote ila karatasi za shashi zilizokuwa na kamasi na **vitaulo vya *stayfree***.

(Wamitila, 1999, Ukur. 115)

33. Babake Bathsheba alikuwa Mkristo. Hakuwa **pasta** kama babangu ila alikuwa mzee wa kanisa na wala sidhani kama alikuwa mkali kama alivyokuwa baba. Labda siku moja angekuwa mkali; siku ambayo angekuwa **pasta**.

(Wamitila, 1999, Ukur. 16)

40. "Utamweleza nini **babako**? aliniuliza mama.

(Wamitila, 1999, Ukur. 22)

41. "***Babako*** akijua atasema nini?" aliuliza mama.
"Hamna ubaya lakini **babako** hapendelei mambo hayo," alisema mama hatimaye.

"Mwanangu **babako** anahofu kusemwa na watu. Kumbuka ni kiongozi wa kanisa. Je, watu watamfikiria nini wakisikia watoto wake wa kike hulala nje?" alieleza mama.
(Wamitila, 1999, Ukur. 186)

42. "Usifanye tendo kama hilo bila ya ruhusa ya **babako**," alisema akimwelekezea Roselyn.
(Wamitila, 1999, Ukur. 187)

43. "Kumbuka huko utakutana na wasichana wa kila aina," alieleza mama.
"Jitunze vizuri mwanangu ili **usiniaibishe mimi**," alisema baba.
"Mm! mwanangu jitahidi **usimwaibishe babako**," alisisitiza mama.
"Kuwa kielelezo kizuri na kumbuka kuwa jamii nzima ime***ni***kodolea macho **mimi babako**!" alimalizia baba.
(Wamitila, 1999, Ukur. 61)

44. Nilikuwa na tamaa ya kufuzu na kuingia chuo kikuu mwakani. **Hamna** msichana yeyote ambaye alishajiunga na chuo kikuu kutoka kijiji cha Misombe.
Sio wasichana peke yao hata wavulana pia; **hamna** hata mmoja aliyewahi kujiunga na chuo kikuu
(Wamitila, 1999, Ukur. 119**)**

45. Fauka ya kusimuliana visa na vitushi mbalimbali tulijadili masuala fulani kuhusu Fasihi. Hili ndilo somo nililolipenda sana, **hamna** mwanafunzi aliyenishinda katika darasa letu. Somo lililonitatiza ni somo la Hisabati. **Hamna** aliyemshinda Kate katika somo hili.
(Wamitila, 1999, Ukur. 123**)**

69. Baba alikuwa ameketi kwenye baraza ya nyumba nilipotokeza. Alikuwa **akisomasoma gazeti**… Niliingia nyumbani… kisha nikatoka kuelekea **jikoni alikokuwa mama**.
(Wamitila, 1999, Ukur. 121)

71. Alikuwepo Masaku aliyekuwa mwanamume. Masaku alikuwa na sifa za ajabu ajabu. Mwalimu alitueleza kuwa shujaa huyo aliacha nyayo zake juu ya jabali fulani **karibu na mlima karibu na mji wa Machakos.**

Alikuwepo **shujaa mwingine wa kike**. Alikuwa na **uwezo** wa kutabiri mambo. **Aliweza** kutabiri majanga ambayo yangeisibu jamii. Huyu alizikwa katika pango fulani **karibu na kijiji chetu**.
(Wamitila, 1999, Ukur. 9)

74. Kwa kiasi kikubwa imani hiyo **ilishampofua** na kumfanya **ashindwe** kuuangalia uhalisi.

(Wamitila, 1999, Ukur. 71)

117. **Sikumwogopa nyoka** kwa kuwa alikuwa na uwezo wa kuua. **Nilimwogopa** kutokana na maelezo ya baba aliyemchukia mnyama huyo. Alituambia mara nyingi kuwa huyo ndiye aliyekuwa chanzo cha uasi wa binadamu katika bustani ya Edeni…..

(Wamitila, 1999, Ukur. 46)

118. [Richard] aliyapitisha matamko mbalimbali [ya mhubiri] katika akili yake.

"Ulimwengu umejaa uchafu wa kila aina …"
"Watu wamegeuka makatili …"
"Uzinzi umeongezeka …"
…
"Amani hamna… Hamna tena amani…"

(Wamitila, 1999, Ukur. 153)

125. Richard Ngunze **alikata kauli**. **Alifikia uamuzi** kwa kutotaka kufikwa na yaliyomfika huyo tajiri aliyezungumziwa na mhubiri. **Aliamua** kumkubali Bwana na kuinua mkono wake wa kulia kama walivyotakiwa… Kila mtu alikuwa ameinua mkono wake kwa hivyo **aliamua** kujiunga na wenzake.

(Wamitila, 1999, Ukur. 154**)**

126. [Richard] **alishindwa kumsamehe** mke wake. Mtumishi wa Mungu aliyesisitiza faida na thamani za huruma katika maisha na aushi za binadamu **aliwiwa vigumu**. **Alishindwa na kuemewa**.

(Wamitila, 1999, Ukur. 183**)**

133 Wakati Nzisa **aliyatega masikio yake** imara na mara hii hayakurudi muflisi ila yalifanikiwa. Ilikuwa sauti ya bundi … Nzisa **alianza kushikwa na hofu kubwa. Moyo wake ulianza kututatuta kwa kasi ya ajabu. Kichomi cha ghafla kilimkata maini**. Aliifahamu fika imani ya jamii yake kumhusu ndege huyo. Watu walisema kuwa kila aliapo ndege huyo karibu na makazi ya watu pangetokea dhara kubwa hasa kama alikuwepo mgonjwa katika mji uliohusika.

(Wamitila, 1999, Ukur. 53)

134. Inaelekea [baba] **alihisi kuwa nilikuwa nikimwangalia**. **Macho yetu yalikutana**. **Aliyarudisha macho yake alipokuwa**; aliliinua parange. Alianza kuyapogoa matanzu ya ule mshomoro.

(Wamitila, 1999, Ukur. 109)

135. Aliinua shoka tena. Alikuwa hajaliachilia **alipomwona nyoka mkubwa** akitambaa na kunyinyirika kuelekea

alipokuwa amesimama. **Alilitupa lile shoka** kisha **akatimua mbio** kuelekea nyumbani. Aliamua kuuacha mkuyu huo.

(Wamitila, 1999, Ukur. 8)

136. Lakini **ghafla alishikwa na mchecheto** fulani. **Hofu ilimtambaa** mwili mzima. **Moyo wake ulipiga kwa kishindo sasa**. **Aligeuka kushoto**. **Macho yake yalitia nanga juu ya joka kubwa** lililonyenyereka kuelekea alipokuwa. **Alipiga usiahi**…. Alizinduka ndotoni.

(Wamitila, 1999, Ukur.27)

137. Richard aliyatupa macho yake juu ya lile karai. Palikuwepo na nzi sugu waliokuwa wakijitahidi kufaidi uhondo wa maji ya nazi. Walikuwepo pia nyuki ambao walikuwa katika harakati zao za kuhemea. **Nzi**. **Nyuki**. **Binadamu**. Wote walikuwa katika kinyang'anyiro cha kujitafutia. Ole wake yule ambaye angemuudhi mwenzake.

(Wamitila, 1999, Ukur. 100**)**

141. "Mfumo tulio nao ndio unaowafanya watu wawe hivi," alieleza June. Hebu angalia maisha ya hapa chuoni. **Karo**, **chakula**, **mavazi**: **pesa**. Kila kitu pesa."

(Wamitila, 1999, Ukur. 159)

176. …nilishaanza kuyadadisidadisi mambo fulani fulani kuihusu dini. …nilishaanza kuwa na wasiwasi mkubwa tarafu ya msimamo wa dini kumhusu mwanamke. …*Labda **mabadiliko ni maji ya kasi** na husemwa yajapo lazima uyape nafasi.*

(Wamitila, 1999, Ukur. 161)

190. Mm…labda ndivyo yalivyokuwa maisha. **Pambano** dhidi ya nguvu wasizoziweza watu. Je, **Mungu aliyaona haya**? [Richard] aliinua macho yake juu na kuyaelekeza mbinguni lakini yakapofushwa kwa muda na jua… **Limelimulika lile eneo sasa**; gimba nene la duara lililozungukwa na viwingu …Labda vile vilikuwa vinyusi vya jicho hilo; vikope vya kulilinda lisifikwe na uchafu. Uchafu wa kulisumbua jicho hilo… **jicho la Mungu.**

(Wamitila, 1999, Ukur. 117)

191. Imani hizo hazina nafasi katika ulimwengu wa leo. Mzee hizo ni fikira za zamani ambazo zimepitwa na wakati.

Umelogwa wewe? Zimepitwa na wakati gani? Imani zetu? …….

Mm. [Wazungu] wametukomboa kutokana na **giza la utamaduni**."

Hakika ni ukombozi huo!

(Wamitila, 1999, Ukur. 6)

192. Kwake [baba] kilichokuwa muhimu ni kuyafuata mafundisho ya dini na kuithamini nguvu ya sala. Kwa kiasi kikubwa imani

hiyo **ilishampofua** na kumfanya ashindwe kuuangalia uhalisi.
(Wamitila, 1999, Ukur. 71)

194. Matokeo ya mtihani wa mwigo yalishatoka sasa. Nilikuwa mwanafunzi wa pili katika orodha ya wanafunzi kumi bora. Wa kwanza alikuwa Catherine Ouko, msichana **mfupi sana**; labda ndiye aliyekuwa **mfupi** kuliko wote shule nzima. Alikuwa na **akili shupavu…**
(Wamitila, 1999, Ukur. 119)

205. Nilimwangalia baba tena na kuuwazia mwito wake wa ***nguvu ya sala*** ambao aliukazania kwa muda mrefu. *Je, ulikuwa wa kufaa au ulikuwa tasa? Je, matatizo mangapi ambayo yangesuluhishwa kwa mwito huo?* ***Umaskini uliowavaa watu nchini kama lubega****, tofauti zilizokuwapo kati ya matajiri na maskini, udhalilishaji wa wanawake katika jamii yetu.*
(Wamitila, 1999, Ukur. 199)

206. Roselyn alilia kwa sauti kutokana na maumivu ya bakora ya babake ambayo **aliachilia kama mtu anayemcharaza punda kihongwe**.
(Wamitila, 1999, Ukur. 193)

207. Baba alinitazama kisha akashusha pumzi ndefu. Alirudi na kuketi kwenye kochi alilokalia mwanzo na **akanywea kizembe kochini kama kifaurongo** kilichoguswa.
(Wamitila, 1999, Ukur. 198)

208. Bethsheba alikuwa nambari ishirini na mbili. Yeye hakujali sana. Hakuona sababu ya kuyaendeleza [masomo]; miaka hiyo ilimtosha. Alidai kuwa waliotakiwa kusoma ni wanaume wala sio wanawake ambao wangeishia kuwa watunzaji wa nyumba tu. Mimi sikuamini hivyo asilani. Hayo yalikuwa mawazo yaliyopitwa na wakati na kwa kiasi kikubwa niliamini kuwa huko kutosoma kwa wanawake ndiko kulikochangia katika kuwafanya wabakie palepale; **kuzungukia palapale kama pia**.
(Wamitila, 1999, Kur. 119 - 120)

221. [Richard] alishangaa. *Mbona binadamu wametovukwa na huruma kiasi hiki?…* Labda **maisha ya mjini yaliwanyang'anya binadamu chembe za huruma** zilizobakia, wameshapokwa hisia zote za kibinadamu…
(Wamitila, 1999, Ukur. 117)

223. Walifyoa na kurereja matusi. Walivurumiza magongo. Yule kijana alikuwa bado analia; alipiga usiahi sasa. Alimsihi Mungu wake amnusuru na hujuma za **wastaarabu** hawa waliokuwa wanatishia kumwua….
(Wamitila, 1999, Ukur. 115)

224. Hakuwa na haraka ya kutoka pale hadi aliporidhika **haki imetendeka**.

(Wamitila, 1999, Ukur. 115)

243. Babake Bathsheba alikuwa Mkristo. Hakuwa pasta kama babangu ila alikuwa mzee wa kanisa na wala sidhani kama alikuwa mkali kama alivyokuwa baba. **Labda siku moja angekuwa mkali; siku ambayo angekuwa pasta.**

(Wamitila, 1999, Ukur. 16)

244. “Imani hizo hazina nafasi katika ulimwengu wa leo. Mzee hizo ni fikira za zamani ambazo zimepitwa na wakati…

…[Wazungu] wametukomboa kutokana na giza la utamaduni.”

“**Hakika ni ukombozi huo!”**

(Wamitila, 1999, Ukur. 6)

251. “Mbona mlikuwa mnaongea Kizungu?” aliuliza baba.

“Kuna ubaya gani kuongea Kiingereza naye baba?” niliuliza.

Hakunijibu wala mama naye hakunijibu lakini wote wawili walinikodolea macho.

“Hiyo iwe mara ya mwisho,” alifoka baba. **Sikumwelewa**. **Sikujua kama alikusudia iwe mara ya mwisho kuongea Kiingereza na James au kuandamana naye**.

(Wamitila, 1999, Ukur. 107)

252. Baba aliichukia sana tabia hii ya kuangua kicheko. Alisema kuwa haikuwa tabia nzuri kwa mtoto wa kike. Nakumbuka jinsi alivyonicharaza siku moja baada ya kunisikia nikicheka kwa sauti ya juu. Niliamini kuwa tabia hiyo ilikuwa mbaya na haikosi **hata Mungu aliichukia**.

(Wamitila, 1999, Ukur. 31)

253. Roselyn alikuwa karibu na dirisa lililoelekea upande wa chini, akinenguanengua kiuno….. Alichelea kukutwa seli na babake; **ingekuwa kiama** kama angetekwa bakunja akiuchezesha mwili wake. **Kufuru si kufuru ile** kuuachia mwili wake hivyo. Baba yake angeghadhibika. **Yaelekea angefanya kitendo kikubwa kuliko alivyofanya Masiha baada ya kuwakuta walanguzi na wachuuza-njiwa katika hekalu la Bwana.**

(Wamitila, 1999, Ukur. 111)

Kiambatisho 3: Madondoo ya Data kutoka *Asali Chungu*

11. Katikati ya bao, **jana-jike** lenye jirim la kiboko linatia gati wenzake huku linapuma.

    …na aghalabu watu watakaopata nafasi hiyo ni kama **huyu kimwana** aliye ndani sasa hivi. Bahati ni ya warembo na wenye sura zao!

    (Mohamed, 1977, Ukur. 8)

12. Muda mrefu ukapita – hata huko, katikati ya kukata tamaa, mlango wa ofisini ukafunguliwa. **Kijanajali** kimoja kikadhihiri, macho kupekupe; haya za kujitia zimemvaa; damu mashavuni imemwiva; mabaka mawili ya damu iliyojikusanya yanaonyesha dhahiri chini ya shingo yake ya mbuni; na nywele zimetimka.

    (Mohamed, 1977, Ukur. 4)

13. [Bi Pili] anachacharika baoni, tayari kumvunjia mbarika **Bwana DC**. ….
    Wote wamekuja kwa dhamiri moja tu – kuonana na **bwana!**
    Wengine …. Wamepanda gari na kushuka hapo kwa tamaa kuwa angalau ‘**Bwana Mkubwa’** atawatazama kwa jicho la rehema.

    (Mohamed, 1977, Ukur. 1)

14. Wanyama wa **bwana huyu** walifungwa kondeni mwangu…. Shoti wameulaula muhogo wangu na migomba yote.
    Basi nd’o nimekuja kwa **huyu bwana**.
    Nawe unatarajia nini kwa **bwana huyu**?
    Shtakia Mungu dada kuliko kumshtakia **kiumbe huyu**…

    (Mohamed, 1977, Kur. 2-3)

15. Lawama na malalamiko juu ya matendo ya **Bwana Zuberi** yakaendelea.

    (Mohamed, 1977, Ukur. 4)

25. Si muhimu ujana au ubichi wake; muhimu ni **mipesa** yake ambayo ndiyo tegemeo lako, au sivyo?

    (Mohamed, 1977, Ukur. 92)

26. Majuto; majuto sina. Nina wasiwasi tu kukosa yale **mapesa** yake ambayo hata wewe uliniasa kuyang’ang’ania. Lakini sasa nakwambia kwa dhati: nimechoka kununuliwa.

    (Mohamed, 1977, Ukur. 8)

27. “Baada ya kuhakikisha hilo, Kabore akapeperukia chumba chengine…” Waliokuwepo walimshindikiza Kabore kwa macho – wakashuhudia **mkanzu** wake….

    (Mohamed, 1977, Ukur. 4)

25. Dude alimwangalia yule mchukuzi aliyemsalimu. Kwenye kibao cha nyuma cha huo **mbaiskeli wake**, palikuwa pamefungwa ndizi mbivu, ndizi mbichi… mtu angalistaajabu mchukuzi huyo aliwezaje kuburura **baiskeli hiyo** bila kupinduka nayo….Dude alimwangalia yule jirani yake kwa muda jinsi alikyokuwa akichapuka huku kailalia mbele baiskeli yake, na nyuma, yale mararu ya suruali na shati lake yanapeperuka.

(Mohamed, 1977, Ukur. 73)

46. Kukosa **kazi** kulikuwa kwingi kuliko kupata, na hata kama kijana mmoja alipata, ilikuwa **kazi** ya kuosha vyombo, kupika au kufagiafagia kwa Wahindi; au pengine iliwabidi wawe wapagazi au wapara samaki Forodha ya Papa. **Kazi** hizi hakuna iliyomfaa Dude, ingawa kwa uhitaji aliokuwa nao hangezionea taabu kama angezipata. Kwa hivyo akawa mmoja wa wale vijana waliobaki kuzurura wanatafuta **kazi**, mpaka siku moja akakata tamaa.

(Mohamed, 1977, Ukur. 65)

47. Mara nyingi aliwatia kazini jamaa zake wa Kihindi au yeyote aliyeweza kumpa tonge.” **Kazi** njema zikawa za mabwana na matajiri; kina Dude mara nyingi wakiangukia utopasi. Na hata hizo za utopasi, huweza kupita mwaka mzima mtu anakwenda akirudi bila kupata lolote, ila kuwaona wale waliokuja mwisho wanatoka ofisini na furaha, wamekwisha pata **kazi**.

(Mohamed, 1977, Ukur. 66)

48. “Hisia zake za ulimwengu… zimebadilika sana. Sasa moyo wake umehodhi chuki… Hatamani **kazi** kwa mtu yeyote zaidi ya ile [**kazi**] ya kupara magondi kwa Shabaani Supu.”
Kazi! **Kazi** gani itakayotafutwa tena na Dude? Labda sasa **kazi** imtafute yeye. Lau kama Bushiri anamwita yeye kwa **kazi**, basi angeliweza kuifikiria **kazi** hiyo; maana imemjia, hakuiendea. **Kazi** kwa wanyonge kama yeye, na lile darasa lake la sita alilomaliza?

(Mohamed, 1977, Ukur. 67)

20. Kwa mbali **uliwazukia ukuta** wa manjano uliozunguka **maskani ya Bwana na Bibi Zuberi**.

(Mohamed, 1977, Ukur. 94)

21. Palikuwa na vyumba vingi vidogovidogo vilivyojipanga sturi moja **kule mabandani** Mabanda yenyewe yalikuwa yamekamatana na jumba kubwa [la Zuberi] …...

(Mohamed, 1977, Ukur. 9)

99. Nawe unataraji nini kwa bwana huyu?
Pana la kutaraji bibi we. **Pana la** kuja tukirudi tu, angalau kudanganya roho…

(Mohamed, 1977, Ukur. 3)

100. **Kuna** walionunuliwa nyumba mama [**kuna**] waliofuliwa vyombo vya dhahabu kochokocho; **kuna** walioandikiwa vikataa na mashamba ya fahari; **kuna** wanaovaa na kubadili; [**kuna**] wanaotumia maisha yao bila ya kujua pesa inaingia wapi inatokea wapi. Nini basi? …iweje mama, bwana kama huyu kakutaka wewe usimjamili? Huoni kwamba unajiharibia hivyo? Eee mwana, unajivunjia riziki zako we!

(Mohamed, 1977, Ukur. 17)

101. Dude hufikiria furaha wanayokuwa nayo matajiri. **Wao ndio** wenye furaha ya kweli; [**Wao**] **ndio** wanaojua kucheka. **Wao ndio** wanaostahili kicheko.

(Mohamed, 1977, Ukur. 77)

102. **Leo ati** Amina anashindwa na la kufanya. **Leo ati** anaogopa watu kujua siri yake. **Leo ati** yeye na Biti Daudi wake wanachelea aibu na fedheha…

(Mohamed, 1977, Ukur. 152)

127. Ata! Kwani mimi nilishindwa? Umesahau Bwana wangu! **Nimeiangusha miamba kweli,** itakuwa kitoto kile? **Nimewatoa watu majumbani kwao**; **nimefungua milango ya chuma** na kupanda ghorofa ngapi, nikateremka na mabibiye kemkem, nikakuletea wewe, ije iwe mwehu yule? Anishinde nini?

(Mohamed, 1977, Ukur. 25)

128. Sio kulipwa tu… **Utaendeshewa** maisha yako. **Utakuwa** bwana wa bibi wa nyumba kubwa. **Utatoka** katika umaskini. **Utavuliwa** guo la unyonge. **Utakuwa** mtu. **Utaona** raha. **Utajua** nini maisha…. Wacha ujinga wako…. Ukitaka langu, ishike fursa hii barabara.

(Mohamed, 1977, Ukur. 88)

139. Chumbani kwa Bwana DC. (Mohamed, 1977, Ukur. 1)

142. Mimi ndiye niliyeufahamu ubaya na uzuri wa kazi yangu; na ikiwa ni utu, utu hautaweza kubadilisha chochote kuhusu **unyonge** wangu. Hauwezi **kunipa starehe**, **kutumia**, **kuvaa**, au **kuishi**. Utu wangu utanipa wapi hayo?

(Mohamed, 1977, Ukur. 92)

145. Hapo ilimlazimu **aabudu, atubie, astaghafiru** na **aombe** kwa Mola wake asimghadhibikie. Labda kwa unyenyekevu huo Mwenyezi Mungu Mwepesi wa kusamehe, ndimo alimotegemea kufutiwa yale maovu aliyoyatenda… akaishi kwa namna aliyoishi; akasahau mipaka yake, kuwa kwa hali yoyote ile yeye ni makhuluku…

(Mohamed, 1977, Ukur. 98)

152. Mara nyingi aliwatia kazini jamaa zake wa Kihindi au yeyote aliyeweza **kumpa tonge**." Kazi njema zikawa za mabwana na matajiri; kina Dude mara nyingi wakiangukia utopasi. Na hata hizo za utopasi, huweza kupita mwaka mzima mtu anakwenda akirudi bila kupata lolote, ila kuwaona wale waliokuja mwisho wanatoka ofisini na furaha, wamekwisha pata kazi.
(Mohamed, 1977, Ukur. 66)

163. Wakapita Ng'ambo ambako majumba, kama kawaida, yalikuwa yamekaliana ovyo, **matonge kwa matone**… 'kila ndege huruka kwa mbawa zake.' Bali kwa dhahiri, **mbawa za watu wengi huku Ng'ambo zilikuwa dhaifu**.
(Mohamed, 1977, Ukur. 89)

167. Hayo ndiyo yalikuwa maisha ya ulimwengu huu… kwa watu wa chini kama Dude.… Kuna maisha kwa wale waliotononoka kiasi cha kuwashibisha na kuwanenepesha mbwa wao … Kuna wengine, kama Dude, walioletwa dunuani **kwa kuteremkia migongo ya ufukara**…
(Mohamed, 1977, Ukur. 67)

168. Katika mushkeli tunamwona Amina na ule utashi wake na ashiki anavyosibu kumpata Dude hatimaye. Kwa kweli si Dude tu, bali anatumia **utajiri wake kuwa ni mtego** wa kumnasia nobe yeyote ampe lile alilolihamu yeye. Dude ambaye toka hapo kalemazwa, kapotoshwa tuseme, na juu yake yaje yale **maisha yake magumu yaliyomvaa** toka kuzaliwa kwake, ilikuwa rahisi kumnasa. Hivi zikaonekana **ncha** mbili tofauti zikikaribiana. Moja ni ile **ya ukarimu na uwezo wa kutoa** ambayo ilidhibitiwa na Amina, na nyengine ni **ya ule ulofa na haja iliyombana Dude**.
(Mohamed, 1977, Ukur. 104)

169. 'We poa bibiye, usitaharuki. Niachie mie; mambo yote yatakuwa waa, waa kabisa. Nitafuzu kama nilivyofuzu kwa yule kijana msalihina, **nikamteka** akawa **mali yako**.'
(Mohamed, 1977, Ukur. 62)

170. 'Basi….Nataka wewe uwe **mali yangu** pasi na mtu kuweza kuniingilia; umesikia hivyo?'

'Nimesikia,' Dude alijibu kwa utiifu. 'Hilo usiogope.'
Yeye mwenyewe alistaajabu kiasi gani alichomwogopa Bi Amina sasa …. **Kweli papa limemmeza.**
(Mohamed, 1977, Ukur. 120)

185. 'Bi Mkubwa nimetumwa nikuite'
Mastura alisita pale alipomtokezea Biti Daudi.
'Nani?' Biti Daudi aliuliza kwa hamasa, kama vile lile jina la Biti Daudi lilikuwa si lake….
'Wewe Bi-mkubwa,' Mastura alijibu kwa unyonge na hadhari ili lile **bomu la asubuhi** lisije likampasukia.
(Mohamed, 1977, Ukur. 22)

186. Lawama na malalamiko juu ya matendo ya Bwana Zuberi yakaendelea; na mara zogo likakua na kuhanikiza…. Ndipo Kabore, yule tarishi, alipoitwa ndani kwa Bwana. Alipotoka ndani akawa **ameunoa ulimi wake**.
'Zogo likiendelea, tamaa ya kuonana na Bwana itakuwa hakuna.
Fanyeni zogo na ufidhuli wenu, maana mnajitia kujua nyie.'
Kwa kujisalimisha, wote wakakubali **kufyata mikia yao**.
(Mohamed, 1977, Ukur. 4)

187. Asubuhi ile, Zuberi alipokwisha kukoga na kunywa chai, alikaa ukumbini akiwaza **mchezo wake wa jana**…..
Mohamed, 1977, Kur. 17 - 18)

188. Lile jina la Semeni lilikuwa na maana kubwa kwa Zuberi. Lilitosha kumpa mseto wa mawazo na fikira za yale yaliyopita ambazo alitoka nazo pale hospitali, zikamchukua kumwonyesha **televisheni ya siku zake za nyuma**, siku za matendo. Aliviona vitakuro vyake siku ile, siku ya siku, vya mchana kuliwa usiku – **siku aliyoiramba asali**. Na Semeni akatoweka.
(Mohamed, 1977, Ukur. 174)

189. Midomo yake ilimtetemeka, akainua mkono wake wa kuonyesha kidole pale alipokiona kivuli cha Semeni; halafu akameza mate. Yalikuwa **mate mazito machungu**. Huo ndio ulikuwa mwisho wa ladha yake. Kweli **utamu umegeuka uchungu**, lakini hakuwa na budi kuumeza. Kama aliwahi kunywa asali, ndipo leo kajua kuwa **asali chungu.**

(Mohamed, 1977, Ukur. 186)

196. Nyumba ilikuwa imeamka. Matayarisho mbalimbali yameshafikia kileleni. **Nyumba hii ilikuwa mfano wa hoteli**; hamkani na shughuli huanza kabla ya jua halijapasua, na kumalizikia pale bwana na bibi mwenye nyumba wanapoingia chumbani mwao kulala.
(Mohamed, 1977, Ukur. 11)

200. Kuunguako ndiko kuteketeako. Hana mtu wa kumwendesha sasa ameshavunja ungo; akawa anatangatanga na ulimwengu – leo kwa huyu, kesho kwa yule. **Akarushwa kama mpira**, naye akafuata. Hakuwa na hila ya kujiokoa; mtoto mdogo mwanamwali akaelekea mjini.
(Mohamed, 1977, Ukur. 46)

204. Alimwepuka [Dude] makusudi; hakupenda kumwangalia. Dude sasa ni kiraha; kinyaa…. Moyo wake ulikuwa umeshaamua, kama ulivyowahi kuamua mara nyingi katika maisha yake. …. **Atamtema Dude kama mate**; na katu hatorudi kumramba. Na yeye Dude hajui kiasi gani alichojivunjia.
(Mohamed, 1977, Kur. 128 – 129)

214. Alikunja pazia la mlango, akapapasa ukuta wake na kuwasha swichi. **Taa zake za therea… zilimwitikia** pamoja, zikamwaya anga la kupendeza…
Madirisha yake yenye virukia vya vioo **yalikuwa yanatazamana huku na huku**. Mapazia ya kitambaa… **yalikuwa yakichezacheza kwa furaha** … Kutani baina ya madirisha, palikuwa pamepachikwa vichwa vya nyemela …. Vimekabiliana… **vikamshuhudia** Zuberi aliyekuwa akikata ukumbi wake kwelekea bewani.
(Mohamed, 1977, Ukur. 7)

215. Ngazi aliiteremka salama pasi na vishindo. **Hapana aliyemsikia wala kumwona, ila milango** ambayo sasa alikuwa akiifungua na kuifunga.
(Mohamed, 1977, Ukur. 9)

216. Jumba hili lilikuwa lile lile. Kuta zake zilizokwenda juu ghorofa moja zilikuwa daima **zikiwakejeli** makafiri na wachochole. Waomba pesa wapitapo, husimama na kuinua nyuso zao kuangalia juu;
(Mohamed, 1977, Ukur. 120)

217. Mbali zile mboga na matunda ya viungo vya mchuzi; vyote vilikuwa **vikichekelea furaha na kuwaita wanunuzi** kujinunulia walichopenda. Kulikuwa na kila kitu sokoni kwa mwenye pesa zake, lakini kwa Dude palikuwa patupu.
(Mohamed, 1977, Ukur.78)

218. Nguzo za umeme na simu zilikumbwa nyuma pale *Vauxhall* ya kijani **ilipokuwa ikitafuna masafa** yaliyobaki kambla ya kufika Maungani… Ikakata upepo huku **upepo ukinguruma** kwenye vioo vyake.
(Mohamed, 1977, Ukur. 89)

219. 'Hili shamba lote ni la Bwana Zuberi. Huku halina mwisho, na huku mpaka bondeni. Halafu linapanda kilima; halafu linateremka, ndio linapakana na Bi Amina. Na **hilo lake linamwambia la Bwana Zuberi sogea huko**,' Bushiri alisema akiashiria.
(Mohamed, 1977, Ukur. 92)

220. Nyumba ya Bi Amina imejengwa karibu na ufukwe nyuma ya kisiwa cha Weba; **imejitenga kutafuta faragha**, mbali na vijumba vya kijiji chenyewe… Kwa pale kisiwani, hiyo ilikuwa nyumba pekee iliyovutia. Kwa ukubwa labda inashindana na ule msikiti; lakini kwa uzuri hapana nyengine iliyoweza **kuivua kilemba**.
(Mohamed, 1977, Ukur. 116)

225. Jikoni mfereji ulikuwa ukimwaya maji. Maji kila pahali – chooni, ambako **waungwana** wakikoga ….
(Mohamed, 1977, Ukur. 12)

226. Wote waliteremka. Mwenyeji wao, Mzee Mbaruku, mwangalizi wa nyumba ya Bi Amina, alifika hima kuwalaki; akawa anatoa mizigo waliyokuja nayo **waungwana**. Dude akafunga vioo vya gari na kutia milango yote kufuli.
(Mohamed, 1977, Ukur. 112**)**

228. Dau la kiasi lililetwa… Mzee Mbaruku akaanza kupakia mizigo kwenye hilo dau, na alipomaliza akawataka **waungwana** waingie. Bi Amina alivua viatu na buibui lake…Kwisha hivyo… alipandisha kanzu yake na kuyawacha huria mapaja yake kulimbukwa kuonekana na wale…
(Mohamed, 1977, Ukur. 114)

229. Baadaye akawa tayari kukikabili chumba cha Semeni. Akaanza kunyatia. Alinyemelea kwa ustadi mkubwa. **Mungu bariki** alikuwa amefunga matambara miguuni.
(Mohamed, 1977, Ukur.**114)**

230. Aliporejea chumbani kwake usiku wa jana, Zuberi alipoa na kuburudika. Hamu yake imezimwa; raghba yake imepozwa…. Yaliyobaki yalikuwa ya kesho, na **kesho ina Mungu**.
(Mohamed, 1977, Ukur. 21)

231. Hawa, aliona Dude walikuwa wapagazi. Naye alikuwa **anawahusudu wapagazi** kila siku – vifua vyao vipana…walikuwa wanaume kweli kweli, mtu hawezi kuwachezea.
(Mohamed, 1977, Ukur. 50)

233. *Labda Kheri Kharibu ndio akacheka namna ile, kwa sababu ulimwengu alikuwa hauoni, hausikii, wala haufuati kuviona viroja na vituko vyake.* ***Watu kama hawa wana nafuu****.*
Dude naye alitamani apate afueni ile.
(Mohamed, 1977, Ukur.77)

234. …niliona bora utumwa wa kuwa mfungwa kuliko kuwa na uhuru katika ulimwengu ambao hauwezi hata kunipa chakula….Nje kuna maonevu, unyonge na utumwa….Yakinijia mawazo hayo, huona nijitie katika hatia ili **nirudi jela ninusurike**. Hustahabu taabu ya kutumwa jela nikapata chochote, mradi silali na njaa, kuliko kutamba na ulimwengu mchana kutwa, au mara nyingi kumeza mate.
(Mohamed, 1977, Ukur. 83)

235. Kwa mafukara, hizo huwa ni **siku ambazo Mwenyezi Mungu humwaya neema zake kwa mlango wa nyuma** ili kuwaneemesha maskini wasiojiweza, japo kwa mwaka mara moja; na hiyo huwa **ni kama kuwarejeshea akali ya matone yao ya damu iliyonyonywa**… hutapikwa.
(Mohamed, 1977, Ukur. 29)

278. Nguzo za umeme na simu zilikumbwa nyuma pale ***Vauxhall* ya kijani** ilipokuwa ikitafuna masafa yaliyobaki kabla ya kufika Maungani.
(Mohamed, 1977, Ukur. 89)

279. Nyuma ***Vauxhall*** **nyengine ya maziwa** ilikuwa imeshafika, na dereva wake Hassani…
(Mohamed, 1977, Ukur. 95)

Kiambatisho 4: Madondoo ya Data kutoka *Kasri ya Mwinyi Fuad*

22. Usiku ule Vuai alirejea nyumbani amechoka…… Hakusimama popote ila alifululiza **bandani kwake** kwenda kupumzika.
(Shafi, 1978, Ukur. 33)

23. Kijakazi aliondoka bandani humo ….alikwenda zake **chumbani kwake nyuma ya banda hilo** [la ng'ombe]….
(Shafi, 1978, Ukur. 88)

34. Sikiliza Mkongwe mwanangu, hayo ndiyo **majaaliwa** yangu. Kuna wengi Bwana Mungu **amewajaalia** na kuwatukuza mabwana wakubwa na wengi **amewajaalia** umaskini. Lazima ufahamu Mkongwe kama kila mtu ana **majaaliwa** yake. Hivyo ndivyo ulimwengu.
(Shafi, 1978, Ukur. 70)

35. Lakini ukitazama hayo ni kweli. Hawa mabwana shamba wanatutesa sana lakini hatuna la kufanya. Ndio **tulivyojaaliwa.**
(Shafi, 1978, Ukur. 26)

50. Kijakazi mbona unafanya **kazi** namna hii? hivi utajiua kwa **kazi**. Halafu unapata faida gani hasa kujivunja kwa **kazi** namna hii? Mkongwe aliuliza.
(Shafi, 1978, Ukur. 17)

51. "Siku zote nimekuwa hivi! Sasa hata sihisi kama ninafanya **kazi** kwa sababu nimelemaa kufanya **kazi** namna hii," Kijakazi alijibu.
(Shafi, 1978, Ukur. 18)

52. "Unasema nini?" **Leo** wewe unakataa kutii amri yangu," Fuad alimkaripia Kijakazi…
"Ama **leo** Kijakazi umefurutu ada! Wewe **leo** unathubutu kuvunja amri yangu na kunieleza maneno kama hayo? Hujapata hata siku moja kufanya utovu wa adabu kama hii **leo**! **Leo** ng'ombe wewe unathubutu kuniasi?
"Mimi… sitopiga magoti tena mbele yako," alisema Kijakazi…
Leo Kijakazi aliazimia kweli na makelele ya Fuad hayakumshtua hata kidogo.
"Zaidi ya miaka hamsini sasa umekuwa shambani hapa pamoja na sisi… **Leo** hii unata…
Fuad aliona **leo** kweli imemdhihiri na Kijakazi si wa kuchezewa tena.
(Shafi, 1978, Kur. 90 - 93)

53. **Pale pale** watu walitoka na kumwacha Fuad amekaa **pale** ukumbini. Alibakia **pale pale** juu ya kiti amepigwa na bumbuazi hajui la kufanya. Hamaki zilikuwa zimemjaa lakini alizidiwa nguvu. Usiku ulikuwa umekwisha ingia na Fuad aliwasha karabai

na baadaye akarejea **pale pale** alipokuwa amekaa juu ya kiti.
(Shafi, 1978, Kur. 79 - 80)

76. "… Bwana Marjebi … nataka unieleze khasa, mana'ke **hawa….**" Fuad alisita kidogo na kumtazama Bwana Marjebi huku akitafuta neno la kusema, "**ng'ombe hawa**, nisamehe…lakini sina vingine vyovyote vya kuwaita ila hivyo – **hawa** siku hizi wamekuwa hata hawaogopi."
(Shafi, 1978, Ukur. 35)

78. "Wewe! Wewe! Mimi nakutafuta wewe tokea saa ile!" alianza Fuad huku akimwelekezea [Vuai] kidole chake….
Juzi ulikuwa unatoka wapi?
"Mkutano," alijibu Vuai **bila ya kumwita Fuad 'Bwana'** kama ilivyo kawaida yao.
(Shafi, 1978, Ukur. 27)

79. **Sikiliza Fuad,** mimi nitakufanyia kila utakalo…..lakini sitopiga magoti tena kukuvua viatu…. Kwa hasira, Kijakazi alimwambia Fuad, ikiwa ndiyo **mara yeke ya kwanza kumkata jina**, yaani kumwita jina lake **bila kutanguliza** '**bwana**'.
(Shafi, 1978, Ukur. 90)

80. **Sikiliza Fuad!** Nakwambia wazi, baada ya leo – nakwambia tena – baada ya leo, **sitokubali** kukutumikia utumwa wa namna yoyote!
(Shafi, 1978, Ukur. 94)

81. "Nafikiri unaelewa kuhusu sheria mpya ya ardhi?" …
"Naam! Nimeisikia **Bwana**!" Fuad alijibu, wakati umemgeukia na sasa naye anajua kuita '**Bwana**'.
(Shafi, 1978, Kur. 54 -55)

82. Baada ya kufika tu gari hilo, alishuka mtu mmoja na kumwuliza Kijakazi, "**Fuad tumemkuta**?"
"**Bwana**? Si … sijui, ngojea nikatazame ndani," Kijakazi alijibu.
... mara [Fuad] **alitoka nje mbio.**
Nipo! **Nipo Bwana!** Je, mnataka kuonana na mimi? Fuad aliuliza …
(Shafi, 1978, Ukur. 95)

83. "Hivyo **Bi Kijakazi** utaendelea kufanya kazi namna hii mpaka lini?" Mkongwe alimwuliza.
Kijakazi alishtuka kwani hajapata kuitwa **bibi** hata siku moja maishani mwake. Bibi aliyemjua yeye duniani ni **Bibi Maimuna** tu ambaye alifariki zamani.
Unasemaje vile? **Umeniita Bibi**? Tafadhali usiniite hivyo; mimi ni **Kijakazi tu**."
(Shafi, 1978, Ukur. 97)

84. Basi sisi tumekuja **kukujuvya** kwamba…. **inakupasa ujue** kwamba … sasa **unaweza** kuendelea na kazi zako mpaka **tutakapokuletea** taarifa nyingine," alieleza yule mtu.
"Nimesikia, Bwana! **Nimesikia**!"
(Shafi, 1978, Kur. 54 -55)

85. Nakumbuka! Nakumbuka vizuri! Sielewi, **Bwana**, na itakuwa vizuri **ukinifahamisha**!
(Shafi, 1978, Ukur. 55)

86. Si muhimu ikiwa **wewe** unaunga mkono au huungi mkono, **sisi** tumekuja kukwambia tu…
(Shafi, 1978, Ukur. 59)

88. Haukupita muda **akang'amua** kuwa utiifu wake ... ulikuwa hauna maana kwa Fuad.
Fikira za Kijakazi zilizidi kubadilika. Alizidi **kuona** wazi kwamba maisha yake yote aliyapoteza pale kwa… **Alizidi kuamini** kwamba siku zote alikuwa akijidanganya …
(Shafi, 1978, Ukur. 89)

103. ...kawaida yake ni ile ya uchovu, ya mtu aliyechakaa, mwenye mikono iliyojaa visuguru na visigino vya miguu vilivyolika kwa kwenda, **si** mvua, **si** jua; **si** usiku **si** mchana, kazi hazikumwisha Kijakazi.
(Shafi, 1978, Ukur. 2)

104. Nimechoka kutumwa na kusumbuliwa na Fuad. Mtu huyu **hana** wema wala ihsani. **Hana** fadhili, ni mtovu wa adabu.
(Shafi, 1978, Ukur. 68)

105. Kwa Kijakazi, Fuad alikuwa ni mtu aliyetimilia; **hakuna** mwenye heshima na adabu kumshinda yeye**, hakuna** mzuri wa kumshinda yeye; **hana** dosari hata kidogo.
(Shafi, 1978, Ukur. 72)

106. "Nimechoka, nimechoka roho yangu na utumwa huu usiokuwa na malipo wala hisani; wewe **huna** haya wala **hujui** vibaya, **huna** heshima na wala **hujui** unajiona nani.
(Shafi, 1978, Ukur. 90)

107. Mara Fuad alikuja matao ya chini na kuanza kuzungumza na Kijakazi kwa upole. "Sikiliza Kijakazi, sharti ujue kama sisi tunakuona kama **wewe ni** mmoja wetu ndani ya nyumba hii, **wewe ni** kama bibi yangu, [**wewe**] **ni** sawasawa na ye yote katika ukoo wangu. **Wewe** wakati wote ulikuwa mtumishi mtiifu. Kijakazi sharti ufahamu kwamba **wewe ni** kama mzee wangu kwani **wewe ndiye** uliyenilea. ….nami nakwambia

waziwazi kama **wewe** umekuwa kama mama yangu wa pili."

(Shafi, 1978, Ukur. 67)

108. Fuad **hakuwa na** la kufanya. **Hakuwa na** njia yoyote ya kuyazuia yaliyokuwa yakitokea. Kila siku alisikia matangazo ya mapinduzi katika redio, matangazo ya kuchukuliwa mali za mabepari, kudhibiti biashara ya nje na ndani… kuzuia kabisa unyonyaji wa mabepari na mabwana shamba. Yeye **hakuwa na** la kusema isipokuwa kulaani na kutukana tu na hayo hayakumsaidia chochote.

(Shafi, 1978, Ukur. 57)

109. Gari lilikwenda mjini abiria akiwa Fuad peke yake. Hakuzungumza na dereva wake njia nzima. Fikra mbalimbali zilikuwa zikimwendea kichwani mwake. Alifikiri ulwa **aliokuwa nao**, pesa **alizokuwa nazo,** amri **aliyokuwa nayo** kwa wapagazi wake wote shambani kwake.
Lakini halafu zilimjia fikra kwamba juu ya yote hayo alikuwa hastarehe kama anavyotaka yeye.

(Shafi, 1978, Ukur. 24)

110. Zaidi ya miaka hamsini sasa umekuwa shambani hapa **pamoja na sisi**, mvua, jua, **tuko pamoja** hapa, shida, raha almuradi **tuko pamoja**.

(Shafi, 1978, Ukur. 91)

130. "Fikira nzuri!" Fuad aliruka na kusema. "Mimi **nakubaliana moja kwa moja** na fikira hizo. **Najua vizuri** kwamba hilo ni jambo zuri na **naliunga mkono** kwa moyo wangu wote. **Niko tayari kabisa** kuishi kijamaa."

(Shafi, 1978, Ukur. 58)

134. Maana yake ni kwamba shamba lako pia itabidi ligawiwe na wewe mwenyewe **utapewa sehemu yako** ili nawe uwe na kitu cha kukuendeshea maisha yako. **Utapatiwa ardhi inayokutosha**, lakini itakubidi uilime wewe mwenyewe….

(Shafi, 1978, Ukur. 56)

132. Tena kitu kimoja ….. usichanganyike naye [Mkongwe]. Usichanganyike naye hata kidogo kwani yeye **amekwisha tutoka** na karibu namwona **atatukimbia** hapa nyumbani. Siku hizi **amezidi**, hafanyi kazi, **amekuwa mvivu** …. **amekuwa mjeuri**.

(Shafi, 1978, Ukur.68)

164. …siku kama hiyo, siku ambayo Fuad huja mjini kuuza karafuu… **huzama katika starehe** za mjini na anaporejea nyumbani huwa yu chopi hajali kitu chochote.
(Shafi, 1978, Ukur. 21)

165. Muda ulivyopita ndivyo meza ya Fuad ilivyojaa watu na ilipofika saa tisa juu ya meza yake palikuwa na **msitu wa chupa** zilizojaa aina tofauti za ulevi.
(Shafi, 1978, Ukur. 22)

166. Jambo lililomshangaza [Kijakazi] lilikuwa kule kumsikia Fuad akiwataja watu kama Pandu, Haji na Makame kama majirani zake; watu ambao, hapo zamani, hakuwa na mahusiano nao yoyote. Watu hao walikuwa wakiishi hapo Koani lakini walikuwa ni katika **mafukara wa kutupwa**.
(Shafi, 1978, Ukur. 56)

182. Baada ya Kijakazi kujiuliza maswali yote yale, kidogo kidogo alianza **kuona mwanga**.
(Shafi, 1978, Ukur. 89)

201. Kwa Kijakazi, mwendo wa kufanya kazi kwa Fuad ulikuwa ni ule ule. Alifanya kazi kama wakati wa uhai wa marehemu Bwana Malik…. **akifanya kazi kama mashine.** Akili yake yote ilikuwa iko katika kufikiria kazi…. **Alifanya kazi kama punda** na hapana binadamu aliyeweza **kufanya kazi mfano wa mwanamke huyo.**
(Shafi, 1978, Ukur. 9)

202. Si kama Mariam alikuwa mkaidi hapo kazini. Alikuwa anajitahidi kufanya kazi zake kama anavyoweza lakini alikuwa hakubali **kutumwa kama punda.** (Shafi, 1978, Ukur. 12)

203. “Hapana kosa lolote kufanya kazi yako vizuri. Sidhani kama kuna mtu atakayekufukuza hapa na pia sioni sababu kwa nini **ufanye kazi yako kama mnyama,**” Mkongwe alimwambia Kijakazi.
Siku nyingi Mkongwe alifanya kazi pamoja na Kijakazi na hakuacha kusema naye ili **afanye kazi kibinadamu….**
(Shafi, 1978, Ukur. 18)

236. Mzee huyu hakujua nia halisi ya matembezi ya Fuad na hata kama angejua **angeona ni fahari kubwa kwake kwa kuwa na binti anayefaa bwana shamba mkubwa yule**.
(Shafi, 1978, Ukur. 14)

237 Fuad alijenga msikiti mdogo, mzuri, karibu na nyumba yake na **ndani ya msikiti huo walisali wale waliokuwa na madhehebu ya kiibadhi tu kama yeye mwenyewe**
(Shafi, 1978, Ukur. 16)

238. …shamba la Bwana Malik lilikuwa daima zuri….Mabondeni, mpunga ulistawi kwa wingi… **yote haya yalimletea Kijakazi furaha maalum ijapokuwa yeye hakupata kitu chochote katika mazao yanayopatikana shambani humo**.

(Shafi, 1978, Ukur. 2)

239. Kusema kweli **kazi zilikuwa zimeshamchosha Kijakazi ijapokuwa kila alilofanya alilifanya kwa furaha**……furaha iliyochanganyika na machovu.

(Shafi, 1978, Ukur. 3)

240. "Hata mimi walipokuja kwangu walinambia maneno hayo hayo! Hawa watu wana wazimu? **Hawajui kama ni dhambi kubwa kumnyang'anya mtu mali yake**," Swelum naye aliingia kati.

(Shafi, 1978, Ukur. 57)

241. "Umaskini ulikuwa umejaa nchini na unyonge umewazonga wananchi. Hata hivyo,….wafanyakazi hawakwisha kufanya migomo, maandamano na mikutano….ya kupinga mabepari na makabaila na kudai uhuru kutoka kwa wakoloni…..
Yeye [Kijakazi] alifurahi kuona yote yaliyotokea [nchini] **hayakumhusu**. Kila mara alikuwa **akishukuru Mungu kwa kumpa uwezo wa kufanya kazi yake vizuri**.

(Shafi, 1978, Ukur. 11)

242. Mambo ya ujamaa hakuyaelewa hata kidogo. Aliona **yote yale hayakumhusu yeye**.

(Shafi, 1978, Ukur. 56)

245. Kijakazi sharti ufahamu kwamba wewe ni kama mzee wangu kwani wewe ndiye uliyenilea. Nakuahidi kwamba **utakapofariki nitakufanyia mazishi makubwa yasiyowahi kufanywa hapa Koani.**

(Shafi, 1978, Ukur. 67)

246. "Usichanganyike naye [Mkongwe] hata kidogo kwani yeye amekwishatutoka … lakini mwache aondoke. **Atakapoondoka itakubidi wewe Kijakazi ufanye kazi zaidi."**

(Shafi, 1978, Ukur. 68)

247. Ole wake Kijakazi kwa msiba mkubwa aliokuwa nao kwa kufiwa na **Bwana wake**, alikuwa mnyonge kuwashinda wote na kila wakati … huomboleza mpaka macho yakavimba. Kifo cha Bwana Malik kilikuwa ni msiba mkubwa kwa Kijakazi**.**

(Shafi, 1978, Kur. 8 - 9)

248. Kiasi cha saa tatu za usiku teksi ilifika pale nyumbani kumleta Fuad. "Oh! Haijambo **bwana** amerudi salama!"

Kijakazi alisema akishusha pumzi na kupumua**…** Alimkunjulia chandarua …. alisimama kwa unyonge pembeni ya kitanda na kumtazama **bwana wake mpenzi** ….
(Shafi, 1978, Kur. 22 - 23)

249. Kijakazi alikuwa akimvua viatu Fuad na wakati huo ilimjia huruma kubwa kumhurumia **Bwana wake, Fuad mpenzi**…
(Shafi, 1978, Ukur. 76)

250. "Mwachilie, sasa nitamwita huku ndani na akifika atashika adabu yake: nitamwita mmoja katika wale mbwa wenzake **aje anisaidie kumkamata**."
Fuad alikuwa mwingi wa mwili lakini kwa ajili ya kukaa bure maisha yake yote, unene aliokuwa nao ulikuwa ni wa maji matupu. Hakumweza Mariam kwa vibiru na ilimbidi ampate mtumishi wake mwingine kumsaidia.
(Shafi, 1978, Ukur. 13)

276. "Ala! Kwani kesho wanakuja?" Bibi Maimuna alijidai kustaajabu kama kwamba hakujua kuwa kila Jumapili Bwana Zein na mkewe huja kwa **gari lao jipya** la aina ya **May flower** kuwatembelea.
(Shafi, 1978, Ukur.6)

277. Siku chache baadaye, Fuad alinunua **gari kubwa** la aina ya ***Rambler*** lenye rangi ya bahari.
(Shafi, 1978, Kur. 24 -25)

Kiambatisho 5: Cheti cha Plagiarism

SR744

ISO 9001:2019 Certified Institution

THESIS WRITING COURSE

PLAGIARISM AWARENESS CERTIFICATE

This certificate is awarded to

KYOMUHENDO VICTOR

SASS/DPHIL/KIS/02/2019

In recognition for passing the University's plagiarism

Awareness test for Thesis **entitled: UCHANGANUZI WA KIMTINDO WA MASUALA YA DINI NA MAMLAKA KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI with** similarity index of 2% and striving to maintain academic integrity.

Word count:55500

Awarded by

Prof. Anne Syomwene Kisilu

CERM-ESA Project Leader   Date: 13/01//2025